# Historia ya Tanzania na Maadili

## Shule za Sekondari

## Kitabu cha Mwanafunzi
## Kidato cha Tano




Taasisi ya Elimu Tanzania

# Historia ya Tanzania na Maadili

## Kitabu cha Mwanafunzi
## Kidato cha Tano

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1527

Jina la Chapisho: Historia ya Tanzania na Maadili Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9912-753-44-0

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 3 Juni 2024 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Kidato cha Tano katika Ngazi ya Elimu ya Sekondari nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa mwaka 2023.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

FOR ONLINE READING ONLY

*Taasisi ya Elimu Tanzania*

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2024

Toleo la Kwanza 2024

ISBN 978-9912-753-44-0

Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es Salaam

Simu: +255- 735041168/ 735041170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

FOR ONLINE READING ONLY

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kudurufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

## Yaliyomo


**Orodha ya vielelezo** ........ v

**Orodha ya vifupisho** ........ vi

**Shukurani** ........ vii

**Dibaji** ........ viii

Sura ya Kwanza ........ 1

Historia, utambulisho na maadili ya taifa ........ 1

**Dhana za historia, utambulisho na maadili ya taifa** ........ 1

**Uhusiano wa kinadharia kati ya historia, utambulisho na maadili ya taifa** ........ 3

**Misingi ya kihistoria iliyounda utambulisho wa taifa** ........ 10

**Misingi ya kihistoria iliyounda maadili ya taifa** ........ 12

**Nafasi ya historia na maadili katika kujenga fahari ya taifa** ........ 15

**Nafasi ya tunu za taifa na maadili katika kujenga misingi ya uongozi bora** ........ 21

**Mikakati ya kulinda historia, utambulisho na maadili ya taifa** ........ 25

Sura ya Pili ........ 31

Mchango wa historia na urithi katika maendeleo ........ 31

**Dhana ya historia na urithi wa taifa** ........ 31

**Historia na urithi wa taifa katika maeneo mbalimbali nchini** ........ 32

**Mchango wa historia na urithi katika maendeleo ya taifa** ........ 35

**Uhusiano kati ya maadili na urithi katika kuleta maendeleo ya taifa** ........ 37

**Uhifadhi wa urithi kwa maendeleo endelevu ya taifa** ........ 39

Sura ya Tatu ........ 46

Fursa za uwekezaji zitokanazo na vivutio vya kihistoria na urithi ........ 46

**Dhana ya uwekezaji** ........ 46

**Fursa za uwekezaji zitokanazo na vivutio vya kihistoria na urithi** ........ 47

**Uwekezaji katika vivutio vya kihistoria na urithi** ........ 51

**Nafasi ya historia na urithi katika ushirikiano na biashara za kimataifa** ........ 55

**Vitendo vya kimaadili vinavyokuza fursa zitokanazo na urithi** ........ 59

**Vitendo visivyo vya kimaadili vinavyodumaza fursa zitokanazo na urithi** ........ 60

Sura ya Nne ........ 64

Jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni ........ 64

**Maana ya maendeleo ya jamii** ........ 64

**Vichocheo vya maendeleo katika jamii za Kitanzania** ........ 64

**Jinsi maadili ya jamii za Kitanzania yalivyochochea maendeleo** ........ 78

**Mifumo ya kusimamia maadili kabla ya ukoloni** ........ 82


FOR ONLINE READING ONLY

Sura ya Tano ........ 86
Uhusiano wa jamii za Kitanzania na jamii nyingine ........ 86
**Uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na jamii nyingine za Afrika........ 86**
**Uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na za Mashariki ya Kati na Mbali........ 92**
**Uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na jamii za Ulaya........ 102**
**Uhusiano wa mifumo ya maadili ya Kitanzania na jamii zingine........ 107**

Sura ya Sita ........ 113
Mifumo ya kihistoria na maadili kabla ya ukoloni........ 113
**Mabadiliko ya kihistoria na maadili Tanzania........ 113**
**Matokeo ya mapokeo ya mifumo ya kihistoria na maadili ........ 117**
**Mapokeo ya kidini yalivyochangia kujenga maadili........ 119**

Sura ya Saba ........ 129
Nguvu ya ukoloni katika kujenga mwelekeo mpya wa jamii ........ 129
**Dhana ya ukoloni, nguvu laini na nguvu ngumu........ 129**
**Chimbuko la ukoloni na kuenea kwake Tanzania........ 136**
**Athari za ukoloni........ 139**
**Uzalendo na ujasiri wa Watanzania dhidi ya ukoloni........ 148**

Sura ya Nane ........ 157
Mchango wa ukoloni katika mfumo wa maadili ya Kitanzania ........ 157
**Maadili na mfumo wa usimamizi kabla na wakati wa ukoloni........ 157**
**Uhusiano wa maadili kabla na wakati ya ukolon........ 162**
**Athari za ukoloni katika mfumo wa maadili ya Kitanzania........ 167**

Faharasa........ 172

**Bibliografia** ........ 173

FOR ONLINE READING ONLY

## Orodha ya vielelezo

1.1: Jengo la Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika....27
2.1: Sarafu za dhahabu zilizotumika katika mji wa Kilwa....33
2.2: Watalii wakitembelea handaki katika kambi ya FRELIMO Kongwa....35
3.1: Ngoma ya Muheme ya jamii ya Wagogo....50
3.2 Jengo la Caravan Serai Bagamoyo....54
4.1 Nyumba ya kabila la Wahaya....76
4.2 Nyumba ya kabila la Wagogo....76
5.1: Njia za biashara ya masafa marefu katika Afrika Mashariki....87
5.2: Njia ya Waajemi na Waarabu kutoka bara la Asia hadi Tanganyika....94
5.3: Njia ya Wareno kutoka bara la Ulaya hadi Tanganyika....103
6.1: Moja ya msikiti uliojengwa katika mji wa Kilwa....123
6.2: Kanisa la kwanza kujengwa Tanzania....125
7.1: Shule ya kwanza ya serikali ya kikoloni (Old Tanga School)....145
7.2: Mtwa Mkwawa....153
7.3: Mangi Meli wa Old Moshi....153
7.4: Liti Kidanka....155

FOR ONLINE READING ONLY

## Orodha ya vifupisho

| | |
|---|---|
| **AU** | **Africa Union** |
| **BAKITA** | **Baraza la Kiswahili la Taifa** |
| **BASATA** | **Baraza la Sanaa la Taifa** |
| **DCEA** | **Drug Control and Enforcement Authority** |
| **ES** | **Ethics Secretariat** |
| **NACSAP** | **National Anti-Corruption Strategy and Action Plan** |
| NAOT | National Audit Office of Tanzania |
| **TAKUKURU** | **Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa** |
| **TANU** | **Tanganyika African National Union** |
| **TRA** | **Tanzania Revenue Authority** |
| **THBUB** | **Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora** |

FOR ONLINE READING ONLY

## Shukurani

**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inautambua na kuuthamini mchango muhimu wa washiriki kutoka taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za serikali zilizoshiriki kufanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi. Kipekee, TET inatoa shukurani kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.**

**Vilevile, TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu kutoka taasisi mbalimbali kama ifuatavyo:**

Waandishi: **Dkt. Jerome S. Machange, Bw. Godlove E. Siara, Bw. Salum S. Momboka, Bw. Davies Mlay, Bw. Bonaventura A. Bazira (TET), Dkt. Hamis M. Mfaume (DUCE), na Dkt. Juma M. Paresso (UDSM).**

Wahariri: **Dkt. Evaristi C. Magoti, Dkt. George Ambindwile na Dkt. Michael A. Mashauri (Mhariri wa Lugha) (UDSM)**

Msanifu: **Bi. Victoria R. Mwinyi**

Mchoraji: **Bw. Hance E. Wawar**

Mratibu: **Dkt. Jerome S. Machange**

**Aidha, TET inatoa shukurani kwa walimu wote wa shule za sekondari walioshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki. Mwisho, TET inaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa rasilimali fedha iliyofanikisha uandishi na uchapaji wa kitabu hiki.**



**Dkt. Aneth A. Komba**
**Mkurugenzi Mkuu**
Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE READING ONLY

## Dibaji

Kitabu hiki cha Historia ya Tanzania na Maadili, Shule za Sekondari kimeandikwa mahususi kwa ajili ya mwanafunzi wa Kidato cha Tano katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kitabu hiki kimeandaliwa kulingana na Muhtasari wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili Kidato cha V – VI uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia mwaka 2023.

Kitabu hiki kina sura nane, ambazo ni: Historia, utambulisho na maadili ya Taifa; Mchango wa historia na urithi katika maendeleo ya Taifa; Fursa za uwekezaji zitokanazo na vivutio vya kihistoria na urithi; Maendeleo ya jamii za Kitanzania na maadili yake kabla ya ukoloni; Uhusiano wa jamii za Kitanzania na jamii nyingine kabla ya ukoloni; Mifumo ya kihistoria na maadili ya Kitanzania kabla ya ukoloni; Nguvu ya ukoloni katika kuujenga mwelekeo mpya wa jamii; na Mchango wa ukoloni katika mfumo wa maadili ya Kitanzania. Maudhui ya kitabu hiki yamewasilishwa kwa njia ya matini, kazi za kufanya na vielelezo vinavyochochea ujenzi wa umahiri unaokusudiwa katika kila sura. Vilevile, kuna mazoezi yenye lengo la kupima na kujenga uelewa pamoja na ujuzi wa somo hili katika kila sura. Hivyo, mwanafunzi unapaswa kufanya mazoezi na kazi zote zilizopo kwenye kitabu hiki pamoja na kazi nyingine utakazopewa na mwalimu. Jifunze zaidi kupitia maktaba mtandao https://ol.tie.go.tz au ol.tie.go.tz

Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Kwanza

# Historia, utambulisho na maadili ya taifa

## Utangulizi

*Taarifa za kihistoria, utambulisho na maadili ya taifa ni sehemu muhimu katika kufahamu hatua mbalimbali za kimaendeleo zilizopitiwa na taifa. Katika sura hii, utajifunza kuhusu uhusiano wa kinadharia kati ya historia, utambulisho na maadili ya taifa, misingi ya historia iliyounda utambulisho na maadili ya taifa na nafasi ya historia na maadili katika kujenga fahari ya taifa. Vilevile, utajifunza kuhusu nafasi ya tunu za taifa na maadili katika kuijenga misingi ya uongozi bora na mikakati ya kuilinda historia, utambulisho na maadili ya taifa. Umahiri utakaoujenga, utakuwezesha kuithamini historia, utambulisho na maadili ya taifa la Tanzania na kuishi kwa kuyafuata.*

**Fikiri**

**Unavyoweza kujitofautisha na watu wa mataifa mengine.**

### Dhana za historia, utambulisho na maadili ya taifa

Dhana za historia, utambulisho na maadili ya taifa ni pana na zinatofautiana kulingana na historia ya taifa linalohusika. Kwa upande wa taifa la Tanzania, dhana hizi zinamaanisha yafuatayo:

#### Historia ya taifa

Historia ni maarifa yanayotokana na shughuli na matukio yaliyoiathiri jamii fulani kwa sehemu kubwa wakati uliopita. Athari hizo zinaweza kuwa chanya au hasi. Pia, historia ni simulizi za utaratibu wa matukio ya zamani kama yanavyohusiana na mtu au watu wa aina fulani, nchi au kipindi fulani, ambazo zilitolewa kwa njia ya masimulizi. Siku hizi matukio hayo tunayasoma kwenye vitabu na majarida mbalimbali. Aidha, historia ni uchambuzi au uchunguzi wa yale yaliyotokea siku za nyuma ili kujua ni lini yalitokea na ni nini kilisababisha kutokea kwake na matokeo yake yalikuwa ni nini. Kwa mantiki hii, historia inakuwa ni uchambuzi wa matukio yanayoweza kuepukika na yaliyoweza kukubalika katika maisha ya binadamu huko nyuma. Kwa maneno mengine, historia ni jitihada za binadamu kufikiria upya yaliyopita kwa nia ya kuboresha

FOR ONLINE READING ONLY

maisha ya kizazi kilichopo. Historia ya taifa haihusishi tu simulizi au maarifa ya kuanza na kukua kwake bali inahusisha pia matukio mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ambayo ama yalilijenga, yalilidhoofisha au yalilisambaratisha taifa au jamii. Baadhi ya matukio hayo ni pamoja na maisha na maendeleo ya watu wa kale, vita, njaa, biashara ya utumwa, ukoloni, na uhuru.

**Utambulisho wa taifa**

Utambulisho ni hali, ishara au alama zinazobainisha tofauti kati ya kitu kimoja na kingine, mtu mmoja na mwingine au jamii moja na nyingine. Kwa ngazi ya mtu binafsi, utambulisho ni jumla ya vigezo mbalimbali kama vile jina, ukoo, mila na desturi, uzoefu, muonekano, maumbile, uhusiano na maadili ambayo huunda utu wa mtu kama alivyo yeye mwenyewe kwa ndani na si kama watu wanavyosema juu yake. Kwa ngazi ya jamii au taifa, utambulisho unahusisha masuala mengi yakiwemo masuala ya mipaka ya nchi, tunu za taifa, utamaduni wa wananchi wa taifa husika, itikadi ya taifa, rangi, makabila, dini, asili ya taifa au jamii, hatua za maendeleo, uwezo wa kisayansi na teknolojia wa taifa na hali ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Utambulisho wa taifa unajumuisha pia sanaa, lugha, mavazi, michezo, dini pamoja na mila na desturi. Taifa la Tanzania linatambulishwa na alama mbalimbali ikiwa ni pamoja na bendera ya taifa, wimbo wa taifa, nembo ya taifa, na fedha.

**Maadili ya taifa**

Dhana ya maadili inahusisha sheria, kanuni, misingi, ukweli, na imani au namna ya kufikiri ambayo inaongoza au inayosadikiwa kuongoza matendo ya watu katika jamii au taifa. Hivi karibuni, hasa baada ya kushamiri kwa usasa kupitia utandawazi, neno hili maadili limekuwa likitumika pia kuelezea jitihada za binadamu za kutumia akili, na si imani, ili kujua anavyopaswa kuishi kama binadamu na wala si kama wanyama wasiokuwa na utashi. Kwa maneno mengine, maadili yana maana ya kile kinachopaswa kufanyika ili watu wawe na tabia za kibinadamu na ili waishi kama binadamu. Katika muktadha huu, tunu za jamii zinakuwa na umuhimu wa pekee katika dhana ya maadili ya taifa. Tanzania, kama taifa, lina sheria, kanuni na misingi ya maadili inayofanana na mataifa mengine. Kwa mfano, ujasiri, ukweli, uaminifu, upendo, uwajibikaji na uwazi, haviko Tanzania tu bali pia katika mataifa mengine. Lakini pamoja na hayo, Tanzania kama taifa limekuwa likiweka mkazo kwenye taratibu, sheria na misingi inayojenga umoja, usawa, ushirikiano, utu, uhuru na amani.

**Kazi ya kufanya 1.1**

Tafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali vya taarifa ikiwamo mitandao, kisha fafanua maadili mengine ya taifa la Tanzania ambayo hayajaelezwa.

FOR ONLINE READING ONLY

## Uhusiano wa kinadharia kati ya historia, utambulisho na maadili ya Taifa

Ingawa dhana za historia, utambulisho na maadili zinaweza kuainishwa tofauti, haina maana kwamba dhana hizo hazihusiani. Kinadharia, kuna uhusiano wa karibu sana kati ya historia na utambulisho wa taifa, historia na maadili ya taifa, na utambulisho na maadili ya taifa.

### Uhusiano kati ya historia na utambulisho wa taifa

Kinadharia kuna uhusiano wa karibu sana kati ya historia na utambulisho wa taifa. Ili kueleweka uhusiano huu kwa usahihi zaidi ni muhimu kufahamu kwanza baadhi ya hali au vitu vinavyolitambulisha Taifa la Tanzania. Utambulisho wa taifa letu unahusisha masuala mengi. Hata hivyo, msisitizo utakuwa katika utambulisho wa mipaka, tunu, utamaduni, itikadi, hali ya uchumi, na Bendera ya Taifa.

#### *Jina na mipaka ya nchi*

Mojawapo ya vitu vinavyolitambulisha taifa letu ni mipaka ya nchi yetu. Taifa letu, kama ilivyo kwa mataifa mengine, lina ardhi ambayo ina mipaka inayotambulika kimataifa. Jina Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaweza kuwa na maana nyingine lakini kijiografia hurejelea sehemu maalumu yenye mipaka na ambayo inapakana na nchi nyingine. Mipaka inayotambulisha nchi yetu ina chimbuko lake katika historia. Mwishoni mwa karne ya 19, mataifa ya Ulaya yalikutana katika mji wa Berlin nchini Ujerumani na kuligawa bara la Afrika. Baadaye, yalifanyika makubaliano kati ya Uingereza na Ujerumani mnamo mwaka 1886 na 1890 ya kuigawa Afrika Mashariki ambapo iliwekwa mipaka iliyotambulisha nchi ya Ujerumani ya Afrika Mashariki (Ruanda-Urundi na Tanzania Bara). Jina hilo lilibadilika kuwa Tanganyika wakati wa utawala wa Waingereza ambapo baada ya uhuru iliungana na Zanzibar na kuwa Tanzania mwaka 1964.

#### *Tunu za Taifa*

Tunu ni hali au mambo ya msingi ambayo jamii au taifa linayaenzi na kuyaheshimu. Pamoja na kuzienzi tunu kama vile uhuru na haki, ambazo zinakubalika pia kwa mataifa mengine duniani kuwa ni tunu za ubinadamu, Tanzania imekuwa ikitilia mkazo zaidi tunu za Kiafrika, kama vile umoja, ushirikiano, usawa, undugu, ukarimu, uhuru, na heshima kwa kila mtu. Tunu zote hizi, pamoja na nyingine ambazo hazikutajwa hapa, zilikuwepo tangu zamani katika jamii za mababu na mabibi zetu wa Kiafrika na ndizo ziliwawezesha kuyashinda matatizo yote ya maisha ya wakati wao. Kwa maneno mengine, tunu hizo zimechotwa kutoka katika historia ya mababu na mabibi zetu ili zitusaidie kuboresha maisha yetu ya sasa. Kwa muktadha huu, historia inakuwa ndiyo chimbuko la Tunu za Taifa letu.

#### *Utamaduni*

Utamaduni ni mfumo mzima wa maisha ya watu katika jamii au taifa. Kwa ufupi, utamaduni ni mfumo wa maisha ya watu katika jamii inayohusika. Kwa mfano, Watanzania wanaishije? Wanafuata utaratibu upi wa maisha ya kisiasa, kiuchumi, na kijamii? Wanakula nini? Wanavaaje? Wanaongea lugha gani? Wakifurahi wanafanya nini? Utamaduni

FOR ONLINE READING ONLY

ni majibu sahihi ya maswali haya. Aidha, utamaduni unahusisha njia zote za maisha ikiwa ni pamoja na sanaa, imani, kanuni, heshima, mavazi, miiko, lugha, mila na desturi, na taasisi ambazo hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Vilevile, uhusiano kati ya utambulisho wa utamaduni na historia ni rahisi kueleweka kwa sababu utamaduni wa taifa au jamii unatokana na historia ya jamii au taifa lenyewe. Kwa hiyo, historia ndiyo chimbuko la utamaduni wa taifa letu. Kupitia historia, jamii inapata maarifa na thamani ya utamaduni wake. Kwa mfano, ngoma na vyakula vya asili, mavazi, michezo na sanaa, vina historia ndefu inayochangia utambulisho huu wa taifa.

*Itikadi ya taifa*

Wakati mwingine utambulisho wa taifa unakuwa na itikadi yake. Itikadi ni falsafa inayoongoza maisha ya watu katika jamii au taifa. Kwa kawaida, itikadi inahusisha mawazo, imani, na mitazamo inayokubalika katika jamiii husika ambayo inaathiri uelewa wa jamii hiyo kisiasa, kiutamaduni na kijamii. Tanzania, kwa mfano, iliwahi kutambulika duniani kote kwa itikadi yake ya Ujamaa na Kujitegemea. Watu walijua kuwa Tanzania ni nchi ya Ujamaa na Kujitegemea. Baadhi ya wasomi wanaandika makala na vitabu kuhusu itikadi hiyo mpaka leo. Uhusiano kati ya ujamaa na historia uko wazi kwani itikadi ya ujamaa ilikuwa na chimbuko lake katika maisha ya familia za Kiafrika za zamani. Maadili na nguzo za itikadi ya ujamaa zilitoka katika historia ya mababu na mabibi zetu ambao waliishi maisha ya kijamaa, maisha ya pamoja na kwa kusaidiana kufanya kazi na kugawana matokeo ya kazi hizo kwa usawa. Kwa hiyo, kwa mara nyingine, historia inajitokeza hapa kama chimbuko la utambulisho wa itikadi ya ujamaa.

Ni muhimu kuzingatia kwamba itikadi ya ujamaa kwa Tanzania iliibuka dhidi ya itikadi ya ubepari ambayo iliwafanya Watanzania wawe watumwa katika nchi yao. Ubepari ulisimamiwa na kutekelezwa na wakoloni wa Kijerumani na Kiingereza. Ubepari uliwanyonya Watanzania, uliwakandamiza, uliwanyanyasa, na kuwapuuza. Ndiyo maana Azimio la Arusha la mwaka 1967 liliamua kuachana na ubepari na kuanza kujenga nchi kwa misingi ya kijamaa (ujamaa wa Kiafrika). Hapa pia inaonekana dhahiri kwamba utambulisho wa itikadi yetu ya ujamaa ulikuwa na chimbuko lake katika historia ya ubepari katika nchi yetu ulioletwa kwa kasi na wakoloni wa Kizungu.

*Hali ya kiuchumi*

Hivi karibuni, na hasa baada ya kukua kwa utandawazi, imekuwa jambo la kawaida kuyatambua mataifa duniani kutokana na uchumi wake. Utambuzi huu uko wa aina mbili: Kuna nchi zilizoendelea (mara nyingi huitwa nchi za ulimwengu wa kwanza, au nchi za viwanda), na kuna nchi maskini (ambazo wakati mwingine huitwa nchi zinazoendelea). Taifa letu linatambulika kama nchi inayoendelea. Mwanzoni mwa miaka ya 1960 hadi mwaka 1985 Tanzania ilitambulika kama nchi maskini. Watu wake walikuwa hawana elimu ya kutosha, hawana mahali pazuri pa kulala, hawana nguo za

FOR ONLINE READING ONLY

kutosheleza, chakula, elimu, na huduma za afya zilikuwa duni.

Pamoja na umaskini huo, wa uchumi na viwanda, nchi yetu ilikuwa na rasilimali nyingi, kama ilivyo sasa. Hali ya umaskini inatokana na historia ndefu ya unyonywaji na mataifa ya nje kwa miaka mingi pamoja na kuendekezwa kwa vitendo visivyo vya kimaadili kama vile rushwa. Vitendo hivi vinajenga matabaka katika jamii ya walionacho, ambao wanajilimbikizia mali kwa njia ya rushwa na wasionacho, ambao rasilimali zao zinachukuliwa na wala rushwa. Kiuhalisia, unyonyaji na vitendo vya rushwa vinaendelea hadi leo kupitia ukoloni mamboleo na watu wachache wanaendelea kujilimbikizia mali na kuwa na matumizi mabaya ya ofisi. Kwa hiyo, utambulisho wetu wa umaskini wa viwanda na uchumi una chimbuko lake katika matukio ya kihistoria.

**Kazi ya kufanya 1.2**

Tafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali, ikiwamo mitandao, kuhusu Mkutano wa Berlin wa mwaka 1884 – 1885 ulioligawa bara la Afrika, kisha eleza mchango wake katika kuujenga utambulisho wa taifa la Tanzania.

### Uhusiano kati ya historia na maadili ya taifa

Kinachoitwa maadili ya taifa ni sheria, kanuni, ukweli, misingi, mawazo na tunu zinazoongoza maisha, matendo na tabia za watu katika taifa letu. Kuna uhusiano wa karibu sana kati ya historia na maadili ya taifa hususani sheria, kanuni na misingi inayosimamia uhuru. Maadili ya taifa ni mengi lakini mkazo utakuwa katika tunu za taifa zifuatazo: uhuru, usawa, umoja, utu na undugu, uadilifu, uwazi na uwajibikaji na amani.

*Uhuru*

Kwa upande mmoja uhuru una chimbuko lake katika historia ya ukoloni na kwa upande mwingine uhuru ndiyo chimbuko la historia. Uhuru, ambao ni hali ya mtu au watu wa jamii moja kutotawaliwa na mtu au kikundi cha watu wengine, ulitafutwa na Watanzania wenyewe. Sababu ni kwamba, huko nyuma, kuanzia karne ya 16- hadi mwanzoni mwa nusu ya pili ya karne ya 20, tulikuwa tumepuuzwa, tumenyanyaswa, na kudharauliwa kwa sababu ya biashara ya utumwa na ukoloni mkongwe. Uhuru ulikuja kama jibu la kukataa hali mbaya ya kutawaliwa na Wazungu. Kwa mtazamo huu, inaonekana wazi kwamba uhuru una chimbuko lake katika historia ya utumwa na ukoloni mkongwe katika kipindi cha karne ya 19 na 20.

Vilevile, uhuru ni matokeo ya historia yenyewe. Historia ina chanzo chake katika matendo au matukio ambayo kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na binadamu. Watu wanapoona maisha fulani ni mabaya hupenda kuyabadilisha ama kwa njia za amani au kwa njia ya vita. Watanzania walipoona maisha ya kutawaliwa na Uingereza ni mabaya, waliamua kupigania uhuru, ambao hatimaye wakaupata kutoka kwa Waingereza. Uamuzi na matendo ya kuutafuta uhuru yalikuwa uamuzi mzuri

FOR ONLINE READING ONLY

na huru. Hakuna mtu aliyewalazimisha waasisi wa taifa letu kufanya uamuzi wa kuupigania uhuru, au kuweka mikakati ya kuomba uhuru. Wapigania uhuru walitekeleza mikakati hiyo kwa uhuru, bila shuruti wala kulazimishwa na watu wengine. Aidha, baada ya Tanzania kuwa huru ilikuwa kinara wa kuzisaidia kutafuta uhuru nchi nyingine zilizopo kusini mwa bara la Afrika kama vile Msumbiji, Angola, Namibia, Zimbabwe na Afrika ya Kusini.

Kwa kufanya uamuzi huru na kushiriki kwa hiari na utashi wao katika shughuli za kutafuta uhuru, waasisi wa taifa letu walifanikiwa kupata uhuru. Tukio hilo lilitengeneza historia ya nchi yetu. Kuliangalia suala hili kwa mtazamo huu, kunasaidia kuelewa kwamba uhuru ni chimbuko la historia. Hivyo, historia na maadili ni maarifa yanayotegemeana kwa sababu uhuru una chimbuko lake katika historia na historia ina chimbuko lake katika uhuru. Uhusiano baina ya dhana hizi si uhusiano tegemezi, bali ni uhusiano wa kutegemeana.

*Usawa*

Hii ni hali ya kutokuhaguana kwa misingi ya rangi, ukabila, dini, au itikadi. Katika taifa letu, hii ni tunu muhimu na ya kuenzi kwa sababu ya historia yetu ya kutengwa na kubaguliwa kwa sababu ya rangi yetu. Watawala wa kikoloni walijenga matabaka kwa misingi ya rangi. Tabaka la kwanza lilikuwa la Wazungu, la pili lilikuwa tabaka la Waasia (Wahindi na Waarabu), na tabaka la tatu lilikuwa la Waafrika (Watanzania). Waafrika walinyanyaswa, walidharauliwa, na walipuuzwa kwa ajili tu ya rangi yao nyeusi. Baada ya uhuru matabaka hayo yote yalifutwa kwa kuamini kwamba binadamu wote ni sawa, licha ya tofauti za rangi yao. Hata hivyo, tusipokuwa makini kama taifa na tunu hii ya usawa isipolindwa kwa kupambana na vitendo vya rushwa, matabaka yataanza kujitokeza tena. Hii ni kutokana na watu wachache kuendelea kuhodhi utajiri unaotokana na mali zilizopatikana kwa njia za rushwa na kuwepo kwa tabaka lingine la wanyonge wasionacho. Hapa pia tunaona kwamba usawa, sheria na kanuni zinazoulinda uhuru hutokana na historia ya kubaguliwa kwa ajili ya rangi. Hata hivyo, uamuzi wa kujenga jamii yenye usawa haukudondoka kutoka hewani. Waasisi wa taifa letu waliangalia katika mila na tamaduni za Kiafrika wakagundua kwamba mababu na mabibi zetu walikuwa hawana sera za kubaguana kwa misingi ya rangi, dini au wenye nacho na wasionacho. Katika hili tunaona pia kwamba historia, ama ya ukoloni au ya mila na desturi zetu, ndiyo chimbuko la maadili ya usawa.

*Umoja*

Umoja ni hali ya watu mbalimbali kuwa wamoja katika nia na matendo. Waswahili wana msemo usemao, "Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu." Maarifa na hekima hii hutokana na hekima za mababu na mabibi zetu huko nyuma, ambao umoja kati yao uliwasaidia kutatua changamoto nyingi katika mazingira yao ambapo mtu mmoja mmoja asingeweza kufanikiwa. Sera za kikoloni zilififisha umoja waliokuwa nao mababu zetu. Hata hivyo, umoja ulitumika katika kupigania uhuru hadi ulipopatikana. Hii inaonesha kwamba

FOR ONLINE READING ONLY

maadili au tunu ya umoja ina chanzo chake katika historia ya mababu zetu na katika historia ya kudai uhuru. Umoja ulitokea kama jibu kwa jamii ambayo huko nyuma ilikuwa imeparaganyika na ambayo ilikuwa imegawanyika kwa sababu ya sera za kikoloni. Waasisi wa taifa letu waliamua kuliunganisha taifa ili liwe na umoja na mshikamano, ambao ulikuwa nguzo muhimu katika kuleta maendeleo mara baada ya uhuru. Kama zilivyo tunu zingine, umoja na mshikamano vinaweza kuharibiwa na ukosefu wa maadili na kuendekeza vitendo visivyo vya kimaadili kama rushwa, ubinafsi na wizi, ambavyo vinaweza kuleta utengano katika taifa la Tanzania.

*Utu na undugu*

Kabla ya ukoloni, jamii zetu zilikuwa zikiishi kama ndugu wanavyoishi pamoja katika familia., watu waliishi pamoja katika familia au ukoo na kufanya kazi pamoja kwa faida ya kila mmoja. Palipokuwa na shida walisaidiana na palipokuwa na matatizo makubwa walishirikiana kuyatatua. Kila mmoja alishiriki katika shughuli za kifamilia au ukoo. Aidha, walikuwa wanajaliana sana; kwa mfano, kama msiba ukitokea, basi ulikuwa msiba wa wote na kila mmoja alishiriki kwa hali na mali. Jamii ilishiriki katika malezi ya watoto na vijana wote, bila kujali hali ya kiuchumi na kisiasa ya anayehusika. Watoto walikuwa wa jamii na yeyote aliyekiuka maadili yale alirekebishwa. Mfumo huu wa maisha una asili yake katika historia ya mila na desturi za Watanzania. Kwa hiyo, inaonekana wazi kabisa kwamba historia ndiyo chimbuko la maadili, ambayo yakienziwa vizuri yatalisaidia taifa na jamii katika kuleta maendeleo. Hii ni kwa sababu, kama ilivyokuwa zamani, watakaokiuka maadili watarekebishwa na jamii nzima. Hivyo, jamii yenyewe inapaswa kusimama imara na kushiriki katika kukemea vitendo vya walewanaokiuka maadili kama vile wezi wa mali ya umma na wala rushwa.

*Amani*

Hii ni hali ya watu kuishi bila mafarakano ya kivita, vurugu au fujo. Ni hali ya kuishi katika taifa kwa maelewano bila migogoro, uadui au chuki. Pia, ni hali ya watu kuishi kwa usalama. Hii hali ya amani ina sheria, kanuni, taratibu na misingi yake. Tunu ya amani na sheria na kanuni zake ina chanzo chake pia katika historia. Uzoefu unaonesha kwamba palipo na umaskini, ukatili, njaa, ubaguzi, rushwa, utawala wa mabavu, na uvunjaji wa haki za binadamu hapana amani. Amani iliyopo sasa katika taifa letu ina chimbuko lake kihistoria kwani wazee wetu waliishi kwa upendo na kutobaguana. Makabila mbalimbali yalifanya biashara bila kudhulimiana wala kuoneana. Vilevile, waasisi wa taifa letu waliunganisha taifa na kukataa misingi ya unyonyaji au ubaguzi kwa kuangalia dini, kabila au eneo la kijiografia. Hivyo, ni dhahiri kwamba amani ya taifa letu chanzo chake ni historia ya Watanzania.

Kwa ujumla, uhusiano kati ya historia na maadili ya taifa ni sawa na uhusiano wa wazazi na wana wao. Kama vile baba na mama wanavyozaa mtoto na kumlea hadi

FOR ONLINE READING ONLY

anakuwa mtu mzima ndivyo ilivyo katika maadili na historia. Historia ni chimbuko na nguzo imara katika kuyaendeleza na kuyadumisha maadili ya taifa. Kupitia historia ya taifa watu wanapata ufahamu wa thamani ya maadili yao ya asili na kuyaweka katika vitendo katika maisha yao ya kila siku.

**Kazi ya kufanya 1.3**

Tafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali, ikiwamo mitandao, kisha fafanua kwa nini uhuru, usawa, umoja, undugu na amani ni sehemu ya maadili ya taifa la Tanzania.

**Zoezi 1.1**

1. "Uhusiano kati ya utambulisho wa taifa na maadili ya taifa si uhusiano tegemezi". Fafanua maana ya kauli hii.
2. Kwa kutumia mifano, eleza dhana ya utambulisho wa taifa la Tanzania.
3. Eleza kwa nini maadili ni suala la kihistoria.
4. Tathmini mchango wa historia katika ujenzi wa tunu za taifa la Tanzania.

### Uhusiano kati ya utambulisho na maadili ya taifa

Utambulisho wa taifa kama ulivyoainishwa hapa ni pamoja na zile sheria, kanuni na misingi inayolinda mipaka, tunu za taifa, utamaduni, itikadi, na hali ya uchumi. Ili kuelewa vizuri na kwa ufasaha uhusiano uliopo kati ya utambulisho na maadili, itakuwa vema kulinganisha utambulisho ulioainishwa hapa na maadili yaliyobainishwa hapa, ambayo ni uhuru na mipaka, usawa na utamaduni, na umoja na hali ya uchumi.

*Uhuru na mipaka*

Mara nyingi si rahisi kuona uhusiano uliopo kati ya uhuru na mipaka ya taifa letu kwa haraka haraka. Hata hivyo, ukiangalia kwa makini utaona kwamba kuna uhusiano wa karibu sana kati ya masuala hayo mawili. Uhuru ni hali ya mtu au watu wa jamii moja kutotawaliwa na mtu au kikundi cha watu wengine. Watu hao au jamii hiyo ni lazima iwe kwenye eneo lenye mipaka yake. Kwa upande wa taifa, mipaka hiyo lazima iwe inaonekana na kutambuliwa duniani.

Uhuru lazima uwe katika eneo maalum au nchi inayohusika na ni lazima kuwe na mipaka. Kwa hiyo, kwa maneno mengine, maana ya uhuru inatofautiana kutoka eneo moja hadi lingine, mathalani, namna Tanzania inavyotafsiri uhuru inaweza kuwa tofauti na namna Kenya inavyotafsiri uhuru wake. Kinachoufunga uhuru ndani ya eneo maalumu liitwalo Tanzania ni mipaka. Kwa lugha nyingine, mipaka inaulinda uhuru wetu. Hata hivyo, mipaka ya kijiografia inaweka uzio au ukuta tu bali walinzi halisi wa uhuru wa Tanzania ni Watanzania wenyewe. Kwa kuwa Watanzania wako ndani ya mipaka inayoeleweka na kwa kuwa mipaka hiyo inawafanya wajisikie wamoja, wanakuwa na shauku ya kulinda uhuru wao ndani ya mipaka ya nchi yao. Kwa hiyo, ni sahihi kusema uhuru na mipaka ni dhana zinazotegemeana. Dhana

FOR ONLINE READING ONLY

moja haiwezi kufanya kazi bila kuwapo kwa dhana nyingine. Hivyo, uhusiano kati ya utambulisho wa taifa na maadili ya taifa si uhusiano tegemezi, ambapo kimoja kinategemea tu kingine, bali ni uhusiano wa kutegemeana.

*Usawa na utamaduni*

Sheria na kanuni zinazolinda usawa zina uhusiano wa karibu sana na utamaduni, hasa pale utamaduni unapoeleweka kama namna au jinsi Watanzania wanavyoyakabili maisha katika taifa lao. Usawa kama dhana inayosisitiza zaidi haki za binadamu unasaidia kuhakikisha kuwa utamaduni unaolitambulisha taifa letu hauvunji haki za binadamu kama vile kunyanyasa watoto, kubagua watu kwa misingi ya rangi, au hata kuwanyima baadhi ya wananchi haki ya elimu kwa sababu yoyote ile. Kwa mantiki hii, usawa unaufanya utamaduni wetu uwe na maadili yanayokubalika duniani. Hivyo, usawa ni chanzo cha maadili katika utambulisho wa utamaduni. Pia, ni muhimu kuelewa kwamba utamaduni wetu ndio chimbuko la maadili ya usawa. Kama ilivyogusiwa hapo awali, tunu ya usawa imetoka kwenye historia ya mababu na mabibi zetu pamoja na uzoefu wetu wa ukoloni. Kwa hiyo, uhusiano kati ya usawa na utamaduni ni uhusiano unaotegemeana. Uhusiano kati ya usawa na utamaduni hauwezi kukamilika bila kuwapo kwa kimojawapo. Hivyo, utambulisho na maadili vinategemeana pia.

*Umoja na hali ya uchumi*

Imeelezwa hapo mwanzo kwamba kuna wakati taifa letu liliwahi kujitambulisha na kutambuliwa ndani na nje ya nchi kwamba ni taifa maskini. Hata hivyo, Tanzania imekuwa ikijitambulisha na kutambuliwa na watu wa nje na ndani ya nchi kwamba ni taifa tajiri, hasa kwa kuzingatia utajiri wa maliasili uliopo nchini. Uhusiano wa utambulisho huu na umoja si mgumu kuueleza. Sheria na kanuni za umoja zina uwezo wa kubadilisha hali ya uchumi kutoka hali ya umaskini hadi utajiri. Kwa wakati umoja na katika nia na matendo unaweza kuuondoa umaskini. Kwa kushirikisha vipawa na karama za kila mmoja katika taifa, inawezekana kupata utaalamu na uwezo wa kuitoa nchi katika dimbwi la umaskini. Kwa mantiki hii, umoja unakuwa nguzo na chimbuko la maendeleo, kwa maana ya utajiri. Pia, umoja ni kigezo cha kupima hali ya uchumi kwani unagawa watu katika taifa, kwenye tabaka la walionacho na wasionacho. Ikiwa uchumi haujengi matabaka na unawasaidia watu wote katika taifa kuishi maisha bora, basi uchumi wa aina hiyo huwa unasadikiwa kwamba ni mzuri. Katika hili, inaonekana pia kwamba umoja na hali ya uchumi vinategemeana. Umoja unajenga na kulinda uchumi na uchumi unaweza kulinda umoja au kuusambaratisha.

### Zoezi 1.2

1. Kwa kutumia mifano mbalimbali, eleza ni kwa namna gani Watanzania wanaweza kunufaika kwa kutumia historia ya taifa.
2. Kwa kutumia mifano, eleza mchango unaotokana na misingi ya historia ya utambulisho na maadili ya taifa.

FOR ONLINE READING ONLY

3. **Fafanua namna vitendo vya rushwa vinavyoweza kuleta umaskini, matabaka katika jamii, na kuathiri amani na kuvunja haki za binadamu.**
4. **"Taifa lolote lisilo na historia ni sawa na binadamu ambaye hajajisitiri." Jadili ukweli wa hoja hii.**

## Misingi ya kihistoria iliyounda utambulisho wa Taifa

Taifa letu linatambulishwa na linatambuliwa ndani na nje ya nchi na vitu mbalimbali. Baadhi ya vitu hivyo ni mipaka yake, utamaduni, bendera, lugha ya Kiswahili, na wimbo wa taifa.

### Mipaka ya nchi

Mipaka ya nchi yetu, ambayo kwa kiasi kikubwa ndiyo utambulisho wa nchi yetu, inatokana na tukio la kihistoria. Kati ya mwaka 1884 na 1885 mataifa ya Ulaya Magharibi yaliligawa bara la Afrika katika vipande vipande kama nchi, katika mkutano uliofanyika katika mji wa Berlin huko Ujerumani. Wakati nchi nyingi za Afrika zikigawanywa katika mkutano huo, kama ilivyosemwa hapo awali, Afrika Mashariki iligawanywa baada ya mkutano huo kupitia makubaliano ya Uingereza na Ujerumani mwaka 1886 na 1890. Katika miaka hii Tanzania Bara ya sasa iligawiwa kwa Ujerumani kama moja ya sehemu ya Ujerumani ya Afrika Mashariki na mara baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia ilikuwa koloni la Uingereza na kubadili jina kuwa Tanganyika mnamo mwaka 1920. Zanzibar iligawiwa kwa Uingereza. Kama ilivyokuwa kwenye Mkutano wa Berlin, mipaka waliyoiweka haya mataifa ya Ulaya ndiyo ikawa mipaka ya nchi za Afrika na Tanzania ya leo inayotambulika kimataifa. Baada ya uhuru, jitihada zilifanyika kuvunja athari mbaya za mipaka ya kikoloni na kuunda Afrika moja. Pamoja na kusuasua kwa umoja wa Afrika, Tanganyika iliweza kuvunja mipaka ya kikoloni na kuungana na Zanzibar, tukio ambalo liliondoa kabisa mipaka ya kikoloni baina ya nchi hizi mbili na kuunda utambulisho wa taifa jipya la Tanzania mwaka 1964. Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa utambulisho (kwa maana ya mipaka ya nchi) wa taifa letu umeundwa na matukio ya kihistoria ya mataifa ya Ulaya Magharibi kwa kuigawa Afrika na Afrika Mashariki pamoja na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

### Utamaduni

Kipengele kingine cha utambulisho wa taifa ni utamaduni. Tanzania ni nchi mojawapo inayojivunia aina mbalimbali za tamaduni. Hii ina maana kwamba Tanzania ni nchi yenye utamaduni mseto, kwa maana kwamba imeundwa na watu wenye tamaduni mbalimbali zinazotokana na jamii mbalimbali kuishi pamoja bila kujali tofauti zao. Inasadikiwa kwamba Tanzania ina makabila zaidi ya 150, ambapo kila moja lina utamaduni wake. Hata hivyo, kuna baadhi ya mila na desturi katika makabila haya zinazofanana.

Misingi ya kihistoria iliyofanya Tanzania ijulikane kama taifa lenye tamaduni nyingi ni uhamiaji wa makundi mbalimbali ya watu kutoka sehemu mbalimbali za Afrika. Uhamiaji huo, uliotokea katikati ya milenia ya 2 kabla ya zama za sasa na milenia ya kwanza ya zama za sasa na kuendelea.

FOR ONLINE READING ONLY

Wakati Wakichembe wakiaminika kuwa ni wenyeji na wazawa wa maeneo haya, makundi yaliyowasili nchini kutoka maeneo mengine, na ambayo yanaifanya Tanzania iwe ni nchi ya makundi yote ya Afrika, ni pamoja na Wanilo, Wakushito na Wabantu. Kundi la Wabantu linawakilishwa na jamii kama vile Wagogo, Wasukuma, Wamakonde, Wahehe, Wachaga na makabila mengine. Wakichembe wanajumuisha makabila ya Wasandawe na Wahadzabe, ambao wanapatikana katika bonde la ufa, kandokando ya Ziwa Eyasi na mbuga ya Serengeti. Aidha, Wanilo chimbuko lao ni mto Nile huko Sudan. Hapa Tanzania Wanilo ni Wamasai, Wajaluo na Wadatoga. Wakushito wanawakilishwa na makabila kama vile Walawa, Wagorowa, Waburungi, Wafyomi na Wairaqw ambao waliingia nchini kutoa pembe ya Afrika, yaani Ethiopia, Eritrea na Somalia.

**Bendera ya Taifa**

Bendera ni alama ya utambulisho wa taifa. Mataifa karibu yote duniani yana bendera zake na hujitambulisha kupitia bendera hizo. Tanzania, kama ilivyo kwa nchi nyingine, ina bendera yake ambayo inatambulika kwa rangi zake. Bendera yetu ni sehemu ya utamaduni au mapokeo ya siku nyingi kwamba nchi huru lazima iwe na bendera yake.

Bendera kama utambulisho wa taifa ina misingi yake katika historia. Tukio la kwanza la kihistoria lilikuwa mwisho wa ukoloni mkongwe na tukio la pili la kihistoria lilikuwa mwanzo wa uhuru wa kujitawala kama taifa huru. Kama alama au utambulisho wa taifa, bendera ina ujumbe mzito sana. Upeperushaji wa bendera unatoa ujumbe kwamba taifa liko hai na kwamba taifa au nchi siyo kitu bandia bali ni kitu halisi kinachojitegemea na hakuna kitu kingine cha kufanana nacho.

Utambulisho wa bendera unatumika katika matukio maalum ya kitaifa na katika taasisi za kiserikali na binafsi kama vile shule na hospitali. Matumizi na utunzaji wake huashiria kwamba bendera ni kitu cha kudumu na chenye thamani na kwamba, kama nchi au taifa litakuwepo, basi na utambulisho huo utakuwepo siku zote. Isitoshe, bendera ni kitu kinachoheshimika sana kwa taifa. Hali hii ndiyo inayofanya iwe na sheria na kanuni zake. Sheria na taratibu zote zinazohusu bendera zinakusudia kuwaeleza wananchi kuhusu heshima yake. Kwa kuisimamisha bendera juu ya ardhi kuipeperusha juu kabisa ya mlingoti, kuwataka wananchi waiheshimu, kusimama wima mbele yake inapopandishwa au kushushwa, na kuapa utii kwenye bendera humaanisha kwamba taifa linatangaza kuwa na madaraka ya mwisho juu ya watu wake na kuwa ni dola huru.

Ukiacha ujumbe unaotolewa na rangi, bendera pia ni alama ya uhai wa taifa, kudumu kwake, heshima na madaraka yake. Haya yote yana misingi yake katika historia kwani huko nyuma nchi zilikuwa zinachukuliwa kama kitu cha bandia, kisichokua na uhai, na ambacho kinapita. Kwa hiyo, nchi zilionekana kuwa hazina madaraka wala heshima yoyote. Hali hii

FOR ONLINE READING ONLY

ilisababisha vita ya mara kwa mara na ya muda mrefu huko Ulaya hata kusababisha kuwapo kwa *Mkataba wa Westphalia wa 1648*. Katika mkataba huo, pamoja na mambo mengine, viongozi wa nchi na dini waliazimia kutenganisha dini na siasa pamoja na nchi moja kuacha kuingilia mambo ya ndani ya nchi nyingine. Kwa maneno mengine, walikubaliana kuheshimu mipaka ya nchi zao na kuondoa masuala ya dini katika uendeshaji wa nchi za Ulaya.

### Lugha ya Kiswahili

Lugha ya Kiswahili ni alama muhimu sana inayoitambulisha Tanzania. Ingawa Kiswahili ni lugha ya Kibantu na inazungumzwa na watu wengi katika nchi za Afrika Mashariki na Kati, Tanzania ndiyo inatambulika zaidi kwa Kiswahili sanifu. Utambulisho huu maalumu haukuzuka tu bali una chimbuko lake katika historia ya Tanzania. Mwingiliano ulichangia kukieneza na kukikuza zaidi Kiswahili ambacho tayari kilikuwepo na kuzungumzwa kwa lahaja mbalimbali. Kiswahili kilienea zaidi Tanzania kwani Waarabu walitumia zaidi Kiunguja kilichozungumzwa Unguja ambacho ndicho kilisanifishwa na kuwa sanifu. Kwa hiyo, tukio la kihistoria lililochangia kukieneza na kukikuza Kiswahili, utambulisho wa taifa letu, ni mwingiliano wa kibiashara kati ya Waarabu na watu wa pwani ya bahari ya Hindi, hasa visiwa vya Zanzibar, maeneo ya Bagamoyo na Kilwa. Pamoja na Waarabu, uhusiano na mataifa mengine ya Ulaya umechangia pia katika kukuza msamiati wa lugha hii adhimu na alama muhimu kwa nchi ya Tanzania.

**Kazi ya kufanya 1.4**

Soma matini kuhusu makubaliano ya mkutano wa *Westphalia* kutoka katika vyanzo mbalimbali, ikiwamo mitandao, kisha fafanua makubaliano ya mkutano huo na umuhimu wake katika ujenzi wa utaifa.

### Misingi ya kihistoria iliyounda maadili ya taifa

Misingi ya kihistoria iliyojenga maadili ya taifa iko mingi, lakini hapa inaelezewa misingi ifuatayo: utumwa, ukoloni, na Azimio la Arusha.

#### Utumwa

Kati ya matukio ya kihistoria yaliyochangia sana uundaji wa maadili ya taifa ni biashara ya utumwa wa Waafrika iliyofanyika kwenye karne ya 16 hadi 19. Biashara hii iliwahusisha Waarabu na Wazungu wa Ulaya Magharibi na washirika wao wengine. Biashara hii iliwadhalilisha sana watu wenye rangi nyeusi na ikawanyima utu wao kama binadamu wengine. Watumwa walisafirishwa kwa ukatili wa kutisha ndani (Zanzibar kwenye mashamba ya minazi na karafuu) na nje ya bara la Afrika ili wakafanye kazi kwenye mashamba ya miwa, katani, pamba, kahawa na chai bila ujira wowote. Vilevile, watumwa walisafirishwa kwenda Uarabuni kufanya kazi za ndani. Kiuhalisia, watumwa walikosa haki zao zote za msingi kama binadamu.

FOR ONLINE READING ONLY

Mfumo huu wa maisha ambao uliwatumikisha watu wengine uliwachukiza sana wapigania uhuru wa Afrika. Baada ya kupata uhuru, waasisi wa taifa letu walipiga marufuku mfumo huu wa maisha na walitunga sheria ambazo zilikataza mtu au kikundi cha watu kuwatumikisha watu wengine kwa kuwafanya watumwa. Ili kuzuia utaratibu huo kuigwa, waasisi walitilia mkazo matendo ya haki, usawa, na heshima kwa watu wote. Kwa namna ya pekee kabisa, walitilia mkazo tamko rasmi la Umoja wa Mataifa kuhusu haki za binadamu ambalo lilikuwa linasisitiza uhuru wa kila binadamu.

**Ukoloni**

Ujio wa wakoloni ulikuwa tukio kubwa la kihistoria ambalo liliathiri kwa kiasi kikubwa maadili ya Watanzania. Wakoloni walipofika walichukua madaraka yote ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kijamii, wakoloni walianzisha elimu ya kikoloni yenye mtazamo wa kimagharibi, walisaidia kuenea kwa dini ya Ukristo, na mambo mengi yenye mrengo wa kimagharibi. Kisiasa, wakoloni ndio walikuwa watawala na wenye madaraka ya mwisho katika koloni. Walianzisha majeshi mbalimbali kama jeshi la polisi, jeshi la kulinda nchi, usalama wa taifa, na jeshi la magereza. Pia, walianzisha bunge na mahakama. Kiuchumi walikuja na utaalamu wa taasisi za mabenki na viwanda. Vilevile, walipora ardhi iliyokuwa inamilikiwa na wenyeji na kuanzisha mashamba makubwa ya mkonge, kahawa, chai, miwa, pamba, pareto, na mengineyo. Kwa kifupi, ukoloni ulikamata njia zote kuu za uzalishaji mali, madini, misitu, na maji. Mfumo wote huu wa ukoloni, ulimwacha Mtanzania akiwa mnyonge na asiyejiamini.

Waasisi wa taifa letu hawakupendezwa na mfumo wa maisha ulioanzishwa na wakoloni. Hivyo, baada ya uhuru jitihada za dhati zilifanyika kubadili mtindo huo wa maisha na kuanzisha mfumo mwingine wa haki na usawa. Kisiasa, madaraka yote yalichukuliwa na Watanzania. Watanzania ndio wakawa na madaraka ya mwisho katika nchi. Jeshi la mkoloni lililokuwa linajulikana kama *King African Rifles* (KAR) lilibadilishwa na kuitwa *Tanganyika African Rifles*, mara tu baada ya uhuru, na baadaye lilibadilishwa kuwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) la mwaka 1964. Polisi na vyombo vyote vya usalama vikawa chini ya Watanzania ili kulinda usalama wa Watanzania na mali zao. Bunge na mahakama vikawa chini ya Watanzania ili kuwahudumia Watanzania. Aidha, taratibu zilibadilika kwenye mabenki na viwanda zikawa na lengo la kuwahudumia Watanzania na siyo wakoloni. Ubaguzi uliokuwa umeshamiri katika elimu, afya, makazi na ajira ulipigwa marufuku na msisitizo ukawekwa katika maadili ya usawa. Kijamii, hatua zilichukuliwa kufufua utamaduni wa Watanzania na kuuheshimu. Haya yote yalichangia kuunda maadili yaliyotufikisha hapa. Hii inaonesha dhahiri kuwa ukoloni ulichangia kuunda maadili ya taifa. Kufanyika kwa hayo yote baada ya uhuru kunafanya lifikiwe hitimisho kwamba tukio la kihistoria la uhuru lilichangia kuunda maadili ya taifa.

FOR ONLINE READING ONLY

Azimio la Arusha

**Miongoni mwa matukio ya kihistoria yaliyochangia kuunda maadili ya taifa letu ni Azimio la Arusha. Azimio hili lilipitishwa wakati wa mfumo wa chama kimoja na Halmashauri Kuu ya TANU, mwezi Januari 1967. Mnamo tarehe 5 Februari 1967 Azimio hilo lilithibitishwa na Mkutano Mkuu wa TANU. Azimio hilo lilikuwa tamko la kimapinduzi na la kihistoria ambalo lilionesha mwelekeo mpya wa Tanzania huru katika nyanja za siasa, uchumi na kijamii. Lilikuwa tamko rasmi la Watanzania wenyewe kuhusu maendeleo ya nchi yao. Hivyo, ni tukio lililobadili mwelekeo wa nchi kimaadili katika siasa, uchumi, na jamii na ndiyo maana linaitwa "Azimio la Utu." Azimio la Arusha lilikuwa linawaelekeza Watanzania jinsi ya kuishi maisha ya utu na ubinadamu.**

*Kisiasa:* **Azimio la Arusha lilitangaza itikadi mpya ya taifa iliyokuwa inajulikana kama siasa ya 'Ujamaa na Kujitegemea'. Hili lilikuwa tangazo la nia ya kujenga taifa ambalo watu wake wanaishi pamoja na kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wote. Ilikuwa siasa iliyokuwa inapinga kabisa itikadi au imani za kibepari. Uanzishwaji wa vijiji vya ujamaa Tanzania nzima ulikuwa na nia ya kulielekeza taifa katika maisha ya maadili ya kijamaa, ambayo ni maisha ya umoja, ushirikiano, usawa, ukarimu, na kujaliana kama ndugu wa familia moja badala ya maisha ya ubinafsi yaliyokuwa yanashabikiwa na ubepari. Kwa ujumla, Azimio la Arusha lilitufundisha katika mfumo wa maadili wa jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. Kwa sasa baadhi ya misingi hiyo imeingizwa kwenye sheria mbalimbali ili kuendelea kuyalinda maadili, ikiwemo Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 inayokataza mambo yafuatayo: hongo, limbikizo la mali, kujipatia manufaa yasiyostahili, ubadhirifu na kuchepusha mali, na matumizi mabaya ya mamlaka.**

**Katika jitihada za kuliekeleza katika maadili ya ujamaa, Azimio la Arusha liliweka misingi ya kwanza ya maadili ya viongozi wa chama na serikali. Ilikuwa lazima kiongozi awe mkulima au mfanyakazi, asiwe na mawazo au imani za kibepari, asiwe mkurugenzi wa kampuni binafsi au kuwa na hisa katika makampuni. Isitoshe Azimio hilo halikutaka kiongozi wa chama au serikali awe na nyumba ya kupangisha au mishahara miwili. Lengo lilikuwa kuzuia viongozi na watumishi wa serikali na chama kujilimbikizia mali na kukuza mwanya wa wenye nacho na wasionacho.**

*Kiuchumi*: **Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ilipiga marufuku mfumo wa maisha ambao unawanyonya watu wengine. Matabaka ya mabwana na watwana yalifutwa na kusisitiza kila mtu afanye kazi kwa akili na bidii. Ili kuondoa unyonyaji, serikali ilipewa jukumu la kumiliki njia kuu zote za uchumi,** zikiwemo ardhi, viwanda, mabenki, usafiri na usafirishaji na makampuni makubwa **yaliyokuwa yamejiimarisha nchini. Kwa hiyo, serikali ilibinafsisha mali nyingi zilizokuwa zinamilikiwa na watu au taasisi binafsi na kuwekwa chini ya umma ili kuufaidisha umma wote wa Tanzania. Azimio lilisisitiza pia maisha ya kujitegemea ambayo hayategemei misaada wala fedha kama chanzo cha maendeleo.**

FOR ONLINE READING ONLY

*Kijamii:* Azimio la Arusha liliwasisitiza wananchi kubadilika kimawazo kwa kuacha mila na desturi za Wazungu na kukumbatia mila zetu za Kiafrika zilizo nzuri ambazo tuliziacha baada ya wakoloni kututawala. Huu ulikuwa mwito wa kujivunia Uafrika wetu, maadili yetu, na utamaduni wetu. Kwa kuliona hilo, mkazo mkubwa uliwekwa kwenye ukuzaji wa lugha yetu ya Kiswahili. Kiswahili kikawa ndiyo lugha ya taifa na kikaanza kufundishwa shuleni, na ikawa ndiyo lugha ya kufundishia elimu ya msingi. Ili kuendeleza utamaduni wetu, waasisi walianzisha wizara ya utamaduni ambayo kazi yake haikuwa tu kukuza ngoma za jadi bali kusimamia masuala yote ya utamaduni wa Watanzania. Ili kuhakikisha itikadi ya ujamaa inarithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, serikali ilianzisha Sera ya Elimu ya Kujitegemea, ambayo kimsingi ilikuwa ililenga kumuandaa kijana wa Kitanzania kusoma kwa vitendo na siyo kwa nadharia. Vilevile, elimu hiyo ililenga kuwawezesha vijana kujitegemea baada ya elimu ya shule ya msingi. Aidha, ililenga kuwashirikisha wanafunzi wa ngazi zote nchini katika shughuli za uzalishaji mali katika taifa.

**Kazi ya kufanya 1.5**

Soma matini kutoka katika vyanzo mbalimbali vya taarifa, ikiwamo mitandao, halafu eleza namna misingi ya Azimio la Arusha inavyoendana na juhudi za mapambano dhidi ya rushwa nchini.

**Zoezi 1.3**

1. Eleza ni kwa namna gani utumwa ulikuwa kinyume cha maadili ya Kitanzania?
2. Chambua maadili ya viongozi wa chama na serikali kama yalivyoainishwa katika Azimio la Arusha.
3. Fafanua ni kwa namna gani alama za taifa zinatumika katika kudumisha maadili ya taifa.
4. Je, ni namna gani misingi ya Azimio la Arusha inaweza kutumika katika mazingira ya sasa?

## Nafasi ya historia na maadili katika kujenga fahari ya taifa

Nafasi ya historia na maadili katika kujenga fahari ya taifa haiwezi kueleweka vizuri kama fahari ya taifa haileweki. Kwa hiyo, ni muhimu kujiuliza maswali yafuatayo: Maana ya fahari ya taifa ni nini? Tanzania inajivunia nini hasa au ni nini fahari ya taifa letu?

Kuna maana mbili za fahari ya taifa: Maana ya kwanza, ni hali ya kujivunia aliyonayo mtu au watu kwa ajili ya taifa lao. Hapa chanzo cha kujivuna ni mambo yote au baadhi ya mambo yaliyofanywa na yanayofanywa na taifa. Kwa mfano, siku ambayo timu ya mpira ya Tanzania itachukua kombe la dunia au la Afrika, Watanzania wengi wataona fahari kwa timu yao na taifa lao kushinda. Maana ya pili inahusisha ufahari au majivuno

FOR ONLINE READING ONLY

ya mtu au watu wanayopata kutokana na utambulisho wa taifa. Hapa chanzo cha ufahari na kujivuna ni utambulisho wa taifa na si mambo yanayofanywa na serikali. Kwa mfano, Watanzania wengi wanajivunia mlima Kilimanjaro au mbuga za wanyama kama vile Serengeti, Ngorongoro, Manyara, Mikumi, Ruaha na nyinginezo. Huu ni ufahari unaotokana na utambulisho wa taifa, ambao wakati mwingine unaweza kuwa umeundwa na serikali.

**Kazi ya kufanya 1.6**

Kwa kutumia vyanzo tofauti vya taarifa, chunguza jinsi matukio muhimu katika historia ya Tanzania yanavyojenga fahari ya taifa.

Taifa letu linajivunia mambo mengi lakini hapa tutajikita kwenye uchambuzi wa nafasi ya historia na fahari zifuatazo za taifa:

### Amani na utulivu

Amani na utulivu ni miongoni mwa fahari kuu za taifa letu. Japokuwa Tanzania ina mjumuiko au mchanganyiko wa makabila zaidi ya 150 na watu wake wana dini na itikadi mbalimbali za kisiasa, wananchi wanaishi kwa amani na utulivu. Hali hii ya maisha ya amani ndiyo imeipa Tanzania sifa ya kuwa "Kisiwa cha Amani" tofauti na nchi nyingine ambazo zimekuwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe, mauaji ya kimbari, mafarakano ya tofauti za kidini, na fujo za uroho wa madaraka.

Hali hii ya utulivu na amani haijaja yenyewe bali imetengenezwa na maarifa ya historia. Tanzania ni nchi ya amani na tulivu kwa sababu waasisi wa taifa hili walijifunza katika historia kwamba vita ni mbaya na kwamba jamii zinazoundwa kwa ncha ya upanga pia husambaratishwa kwa ncha ya upanga. Japokuwa mababu zetu kama vile Mkwawa wa Wahehe, Machemba wa Wayao, Mangi Sina wa Wachaga, na wengine walipigana vita ili kulinda uhuru wao, walishindwa kupata uhuru kwa njia ya vita. Hivyo, waasisi wa taifa letu wakaona ni vizuri kutafuta uhuru kwa njia ya amani na mazungumzo ambayo ilikuwa imejikita kwenye hoja za maadili. Hata baada ya uhuru, viongozi wetu wa serikali walichukua hatua mbalimbali za kuleta amani na utulivu kama vile kuleta umoja kwa kuamua kuua ukabila. Kwa hiyo, historia imechukua nafasi kubwa sana katika kujenga ufahari huu wa taifa letu.

Pamoja na hayo, amani na utulivu havikujengwa na historia tu bali pia na maadili. Amani na utulivu ni nadharia ambazo hazijijengi zenyewe. Ili kuweza kuishi kwa amani na utulivu ni lazima kuwapo na sheria, kanuni na misingi inayolinda amani. Msingi mkubwa wa amani ni haki. Pasipokuwa na haki hakuna amani. Aidha, mahali fulani hapawezi kuwa na haki kama kuna ukiukaji wa maadili, ikiwemo kujihusisha na vitendo vya rushwa. Katika hali hizo watu watapigana kutafuta haki zao na wengine watanyimwa haki zao kwa sababu ya rushwa ambapo matokeo yake ni kukosekana kwa amani na utulivu. Msingi mwingine wa amani ni utii wa sheria. Sheria zinazolinda amani ni muhimu kuheshimiwa. Kama katika nchi

FOR ONLINE READING ONLY

fulani watu hawatii sheria na kutumia ofisi za umma kwa manufaa yao, basi katika nchi hiyo kutazuka fujo na mafarakano. Mifano hii inatosha kuonyesha kwamba historia pekee yake haiwezi kujenga amani bali, ili amani iwepo, historia inapaswa kushirikiana na maadili, yaani haki na utii wa sheria.

### Umoja na mshikamano

Miongoni mwa mambo mengi ambayo Tanzania inajivunia ni hali ya umoja na mshikamano. Katika nchi ambayo ina makabila mengi, dini nyingi, tamaduni mbalimbali, na itikadi mbalimbali si rahisi watu wake kushikamana na kuwa wamoja. Lakini pamoja na tofauti zote hizo, Tanzania imeweza kuonesha umoja na mshikamano miongoni mwa watu wake. Wananchi wanashirikiana katika harakati za maendeleo na kusaidiana katika nyakati za shida na raha. Tabia hii inawapa watu wengi fahari ya kujivunia taifa lao. Umoja na mshikamano huu una misingi yake katika historia. Licha ya kufuata umoja na mshikamano waliokuwa nao mababu na mabibi zetu, waasisi wa taifa letu pia walisisitiza umoja. Azimio la Arusha, ambalo tumelielezea, lilikuwa tukio la kihistoria ambalo lilisisitiza umoja, yaani ujamaa. Uamuzi wa kuondoa matabaka ya mabwana na watwana, kutaifisha njia kuu za uchumi na kuziweka chini ya serikali, kuondoa unyonyaji, kuwaelekeza wananchi waishi na kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wote, na uondoaji wa ubaguzi kwa misingi ya rangi ni baadhi ya jitihada za mwanzo za kihistoria ambazo zimechangia sana watu wa nchi hii kuishi kwa umoja na mshikamano. Ubaguzi kama vile wa rangi, ukabila, na dini ungeendekezwa na matabaka ya matajiri na maskini yakaachwa yashamiri na Kiswahili kikapuuzwa ingekuwa vigumu sana leo hii kwa taifa letu kuwa na umoja na mshikamano. Kwa hiyo, umoja upo nchini kwa sababu ya mchango mkubwa wa historia ya taifa letu.

Kwa nyongeza, lazima ikumbukwe kwamba umoja na mshikamano haujengwi na historia tu bali na maadili pia. Historia peke yake itaujenga umoja lakini bila maadili umoja huo utadhoofika na kupotea. Ili kuwa na umoja na mshikamano ni lazima kuwe na sheria na taratibu zinazolinda umoja na mshikamano. Umoja, kama ilivyo kwa amani, unalindwa na misingi ya haki, ambapo haki za kila mwananchi zinaheshimiwa na kulindwa. Kama katika taifa haki za kila mmoja zinalindwa na kama kila mmoja anajiona ni sawa na mwingine, hapo umoja utakuwepo. Isitoshe, sheria zile zinazolinda umoja lazima ziheshimiwe na kila mmoja katika taifa. Pale tu mambo haya yanapofuatwa ndipo tunaweza kuwa na umoja. Aidha, tunaona pia kwamba historia pekee yake haiwezi kujenga umoja ikiwa umoja huo hausaidiwi na maadili ya kuheshimiana, kujaliana, kupendana, kushirikiana, na kutii sheria.

### Lugha ya Kiswahili

Kama kuna kitu ambacho Watanzania wanajivunia sana basi ni lugha ya Kiswahili. Kuna sababu nyingi za ufahari huu: Kwanza, Kiswahili ni lugha ya Kibantu ingawa ina maneno mengi pia ya Kiarabu,

FOR ONLINE READING ONLY

Kiingereza, Kireno na lugha nyinginezo; pili, ni rahisi kujifunza; tatu, inatumika sehemu nyingi duniani ikiwa ni pamoja na Afrika ya Mashariki na Kati; nne, ni lugha inayokua kwa kasi katika Afrika, Ulaya, Asia na Amerika; tano, ni lugha ambayo inafundishwa katika mataifa ya nje kwa muda mrefu sasa; sita, ni miongoni mwa lugha za kimataifa zinazotambuliwa na UNESCO na ina siku yake maalumu ya kuiadhimisha kidunia (tarehe 7 Julai); na saba, ni lugha ambayo imewaunganisha Watanzania na kuwafanya wajione ni wamoja.

Kama zilivyo fahari nyingine za taifa, lugha hii ya Kiswahili nayo imepata ufahari wake kwa sababu ya historia. Ikumbukwe kwamba Kiswahili kama lugha ya mawasiliano, "kilitokana na mwingiliano wa lugha za Kibantu za pwani na baadaye kikapata athari za Kiarabu na lugha nyingine za kigeni" kama ilivyo kwa lugha yoyote inayokua. Lugha hizo ni pamoja na Kihindi, Kireno, Kiingereza na Kiarabu. Kilicholeta mwingiliano huo uliochangia kukua na kuenea kwa Kiswahili ni masuala ya biashara kati ya Waarabu na watu wa pwani, masuala ya ukolono na utandawazi. Ili kukieneza, wapigania uhuru kama Mwalimu Nyerere walikitumia katika harakati zao za kisiasa, na hasa katika mikutano ya hadhara. Baada ya kupata uhuru, Kiswahili kilipandishwa hadhi na kuwa Lugha ya Taifa. Hapa tunaona kwamba historia ya mwingiliano na watu wengine, historia ya harakati za uhuru, na historia ya baada ya uhuru, vilichangia sana kuujenga ufahari huu wa taifa, yaani Kiswahili.

Hata hivyo, mkazo unaowekwa kwenye nafasi ya historia katika kujenga Kiswahili unapaswa pia kuwekwa kwenye nafasi ya maadili kwa sababu bila maadili Kiswahili kisingejengeka hata kufika kilipo sasa. Kiswahili kimejengeka hivi kwa sababu watu wanakipenda. Kupenda ni msingi muhimu sana katika ujenzi wa lugha. Kama watu wasingekipenda Kiswahili, ingekuwa vigumu sana kukijenga na kukiendeleza. Aidha, maadili yalichangia kukijenga Kiswahili pale watu walipokiheshimu. Japokuwa wakati wa ukoloni, na hata baada ya ukoloni, kulikuwa na kasumba ya kudharau lugha za Kiafrika na kuthamini lugha ya Kiingereza, lugha ya Kiswahili haikudharaulika kwa sababu kwa kiasi kikubwa ilikuwa tayari inaheshimika. Pamoja na dharau walizokuwa nazo wakoloni juu ya utamaduni wa Mwafrika bado walikiheshimu Kiswahili kwani waliona kina umuhimu katika kutekeleza malengo yao. Kwa mfano, ili wakoloni wawasiliane na kuelewana na manamba, yaani vibarua, waliokuwa wanatoka sehemu mbalimbali za Tanzania kwenda kufanya kazi katika mashamba yao, ilibidi pande zote mbili zitumie Kiswahili. Hali kadhalika, Kiswahili kilitumika katika shughuli za utamaduni (mfano, ngoma na muziki), shughuli za dini, kusikiliza kesi za Waafrika, kilimo, majeshi, vyombo vya habari, mfumo wa elimu na hata katika harakati za uhuru. Mifano hii yote inaonesha jinsi maadili kama upendo, na heshima yalivyochangia kuijenga lugha ya Kiswahili, ambayo leo tunajivunia.

FOR ONLINE READING ONLY

Kiingereza, Kireno na lugha nyinginezo; pili, ni rahisi kujifunza; tatu, inatumika sehemu nyingi duniani ikiwa ni pamoja na Afrika ya Mashariki na Kati; nne, ni lugha inayokua kwa kasi katika Afrika, Ulaya, Asia na Amerika; tano, ni lugha ambayo inafundishwa katika mataifa ya nje kwa muda mrefu sasa; sita, ni miongoni mwa lugha za kimataifa zinazotambuliwa na UNESCO na ina siku yake maalumu ya kuiadhimisha kidunia (tarehe 7 Julai); na saba, ni lugha ambayo imewaunganisha Watanzania na kuwafanya wajione ni wamoja.

Kama zilivyo fahari nyingine za taifa, lugha hii ya Kiswahili nayo imepata ufahari wake kwa sababu ya historia. Ikumbukwe kwamba Kiswahili kama lugha ya mawasiliano, "kilitokana na mwingiliano wa lugha za Kibantu za pwani na baadaye kikapata athari za Kiarabu na lugha nyingine za kigeni" kama ilivyo kwa lugha yoyote inayokua. Lugha hizo ni pamoja na Kihindi, Kireno, Kiingereza na Kiarabu. Kilicholeta mwingiliano huo uliochangia kukua na kuenea kwa Kiswahili ni masuala ya biashara kati ya Waarabu na watu wa pwani, masuala ya ukolono na utandawazi. Ili kukieneza, wapigania uhuru kama Mwalimu Nyerere walikitumia katika harakati zao za kisiasa, na hasa katika mikutano ya hadhara. Baada ya kupata uhuru, Kiswahili kilipandishwa hadhi na kuwa Lugha ya Taifa. Hapa tunaona kwamba historia ya mwingiliano na watu wengine, historia ya harakati za uhuru, na historia ya baada ya uhuru, vilichangia sana kuujenga ufahari huu wa taifa, yaani Kiswahili.

Hata hivyo, mkazo unaowekwa kwenye nafasi ya historia katika kujenga Kiswahili unapaswa pia kuwekwa kwenye nafasi ya maadili kwa sababu bila maadili Kiswahili kisingejengeka hata kufika kilipo sasa. Kiswahili kimejengeka hivi kwa sababu watu wanakipenda. Kupenda ni msingi muhimu sana katika ujenzi wa lugha. Kama watu wasingekipenda Kiswahili, ingekuwa vigumu sana kukijenga na kukiendeleza. Aidha, maadili yalichangia kukijenga Kiswahili pale watu walipokiheshimu. Japokuwa wakati wa ukoloni, na hata baada ya ukoloni, kulikuwa na kasumba ya kudharau lugha za Kiafrika na kuthamini lugha ya Kiingereza, lugha ya Kiswahili haikudharaulika kwa sababu kwa kiasi kikubwa ilikuwa tayari inaheshimika. Pamoja na dharau walizokuwa nazo wakoloni juu ya utamaduni wa Mwafrika bado walikiheshimu Kiswahili kwani waliona kina umuhimu katika kutekeleza malengo yao. Kwa mfano, ili wakoloni wawasiliane na kuelewana na manamba, yaani vibarua, waliokuwa wanatoka sehemu mbalimbali za Tanzania kwenda kufanya kazi katika mashamba yao, ilibidi pande zote mbili zitumie Kiswahili. Hali kadhalika, Kiswahili kilitumika katika shughuli za utamaduni (mfano, ngoma na muziki), shughuli za dini, kusikiliza kesi za Waafrika, kilimo, majeshi, vyombo vya habari, mfumo wa elimu na hata katika harakati za uhuru. Mifano hii yote inaonesha jinsi maadili kama upendo, na heshima yalivyochangia kuijenga lugha ya Kiswahili, ambayo leo tunajivunia.

FOR ONLINE READING ONLY

### Urithi wa asili

Urithi wa asili ni rasilimali kama vile miti, misitu, madini, maporomoko au hifadhi za wanyama ambazo binadamu amezikuta. Kuwepo kwake hakukumtegemea binadamu bali zimekuwepo kwa sababu Mungu aliziumba. Urithi wa asili ni rasilimali ambazo hazijatengenezwa na binadamu. Urithi wa namna hii hapa Tanzania ni mwingi. Hata hivyo, Watanzania wengi wanajivunia zaidi mlima Kilimanjaro na mbuga za wanyama kama vile Ngorongoro, Tarangire, Mikumi, na Ruaha ambazo zina wanyama wengi na mandhari ya kuvutia.

Aidha, visiwa vya Zanzibar vina fukwe nzuri, kina kirefu cha bahari, bahari yenye aina mbalimbali za samaki na visiwa vingi vidogovidogo vinavyovutia. Tanzania ya leo inajivunia urithi huu ambao tumepewa na Mungu kwa sababu mababu na mabibi zetu waliotutangulia hawakuuharibu. Hakukuwa na vitendo vya ukiukaji wa maadili kama vile kutumia rushwa ili kuharibu urithi wa asili bali waliutunza hadi sisi tukajaliwa kuuona. Wangechoma misitu moto, wakaua wanyama wote kwenye hifadhi, wakalima kwenye vyanzo vya maji, au wakapulizia sumu kwenye maziwa na mito ya asili, kizazi chetu kisingeweza kuziona rasilimali hizi. Vilevile, kama hayo yangefanyika, kusingekuwepo kitu cha asili cha kuonea fahari. Hivyo, tunaona wazi kabisa kuwa maadili na historia ya utunzaji wa mazingira vimekuwa na mchango mkubwa sana katika kujenga fahari ya urithi wa asili.

Mchango wa historia katika ulinzi wa urithi wa asili unakamilika pale maadili yanapozingatiwa na kufanya mambo kadhaa ikiwemo kutoruhusu watu wachache watumie vishawishi mbalimbali kama rushwa kuharibu mazingira yaliyotunzwa na vizazi vilivyopita. Kama urithi wa asili ungelindwa na historia tu bila maadili, basi usingekuwepo. Bila maadili hakuna kitu kizuri ambacho kingeendelea kuwepo mpaka sasa. Urithi wa asili wa nchi yetu umeendelea kuwepo hadi sasa kwa sababu watu wanaupenda urithi huo na unawasaidia. Mathalani, mito, maziwa, mabonde, na milima hupendwa kwa sababu husaidia kujenga maisha bora kwa watu. Kwa mfano, mito na maziwahuwapa watu maji na samaki, mabonde yanawasaidia watu kwa shughuli za kilimo ambacho kinawapa chakula na uwezo wa kibiashara, na milima kama vile Kilimanjaro hupendwa kwa sababu ni kivutio cha utalii, ambacho kinaliingizia taifa fedha za kigeni.

Mbali na maadili ya upendo, ufahari wetu katika urithi wa asili unajengwa pia na maadili ya heshima kwa watu na viumbe wote. Mababu na mabibi zetu waliyaheshimu mazingira pamoja na viumbe vilivyopo juu na chini ya ardhi au majini. Heshima kwa urithi wa asili ndiyo uliwezesha mababu na mabibi zetu kuutunza urithi huo. Waliutunza kwa kutoharibu mazingira yao ya kuishi na kuutumia kwa njia endelevu. Mababu na mabibi zetu waliwaheshimu wanyama na hata mimea kwa namna sawa na viumbe hai wengine ambao wameumbwa na Mungu. Hivyo, urithi wa asili tulionao hadi sasa ulitunzwa na kuendelezwa kwa sababu katika mila na desturi za Kiafrika viumbe vyote vilichukuliwa kama vitu muhimu na vinavyotakiwa kutunzwa. Aidha, baadhi ya urithi wa asili tulio nao kama vile wanyama,

FOR ONLINE READING ONLY

misitu, miti, mito, maziwa, na milima vilichukuliwa kuwa ni vitu vyenye nguvu za kiroho na za kimungu. Tena vilionekana kuwa na uwezo wa kulinda na kutoa maisha ya binadamu; kwa hiyo, viliheshimiwa. Kwa mfano, kuna baadhi ya misitu ambayo ilikuwa haiguswi kwa sababu ilisadikiwa kuwa ni makazi ya miungu na sehemu takatifu za kufanyia matambiko. Pia, kuna wanyama ambao kimila ni ndugu wa familia, ukoo na hata kabila. Urithi wa asili kama wanyama, wadudu, majani, na hata miti wenye undugu na familia haukuguswa au kuvunwi. Katika hili pia tunaona kwamba maadili ya heshima, upendo na undugu yalichangia sana kujenga na kulinda urithi wetu wa asili.

**Muungano wa Tanganyika na Zanzibar**

Kitendo cha waasisi wa nchi yetu kuunganisha nchi mbili huru, yaani Tanganyika na Zanzibar, mwaka 1964 kiliiletea sifa kubwa sana nchi yetu. Pamoja na kwamba jitihada za kuiunganisha Afrika ili iwe nchi moja zimekuwa zikisuasua, Tanzania ni nchi pekee ya mfano iliyoweza kulichukulia wazo la muungano kwa umuhimu wake na kuungana. Mpaka leo, Tanzania ndiyo nchi pekee ya Afrika ambayo imeungana. Muungano unawafanya Watanzania wengi wajivunie na kuwastaajabisha wageni wa ndani na nje ya Afrika. Kitendo cha kuunganisha nchi mbili si mafanikio madogo. Watanzania wanapaswa kujivunia muungano huu ambao ni wa mfano. Pamoja na kuufurahia na kujivunia, ni muhimu kukumbuka daima kwamba hata huu muungano wenyewe umejengwa na historia. Kama wakoloni wasingeligawa bara la Afrika katika vipande vipande, na kama Waafrika wasomi wa mwanzo wasingeona umuhimu wa Waafrika kuungana na kuwahamasisha kufanya hivyo; na kama waasisi wetu, baada ya uhuru wasingeona umuhimu wa kuunganisha nchi hizi mbili ili kujenga umoja zaidi, basi ufahari tulionao leo kupitia Muungano wa Tanganyika na Zanzibar usingekuwapo.

Ikumbukwe kwamba muungano haujengwi na historia tu bali kuwepo na kuzingatiwa kwa maadili. Bila kuwepo kwa maadili, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar pengine ungekuwa umeshavunjika. Muungano huu upo mpaka leo kwa sababu ya upendo uliopo baina ya wananchi wa nchi hizi mbili. Isitoshe, muungano umedumu kwa sababu ya maadili ya heshima. Wananchi wa sehemu zote mbili wanaheshimiana bila kujali wanatoka upande gani wa nchi na wanashirikiana bila kubaguana. Pia, muungano umedumu kwa sababu ya utii wa sheria, kanuni na misingi inayoulinda muungano. Kama kusingekuwa na utii wa sheria hizo, pengine muungano huo ungekuwa umeshavunjika.

Maelezo haya yanatosha kuonyesha kwamba si historia tu yenye mchango katika ujenzi wa fahari za nchi yetu bali maadili pia yanachangia kwa kiasi kikubwa katika kujenga na kulinda fahari hizi.

**Zoezi 1.4**

1. Eleza namna vitendo vya rushwa vinavyoweza kuathiri mambo yafuatayo:

   (a) Utambulisho na maadili ya taifa;

FOR ONLINE READING ONLY

**(b) Utoaji wa haki;**

**(c) Udhibiti wa uhalifu (Mfano: biashara ya dawa za kulevya, uhamiaji haramu, utoroshaji wa nyara za taifa, haki za binadamu na utawala bora); na**

**(d) Ulinzi wa mazingira na maliasili.**

2. Eleza ni kwa namna gani Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni kielelezo cha maadili ya Tanzania.
3. Jadili ni kwa namna gani maadili ya Kitanzania yamechangia katika kutunza fahari yetu.
4. Je, ni kwa njia gani lugha ya Kiswahili imechangia katika kuimarisha utambulisho na maadili ya taifa?

## Nafasi ya Tunu za Taifa na maadili katika kujenga misingi ya uongozi bora

Tunu za Taifa zina nafasi kubwa sana katika kujenga misingi ya uongozi bora. Dhana ya uongozi bora imejengeka juu ya misingi ifuatayo: uadilifu, uwajibikaji, uwazi, utii wa sheria, uzalendo na utu.

### Uadilifu

Uadilifu ni uaminifu, na uaminifu ni tabia ya kuzingatia kanuni za maadili. Mtu mwenye uadilifu hana tabia ya kukiuka kanuni, sheria au maadili. Tunu za taifa zina nafasi kubwa katika kujenga misingi ya uadilifu; kwa mfano, uhuru ndio chimbuko la uadilifu. Uadilifu si tabia ya lazima au ya kushurutishwa. Hujengwa na familia, ukoo na hata kabila tangu utotoni mpaka katika utu uzima na huwa sehemu ya utu wa mtu. Kwa hiyo, uadilifu wa kweli unatoka kwenye utashi wa mtu aliye huru na anayejitambua. Uadilifu wa kulazimisha si endelevu kwani huwa haudumu kwa muda mrefu kwa sababu ni wa bandia; hivyo, hupotea baada ya muda mfupi. Isitoshe, uadilifu bandia au wa kinafiki hauwezi kufanikisha malengo ya mtu binafsi au ya jamii kwa sababu ni rahisi kwa jamii kuutambua. Uongozi bora unaleta tija pale ambapo kiongozi ana uadilifu unaotoka moyoni mwake, ambao umeshakuwa sehemu ya utu wake na si uadilifu wa kinafiki au wa kuigiza ili kupata masilahi binafsi.

Maadili pia yana nafasi yake katika kujenga uadilifu. Tabia ya ukweli, heshima kwa watu na viumbe, na upendo ni nguzo muhimu sana katika kujenga uadilifu. Kiongozi muongo, asiye na upendo na ambaye hana heshima kwa watu na mazingira yao hawezi kwa namna yoyote ile kuwa kiongozi mwenye uadilifu. Uongozi kama huo husambaratisha jamii; na mara nyingi kuwa chanzo cha mafarakano katika jamii. Kwa ufafanuzi huu, ni wazi kuwa tunu za taifa na maadili vina mchango katika kujenga misingi ya utawala bora.

### Uwajibikaji

Hii ni tabia ya kiongozi kuwa tayari kujibu hoja na changamoto, kubeba dhamana na kutoa maelezo kwa anaowaongoza kuhusu uamuzi au matendo aliyoyafanya katika kuyatekeleza majukumu yake kama kiongozi. Usawa unasaidia sana kujenga misingi ya uongozi kwani kiongozi anayeamini katika usawa anawajibika kwa watu wake. Hii ina maana kwamba

FOR ONLINE READING ONLY

kiongozi hajioni kama yeye ni tofauti na anaowaongoza. Pia, hajioni kama yeye ni wa juu zaidi kuliko wengine, au yeye ni bora zaidi kuliko wengine na kwamba ana haki zaidi kuliko anaowaongoza. Hapa tunaona nafasi ya usawa katika uwajibikaji, ambao ni msingi muhimu wa utawala bora. Kama zilivyo tunu za taifa, ndivyo maadili yalivyo pia. Maadili yana nafasi kubwa na ya muhimu sana katika kujenga misingi ya uwajibikaji.

Kuwajibika ni kubeba dhamana ya watu na vitu. Lakini, ili uweze kubeba dhamana ya watu lazima uwapende, uwajali, na uwaheshimu bila kuwa na upendeleo au kutumia rushwa. Kiongozi hawezi kuwajibika kama hawapendi watu wake na kama atajihusisha na vitendo visivyokuwa vya kimaadili. Akiwapenda watu wake, atawajali, atawaheshimu, atawasikiliza na kuwashirikisha katika uamuzi unaogusa maisha yao. Bila tabia ya kuwapenda watu, kuwajali na kuwaheshimu hakuna uwajibikaji. Uwajibikaji utakuwepo pale tu kiongozi anapowapenda watu wake. Kwa hiyo, maadili kama upendo, na heshima si tu kwamba yanachangia kujenga misingi ya uwajibikaji bali pia ndiyo chanzo au nguzo kuu ya uwajibikaji. Maadili ya upendo kwa watu ndiyo yanamsukuma kiongozi kuwajibika kwao.

**Uwazi**

Uwazi ni hulka ya kuwashirikisha watu kutoa maoni na ushauri wao kuhusu namna ya kutenda jambo fulani au matumizi sahihi ya rasilimali kwa maendeleo yao binafsi na kwa na maendeleo ya nchi yao. Uwazi pia ni tabia ya kuwashirikisha wananchi katika uamuzi unaoyagusa maisha yao au masilahi ya nchi. Tunu za taifa kama umoja ina nafasi kubwa sana katika kujenga misingi ya uwazi, ambayo ni nguzo muhimu ya utawala bora. Umoja ni muhimu katika uwazi kwa sababu unapunguza majungu ya mtu mmoja mmoja au kikundi cha watu. Uamuzi unaotolewa kwa pamoja na kwa kushirikiana unakuwa kwa ajili ya wote na si kwa ajili ya mtu mmoja au kikundi cha watu wachahe. Jambo la muhimu ni kwamba, ushauri wa wengi una nafasi kubwa ya kuwa sahihi kuliko wa mmoja au wachache. Isitoshe, sauti ya umoja huwa inasikika zaidi kuliko sauti ya mtu mmoja mmoja. Kwa maneno mengine, sauti ya umoja iko wazi zaidi, inasikika zaidi na ina nguvu zaidi kuliko sauti ya mtu mmoja. Hapa tunaona kuwa umoja una nafasi kubwa katika kujenga misingi ya uwazi.

Kama zilivyo tunu za taifa, maadili pia yana nafasi muhimu katika uwazi kwa sababu maadili ndiyo chanzo cha uwazi. Kinachomsukuma kiongozi kushirikisha watu katika uamuzi unaohusu maisha yao si rushwa au umaarufu bali upendo alionao kwa hao anaowaongoza. Kiongozi asiposukumwa na upendo hawezi kujali kuwashirikisha watu katika masuala yao. Pia, kiongozi asiyeheshimu watu wake hawezi kuwashirikisha katika uamuzi kwa sababu atakuwa anawadharau. Kwa hiyo, maadili kama upendo na heshima kwa watu ndiyo chimbuko na nguzo ya kujenga na kuimarisha uwazi, ambao ni nguzo muhimu katika utawala bora.

FOR ONLINE READING ONLY

**Utii wa sheria**

Kiongozi bora ni yule anayeongoza kwa kufuata sheria na kanuni zilizopo na si kwa akili zake mwenyewe. Kiongozi ana wajibu wa kujua sheria zinazomwongoza, kuziheshimu na kuzitii. Pia, ana wajibu wa kuwasaidia walio chini yake kuishi kwa kufuata sheria na kanuni za maisha katika nchi au jamii. Kwa ufupi, utii wa sheria ni msingi muhimu unaowezesha taifa kuishi kwa amani na salama.

Tunu za Taifa kama vile undugu ndiyo chanzo cha utii wa sheria. Watu wanaoishi kama ndugu na kwa kujaliana wanasaidiana kutii sheria za nchi. Iwapo mmoja kati ya ndugu hao atakiuka sheria ataonywa ili asikiuke tena sheria zilizowekwa. Watu waishio kama ndugu hawaishi kwa kufuata sheria za msituni au zile zinazoruhusu mwenye nguvu aishi au atumie nguvu ya fedha aliyonayo kutoa rushwa bali wote huishi kwa kufuata sheria zinazotoa haki sawa kwa wote. Kiongozi anayetii sheria, hutoa huduma bila kujali jinsia, kabila, ukanda, dini na uwezo wa kifedha. Hii husaidia kuwa na jamii inayosimamia haki na usawa kwa maendeleo ya wote. Kwa hiyo, tunu kama undugu ndiyo chanzo cha utii wa sheria. Watu wasipojiona kama ni ndugu watatunga sheria mbovu za ubaguzi na unyanyasaji wa mtu mmoja na mwingine au wa kikundi kimoja dhidi ya kingine.

Maadili ya taifa pia yana mchango mkubwa sana katika kukuza watu waadilifu. Inawezekana kukawa na sheria zinazoongoza jamii, lakini kama hakuna maadili sheria haziwezi kufanya kazi. Sheria huwasaidia watu kuwa waadilifu. Kwa mfano, pasipo sheria wananchi watashindwa kuwajibika kulipa kodi ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi, haki zitapindishwa na urithi wa asili utaharibiwa au kupotea. Hivyo, bila kuzingatia maadili, sheria zitapindishwa kwa sababu ya rushwa, wenye haki watafungwa, na sheria zitawasaidia wenye fedha na wenye nguvu na si watu wote. Kwa ufupi, sheria zinafanya kazi pale palipo na maadili, na pasipo na rushwa hutawala. Kwa upande mwingine, maadili ndiyo chanzo cha sheria. Sheria zipo ili kuyalinda na kuyaendeleza maadili ya jamii. Kwa hiyo, sheria zinatokana na maadili. Hapa ndipo tunaona kwa mara nyingine nafasi ya maadili katika kujenga misingi ya utii wa sheria, ambao ni msingi muhimuwa utawala bora.

**Uzalendo**

Uzalendo ni sifa muhimu ambayo kiongozi yoyote anapaswa kuwa nayo, hii ni hali ya kuipenda nchi yako na ikibidi kuwa tayari hata kufa kwa ajii yake. Kiongozi ambaye ni mzalendo anajituma kwa kwa manufaa ya taifa lake, anatunza rasilimali za taifa lake na si mla rushwa hata akishawishiwa na watu wengine. Aidha, wananchi wanapofahamu kiongozi wao ni mzalendo huwa wanatoa ushirikiano wa kutosha kwa kuamini kuwa yanayofanywa na kiongozi wao ni kwa ajili ya manufaa ya umma. Uzalendo unawatia moyo wananchi kushirikiana katika kutatua changamoto za kitaifa na kujenga mustakabali mwema. Mtazamo wa kizalendo huhimiza uvumbuzi, ushiriki wa wananchi katika kutafuta maendeleo. Hii inasaidia kukuza ukuaji wa uchumi, maendeleo ya kijamii na utawala bora. Uzalendo unaweza kuunganisha watu mbalimbali karibu na maadili na

FOR ONLINE READING ONLY

taasisi za kidemokrasia. Wakati utaifa unawaunganisha watu, uzalendo unajenga fahari, umoja na ujasiri kwa raia.

### Utu

Utu ni sifa muhimu katika kuongoza watu husaidia katika kujenga mazingira ambayo raia wanaheshimiwa na kulindwa haki zao. Utu ni ile hali ya mtu kuthamini, kuheshimu na kuwajali watu kama anavyojipenda yeye. Kimsingi mtu mwenye utu hafanyi mambo ambayo yeye hapendwi kufanyiwa na watu wengine. Mtu mwenye utu husaidia na kuwa mlinzi wa haki za binadamu hivyo hunahakikisha kwamba watu wote wanatendewa kwa usawa na bila ubaguzi na kwa kuzingatia haki za binadamu na uhuru pamoja na haki za msingi, hii inajumuisha haki ya kushiriki katika masuala ya umma, haki ya afya, na haki ya kuishi katika mazingira yenye afya. Vilevile, mtu mwenye utu huwa muwazi na mwajibikaji pamoja na kulinda haki za wanyonge kama walemavu, wazee, maskini, wanawake na watoto. Tunu ya utu husaidia katika utoaji wa huduma za umma zenye ufanisi na kwa usawa. Utawala unaozingatia utu unalenga katika kutoa huduma bora za umma zinazokidhi mahitaji ya wananchi wote, na kuimarisha ustawi na utu wao kwa ujumla pamoja na kupambana na rushwa:

#### Zoezi 1.5

1. Kwa kutumia **mifano** katika mazingira **unamoishi,** eleza umuhimu wa tunu za taifa kwa maendeleo endelevu ya Tanzania.
2. Eleza madhara ya rushwa katika utoaji haki, uwajibikaji, uwazi na utii wa sheria.
3. "Taifa lisilokuwa na sheria ni sawa na wanyama mwituni." Jadili sentensi hii kwa kutumia mifano dhahiri..
4. Ni kwa namna gani rushwa imekuwa ikiathiri utambulisho wa taifa?
5. Ni namna gani misingi ya historia ya utambulisho na maadili ya taifa la Tanzania imechangia katika kuleta heshima na sifa nzuri kwa nchi yetu?

FOR ONLINE READING ONLY

#### Kazi ya kufanya 1.7

Tunu za taifa la Tanzania ni pamoja na uhuru, umoja, amani, mshikamano, uzalendo, utu na undugu. Tafuta taarifa kuhusu tunu hizo kutoka katika vyanzo mbalimbali, kisha eleza mchango wake katika kujenga uongozi bora.

### Mikakati ya kulinda historia, utambulisho na maadili ya taifa

Historia, utambulisho na maadili ya taifa ni sehemu muhimu ya urithi wa taifa lolote. Ni muhimu kulinda urithi huo ili vizazi vya sasa na vijavyo viweze kuelewa na kuthamini asili na misingi ya taifa lao. Katika ulimwengu wa leo wenye mabadiliko ya haraka, ni muhimu kuweka mikakati madhubuti ya kulinda historia, utambulisho na maadili ya taifa. Tanzania ina mikakati mbalimbali yenye lengo la kulinda historia, utambulisho na maadili ya taifa kwa kutumia mihimili yake, ikiwemo bunge linalotunga sheria, mahakama inayotafsiri sheria zilizotungwa

pamoja na serikali inayotekeleza sheria kwa kutumia vyombo vyake vinavyosimamia urithi wa kihistoria na maadili vilivyoundwa kwa mujibu wa sheria. Vyombo hivyo ni kama vile Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(National Audit Office of Tanzania - NAOT)*, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma *(Ethics Secretariet - ES)*, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika (*African Liberation Heritage Centre – ALHC*), Mamlaka ya Mapato Tanzania *(Tanzania Revenue Authority - TRA)*, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya *(Drug Control and Enforcement Authority - DCEA)* na zinginezo.

### Mikakati ya kuhifadhi historia

Baadhi ya mikakati ya kuhifadhi historia ya Tanzania ni hifadhi za nyaraka, uendelezaji wa makumbusho ya taifa, elimu ya historia, kuanzishwa kwa taasisi za utamaduni, na utafiti wa kihistoria.

#### *Uhifadhi wa nyaraka za kihistoria*

Uhifadhi wa nyaraka za kihistoria ni moja ya mikakati muhimu ya kulinda na kuitunza historia ya taifa. Tanzania imeanzisha makavazi ya taifa yenye jukumu la kuzihifadhi nyaraka za kihistoria kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo. Makavazi haya huhifadhi nyaraka mbalimbali kama vile picha za zamani, barua za kihistoria, makabrasha ya taarifa za kihistoria, rekodi za serikali, vitabu vya kumbukumbu, na filamu za kihistoria. Nyaraka nyingine ni pamoja na vitu vya kale, sanaa za jadi, mikataba na nakala za magazeti na majarida ya zamani, urithi na ukombozi wa bara la Afrika. Uhifadhi wa nyaraka hizi hutusaidia kuelewa matukio muhimu ya zamani na maendeleo ya taifa letu. Pia, nyaraka hizi hutumika katika tafiti, elimu, na maendeleo ya taifa. Kwa kufanya hivyo, historia yetu inabaki salama na itaendelea kuwapo kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Aidha, Tanzania baada ya kupewa dhamana ya kuulinda na kuhifadhi urithi wa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika mwaka 2011, ilianzisha Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika ambacho kinahifadhi nyaraka mbalimbali zikiwemo vitabu, picha, vifaa, hotuba za viongozi, ramani, magazeti na majarida ya harakati za ukombozi wa Tanzania na maeneo mengine ya Afrika. Pamoja na kuthamini mchango mkubwa wa hali na mali uliofanywa na Tanzania wakati wa harakati za ukombozi, kituo hiki kinasimamia maeneo zaidi ya 200 ambayo yalitumiwa na wapigania uhuru kutoka nchi mbalimbali, ambayo sasa yanatumika kama vituo vya utalii wa historia ya ukombozi.

#### *Uendelezaji wa makumbusho ya taifa*

Uendelezaji wa makumbusho ya taifa ni muhimu katika kulinda na kuhifadhi historia ya taifa letu. Makumbusho hutoa fursa ya kipekee kwa jamii kujifunza asili ya kihistoria na vitu vya kipekee kama vile mabaki ya akiolojia na nyaraka adimu. Uendelezaji wa makumbusho ya taifa ni moja ya mikakati ya Serikali ya Tanzania katika kuhifadhi historia, utambulisho na maadili ya taifa. Tanzania ina makumbusho mbalimbali kama vile Kijiji cha Makumbusho na Makumbusho,

FOR ONLINE READING ONLY

Nyumba ya Sanaa iliyopo Dar es Salaam na Jumba la Makumbusho Zanzibar. Pia, kuna Makumbusho ya Azimio la Arusha, Makumbusho ya Vita ya Maji Maji, Songea na Makumbusho ya Daktari Livingstone yaliyopo Ujiji, Kigoma. Uendelezaji wa makumbusho ni muhimu katika kuielimisha jamii na kusambaza uelewa wa historia yetu kwa vizazi vijavyo.

*Elimu ya historia*

Elimu ya historia ni muhimu katika kulinda, kuhifadhi, na kuendeleza historia ya taifa letu. Husaidia kuyaelewa matukio muhimu, viongozi wa zamani, utamaduni, na mila zetu. Historia ni msingi wa utambulisho wetu wa kitaifa na inatuwezesha kujenga uzalendo. Kupitia elimu tunajifunza asili yetu na jinsi tulivyofika hapa tulipo leo. Elimu ya historia inawawezesha wanafunzi pamoja na wadau mbalimbali kutambua mchango wa historia na kuwafanya kuwa mabalozi wazuri wa taifa letu. Elimu ya historia inajenga umoja, mshikamano, na kuwawezesha vijana kuwa raia wema na wazalendo. Pia, serikali imeanzisha somo la Historia ya Tanzania na Maadili kama somo la lazima. Somo hili linafundishwa katika ngazi za elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu. Lengo ni kuongeza uelewa kwa wanafunzi, wadau na wananchi kuhusu historia, utambulisho na maadili ya taifa la Tanzania. Pia, somo hili linawawezesha Watanzania kuthamini mchango wa mababu na mabibi zetu katika maendeleo ya nchi yetu ili kujenga uzalendo kwa nchi yetu.

*Kuanzishwa kwa vyombo na taasisi za kiutamaduni*

Vyombo na taasisi mbalimbali zimeanzishwa ili kulinda historia, utambulisho na maadili ya taifa. Baadhi ya vyombo hivyo ni:

(a) Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA): BASATA ni chombo kinachosimamia na kuikuza sekta ya sanaa nchini Tanzania. Chombo hiki kinafanya kazi ya usimamizi wa shughuli za sanaa, kuendeleza vipaji vya wasanii, na kusaidia maendeleo ya sekta ya sanaa kwa ujumla.

(b) Bodi ya Filamu Tanzania: Hii ni bodi inayoisimamia tasnia ya filamu nchini Tanzania. Ina jukumu la kudhibiti na kusimamia uzalishaji wa filamu, kutoa leseni kwa waandaaji wa filamu, na kusimamia ubora wa kazi za filamu. Bodi hii huhakikisha kwamba filamu zote zinazozalishwa ndani ya nchi au zile zinazotoka nje ya nchi hazikinzani na maadili, mila na desturi za Kitanzania.

(c) Idara ya Maendeleo ya Utamaduni: Idara hii ni sehemu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Inajihusisha na mipango na sera za kuukuza na kuulinda utamaduni wa Mtanzania. Hufanya kazi katika maeneo kama vile kudumisha urithi wa kitamaduni, kukuza tamaduni za makabila mbalimbali, na kusaidia matamasha na matukio ya kitamaduni.

FOR ONLINE READING ONLY

(d) **Makumbusho ya Taifa: Chombo hiki, pamoja na kuwa na aina mbalimbali za makumbusho katika maeneo tofauti tofauti hapa nchini, kina jukumu la kuukusanya, kuuhifadhi, na kuukuza urithi wa kitamaduni wa Tanzania. Hutoa elimu kuhusu utamaduni wa Tanzania kupitia maonesho ya kisanii, makumbusho, na shughuli nyingine za elimu.**

(e) **Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika: Kituo hiki kipo chini ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Jukumu lake ni kuutunza, kuulinda na kuuhifadhi urithi wa ukombozi wa bara la Afrika. Kituo hiki kimeanzishwa baada ya Tanzania kupewa dhamana ya kuulinda na kuuhifadhi urithi wa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) tangu mwaka 2011 kupitia Azimio la kuanzishwa programu mahususi ya kuhifadhi kumbukumbu za ukombozi wa Afrika. Kielelezo 1.1 kinaonesha jengo la Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.**



Kielelezo 1.1: *Jengo la Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Africa*

*Utafiti wa kihistoria na uchapishaji*

Utafiti wa kihistoria na uchapishaji ni **muhimu katika kulinda na kuendeleza** historia ya taifa letu. Utafiti husaidia **kuchunguza matukio muhimu ya watu mashuhuri, jamii, taasisi au nchi na kusambaza maarifa haya kwa jamii.** Utafiti ni njia ya kuimarisha urithi wetu **wa kihistoria na kuelimisha vizazi vijavyo. Kwa kufanya hivyo, tunajenga msingi imara** kwa mustakabali wetu. Utafiti wa kihistoria **na uchapishaji huhakikisha kuwa historia yetu inaendelea kudumishwa na kupatikana kwa wote. Njia hii pia husaidia kujivunia** tamaduni zetu za zamani. Kupitia tafiti **za kihistoria, tunaimarisha ufahamu wetu juu ya asili na tamaduni zetu na kuongeza maarifa kuhusu tulikotoka, tulipo na tunakoelekea katika maendeleo kama taifa.**

FOR ONLINE READING ONLY

**Kazi ya kufanya 1.8**

Tafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali, ikiwamo mitandao, kisha bainisha mikakati mingine ya kuhifadhi historia ya Tanzania.

**Mikakati ya kulinda maadili**

Maadili ni muhimu sana katika maendeleo ya taifa. Bila jamii kuwa na maadili ni vigumu kupata maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Ili kufanikiwa katika hilo, serikali, taasisi zisizo za serikali na jamii kwa ujumla zimeandaa mikakati mbalimbali kuhakikisha maadili ya jamii yanalindwa. Baadhi ya mikakati ya kulinda maadili ni pamoja na elimu kwa umma, uanzishwaji wa taasisi kama TAKUKURU, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

*Utoaji wa elimu kwa umma*

Maadili ni eneo mtambuka linalosimamiwa na wadau mbalimbali. Serikali imekuwa inayatumia majukwaa mbalimbali ili kuufikisha ujumbe wa maadili kwa jamii. Mathalani, inatoa elimu ya mlipa kodi inayotolewa na kusimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Mahakama ya Tanzania inatumika kutoa eleimu kuhusu mambo ya sheria pamoja na elimu inayotolewa na Taasisi mbalimbali zinazosimamia maadili na urithi wa historia. Aidha, baadhi ya taasisi za umma zinazosimamia maadili zimekuwa zikishirikiana kwenye matukio mbalimbali kama vile kwenye Siku ya Maadili na Haki za Binadamu inayoadhimishwa kitaifa tarehe 10 Disemba kwa kila mwaka. Siku ya Maadili imetokana na uamuzi wa serikali ya kuunganisha Siku ya Kimataifa ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inayoadhimishwa tarehe 9 Disemba na Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inayoadhimishwa tarehe 10 Disemba ili kupisha tarehe 9 Disemba ambayo ni siku ya Uhuru wa Tanganyika. Taasisi zinazoshirikiana kuadhimisha Siku ya Maadili ni pamoja na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mamlaka ya Manunuzi ya Umma, Tume ya Utumishi wa Umma, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mahakama, Polisi, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na nyinginezo.

Taasisi hizi zinashirikiana katika matukio anuai kwa lengo la kuelimisha na kushirikisha umma katika kujenga na kukuza maadili, haki za binadamu, uwajibikaji, utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa. Mbinu za uelimishaji ni pamoja na kushiriki katika vipindi vya redio na televisheni, kuchapisha habari na makala magazetini, kuwa na wiki maalumu ya kutoa huduma kwa wananchi na kuchapa na kusambaza machapisho mbalimbali. Kwa upande mwingine, kutokana na umuhimu wa kujenga maadili kwa vijana, somo la Historia ya Tanzania na Maadili limeingizwa kwenye mitaala ya elimu kuanzia shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu. Vilevile, elimu inatolewa kupitia vyombo vya habari kama vile redio, runinga, magazeti, mitandao ya kijamii

FOR ONLINE READING ONLY

na taasisi za kiraia. Aidha, kumekuwa na vipindi maalumu vinavyofundisha umuhimu wa umoja, heshima, usawa na mshikamano katika jamii ambapo mambo yasiyo ya kimaadili yamekuwa yakibainishwa na kukemewa. Jamii imekuwa ikielemishwa umuhimu wa maadili na madhara ya kudharau maadili ya taifa.

*Kuanzishwa kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)*

Kuanzishwa kwa TAKUKURU ni mwendelezo wa juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya rushwa. Msingi wa mwelekeo huo umejengwa katika falsafa ya aliyekuwa Rais wa awamu ya kwanza, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipokuwa analihutubia Bunge jipya Mwaka 1965 na kusema: *RUSHWA ishughulikiwe bila huruma kwa sababu mimi naamini kuwa RUSHWA na HONGO ni adui mkubwa zaidi kwa ustawi wa wananchi wakati wa amani kuliko wakati wa vita. Mimi ninaamini kuwa rushwa katika nchi inatakiwa ishughulikiwe karibu sawa sawa na unavyoshughulikiwa UHAINI.* Wakati maadili ni mwenendo mwema, rushwa ni zao la uozo wa kimaadili unaomsukuma mtu kufanya jambo lenye sura ya uhalifu. Serikali imeweka mikakati ya kuanzisha taasisi mbalimbali zinazosimamia maadili ikiwemo TAKUKURU inayosimamia mapambano dhidi ya rushwa nchini.

Aidha, mwelekeo wa serikali kwenye vita dhidi ya rushwa umejengwa katika masharti ya Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inayosema: *Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, na kwa hiyo, lengo kuu la serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi.* Ibara ya 9 (h) ya Katiba ya Tanzania inaelekeza kwamba: *Taasisi na Vyombo vyote nchini kuhakikisha tunaondoa rushwa katika jamii yetu.* Kwa kuitikia agizo la katiba, serikali ilitunga Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329, ambayo ndiyo ilianzisha TAKUKURU mwaka 2007 baada ya kufutwa kwa Sheria ya Kuzuia Rushwa Na. 16 ya Mwaka 1971 na baada ya kufanyiwa marekebisho Sheria ya Kuzuia Rushwa (Cap.400) ya mwaka 1970 iliyokuwa imerithi sheria ya kikoloni, yaani Sheria ya Kuzuia Rushwa *(The Prevention of Corruption Ordinance Cap.400)* ya Mwaka 1958.

Kifungu cha 5 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 kinaipa TAKUKURU jukumu la kuongoza na kuratibu mapambano dhidi ya rushwa na Kifungu cha 4 kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7, kimeainisha majukumu mawili ya TAKUKURU ambayo ni kuzuia rushwa na kupambana na rushwa. Majukumu hayo mawili yanatekelezwa na TAKUKURU kwa kufanya kazi zifuatazo:

(a) Kuuelimisha umma ili kuishirikisha jamii;
(b) Kufanya utafiti na udhibiti kwenye mifumo ili kuziba mianya ya rushwa; na
(c) Kuchunguza na kufikisha watuhumiwa mahakamani mara baada ya ushahidi kupatikana.

*Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora*

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ni idara huru ya serikali

FOR ONLINE READING ONLY

iliyoanzishwa kama taasisi ya kitaifa iliyo na jukumu la kukuza na kuzilinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania. Tume hii hufuatilia utendaji kazi wa taasisi mbalimbali kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jukumu la tume hii ni kukuza ulinzi na haki za binadamu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na makubaliano ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora pia hupokea malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Hufanya uchunguzi wa ukiukwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa kanuni za utawala bora. Vilevile, tume hufanya utafiti na kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na mambo yanayohusiana na utawala bora. Pia, tume huanzisha kesi kwa viongozi wanaokiuka miongozo ya kimaadili. Mwisho, tume hii huzirekebisha sheria zinazokiuka haki za binadamu katika jamii.

*Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma*

Hii ni idara ya maadili ya viongozi wa umma ambayo ina mamlaka ya kuchunguza tabia na mienendo ya viongozi na watumishi wa umma kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa masharti ya sheria ya maadili ya viongozi wa umma yanazingatiwa ipasavyo. Idara hii imeundwa mahususi kama mkakati wa kudumisha maadili ya viongozi wa umma kulingana na nafasi zao. Kiongozi wa umma anatakiwa kuwa mwadilifu, mchapakazi, mwenye ujuzi, muungwana na mvumilivu. Kama kiongozi anashindwa kufuata miongozo hii, atakuwa amekiuka sheria ya maadili ya umma; na hivyo, yuko hatarini kuchukuliwa hatua au kuwajibishwa.

**Kazi ya kufanya 1.9**

Fanya utafiti katika jamii unamoishi, kisha ainisha mikakati mingine ya kuyalinda maadili ya Kitanzania.

**Zoezi la marudio**

1. Eleza chimbuko la utambulisho wa taifa la Tanzania.
2. Jadili ni kwa namna gani Serikali ya Tanzania imefanikiwa kujenga umoja na mshikamano nchini.
3. Mwalimu Nyerere aliwahi kusema kuwa, "Azimio la Arusha lilikuwa azimio la utu." Jadili sentensi hii kwa mifano dhahiri.
4. Ni kwa namna gani elimu inaweza kutumika kama njia ya kulinda historia, maadili na utambulisho wa taifa?
5. Jadili mchango wa TAKUKURU katika ujenzi wa maadili ya taifa la Tanzania.
6. Ni changamoto gani Tanzania inakabiliana nazo katika uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka za kihistoria?
7. Ainisha faida za kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu kwa taifa la Tanzania.
8. Eleza namna maliasili za taifa zinavyoweza kutumika kama sehemu ya utambulisho wa taifa.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Pili
# Mchango wa historia na urithi katika maendeleo

## Utangulizi

*Historia na urithi ni hazina muhimu katika maendeleo ya taifa. Katika sura hii, utajifunza dhana ya historia na urithi wa taifa, maeneo mbalimbali nchini yenye historia na urithi wa taifa, na mchango wa historia na urithi katika maendeleo ya taifa. Vilevile, utajifunza uhusiano uliopo kati ya maadili na urithi katika kuchochea na kuleta maendeleo ya taifa na njia bora na endelevu za uhifadhi wa historia na urithi ili kuleta maendeleo endelevu ya taifa. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuienzi historia na urithi wa taifa, kutumia urithi uliopo kuleta maendeleo yako binafsi na jamii pamoja na kutumia njia bora kuihifadhi historia na urithi wa taifa.*

**Fikiri**

**Nafasi ya historia na urithi katika kuleta maendeleo ya taifa.**

FOR ONLINE READING ONLY

## Dhana ya historia na urithi wa taifa

Kila taifa duniani lina historia na urithi wake. Kuna uhusiano kati ya historia na urithi wa taifa. Urithi ni vitu vyenye thamani vinavyotunzwa na kuthaminiwa kwa ajili ya vizazi vya sasa na vya baadaye. Vitu vinavyohusika katika urithi ni kama vile majengo ya kihistoria ambayo yalitumiwa na vizazi vilivyotangulia, vitu na vifaa vya kiutamaduni vilivyofaa kuhifadhiwa pamoja na vitu visivyooneka kama vile mila na desturi. Kwa maana nyingine, kuna urithi wa aina mbili: urithi unaoshikika na urithi usioshikika. Aina zote hizo mbili huhusu vitu vinavyorithiwa na taifa ambavyo vina thamani ya kihistoria au utamaduni.

### Historia ya taifa

Historia ya taifa ni kumbukumbu za matukio na mabadiliko muhimu katika maendeleo ya taifa linalohusika. Historia ya taifa hutuwezesha kuifahamu misingi na hatua za uanzishwaji wake. Pia, hutuwezesha kuelewa matukio mbalimbali katika taifa na jinsi matukio hayo yalivyochangia kupata maendeleo au kukwamisha maendeleo. Tanzania ni miongoni mwa nchi za Kiafrika zenye historia ndefu iliyosheheni utajiri wa urithi. Historia ya taifa hili inajumuisha mfumo wa maisha kabla ya ukoloni, wakati

wa ukoloni wa Wajerumani na baadaye Waingereza na kipindi cha harakati za kupigania uhuru. Pia, historia ya taifa hili inayajumuisha mageuzi ya kisiasa, kijamii na kiuchumi yaliyofanyika baada ya uhuru mwaka 1961, chini ya waasisi wa taifa la Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Sheikh Abeid Amani Karume na wengineo. Historia hiyo inaendelea katika vipindi tofauti baada ya uhuru kama vile kipindi cha siasa za ujamaa na utekelezaji wake na baadaye kipindi cha uliberali mpya mpaka wakati wa utandawazi. Kupitia kumbukumbu za matukio haya, tunajifunza taifa la Tanzania lilikotoka, lilipo sasa, na linakoelekea.

### Urithi wa taifa

Urithi wa taifa ni mkusanyiko wa mali, kumbukumbu za kihistoria, utamaduni, na maadili ambayo ni muhimu kwa utambulisho na maendeleo ya taifa. Urithi wa taifa hujumuisha maeneo ya asili kama vile mbuga za wanyama, milima, mito, maziwa na bahari. Pia, unajumuisha urithi wa utamaduni kama vile majengo ya kihistoria, lugha, ngoma za asili, mavazi ya asili na vyakula. Tanzania ni miongoni mwa mataifa ya Afrika yenye utajiri mkubwa wa urithi ambao ni utambulisho muhimu wa taifa hili. Baadhi ya mifano ya urithi wa kihistoria wa taifa la Tanzania ni pamoja na majengo ya kale yaliyopo Zanzibar, Bagamoyo, na Kilwa Kisiwani na michoro ya mapangoni iliyopo Kondoa-Irangi, na Isimila, pamoja na ufundi chuma na kilimo huko Engaruka.

### Historia na urithi wa taifa katika maeneo mbalimbali nchini

**Kazi ya kufanya 2.1**

Tafuta taarifa kutoka vyanzo mbalimbali, ikiwemo mitandao, kisha fafanua historia na urithi wa taifa unaopatikana katika maeneo mengine nchini Tanzania.

Tanzania ni nchi yenye utajiri wa historia na urithi uliotawanyika katika maeneo mbalimbali. Historia na urithi huo vimekuwa vikitambuliwa na kutunzwa kwa miaka mingi iliyopita. Historia yenyewe ni urithi wa kipekee unaopatikana katika maeneo mbalimbali ya nchi na umekuwa chanzo muhimu cha maarifa na ufahamu kuhusu utamaduni na harakati za maisha za jamii za Kitanzania katika nyakati na maeneo tofauti. Maeneo maarufu ya kihistoria na yenye urithi wa taifa ni pamoja na Oldupai Gorge, Bagamoyo na Kilwa Kisiwani pamoja na Nyumba ya Maajabu huko Zanzibar.

### Oldupai Gorge

Oldupai Gorge iko katika bonde la Ngorongoro mkoani Arusha. Sehemu hii ni miongoni mwa maeneo yenye kuibeba historia kubwa ya nchi na ni miongoni mwa urithi muhimu wa taifa la Tanzania. Pia, eneo hili ni miongoni mwa maeneo muhimu zaidi duniani kutokana na historia yake ya kugundulika kwa mabaki ya mtu wa kale zaidi duniani. Oldupai Gorge imekuwa ikifanyiwa tafiti tangu miaka ya 1930 ambako yamegundulika mabaki ya binadamu wa kale yaliyobadilisha uelewa wetu juu ya asili ya binadamu.

FOR ONLINE READING ONLY

### Bagamoyo

Bagamoyo ni mji mkongwe uliopo katika mkoa wa Pwani. Ni mahali ambapo alama za historia ya biashara ya utumwa zinaonekana wazi. Bagamoyo ilikuwa kituo muhimu cha biashara ya utumwa katika Afrika Mashariki kati ya karne ya 18 na 19. Pia, eneo hili lilikuwa njia kuu ya kusafirisha watumwa kwenda Zanzibar na sehemu nyingine duniani kama vile Amerika, Uarabuni na Madagaska. Katika mji huu, kuna mabaki mbalimbali ya kale ikiwa ni pamoja na majengo ya zamani, makaburi ya watumwa na watawala wa Kiarabu pamoja na maeneo mengine ya kihistoria. Vilevile, mji huu umesheheni historia ya ukoloni wa Wajerumani ambao katika majengo mengi walirithi usanifu wa Kiarabu na kuongeza aina yao ya usanifu. Aidha, katika mji wa Bagamoyo kuna mabaki ya misikiti miwili, kanisa na makaburi ya Washirazi kutoka karne ya 13 ya zama za sasa katika eneo la Kaole.

### Kilwa Kisiwani

Kilwa Kisiwani ni kisiwa katika wilaya ya Kilwa, mkoa wa Lindi. Ni moja ya maeneo ya urithi wa Tanzania unaotambuliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni. Kilwa Kisiwani ulikuwa moja ya miji muhimu zaidi ya pwani ya Afrika Mashariki katika karne za 13 hadi 16. Mji huu ulikuwa kituo kikubwa cha biashara na utamaduni wa Kiswahili. Pia, mji wa Kilwa ulitengeneza fedha yake iliyokuwa inatumika katika biashara kati yake na fedha zingine. Aidha, Kilwa Kisiwani ilikuwa na makao makuu ya Sultani. Leo hii, mabaki ya kale ya mji wa Kilwa Kisiwani yanaweza kutembelewa ili kujua historia ya eneo hilo na namna lilivyoathiri Tanzania kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa. Kielelezo 2.1 kinaonesha sarafu zilizokuwa zinatumika katika mji wa Kilwa.

FOR ONLINE READING ONLY



**Kielelezo 2.1:** *Sarafu za dhahabu zilizotumika katika mji wa Kilwa*

**Ngorongoro na Serengeti**

Haya ni maeneo ya hifadhi za mbuga za wanyama. Ngorongoro iko mkoani Arusha na Serengeti iko mkoani Mara. Hifadhi ya Ngorongoro inajulikana kwa kuwa na kreta kubwa zaidi duniani ambayo ni makazi ya wanyama mbalimbali kama vile simba, tembo, na twiga. Hifadhi hii imekuwa maarufu duniani tangu kuanzishwa kwake katika kipindi cha utawala wa Wajerumani kisha utawala wa Waingereza hadi sasa. Hali kadhalika, hifadhi ya Serengeti inajulikana kwa kuwa na uhamaji mkubwa wa wanyama pori duniani, ikiwa ni pamoja na nyumbu na pundamilia. Pia, hifadhi hii imekuwa kivutio kwa watalii kote duniani na chanzo kikubwa cha mapato kwa taifa la Tanzania.

**Nyumba ya Maajabu**

Visiwa vya Zanzibar vina historia na urithi ambao unaotambulika kitaifa na kimataifa. Kwa mfano, *Jengo la Beit Eil Ajaib* (Nyumba ya Maajabu) linapatikana katika Mji Mkongwe wa Zanzibar. Jengo hili lilijengwa mwaka 1883 na Sultani Said Barghash. Pia, katika eneo hili kuna Ngome Kongwe ambayo ilijengwa na Wareno katika karne ya 16 kwa ajili ya kujihami na kujilinda dhidi ya maadui. Aidha, katika kisiwa cha Pemba kuna Ngome Kongwe nyingine ambayo nayo ilijengwa na Wareno kwa ajili ya kujilinda. Maeneo haya na majengo mengine ni mojawapo ya historia na urithi wa taifa letu. Historia na urithi huu vimekuwa kivutio kwa watalii na wageni mbalimbali na kutoa ufahamu wa utamaduni na maisha ya zamani ya maeneo hayo.

**Maeneo ya urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika**

Kwa kuwa nchi mwenyeji wa Kamati ya Ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika, Tanzania, ilipewa hadhi ya kuanzisha Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika. Pamoja na kuwa na kituo hiki, nchini Tanzania kuna maeneo mbalimbali yaliyobeba historia ya harakati za urithi wa ukombozi wa Afrika. Maeneo hayo yako zaidi ya 200 ambayo ni pamoja na Kongwa mkoani Dodoma, Mazimbu mkoani Morogoro, Nachingwea mkoani Lindi na Kaole mkoani Pwani. Katika maeneo haya kulikuwa na kambi ambazo wapigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika walizitumia ili kupata mafunzo ya kupambana na wakoloni katika nchi zao. Kielelezo 2.2 kinaonesha watu wakitembelea handaki lililotumika kuhifadhia silaha na kujificha katika kambi ya FRELIMO iliyokuwa Kongwa, Dodoma.

FOR ONLINE READING ONLY



Kielelezo 2.2: **Watalii wakitembelea handaki katika kambi ya FRELIMO, Kongwa Dodoma**

**Kazi ya kufanya 2.2**

**Soma matini kutoka vyanzo mbalimbali kuhusu maeneo yenye urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika nchini Tanzania na kisha chambua vitu vinavyopatikana katika maeneo yanayohusika.**

**3. Chambua maeneo yenye historia na urithi nchini Tanzania.**

**4. Andaa mpangokazi wa kuelimisha jamii kuhusu maeneo yenye historia na urithi nchini Tanzania.**

**Kwa ufupi, Tanzania ina historia na urithi mwingi ambao umekuwa kivutio kwa watalii na wageni kutoka ndani na nje ya nchi, ambao kwa njia ya utalii na utafiti wameweza kufahamu utamaduni na maisha ya zamani ya Watanzania katika maeneo mbalimbali nchini.**

### Zoezi 2.1

1. **Linganisha urithi unaotokana na majengo ya kihistoria na ule unaotokana na maliasili nchini Tanzania.**
2. **Eleza urithi uliotokana na biashara ya utumwa.**

### Mchango wa historia na urithi katika maendeleo ya taifa

**Historia na urithi wa taifa umekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa, hususani katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, na kijamii.**

#### Kiuchumi

**Historia na urithi wa taifa vina mchango mkubwa sana katika maendeleo ya kiuchumi ya taifa letu. Historia imetuwezesha kuelewa fursa, mafanikio na changamoto za kiuchumi ambazo taifa letu limepitia katika nyakati mbalimbali. Hii ni muhimu kwani imesaidia kuelewa mapungufu na kutafuta njia sahihi za utumiaji fursa na utatuzi wa changamoto zilizojitokeza katika nyakati mbalimbali. Historia na urithi wa taifa letu vimekuwa muhimu katika maendeleo ya kiuchumi kwani vimeendelea kuvutia**

FOR ONLINE READING ONLY

uwekezaji wa ndani na wa kimataifa. Uwekezaji huo umechangia kuendeleza miundombinu na ukuaji wa teknolojia, ujuzi, na mitaji. Ukuaji wa nyanja hizo umesaidia maendeleo ya kiuchumi ya taifa letu kwa kutoa fursa za ajira, kuboresha maisha ya raia na ukuaji wa pato la taifa. Aidha, historia na urithi vimeimarisha sekta ya utalii ambao huvutia watalii na wageni kutoka sehemu mbalimbali duniani kuja Tanzania na kununua bidhaa na huduma mbalimbali; hivyo, vimesaidia kuingiza fedha za kigeni na kuchochea ukuaji wa uchumi.

**Kisiasa**

Kisiasa, historia na urithi wa taifa vimejenga msingi imara wa demokrasia na utawala bora kwa taifa la Tanzania. Kwa mfano, kihistoria Tanzania imekuwa ikifanya chaguzi huru na za kidemokrasia tangu uhuru. Historia hii imewezesha mifumo ya kisiasa kuboreshwa kwa uhuru na uwazi ili kuhakikisha kuna usawa, haki, na uwajibikaji katika jamii na serikalini. Historia ya Tanzania, kupitia harakati za ukombozi na mapambano ya kisiasa, imesaidia kujenga na kudumisha utamaduni wa kujitolea, kushirikiana na kuvumiliana ambao umekuwa nyenzo muhimu katika maendeleo ya taifa. Vilevile, historia inasaidia katika kuelewa na kujua jinsi matukio kama vile vita au jinsi mabadiliko ya utawala yalivyotokea na madhara yake. Hapa historia inatoa somo si tu kueleza jinsi hali ilivyokuwa bali inatujengea uwezo wa kutoweza kufanya makosa na kutafuta njia nzuri zaidi kwa maendeleo ya jamii zetu na taifa letu kwa ujumla. Mathalani, tunaona kuwa vita haikuwa njia yetu ya kupigania ukombozi wa taifa letu au kutatua migogoro mingine. Hiyo haikuwa njia yetu ya kutatua matatizo. Jambo hili ni somo tulilojifunza kutoka katika matukio ya vita kama ile ya Maji Maji ya mwaka 1905-1907. Kutumia diplomasia kumekuwa njia bora sana katika nchi yetu na kuleta faida nyingi zaidi za kimaendeleo.

**Kijamii**

Kijamii, historia na urithi wa Tanzania vimesaidia kujenga umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi. Kwa mfano, utamaduni kama vile mila na desturi, lugha na imani za kidini vimekuwa msingi madhubuti wa kuhamasisha upendo na umoja wa kitaifa. Aidha, historia ya mapambano ya ukombozi dhidi ya ukoloni, changamoto na harakati za pamoja za kijamii baada ya uhuru zimejenga msingi imara wa mshikamano, amani na utulivu miongoni mwa wananchi na kusaidia kukua kwa maendeleo na ustawi wa jamii imara. Aidha, historia na urithi vimesaidia kukuza ufahamu wa jamii juu ya utamaduni wetu na kusaidia kuenzi na kudumisha mila na desturi zetu za jadi. Hali hii imejenga na kudumisha utambulisho na heshima ya jamii zetu kama taifa. Pia, historia na urithi wa taifa letu vimekuwa na athari chanya katika ukuaji wa sekta ya elimu. Kupitia kujifunza historia na kufanya tafiti kuhusu urithi wa taifa, jamii imeweza kuvumbua maarifa mapya, kukuza ufahamu na kuzalisha wasomi wabobevu katika nyanja mbalimbali za kijamii. Kwa ujumla, historia na urithi vimesaidia kuleta maendeleo ya taifa letu kwa kuwatambulisha Watanzania kama wamoja katika taifa moja na kufanya

FOR ONLINE READING ONLY

washirikiane katika kuleta maendeleo ya taifa kama wamoja.

**Kazi ya kufanya 2.3**

Fanya utafiti mdogo katika jamii inayokuzunguka, kisha bainisha aina mbalimbali za urithi wa asili na mchango wake katika maendeleo ya jamii hiyo.

**Zoezi 2.2**

1. Ni kwa jinsi gani historia na urithi wa taifa vinaweza kuathiri maendeleo?
2. Jadili namna urithi wa kitamaduni unavyoweza kusaidia kuondoa umasikini katika jamii inayokuzunguka.
3. Fafanua jinsi historia ya taifa imekuwa nguzo ya umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi wa Tanzania?
4. Eleza ni kwa namna gani unaweza kutumia historia na urithi wa taifa lako kama chanzo cha kujifunza na kuboresha maendeleo ya jamii yako.
5. Ni kwa njia gani kijana wa Kitanzania anaweza kuhakikisha kwamba historia na urithi wa taifa vinatunzwa na kuheshimiwa kwa ajili ya vizazi vijavyo?

### Uhusiano kati ya maadili na urithi katika kuleta maendeleo ya taifa

Maadili na urithi ni nyenzo muhimu katika ujenzi wa taifa imara na lenye mafanikio. Maadili ni kanuni, miiko na miongozo inayosimamia tabia na mienendo inayokubalika katika jamii. Urithi wa taifa nao ni jumla ya vitu au mambo ya kiutamaduni, kihistoria, sanaa, lugha, na maadili yanayojenga utambulisho wa taifa fulani. Uhusiano kati ya maadili na urithi huchangia katika kuleta maendeleo ya taifa kwa namna mbalimbali kama inavyoelezwa hapa chini.

(a) Maadili ni sehemu ya utamaduni ambao pia ni urithi wa taifa. Hivyo, maadili huchangia maendeleo ya taifa kwa kusaidia kuudumisha na kuendeleza urithi huo. Kwa mfano, uwajibikaji, heshima, utu, uadilifu, kuzuia na kupambana na rushwa na ushirikiano kama sehemu ya maadili ya Kitanzania ni urithi unaosaidia kuudumisha utambulisho wa taifa la Tanzania na kuchangia maendeleo ya taifa katika nyanja mbalimbali za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

(b) Maadili ni sehemu ya urithi wa taifa ambayo husaidia kutoa mwongozo katika kufanya uamuzi sahihi na kujenga heshima, uaminifu, na uadilifu katika masuala mbalimbali ya kifamilia, kijamii na kitaifa. Hali hii hujenga msingi imara wa haki, usawa, amani na utulivu katika jamii na hatimaye kuchangia maendeleo endelevu ya mtu binafsi na ya taifa kwa ujumla. Hivyo basi, Watanzania tunapaswa kuyaheshimu na kuyadumisha maadili katika jamii pamoja na kushiriki kuzuia na kupambana na rushwa ili kuudumisha urithi huo unaochochea maendeleo ya taifa letu. Kwa kufanya hivyo, tunaweza kusaidia kuijenga na kuilinda nchi yetu kwa masilahi mapana ya vizazi vya sasa na vijavyo.

FOR ONLINE READING ONLY

(c) Kuishi kwa kufuata maadili ni moja ya hatua muhimu katika kuujenga urithi imara wa taifa lenye heshima, ukarimu, utu na uvumilivu. Watu wanaoishi kwa kufuata maadili na kuviepuka vitendo vya rushwa wana uhusiano mzuri na wenzao na husaidia kujenga taifa lenye kuheshimu maadili na haki za raia wake. Taifa lenye kuyaheshimu maadili hujenga uhusiano mzuri miongoni mwa raia wake na kuidumisha amani na utulivu. Uhusiano mzuri, amani na utulivu ni vichocheo vikubwa vya maendeleo ya taifa.

(d) Maadili ni urithi wa kiutamaduni ambao umejengwa kihistoria katika taifa letu. Hii ina maana kuwa maadili yamejengwa kutokana na historia ambayo imerithishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Urithi huu hutusaidia kuielewa, kuithamini na kuidumisha asili yetu kama taifa. Pia, husaidia kuujenga utu na utambulisho wetu kiutamaduni. Hivyo, ni jukumu la kila mwananchi kuyadumisha na kuyalinda maadili yetu kwani ni urithi ambao unachochea maendeleo katika taifa letu.

(e) Maadili yetu huchangia sana katika kuuendeleza na kuuimarisha urithi wa taifa letu. Maadili hutujengea uadilifu katika matumizi ya urithi wa rasilimali zetu. Jamii yenye maadili hufuata taratibu za kuyahifadhi na kuyalinda mazingira na rasilimali zake. Pia, huepuka ufisadi na huulinda utamaduni wa taifa kwa gharama yoyote. Kupitia maadili haya tunajenga urithi endelevu wenye manufaa kwa maendeleo ya taifa letu. Kwa upande mwingine, utunzaji wa urithi wetu huchangia kwa kiasi kikubwa katika kuyaimarisha na kuyaendeleza maadili yetu ya kiutamaduni kama taifa.

(f) Maadili na urithi vinachangia ujenzi wa jamii imara na iliyo tayari kushiriki kikamilifu katika shughuli za kujiletea maendeleo. Maadili yanapokuwa msingi wa maisha yetu ya kila siku huisaidia jamii kuona fahari na kuulinda na kuutumia urithi kwa uadilifu mkubwa. Kwa kufanya hivyo, tunathibitisha thamani yetu ya kuuhifadhi utajiri huu wa kiutamaduni na kihistoria kwa manufaa ya vizazi na vizazi, jambo ambalo linaleta maendeleo endelevu kwa taifa.

(g) Utamaduni na historia kama sehemu ya urithi wetu vina jukumu muhimu katika kuyaimarisha maadili yetu. Kupitia maarifa tunayoyapata kutokana na urithi huu, tunaweza kuihamasisha na kuelimisha jamii yetu kuhusu maadili. Kwa mfano, kupitia makosa kutoka katika utamaduni na historia yetu, taifa limeweza kuunda miongozo sahihi ya maadili inayotumika kama hazina ya zana za maendeleo ya taifa letu.

(h) Maadili ni urithi unaojenga misingi ya utawala bora na umoja katika taifa. Taifa lenye viongozi na wananchi wenye maadili hupata maendeleo kwa kusimamia haki na uwajibikaji katika kuihifadhi historia na urithi kwa maendeleo ya taifa. Urithi wa utamaduni na historia kama rasilimali zilizosimamiwa kwa kuzingatia

FOR ONLINE READING ONLY

maadili huchochea maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwani huondoa chuki na migogoro katika taifa.

**Kazi za kufanya 2.4**

Uliza watu mbalimbali katika jamii unamoishi jinsi urithi wa kiutamaduni unavyoweza kuchangia maendeleo ya jamii.

**Zoezi 2.3**

1. Fafanua maadili na urithi ambao hutoa mchango mkubwa katika kuleta maendeleo ya jamii.
2. Eleza jinsi uadilifu katika matumizi ya urithi wa rasilimali zetu unavyoweza kuleta maendeleo ya taifa.
3. Fafanua jinsi kuwepo kwa vitendo vya rushwa kunavyoweza kuuathiri urithi wa taifa.
4. Kama raia wa Tanzania una jukumu gani katika kuhakikisha kwamba maadili na urithi wa taifa vinachangia maendeleo yetu?
5. Pendekeza mikakati mitano ya kutumia maadili na urithi wetu ili kuleta maendeleo endelevu katika taifa letu.

## Uhifadhi wa urithi kwa maendeleo endelevu ya taifa

Urithi wa taifa ni rasilimali muhimu katika kuyaleta maendeleo endelevu ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa taifa lolote lile duniani. Tanzania ni miongoni mwa mataifa yenye utajiri mkubwa wa urithi wa kihistoria. Hivyo, uhifadhi wa urithi huo ni hatua muhimu ya kuudumisha ili kuchangia katika mchakato wa kuleta maendeleo. Uhifadhi wa urithi wa taifa ni shughuli za kuyalinda na kuyatunza maeneo muhimu ya kihistoria, utamaduni, nyaraka za kihistoria, lugha na maliasili za taifa kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo. Hivyo, kila raia au Mtanzania anapaswa kushirikiana na serikali katika kuuhifadhi urithi wa taifa kama wajibu wake.

### Wajibu wa raia mmoja mmoja katika uhifadhi wa urithi wa taifa

Kila raia wa Tanzania ana jukumu na wajibu wa kushiriki katika kuuhifadhi urithi wa taifa kwa namna mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) Kuuhifadhi urithi wa taifa kwa kuheshimu na kuuenzi utamaduni, mila na desturi za taifa. Pia, kushiriki katika matamasha na mashindano ya kiutamaduni, kudumisha lugha za asili, na kuhifadhi maeneo ya kihistoria;

(b) Kuihamasisha jamii na kutoa elimu kuhusu umuhimu wa urithi, madhara ya uharibifu wa urithi wetu na njia sahihi za kuuhifadhi urithi wa taifa letu. Raia anaweza kutumia njia mbalimbali kama sanaa, kampeni na vyombo vya mawasiliano katika kuwaelimisha na kuwahamasisha watu kuhusu umuhimu na njia za kuhifadhi historia na urithi wa taifa;

FOR ONLINE READING ONLY

(c) Kuzuia na kupambana na rushwa, dawa za kulevya na kulipa kodi kwa wakati ili kuwezesha ulinzi na uendelezaji wa uhifadhi wa urithi au kuzuia vitendo vinavyoweza kusababisha uharibifu wa urithi wa taifa; na

(d) Kuzuia na kupambana na rushwa katika shughuli mbalimbali za uhifadhi wa urithi au vitendo vinavyoweza kusababisha uharibifu wa urithi wa taifa. Raia anatakiwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwenye ofisi za serikali ikiwemo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kupitia njia zifuatazo: (i) Kufika ofisi za TAKUKURU zilizopo kila wilaya nchini; (ii) Kupiga simu ya bure au kuandika ujumbe (sms) kwenda namba 113 au kupiga *113# kisha kufuata maelekezo; na (iii) Kutumia simu ya kiganjani kupakua programu tumizi ya TAKUKURU (TAKUKURU APP) kwenye *Playstore* kisha kuitumia kupiga picha, kuzirekodi sauti au nyaraka na kuzituma kupitia programu tumizi hiyo au kujaza na kuituma fomu iliyopo kwenye tovuti ya TAKUKURU (www.pccb.go.tz). Aidha, kila raia awe na ujasiri wa kukubali kutoa ushahidi mahakamani dhidi ya watuhumiwa watakaofikishwa mahakamani kutokana na vitendo vya rushwa na kuhusu uharibifu wa historia au urithi wa taifa.

**Wajibu wa jamii katika uhifadhi wa urithi wa taifa**

Jamii ina jukumu kubwa la kuuhifadhi urithi wa taifa kwa sababu urithi huo ni sehemu muhimu ya historia na utambulisho wa taifa. Katika kutekeleza jukumu hili, jamii ina wajibu ufuatao:

(a) Kushiriki katika shughuli za uhifadhi wa urithi kwa kuchangia nguvukazi katika shughuli za upandaji miti pamoja na ujenzi na ukarabati wa maeneo ya urithi. Ushiriki katika shughuli hizi utasaidia kuyafanya maeneo ya urithi yaendelee kuwa katika hali ya ubora na kuvutia utalii wa ndani na nje. Pia, ni wajibu wa jamii kujitolea kuchangia rasilimali zao kwa ajili ya kuendeleza miradi ya uhifadhi katika maeneo yao. Aidha, ni wajibu wa viongozi wa kijamii kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo katika kutoa elimu kwa wanajamii kuhusu njia na umuhimu wa uhifadhi wa maeneo ya kihistoria na urithi. Hii itawasaidia wanajamii kutambua na kuongeza uelewa juu ya urithi na umuhimu wake katika kuleta maendeleo endelevu. Elimu ya uhifadhi wa urithi wa taifa itamwezesha kila mwanajamii kuuthamini na kuuenzi urithi huo kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

(b) Kuyalinda na kuyahifadhi maeneo ya urithi kwa kuchukua hatua mbalimbali. Miongoni mwa hatua hizo ni kushiriki katika shughuli za usafi na ulinzi wa maeneo ya urithi. Vilevile, jamii inapaswa

FOR ONLINE READING ONLY

kushiriki katika kuzuia vitendo vya uhalifu au uharibifu wa maeneo ya urithi kwa kutoa taarifa za uhalifu kwenye mamlaka za ulinzi na usalama. Kwa kufanya hivyo jamii itakuwa imetimiza wajibu wake katika kuulinda, kuuendeleza na kuudumisha urithi wa taifa. Ili kulifanikisha jukumu hili, ni muhimu kuimarisha ushirikiano kati ya jamii, asasi au taasisi zinazohusika na uhifadhi wa maeneo ya urithi pamoja na serikali. Ushirikiano kati ya jamii, taasisi na serikali utasaidia kubadilishana ujuzi na uzoefu juu ya namna bora ya kulinda urithi wetu kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

(c) Kuuhifadhi urithi wa taifa kwa kuhakikisha unasambaza maarifa ya urithi kwa vizazi vijavyo. Katika kufanikisha hili jamii inapaswa kuzikusanya, kuzihifadhi na kuzisambaza taarifa na maarifa juu ya urithi wa taifa toka kizazi kimoja na kingine. Upatikanaji wa taarifa na maarifa hayo kwa watu wote kutatoa fursa kwa kila mwanajamii kujifunza na kufahamu kwa kina juu ya urithi wa taifa kupitia vyanzo kama vile vitabu, mitandao ya kidijiti, na njia nyingine za kiteknolojia. Kwa kufanya hivyo, jamii itakuwa nguzo muhimu katika kuuhifadhi urithi wa taifa kwa vizazi vijavyo.

(d) Kuwaelimisha vijana kuanzia ngazi ya familia ili wafuate maadili ya kujali na kutunza urithi wa taifa na kutojihusisha na vitendo vya kihalifu ikiwemo matumizi ya dawa za kulevya na ukwepaji kodi. Pia, wawe tayari kuzuia na kupambana na rushwa kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa vinavyotishia uharibifu wa urithi wa taifa kwenye ofisi za serikali ngazi ya kijiji au mtaa, wilaya au ofisi za TAKUKURU zilizopo katika kila wilaya hapa nchini. Pia, wanaweza kuripoti kwa kupiga simu ya bure au kuandika ujumbe mfupi (sms) kwenda namba 113 au kupiga *113# kisha kufuata maelekezo.

**Wajibu wa serikali katika uhifadhi wa urithi wa taifa**

Kama wadau wengine, serikali ina wajibu mkubwa sana katika uhifadhi wa urithi wa taifa. Miongoni mwa wajibu wa serikali katika uhifadhi wa urithi wa taifa ni pamoja na:

(a) Kutunga sera na sheria za kuulinda na kuutunza urithi wa taifa. Serikali ina wajibu wa kuzitunga sera kuhusu namna ya kuyahifadhi maeneo ya urithi wa taifa. Kupitia sera hizo jamii na wadau wanapata miongozo inayowawezesha kuweka mikakati madhubuti ya kusimamia uhifadhi wa urithi wa taifa. Aidha, kuwepo kwa usimamizi wa utekelezaji wa sheria za uhifadhi ni hatua muhimu sana katika kuyalinda maeneo ya urithi. Sheria hizi zitatoa kanuni na taratibu za kuzingatia katika matumizi ya rasilimali na zinaainisha adhabu mbalimbali kwa mtu au watu wataokiuka au kuvunja taratibu za kisheria zinazohusiana na uhifadhi wa urithi wa taifa.

FOR ONLINE READING ONLY

Mfano wa sheria na sera za uhifadhi wa urithi zilizotungwa na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni pamoja na Sheria ya Malikale na Sera ya Malikale ya mwaka 2008. Kwa minajili hii, wizara, kupitia Idara ya Mambo ya Kale, ina wajibu wa kutambua, kulinda, kutunza na kuhifadhi Kumbukumbu na Urithi wa Taifa na Urithi wa Dunia kwa mujibu wa Sera ya Malikale ya 2008, Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 (R.E 2002) na Mkataba wa Kimataifa wa 1972 wa UNESCO. Kumbukumbu na Urithi huu unatokana na rasilimali za utamaduni zinazoshikika na zisizoshika; zinazohamishika na zisizohamishika kama zinavyoainishwa katika Sera ya Malikale (2008) na Sheria ya Mambo ya Kale, Sura 333. Malengo mahususi ya Sera ya Malikale 2008 ni pamoja na kufafanua dhima na majukumu ya serikali za mitaa, jamii, watu binafsi, mashirika na asasi mbalimbali katika kuhifadhi na kusimamia malikale; kuweka ufafanuzi sahihi wa kulinda, kusimamia, kutunza, kuhifadhi, kuendesha na kuendeleza malikale; kuweka Kumbukumbu za Urithi wa Taifa kwa ujumla, na kuainisha namna bora ya kusimamia utafiti na uhifadhi wa malikale.

(b) Kupanga mikakati ya uhifadhi na kusimamia utekelezaji wake. Serikali ina wajibu wa kupanga na kusimamia utekelezaji wa mikakati madhubuti ya kuulinda na kuutunza urithi wa taifa. Mikakati hiyo ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uhifadhi wa urithi kwa ufanisi. Kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa mikakati iliyowekwa kwa kiwango kinachohitajika ni hatua muhimu katika uhifadhi wa urithi kwa manufaa ya vizazi vijavyo na ustawi wa taifa kwa ujumla.

(c) Kuunda taasisi na vyombo maalumu vya kuusimamia uhifadhi wa urithi wa taifa. Serikali inapaswa kuunda taasisi na vyombo maalumu vya kuusimamia uhifadhi wa urithi wa taifa letu. Katika kutekeleza jukumu hili muhimu, serikali imefanikiwa kuunda taasisi mbalimbali ikiwemo Makumbusho ya Taifa ambayo ni taasisi ya kielimu na kiutamaduni yenye wajibu wa kukusanya, kutunza na kufanya utafiti wa vifaa vya kiutamaduni na kisayansi vinavyohusu urithi wa kiutamaduni na asili wa Tanzania. Pia, kuna Idara ya Malikale yenye jukumu la kuzisimamia na kuzihifadhi rasilimali za utamaduni, zinazoshikika na zisizoshikika pamoja na zile zinazohamishika na zisizohamishika zilizo nchi kavu na majini zenye umri wa miaka mia moja (100) na kuendelea. Taasisi nyingine ni pamoja na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) lenye wajibu wa kuikuza lugha ya Kiswahili na Baraza la Sanaa la Tanzania (BASATA) lenye wajibu wa kuongeza uhifadhi na maendeleo ya uzalishaji wa kazi tofauti za sanaa.

FOR ONLINE READING ONLY

(d) Kutenga bajeti ya kufanikisha utekelezaji wa shughuli za uhifadhi wa urithi wa taifa. Serikali ina wajibu mkubwa wa kutenga fedha ili kuhakikisha kuwa shughuli za uhifadhi zinafanyika kwa ufanisi. Fedha hizo zitatumika katika shughuli za uhifadhi kama vile ukarabati wa miundombinu iliyo kwenye maeneo ya urithi, kuhakikisha utunzaji wa rasilimali na kumbukumbu za kihistoria, na kuwezesha shughuli za utafiti kuhusiana na urithi wa taifa. Aidha, fedha zinatumika katika utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu faida za kuuhifadhi urithi wa taifa letu.

(e) Kuielimisha jamii kuhusu uhifadhi wa urithi wa taifa. Serikali ina jukumu muhimu la kuhakikisha kuwa jamii inapata elimu ya kutosha kuhusu umuhimu na njia mbalimbali za uhifadhi wa urithi wa taifa. Serikali inatakiwa kulitekeleza jukumu hili kupitia mikutano ya hadhara, semina, taasisi za elimu na vyombo vya habari. Elimu na mafunzo ni nyenzo muhimu katika uhifadhi kwani husaidia kujenga jamii yenye kuuthamini na kuuenzi urithi kwa manufaa ya taifa.

(f) Kufanya na kusaidia kufanyika kwa tafiti mbalimbali zinazohusu urithi wa taifa. Kwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali, serikali inatakiwa kufanya tafiti au kuziwezesha taasisi na wadau mbalimbali wa uhifadhi kufanya tafiti kuhusu urithi wa taifa. Hii itasaidia kubaini maeneo mapya ya urithi, changamoto za uhifadhi na njia sahihi za kuuhifadhi urithi wa taifa. Serikali inatakiwa kuhakikisha kwamba tafiti zinakamilika na matokeo ya tafiti hizo yanatolewa, yanatunzwa na kutumika ipasavyo kwa maendeleo endelevu ya urithi wa taifa letu. Tafiti hizi ni pamoja na zile za kihistoria, kiakiolojia na kitamaduni ambazo zitatoa mwelekeo bora wa kuuhifadhi na kuutunza urithi wa taifa.

(g) Kuutekeleza kikamilifu Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji *(National Anti-Corruption Strategy and Action Plan)* ili kuweka mifumo imara ya ndani inayoimarisha uadilifu na kuzuia rushwa katika taasisi zinazohusika ikiwemo kuunda Kamati za Kusimamia Maadili *(Integrity Committees)*, kutengeneza miongozo ya kuyasimamia maadili na mapambano dhidi ya rushwa na kuchukua hatua kwa watumishi wanaokiuka maadili na kuhusisha na vitendo vya rushwa.

### Njia bora za uhifadhi wa urithi wa taifa kwa maendeleo endelevu

Katika kufikia maendeleo endelevu nchini Tanzania, uhifadhi wa urithi wa taifa ni jambo lisiloepukika. Taifa linahitaji njia bora za uhifadhi wa urithi ili kuyaleta maendeleo yenye tija. Kuna njia mbalimbali za uhifadhi wa urithi wa taifa. Kila njia ina umuhimu na mchango wake katika kuuendeleza urithi wa taifa. Hata hivyo, zifuatazo ni miongoni mwa njia bora zinazotumika kuhakikisha kunakuwapo na uhifadhi madhubuti wa urithi wetu kwa

FOR ONLINE READING ONLY

maendeleo endelevu ya taifa.

(a) Kuyatangaza maeneo ya kihistoria: Kupitia njia hii, serikali inayatangaza maeneo yote yenye historia na urithi wa kipekee kuwa maeneo muhimu za taifa. Njia hii inahusisha hatua muhimu za uhifadhi kama vile kuiweka mipaka na ulinzi ili kuzuia uvamizi na uharibifu wa maeneo yanayohusika. Pia, kuhakikisha upatikanaji wa taarifa muhimu kuhusu maeneo hayo kunawezesha utunzaji wake. Miongoni mwa maeneo yaliyotangazwa na serikali ya Tanzania ni majumba ya kale ya Bagamoyo na Zanzibar. Oldupai Gorge na michoro ya mapangoni ya Isimila na Kondoa Irangi. Njia hii imechangia sana katika kuhifadhi na kulinda urithi wetu kwa maendeleo endelevu.

(b) Kuzikuza na kuzihifadhi lugha za asili na tamaduni zake: Kuzikuza na kuzihifadhi lugha zetu za asili na utamaduni wa jamii zetu ni moja ya njia bora ya kuuhifadhi urithi wa taifa. Lugha za asili ni muhimu katika kuujenga na kuudumisha utambulisho wa taifa na kuzuia kupotea kwa utamaduni wa jamii yetu. Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanzisha mipango ya kuzikuza na kuzidumisha lugha na tamaduni za asili. Mipango hiyo ni pamoja na kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa lugha na tamaduni zao. Aidha, jamii imekuwa ikihamasishwa kushiriki katika shughuli mbalimbali za kitamaduni kama vile matamasha ya kiutamaduni. Pia, jamii zinahamasishwa kuzirekodi na kuzihifadhi lugha na tamaduni za asili. Aidha, serikali imeitambua lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa katika shughuli za kiserikali, kijamii na kielimu.

(c) Kuhifadhi makumbusho na nyaraka za kihistoria: Uhifadhi wa makumbusho na nyaraka za kihistoria ni njia bora ya kuihifadhi historia na utamaduni wa taifa letu. Makumbusho na nyaraka hutoa fursa kwa jamii kujifunza na kuielewa historia, mila na desturi zao. Pia, hutoa fursa adhimu kwa watafiti na wataalamu mbalimbali kupata taarifa za kihistoria na kitamaduni. Njia hii inachangia kikamilifu katika kuulinda urithi wa taifa letu na kuleta maendeleo endelevu katika sekta za elimu na utamaduni. Mifano ya njia hii ni pamoja na uanzishwaji wa Ofisi ya Nyaraka za Taifa Tanzania (*Tanzania National Archives*) iliyoko mkoani Dar es Salaam, Kituo cha Nyaraka za Taifa kilichopo Dodoma na Arusha pamoja na Idara ya Nyaraka za Taifa (Makavazi) za kikanda kama Mbeya na Mwanza.

(d) Kuvihifadhi vitu vya kale: Hii ni miongoni mwa njia bora ya uhifadhi wa urithi wa taifa. Njia hii inahusisha utunzaji wa vitu vyenye thamani kubwa kihistoria, kitamaduni na kisanaa. Vitu hivyo ni pamoja na majengo ya kihistoria, kazi za sanaa za asili za mababu na mabibi zetu, na vitu vingine vya

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Tatu: Fursa za uwekezaji zitokanazo na vivutio vya kihistoria na urithi

## Utangulizi

*Tanzania ni nchi yenye vivutio vya kihistoria na urithi ambavyo ni fursa kwa wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi. Katika sura hii, utajifunza maana ya uwekezaji, fursa za uwekezaji zitokanazo na vivutio vya kihistoria na urithi pamoja na kujenga ushirikiano na kukuza biashara ya kimataifa. Aidha, utajifunza vitendo vya kimaadili vinavyokuza fursa zitokanazo na urithi na vitendo visivyo vya kimaadili ikiwemo rushwa vinavyodumaza fursa zitokanazo na urithi. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kubaini na kutumia fursa mbalimbali zitokanazo na vivutio vya kihistoria na urithi.*

**Fikiri**

**Fursa za uwekezaji katika vivutio vya kihistoria na urithi nchini Tanzania.**

FOR ONLINE READING ONLY

### Dhana ya uwekezaji

Uwekezaji ni kitendo cha kimkakati cha kuweka rasilimali kama vile pesa au mali katika miradi au shughuli mbalimbali za uzalishaji mali na huduma za kibiashara kwa lengo la kupata faida yenye tija. Uwekezaji huu hufanywa na serikali, kampuni, vikundi vya wajasiriamali au watu binafsi kwa kuzingatia sekta tofauti za uchumi. Fursa za uwekezaji ni nafasi zinazopatikana kwa kuwekeza katika miradi mbalimbali kwa matarajio ya kupata faida. Fursa hizi zinaweza kuwa katika kilimo, viwandani, utamaduni, teknolojia, utalii, biashara na nishati. Uwekezaji unahusisha kuweka fedha, muda na juhudi katika miradi yenye uwezo wa kukuza mtaji na kupata faida. Kwa mfano, fursa za uwekezaji katika sekta ya utalii zinajumuisha ujenzi wa migahawa, hoteli, vyuo vya mafunzo ya utalii, biashara ya usafiri na usafirishaji, biashara ya mbogamboga na vyakula.

Lengo kuu la uwekezaji ni kuongeza thamani ya rasilimali ili kupata mapato ya uhakika na endelevu ambayo yatasaidia katika kuuendesha uchumi wa mtu binafsi, kampuni au taifa na kuchangia katika maendeleo katika nyanja zote, yaani kijamii, kiuchumi, na kisiasa. Hivyo, uwekezaji una

jukumu kubwa katika kutengeneza ajira, kuongeza uzalishaji, na kuboresha hali ya maisha ya watu. Kabla ya kuwekeza, ni muhimu kufanya utafiti ili kufahamu kwa kina soko, sheria na kanuni za uwekezaji pamoja na mwelekeo wa uchumi ili kufanya uamuzi sahihi na wenye tija. Vilevile, ni muhimu kuwa na mipango madhubuti na mikakati ya utekelezaji ili kufikia malengo ya uwekezaji. Mipango na mikakati hii inapaswa kuwa ya uwazi na uwajibikaji katika mchakato wa uwekezaji ili kukuza imani ya wadau na kudumisha uaminifu katika soko la uwekezaji. Katika ulimwengu wa leo wenye ushindani mkubwa, uwekezaji ni njia mojawapo ya kukuza uchumi na kuleta maendeleo endelevu katika taifa. Tanzania, kama ilivyo kwa nchi nyingine, ilichukua hatua kwa kufungua fursa za uwekezaji katika maeneo ya kihistoria na urithi. Sekta binafsi na wadau wengine walipewa fursa kwa kushirikiana na serikali ili kuinua utalii huu wa utamaduni kwa maendeleo ya taifa.

### Fursa za uwekezaji zitokanazo na vivutio vya kihistoria na urithi

Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye historia ndefu, yenye kuvutia na kitovu cha biashara. Pia, Tanzania ilikuwa na ushawishi mkubwa katika harakati za ukombozi wa nchi za bara la Afrika, na hasa nchi za kusini mwa Afrika. Vilevile, imejaliwa kuwa na utajiri wa vivutio vya kihistoria na urithi wa aina mbalimbali. Vivutio vya kihistoria na urithi wa Tanzania ni pamoja na majengo ya kale, maeneo ya kumbukumbu na matukio muhimu na maalumu pamoja na utamaduni wa makabila mbalimbali. Vivutio hivi vina historia na utamaduni wa pekee unaotoa fursa mbalimbali za uwekezaji. Miongoni mwa fursa hizo ni pamoja na:

#### Ujasiriamali na biashara

Uwekezaji katika vivutio vya kihistoria na urithi wa Tanzania hutoa fursa ya kukuza ujasiriamali na biashara. Sekta ya utalii inayotokana na vivutio hivi inaleta fursa kwa wafanyabiashara na wajasiriamali katika sekta za malazi, vyakula na vinywaji, usafiri na biashara nyinginezo zinazohusiana na utalii. Hivyo, uwekezaji katika kuhifadhi na kuendeleza vivutio hivi si tu unachochea mapato ya taifa bali unapanua pia wigo wa fursa za kiuchumi kwa wananchi. Kwa minajili hii, uwekezaji katika vivutio vya kihistoria na urithi hutoa fursa kwa wafanyabiashara kuanzisha na kufungua hoteli, nyumba za kulala wageni, baa na maduka. Kwa mfano, ujenzi wa hoteli za kitalii karibu na maeneo ya vivutio utawavutia watalii wengi zaidi na kuongeza mapato ya serikali. Hoteli hizi zinawapa watalii fursa ya kuishi karibu na vivutio vya kihistoria na kuwawezesha kufurahia na kujifunza zaidi kuhusu historia na utamaduni wa Tanzania. Hali hii inajidhihirisha kwa wazi zaidi katika maeneo yenye vivutio vya kihistoria na urithi kama vile Kilwa, Bagamoyo, Unguja na Pemba. Aidha, uwekezaji huu unachangia katika ukuaji wa sekta ya utalii na kukuza ajira kwa Watanzania.

#### Ajira

Uwekezaji katika vivutio vya kihistoria na urithi wa Tanzania unatoa fursa kubwa katika maendeleo ya sekta ya ajira. Sekta ya utalii inayohusiana na vivutio hivi inatoa fursa za ajira kwa watu wa ndani, hasa

FOR ONLINE READING ONLY

wale waliopo karibu na vivutio hivyo. Ajira mbalimbali ambazo zinaweza kutokana na uwekezaji katika urithi wa kihistoria ni kama vile kuongoza watalii, udereva, ukalimani, wafanyakazi wa hotelini, wanamuziki, walinzi, wabeba mizigo pamoja na sanaa bunifu kama vile kuchonga vinyago. Ajira hizi zinaweza kuwa za kudumu au za msimu kutokana na uingiaji wa wageni katika vivutio hivyo. Hivyo, uwekezaji mkubwa katika sekta hii unaweza kusaidia kupunguza ukosefu wa ajira na kukuza ustawi wa jamii za wenyeji katika maeneo yanayozunguka vivutio hivi vya kihistoria na urithi.

**Kazi ya kufanya 3.1**

Vijana wengi wasomi wanalalamika kuhusu ukosefu wa ajira katika nchi yetu. Pendekeza namna vijana wanavyoweza kutumia fursa zitokanazo na vivutio vya kihistoria na urithi kukabiliana na changamoto hiyo.

### Elimu na utafiti

Uwekezaji katika vivutio vya kihistoria na urithi wa Tanzania kunasaidia kutoa fursa ya elimu na utafiti. Vivutio hivi ni vyanzo vya maarifa muhimu kuhusu historia, utamaduni, na maisha ya zamani ya jamii za Kitanzania. Kuwekeza katika maeneo haya kunachochea shughuli za utafiti na kusaidia kueneza maarifa kwa jamii ya sasa na kizazi kijacho. Wanataaluma na wanafunzi wengi wanaofanya utafiti na kusoma kuhusu mambo ya kale au akiolojia, utalii wa utamaduni, urithi na historia wamekuwa watumiaji wazuri wa vivutio hivi kama maeneo yao ya utafiti na ya kujifunzia masomo kwa vitendo. Tafiti zao zinasaidia uzalishaji wa machapisho mengi kuhusu vivutio hivi. Pia, huwasaidia wanataaluma wengi kupanda vyeo vya kitaaluma na wanafunzi kupata fursa ya kujifunza kivitendo na kuviona vitu wanavyojifunza darasani katika eneo la vivutio vya kihistoria na urithi.

### Serikali kuongeza pato la taifa

Vivutio hivi ni vyanzo vikubwa vya mapato ya taifa kupitia sekta ya utalii. Pamoja na watalii kuendelea kuvutiwa na maliasili kama milima na mbuga za wanyama, watalii kutoka ndani na nje ya nchi wamezidi kuvutiwa na historia na urithi wa Tanzania kama vile miji ya kale, makumbusho, na utamaduni kwa kasi zaidi. Hivyo, uwekezaji katika kuhifadhi na kukuza vivutio hivi ni fursa adhimu kwa serikali katika kuongeza pato la taifa, kutoa ajira kwa wananchi na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi. Ongezeko la watalii linaendana na ongezeko la pato la taifa kutoka kwenye viingilio vya watalii, kodi za mapato kutoka katika maeneo yanayofanyiwa uwekezaji katika vivutio hivyo pamoja na mapato ya kawaida. Ingawa ni vigumu kupata mapato kamili kutoka katika utalii wa utamaduni pekee yake kwa sasa, ila tunaweza kutumia mapato ya jumla kutoka kwenye utalii ambayo yanatoa picha ya ukuaji wa pato la taifa na kuongeza mchango wake katika bajeti ya nchi, ambapo utalii katika vivutio vya kihistoria na urithi huchangia pia.

**Kazi ya kufanya 3.2**

Tumia vyanzo mbalimbali vya taarifa, ikiwamo mitandao, kuchunguza idadi ya watalii nchini na mchango wao katika pato la taifa.

FOR ONLINE READING ONLY

### Kujenga uhusiano mzuri wa kimataifa

**Uwekezaji katika vivutio vya kihistoria na urithi wa Tanzania husaidia kujenga na kuendeleza uhusiano wa kimataifa. Mataifa mengine yanavutiwa na utajiri wetu wa kiutamaduni na kihistoria na kuamua kushirikiana nasi katika kuhifadhi na kutangaza urithi wetu. Hali hii inaleta fursa za ushirikiano wa kiutamaduni na kubadilishana maarifa na uzoefu, hali ambayo huimarisha uhusiano wa kidiplomasia na kusaidia katika maendeleo ya taifa. Mathalani, mpaka sasa historia ya Tanzania ina upekee katika historia ya mapambano dhidi ya udhalimu na ukoloni kusini mwa bara la Afrika. Kama eneo la kimkakati, Tanzania ilikuwa kituo kikuu cha mafunzo ya kijeshi na kidiplomasia kwa wapigania uhuru kusini mwa Afrika, hasa kwa Waafrika Kusini, Wamsumbiji na Wanamibia. Hivyo, hapa nchini pamesheheni historia na urithi wa mataifa hayo ambao unawavutia sana watu hawa na kuona Tanzania ni kwao na hatimaye kujenga uhusiano mzuri nan chi hizo. Maeneo kama Mazimbu – Morogoro; Kongwa – Dodoma na Nachingwea – Lindi ni maeneo yenye utajiri wa kihistoria na urithi wa mapambano dhidi ya udhalimu na ukoloni. Maeneo haya yamebaki kuwa kiungo muhimu cha mataifa hayo na Tanzania, si kihistoria tu bali hata kidiplomasia. Zanzibar ina uhusiano mzuri sana na nchi za Falme za Kiarabu kama vile Oman. Uhusiano huu uliojengeka kutoka katika historia ulitengeneza vivutio vya urithi na historia kama vile soko la utumwa, Beit al Ajaib, na mji mkongwe Zanzibar. Hata wanapotembelea Zanzibar hujiona kama wanarudi nyumbani na kwa ndugu zao.**

#### Kazi ya kufanya 3.3

**Soma katika vyanzo mbalimbali vya taarifa na bainisha fursa mbalimbali zitokanazo na mila na desturi za jamii za Kitanzania.**

### Uwekezaji katika utalii wa kiutamaduni

**Utalii wa kiutamaduni hutoa fursa nzuri za uwekezaji nchini Tanzania. Moja ya fursa hizi ni kuendeleza tamaduni za makabila mbalimbali ya Tanzania. Kuna tamaduni nyingi zinazopatikana nchini Tanzania ambazo zinaweza kuwavutia watalii kutoka katika maeneo mbalimbali. Hivyo, kuimarisha maonesho ya utamaduni na matamasha ya kiutamaduni ni fursa nyingine ya uwekezaji. Kuendesha matamasha na maonesho ya utamaduni huwavutia watalii na kuchangia katika ukuaji wa utamaduni. Maonesho ya utamaduni na matamasha ya kiutamaduni ni fursa muhimu ya uwekezaji katika utalii wa kihistoria nchini Tanzania. Kwa kuimarisha maonesho haya, tunaweza kuonesha utajiri na tofauti za tamaduni za makabila mbalimbali ya Tanzania. Hii inaweza kufanyika kupitia maonesho ya muziki, ngoma, mavazi, na mila za asili. Fursa hii inaweza kuongeza uhamasishaji wa utalii na kuwavutia watalii kutoka sehemu mbalimbali za dunia. Pia, inaweza kuwawezesha wageni wa kimataifa kuelewa na kuheshimu utamaduni wa Tanzania. Serikali na wadau wa utalii wanaweza kuwekeza katika kuboresha miundombinu ya maonesho, kukuza vipaji, ufundi, na sanaa. Hii itasaidia kuongeza ajira kwa vijana na kuinua uchumi wa nchi. Ngoma**

FOR ONLINE READING ONLY

za asili ni kivutio kikubwa kwa watalii na ni ajira pia. Kielelezo 3.1 kinaonesha watu wakicheza ngoma ya Muheme ambayo huchezwa na Wagogo.



**Kielelezo 3.1** Ngoma ya Muheme

FOR ONLINE READING ONLY

### Kazi ya kufanya 3.4

Kwa muda mrefu uendeshaji wa shughuli za maendeleo ya utalii wa vivutio vya kihistoria na urithi zimekuwa zikigharamiwa na serikali na mashirika ya kimataifa. Tafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali, kisha pendekeza njia mbadala za uendeshaji wa shughuli za utalii wa kihistoria na urithi nchini.

### Zoezi 3.1

1. Jadili umuhimu wa serikali kuweka sera na miongozo thabiti kuhusu uwekezaji katika utalii wa urithi.
2. Changamoto zipi zinazoweza kujitokeza wakati wa kuendeleza miundombinu katika maeneo ya kihistoria? Hatua gani zinazoweza kuchukuliwa kukabiliana na changamoto hizo?
3. Kulingana na muktadha wa utalii katika vivutio vya kihistoria, fafanua namna vyombo vya habari vinavyoweza kutumika kama vyombo vya uendelezaji na uhamasishaji wa uwekezaji wa utalii huo.
4. Hatua zipi zinaweza kuchukuliwa na jamii ili kukuza na kuthamini utalii wa kiutamaduni?
5. Toa maoni yako kuhusu namna sanaa-bunifu inavyoweza kutumika kwenye vivutio vya historia na urithi.

**Kuendeleza vivutio vya kihistoria katika maeneo ya vijijini**

Kuendeleza vivutio vya kihistoria katika maeneo ya vijijini ni fursa muhimu katika

kuboresha utalii wa vivutio vya kihistoria nchini Tanzania. Ingawa maeneo haya yana vivutio vingi vya kihistoria, kuna uwekezaji mdogo sana katika maeneo hayo. Hii ni fursa nzuri sana ya kuwekeza katika maeneo haya kwani yana hazina kubwa ya vitu vya kale kama vile majengo na maeneo ya kihistoria ambayo yanaweza kuwavutia watalii wa ndani na wa nje. Kwa hiyo, ni muhimu kuendeleza vivutio vya kihistoria katika maeneo yote vinakopatikana. Uendelezaji huu ujikite katika utambuzi au ubainishi, ukarabati, uhifadhi, ukuzaji na utangazaji wa vivutio hivi. Kwa kufanya hivyo, tutaongeza mvuto wa vivutio hivyo na kuongeza si idadi ya wawekezaji tu bali na idadi ya watalii (wa ndani na nje) watakaovitembelea. Aidha, vitawapa fursa ya kujifunza na kufahamu historia na utamaduni wa Tanzania. Pia, kuendeleza vivutio hivyo kunaweza kuchochea ukuaji wa uchumi wa maeneo ya vijijini na kuboresha maisha ya jamii zinazopakana na vivutio hivyo.

**Kazi ya kufanya 3.5**

Tumia vyanzo mbalimbali vya taarifa ikiwamo mitandao kufafanua fursa za kipekee za uwekezaji zinazopatikana katika miji mikongwe ya Zanzibar na Bagamoyo.

**Zoezi 3.2**

1. Je, unafikiri ni changamoto gani zinawakabili wajasiriamali katika kuanzisha biashara zinazohusiana na vivutio vya kihistoria na urithi wa Tanzania?
2. Ni kwa namna gani serikali inaweza kuwasaidia wajasiriamali kuchangia uhifadhi na uendelezaji wa vivutio vya kihistoria na urithi wa Tanzania?
3. Kuna umuhimu gani wa kuwekeza katika utalii wa kihistoria katika maeneo ya vijijini?
4. Eleza jinsi utalii wa urithi wa kihistoria unavyoweza kusaidia katika kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na mataifa mengine.

### Uwekezaji katika vivutio vya kihistoria na urithi

Uwekezaji katika vivutio vya kihistoria na urithi ni muhimu si kwa serikali na watu binafsi tu bali ni muhimu pia katika utunzaji na uendelezaji wa vivutio hivyo. Ili vivutio hivyo vilete tija stahiki, basi ni muhimu kutumia njia na mbinu sahihi za uwekezaji kama zinavyojadiliwa hapa chini.

**Njia shirikishi**

Matumizi ya njia shirikishi ni aina ya uwekezaji ambapo serikali inaihusisha jamii katika uanzishaji, utunzaji na usimamizi wa vivutio vya kihistoria na urithi. Njia hii ni muhimu kwani huwafanya wananchi wajione kuwa na wao ni wamiliki halali wa vivutio hivyo kwa sababu wanahusishwa kuwekeza katika vivutio hivyo vya kihistoria na urithi. Aidha, wananchi wanaweza kushirikishwa katika kutengeneza vitu vya kihistoria kama vile nguo, mikufu, vinyago, shanga na vinginevyo. Katika aina hii ya uwekezaji, wananchi wanashirikishwa katika kubuni, kuandaa na kuwekeza katika vivutio vya utalii na urithi wetu. Mifano ya

FOR ONLINE READING ONLY

uwekezaji wa sanaa-bunifu kama uchongaji wa vinyago na uchoraji wa picha upo katika maeneo mbalimbali ya Dar es salaam, Bagamoyo, Zanzibar na Arusha.

**Ubia kati ya serikali na sekta binafsi**

Njia nyingine ni ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi katika kuwekeza kwenye vivutio vya kihistoria na urithi wa kiutamaduni. Hii inasaidia katika kupata mitaji na rasilimali kwa maendeleo endelevu. Serikali inajenga mazingira bora ya uwekezaji kama vile ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, na viwanja vya ndege, kutunga sera nzuri na kuwavutia wawekezaji katika maeneo yenye urithi wa kiutamaduni kama vile majengo, mabaki ya kihistoria, ngoma za asili na mavazi. Wakati huo huo serikali inaweka mazingira mazuri kwa watu binafsi kuwekeza mitaji yao katika maeneo hayo kwa kuwa ni rafiki na yanavutia kiuwekezaji. Mbinu hii imekuwa na faida kubwa Zanzibar, hasa pale Mji Mkongwe na Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam na maeneo mengi mkoani Arusha.

**Njia za kidigiti na vyombo vya habari**

Maendeleo ya sayansi na teknolojia yamewezesha uwekezaji katika vivutio vya kihistoria na urithi kwa njia ya kidigiti na vyombo vya habari. Uwekezaji unafanyika kupitia matangazo katika vyombo mbalimbali vya habari na kidigiti kama runinga, redio, tovuti, wavuti, na mitandao mbalimbali ya kijamii kama vile *Facebook*, *Instagram* na mifumo mingine ya kidigiti. Matangazo hayo yanasaidia kuongeza uelewa wa utajiri wa vivutio husika na kuchangia kuongeza ujio wa wageni nchini na kuwafanya raia wa Tanzania wapende kutembelea vivutio vya kiutamaduni. Mfano mzuri ni filamu ya *Royal Tour* iliyochezwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, na waigizaji wengine, ambayo imeonesha maeneo mengi yenye vivutio vya kihistoria na urithi kama vile Mji Mkongwe, Zanzibar; Mji wa Dar es Salaam; Bagamoyo na sehemu nyingine nyingi. Kwa mujibu wa taarifa mbalimbali za serikali, hasa Wizara ya Utalii na Maliasili, filamu hii imesaidia kuongeza idadi ya watalii wanaokuja nchini kwa kiasi kikubwa.

Kwa ujumla, mbinu za uwekezaji katika vivutio vya kihistoria na urithi ni chachu ya mafanikio ya uwekezaji wenye tija. Kipekee, serikali ya Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa uwekezaji katika vivutio vya kihistoria na urithi unavutia. Pamoja na mambo mengine, serikali imekuwa ikifanya yafuatayo:

**Kuandaa wataalamu**

Miaka michache baada ya uhuru Tanzania iliamua kuwekeza katika kuwaandaa wataalamu watakaofanya kazi katika sekta ya utalii. Uwekezaji huu ulijikita katika kuanzisha vyuo vya utalii ili kuzalisha wataalamu kwa lengo la kuimarisha sekta ya utalii. Chuo cha mwanzo kuanzishwa ni Chuo cha Taifa cha Utalii, kilichoanzishwa mwaka 1969 mjini Dar es Salaam. Kwa sasa chuo hiki kina matawi katika mkoa wa Arusha na Mwanza. Tangu mwanzo chuo hiki kilijikita katika eneo la utalii kwa ujumla. Baadaye, utalii wa utamaduni ulipoanza kupata umaarufu na kuwavutia watalii wengi, kozi kuhusu utalii wa

FOR ONLINE READING ONLY

utamaduni (kihistoria na urithi) zilianzishwa katika vyuo vya elimu ya juu kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika Idara za Historia na Akiolojia na Taaluma za Urithi, Chuo Kikuu cha Dodoma katika Idara ya Historia na Chuo Kikuu cha Iringa. Msisitizo katika vyuo hivi umekuwa katika utayarishaji wa wataalamu katika eneo la utalii wa utamaduni, eneo ambalo halikupewa kipaumbele wa kutosha hapo mwanzo. Kukosa kipaumbele hukokulibabisha uchache wa wataalamu katika maeneo ya vivutio vya kihistoria na urithi. Hivyo, vyuo hivi sasa vimezalisha na vinaendelea kuzalisha wataalamu wengi kwenye eneo la historia na urithi.

### Uboreshaji wa miundombinu

Serikali imejitahidi pia katika uwekezaji wa miundombinu kama vile viwanja vya ndege, barabara, maegesho, na huduma za umeme ambayo ni muhimu katika kurahisisha usafiri na kuifanya iwe na mvuto kwa wageni. Hii ni pamoja na kuboresha miundombinu ya usafiri kuelekea katika maeneo yenye vivutio vya kiutamaduni, mathalani, miundombinu kama vile reli, barabara na viwanja vya ndege vinavyohudumia eneo husika. Serikali imeendelea kufungua milango ya uwekezaji kwa kujenga barabara zinazounganisha maeneo ya utalii na urithi kama vile barabara ya Makuyuni kupitia Karatu kuingia geti la Ngorongoro. Barabara hii imechangia sana katika kuongeza idadi ya watalii kufika maeneo ya Karatu na Ngorongoro ambako utalii wa utadamuni umeshamiri. Pia, serikali kupitia Wizara ya Michezo na Utamaduni na Wizara ya Maliasili na Utalii imekuwa ikishirikiana na watu binafsi kuandaa na kuendeleza shughuli za utalii na utamaduni. Matukio maalum kama vile maonesho ya kiutamaduni, maadhimisho ya kihistoria au semina za elimu yameongeza ufahamu na kuongeza idadi ya wageni wanaovutiwa na vivutio hivyo. Matukio haya yamechangia katika kutoa fursa za kipekee kwa wageni kujifunza na kushiriki katika utamaduni na historia ya eneo husika. Vilevile, matukio haya yamesaidia kuwafanya watu wawekeze kwenye biashara ya hoteli, migahawa, usafiri na biashara zingine kama za nguo, urembo na vitu vingine katika maeneo husika.

### Ujenzi na utunzaji wa vivutio vya kihistoria na urithi

Serikali imejenga na kuendesha Makumbusho ya Taifa ambayo yanasimamia makumbusho mbalimbali ya umma hapa nchini. Pamoja na mambo mengine, makumbusho yana jukumu la kuuhifadhi, kuuonesha, kuulinda na kuendeleza urithi na historia ya Tanzania. Makumbusho hayo ni kama Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni, Dar es Salaam; Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam; Makumbusho ya Azimio la Arusha yaliyopo Arusha; Makumbusho ya Nyerere, Butiama-Mara; Makumbusho ya Maji Maji, Songea na makumbusho mengine. Wakati huo huo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pia imeanzisha Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale yaliyoundwa mwaka 2010. Idara hii ilianzishwa kwa lengo la kuyahifadhi, kuyalinda na kuyaendeleza majengo na maeneo ya kihistoria ya Unguja na Pemba. Idara hii ina majukumu mahususi yafuatayo:

(a) **Kuyahifadhi, kuyalinda na**

FOR ONLINE READING ONLY

kuyaendeleza majengo na maeneo ya kihistoria ya Unguja na Pemba;

(b) Kuendesha tafiti za kihistoria na akiolojia;

(c) Kuvumbua na kuyatambua maeneo mapya ya kihistoria;

(d) Kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kutunza historia ya nchi;

(e) Kuhifadhi kumbukumbu za historia na utamaduni wa Zanzibar kwa njia ya maonesho;

(f) Kutangaza maeneo ya kihistoria na makumbusho ndani na nje ya Zanzibar;

(g) Kusimamia sheria na sera za Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale;

(h) Kuhakikisha rasilimali za historia na urithi wa utamaduni zinatumiwa ipasavyo; na

(i) Kushirikiana na taasisi nyingine za kitaifa na kimataifa katika nyanja mbalimbali za urithi wa utamaduni.

Moja ya makumbusho maarufu Zanzibar ni Makumbusho ya Jumba la Ajabu (*Beit al Ajaib*) na Kasiri la Sultan (*House of Wonders and Palace Museum*) ambapo inatunza na kuonesha utamaduni na usanifu wa Wazanzibar, Waarabu, Waingereza na hata Wareno. Aidha, serikali imewekeza katika kuhifadhi na kuendeleza majengo na maeneo mengi ya kihistoria na yenye urithi wa kiutamaduni. Hii imesaidia katika utunzaji endelevu wa vituo vya urithi wa utamaduni na kukusanya mapato, zikiwamo pesa za kigeni. Mfano wa majengo hayo hapa nchini ni Ngome Kongwe, Jumba la Ajabu (*Beit al Ajaib*) na soko la watumwa yaliyopo Zanzibar. Maeneo mengine ni kama vile makanisa ya kale, mabaki ya makaburi na misikiti ya Kaole yaliyopo Bagamoyo na Msikiti wa kale Kilwa Kisiwani, Husuni ndogo na Husuni kubwa na jengo la *Caravan Serai* lililopo Bagamoyo. Kielelezo 3.2 kinaonesha jengo la *Caravan Serai* lililotumiwa na waarabu katika kipindi cha biashara ya utumwa.



**Kielelezo 3.2**: Jengo la *Caravan Serai*

FOR ONLINE READING ONLY

Hali kadhalika, serikali ilianzisha juhudi za uhifadhi wa vivutio vya kihistoria. Kisheria, historia ya uhifadhi wa malikale inaanzia mwaka 1937 ilipoanzishwa Sheria ya Uhifadhi wa Majengo ya Kihistoria. Mwaka huo pia yalianzishwa Makumbusho ya Kumbukumbu ya Mfalme George V. Idara ya Mambo ya Kale nayo ilianzishwa rasmi mwaka 1957. Wakati huo Idara ilijihusisha zaidi na kuzitafuta na kuziorodhesha sehemu zilizokuwa na kumbukumbu za kihistoria, hususani sehemu ya mwambao wa Tanzania. Mwaka 1962 yalitokea mabadiliko mawili muhimu katika sekta ya urithi wa utamaduni. Kwanza iliundwa wizara ya kushughulikia masuala haya ambayo iliitwa Wizara ya Utamaduni na Vijana na pili, Makumbusho ya Kumbukumbu ya Mfalme George V yalibadilishwa na kuitwa Makumbusho ya Taifa. Miaka miwili baadaye, yaani 1964, ilipitishwa Sheria ya Mambo ya Kale Cap. 330. Sheria hii ilifanyiwa marekebisho makubwa mara ya mwisho mwaka 1979 na ndiyo inayoongoza shughuli zote za utafiti, uhifadhi, utunzaji na uendeshaji wa malikale hapa nchini Tanzania hadi leo.

Katika kipindi hiki chote, sekta ya malikale imepata mafanikio mengi. Licha ya kuimarisha utafiti, serikali kwa kushirikiana na jumuiya ya kimataifa imefanikiwa kuratibu na kuhifadhi maeneo mbalimbali ya kihistoria. Pia, imeendelea kukarabati baadhi ya majengo ya kihistoria kama vile maboma ya Wajerumani ya Mikindani, mkoani Mtwara na Mahenge mkoani Morogoro; Hospitali ya Ocean Road, Dar es Salaam na baadhi ya majengo ya kihistoria kama vile Jengo la Ikulu, Dar es Salaam na majengo yaliyopo katika mji wa Bagamoyo.

Maeneo mengine yaliyohifadhiwa ni pamoja na eneo la Bonde la Oldupai mkoani Arusha na sehemu yenye visukuku vya nyayo Laetoli, michoro ya miambani wilayani Kondoa-Irangi na Singida Vijijini, na Mapango ya Amboni mkoani Tanga. Idara pia imefanikiwa kuandikisha magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara kwenye orodha ya urithi wa utamaduni wa dunia chini ya mpango wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO). Aidha, imeanzisha makumbusho vituoni Kaole, Oldupai, Ujiji, na Kalenga. Vilevile, vituo vya kumbukumbu na taarifa vimeanzishwa katika baadhi ya maeneo kama vile Isimila, Kondoa na Bagamoyo.

**Kazi ya kufanya 3.6**

Andaa mpangokazi wa kuhamasisha uwekezaji katika vivutio vya kihistoria na urithi.

### Nafasi ya historia na urithi katika ushirikiano na biashara za kimataifa

Ushirikiano na biashara za kimataifa vimekuwa vikiathiriwa au kujengwa na nguvu ya tamaduni na historia. Historia na tamaduni zimeathiri jamii, sera, uchumi wa nchi na hata utambulisho wa mtu mmoja mmoja. Kwa hiyo, historia na utamaduni au urithi vina nguvu katika uhusiano wa kimataifa kwani ndivyo vinaongoza jinsi nchi na wananchi wanavyoiona na kuielewa dunia. Pia, historia ina mchango mkubwa katika namna nchi zinavyoshirikiana na nchi nyingine duniani. Aidha, ina mchango mkubwa katika uhusiano wa kimataifa

FOR ONLINE READING ONLY

katika nyanja zote, yaani utamaduni, siasa na uchumi. Kwa ujumla, historia na urithi wa Tanzania vimekuwa nguzo muhimu katika kujenga ushirikiano na kukuza biashara za kimataifa.

Historia na urithi wa kiutamaduni vina mchango mkubwa sana katika kujenga na kuendeleza uhusiano kati ya nchi na nchi. Kwa mfano, historia ya ukoloni imeacha urithi ambao umekuwa msingi mkubwa wa kuanzishwa kwa uhusiano na kukuza biashara ya kimataifa baina ya waliokuwa wakoloni na waliokuwa watawaliwa. Hii iko wazi katika uhusiano kati ya Tanzania na mataifa mengine kama vile Uingereza. Mara baada ya ukoloni, Uingereza iliunda chombo kiitwacho Jumuiya ya Madola kilichojumuisha mataifa yaliyowahi kutawaliwa na Uingereza. Kupitia chombo hicho Tanzania imefanikiwa kujenga uhusiano na kukuza biashara na nchi ya Uingereza na hata mataifa mengine wanachama. Kupitia jumuiya hii, Tanzania imeendelea kujenga, si uhusiano wa kibiashara tu bali uhusiano wa kimichezo pia. Kila baada ya miaka miwili nchi yetu inashiriki katika michezo mbalimbali kama vile mbio, ngumi na michezo mingine. Katika michezo hii Tanzania inakutana na mataifa 56 tofauti. Ingawa watu wengine wanaona uhusiano huo kati ya Uingereza na Tanzania ni ukoloni mamboleo, bado hii inaonesha nguvu ya historia katika kujenga na kukuza uhusiano wa kimataifa. Kutokana na uhusiano kati ya Tanzania na Uingereza, Uingereza imekuwa miongoni mwa nchi zinazowekeza nchini Tanzania na zinazofanya biashara na Tanzania kwa kiasi kikubwa.

Aidha, historia na urithi wa ukoloni katika nchi ya Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla vina nafasi kubwa katika kuujenga uhusiano wa kikanda na kuikuza biashara katika upande huu wa Afrika. Kenya, Tanzania na Uganda zimekuwa na historia ya muda mrefu katika ushirikiano wa kikanda wakati wa ukoloni. Kabla ya kuwa na ushirikiano baada ya uhuru, yaani mwaka 1967, nchi zilianza ushirikiano wakati zote zikiwa chini ya utawala wa Waingereza. Wakati huo ulianzishwa Umoja wa Forodha kati ya Kenya na Uganda (*the Customs Union between Kenya and Uganda*) mwaka 1917 na Tanganyika alijiunga nao mwaka 1927. Mwaka 1948 walianzisha Kamisheni ya Afrika Mashariki. Ushirikiano huu wa mwanzo ndio ulikuwa msingi wa uanzishwaji wa Umoja wa Afrika Mashariki (EAC) mwaka 1967 ukijumuisha nchi zilezile tatu, na baadaye kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mpya iliyoundwa 1967. Jumuiya hii ilivunjika mwaka 1977. Jumuiya mpya iliundwa tena mwaka 1999 na mataifa hayo matatu na baadaye jumuiya hiyo ilipanuka zaidi na kuongeza nchi wanachama wapya ambao ni Rwanda, Burundi, Sudani ya Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Somalia. Historia na urithi wa ushirikiano wa wakati wa ukoloni ndivyo vyanzo vya umoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kupitia umoja huu, uhusiano wa kikanda umejengwa ukiishirikisha Tanzania na kukuza biashara baina ya Tanzania na nchi wanachama.

Pia, Tanzania imekuwa na historia na urithi wa kiutamaduni uliotokana na historia ya uhusiano wa kibiashara wa muda mrefu

FOR ONLINE READING ONLY

sana na mataifa mbalimbali hapa duniani. Kwa mfano, Tanzania imekuwa na uhusiano mzuri wa kibiashara na Waarabu wa Oman. Ingawa uhusiano wao umekuwepo hata kabla ya karne ya 19, uhusiano huu uliongezeka sana katika karne ya 19, hasa katika eneo la Pwani ya Tanzania hususani Zanzibar. Historia hii imekuwa msingi mkubwa katika kujenga uhusiano na kukuza biashara ya kimaitaifa baina ya nchi hizi mbili.

Sanjari na hayo, uhusiano wa Tanzania na India umejengeka pia katika historia na urithi uliotokana na uhusiano uliokuwapo hata kabla ya kipindi cha ukoloni. Uhusiano huu ulianza pale biashara baina ya wakazi wa pwani ya Tanzania na wenzao kutoka India ulipoanza kurekodiwa rasmi. Mtandao huu wa biashara ulipokua, uhusiano baina ya watu wa pwani ya Tanzania na India ulizidi kuimarika. Ulianza kama uhusiano baina ya watu wenyewe kwa wenyewe na baadaye ikawa rahisi kwa serikali za nchi hizi mbili kushirikiana hata baada ya uhuru wao. Hii ilisababisha kufunguliwa kwa balozi katika nchi hizi mbili, Tanganyika na India mwaka 1961 na 1962 mtawalia. Jambo hilo liliimarisha uhusiano wa nchi hizi mbili ambapo wengi waliuita uhusiano huo kuwa uhusiano wa kidugu. Kwa hiyo, historia hii imefanikisha kujenga uhusiano na kukuza biashara baina ya nchi hizi mbili. Mwaka 2023, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliitaja India kuwa nchi ya nne kwa kufanya biashara kwa wingi na Tanzania. Biashara ya nchi hizi mbili ilikadiriwa kuwa na thamani ya dola za kimarekani bilioni 6.5 kwa mwaka 2022/23. Vilevile, India ni kati ya vyanzo vitano (5) vikubwa vya mitaji ya uwekezaji inayoingia Tanzania.

Nafasi ya historia na urithi katika kujenga ushirikiano na kukuza biashara ya kimataifa imejidhihirisha katika harakati na mapambano ya ukombozi wa Afrika, hasa zile zilizotokea kusini mwa bara la Afrika. Tanzania imeshiriki katika mapambano ya kuzikomboa nchi za ukanda huo kama vile Namibia, Msumbiji, Zimbabwe, Afrika Kusini na Angola. Wapigania uhuru wa nchi hizo walikaribishwa na kuruhusiwa kuendesha shughuli zao za kupigania uhuru katika ardhi ya Tanzania. Pamoja na hayo, Tanzania iliwasaidia katika mafunzo ya kijeshi na kujenga kambi zao za kijeshi maeneo mbalimbali hapa nchini kama vile Mazimbu - Morogoro, Nachingwea - Lindi, Tunduru - Ruvuma na Kongwa - Dodoma. Maeneo haya hivi sasa yamebaki kuwa maeneo muhimu ya kihistoria na urithi wa ukombozi kusini mwa Afrika. Historia na urithi huu una nafasi kubwa katika kujenga uhusiano na kukuza biashara baina ya Tanzania na nchi hizi tulizozisaidia kupata uhuru wao. Kwa mfano, Afrika Kusini ni miongoni mwa nchi zilizowekeza uwekezaji mkubwa hapa Tanzania. Hii inachangia katika kukua kwa biashara baina ya nchi hizi mbili.

Vilevile, amani na utulivu vimekuwa nguzo na urithi muhimu katika kujenga uhusiano na kukuza biashara za kimataifa katika nchi yetu. Amani na utulivu ni urithi uliotokana na historia yetu, si zawadi au tukio la siku moja. Mara baada ya kupata uhuru, Tanzania, chini ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, imepita katika vipindi tofauti vya mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Hata

FOR ONLINE READING ONLY

hivyo, katika wakati wote huo siasa zake zimeendelea kufanikiwa kujenga amani na utulivu katika nchini. Hii imekuwa tunu na urithi murua uliopelekea Tanzania kujenga uhusiano na kukuza biashara na mataifa mengi hapa duniani. Wakati mataifa mengine yakiwa wahanga wa vita, ukabila na vurugu, Tanzania iligeuka kuwa "kisiwa cha utulivu na amani." Tanzania ilifanikiwa kujenga utaifa kwa kudhoofisha ukabila. Kwa mfano, mwaka 1962 serikali ilizuia utawala wa jadi ili kudhoofisha ukabila. Pia, serikali ilitumia shule na jeshi la kujenga taifa kuwachanganya watu wa makabila tofauti na kufanikiwa kutengeneza taifa moja lenye utilivu na amani.

Utulivu huu ulijenga upendo, umoja, ukarimu na mshikamano wa Watanzania unaojulikana duniani kote. Amani na utulivu wa Tanzania umekuwa msingi muhimu katika kujenga ushirikiano na kukuza biashara ya kimataifa kwa kiwango kikubwa. Hali ya utulivu wa kisiasa na kijamii imekuwa kichocheo cha kuwavutia wawekezaji. Wawekezaji wakiwa na uhakika wa usalama na mazingira rafiki ya biashara zao, wako tayari kuwekeza mitaji katika biashara mbalimbali. Hali hii hukuza uwekezaji na teknolojia na kuchochea ukuaji wa uchumi na biashara ya kimataifa.

Fauka ya hayo, utulivu huimarisha uaminifu katika uhusiano wa kimataifa. Mataifa na makampuni ya kimataifa huwa na imani na nchi zenye utulivu. Aidha, utulivu husaidia kuanzisha ushirikiano wa kibiashara na kuwezesha ukukuzaji wa biashara ya kimataifa. Vilevile, utulivu wa kisiasa na kijamii huwa na athari chanya katika tasnia ya utalii. Watalii hupendelea kuzuru nchi ambazo zina amani na usalama. Hali hii huchochea ukuaji wa tasnia ya utalii na kukuza na kuimarisha biashara ya kimataifa ya utalii. Tangu tupate uhuru, Tanzania imesifika duniani kote kuwa nchi yenye amani na utulivu duniani.

**Kazi ya kufanya 3.7**

**Fanya utafiti kuhusu ufanisi wa matamasha ya kiutamaduni kama fursa ya kihistoria na urithi katika kukuza ushirikiano wa kibiashara kimataifa.**

FOR ONLINE READING ONLY

**Zoezi 3.3**

1. Kuna umuhimu gani wa uwekezaji katika kuhifadhi na kuendeleza vivutio vya kihistoria na urithi wa Tanzania katika kuwavutia watalii na kukuza biashara za kimataifa?
2. Athari zipi zinazoweza kutokea iwapo Tanzania itashindwa kusimamia vyema vivutio vya kihistoria na urithi wake?
3. Kwa kutumia mifano halisi, eleza jinsi usimamizi thabiti wa vivutio vya kihistoria na urithi vinavyochangia katika ukuaji wa uchumi na biashara nchini Tanzania.
4. Je, unafikiri ni kwa namna gani hatua zilizochukuliwa na serikali ya Tanzania katika kuboresha mazingira ya vivutio vya kihistoria na urithi zinawavutia wawekezaji wa kimataifa?

### Vitendo vya kimaadili vinavyokuza fursa zitokanazo na urithi

**Kama ilivyoelezwa hapo awali, urithi ni chanzo muhimu katika kutengeneza fursa kwa maendeleo ya taifa na watu binafsi. Pamoja na hayo, ili urithi utengeneze fursa endelevu ni lazima kuwe na vitendo vya kimaadili vinavyoambatana na urithi. Kwa hiyo, vitendo vya kimaadili ni muhimu sana katika kukuza fursa zitokanazo na urithi. Baadhi ya vitendo vya kimaadili vinavyoweza kuchangia katika kujenga fursa zitokanazo na urithi ni hivi vifuatavyo:**

#### Uadilifu

**Dhana ya uadilifu inahusisha tabia ya uaminifu kwa watu, mtu mwenyewe, taasisi, na nchi au jamii. Mtu mwadilifu anafuata kanuni za maadili hata kama haonekani kwa watu. Uadilifu ni hali na ni tabia pia ya mtu au jamii. Uadilifu ni jambo muhimu katika kukuza na kuendeleza fursa za urithi. Ili kuhakikisha kwamba rasilimali za urithi zinatumika ipasavyo, Tanzania imekuwa ikiweka mkazo katika tabia ya uadilifu kwenye masuala ya kusimamia mali zetu za urithi. Pamoja na mambo mengine, imekuwa ikiheshimu haki miliki, kuzuia na kupambana na rushwa, na kuzingatia miongozo na taratibu za kifedha. Serikali imeendelea kuhimiza tabia ya uadilifu katika matumizi ya urithi wa taifa ili kuhakikisha kwamba fursa zinazopatikana katika urithi zinakuwa na manufaa kwa wote. Katika kutekeleza majukumu ya usimamizi wa rasilimali za kihistoria na urithi, serikali iliweka mkazo zaidi katika usimamizi wa sheria na miongozo mbalimbali iliyowekwa. Hii ni pamoja na utoaji wa leseni, utoaji wa vibali kwa ajili ya shughuli za uendelezaji na ulinzi wa maeneo yenye rasilimali za urithi pamoja na adhabu kwa ajili ya ukiukwaji wa sheria.**

#### Kuheshimu fursa za urithi

**Kuwa na dhamira thabiti ya kuheshimu na kuendeleza fursa za urithi ni suala lenye manufaa makubwa katika kukuza maendeleo endelevu ya jamii. Dhamira hii thabiti iliwafanya Watanzania waone umuhimu wa uadilifu na kuzuia vitendo vya rushwa kwenye urithi wetu katika kuhifadhi, kulinda na kutunza rasilimali za urithi kwa ajili ya vizazi vijavyo. Serikali iliweka bayana kuwa ni jukumu la kila Mtanzania kuweka mazingira bora ya kuhifadhi urithi ambayo yanajumuisha uhifadhi wa mazingira na kuendeleza njia za utalii endelevu zinazozingatia masilahi ya jamii na taifa kwa ujumla. Serikali na wadau mbalimbali waliendelea kuwa na dhamira thabiti ya kuheshimu na kuthamini utamaduni na desturi za jamii zinazohusiana na urithi huu wenye manufaa kwa taifa na vizazi vijavyo. Kwa hiyo, jamii zimekuwa zikijenga msingi imara wa utambulisho wao na kudumisha uhusiano wao na mazingira yao. Aidha, serikali pamoja na wadau wengine wa utalii nao wameendelea kuheshimu na kuzitumia fursa za urithi wetu zilizopo katika maeneo mbalimbali. Hali hii imeendelea kuinua mapato ya serikali na mwananchi mmoja mmoja, hususani wale wanaoishi katika maeneo yanyozunguka vivutio hivyo vya urithi.**

#### Kuheshimu na kutii sheria

**Watu, kampuni na taasisi zinazoshughulika na urithi hulazimika kuzingatia sheria za**



FOR ONLINE READING ONLY

kitaifa na kimataifa kuhusu matumizi na utunzaji wa urithi. Hii ni pamoja na sheria za uhifadhi wa mazingira, sheria za utalii, sheria za kuzuia na kupambana na rushwa, kanuni zinazosimamia maadili pamoja na kanuni za utunzaji wa urithi wa kitamaduni. Kwa mfano, kampuni za utalii zinapaswa kufuata sheria za uhifadhi wa mazingira na sheria za kupambana na rushwa ili kuepuka uharibifu wa aina zote wa urithi na kutokujiingiza kwenye vitendo vya rushwa vilivyokatazwa na sheria. Hii inaweza kujumuisha kudhibiti idadi ya watalii, kutumia njia za kudumu za utalii, na kutoa elimu kuhusu uhifadhi wa urithi. Katika utunzaji wa urithi wa kiutamaduni, ni muhimu kufuata kanuni za kimataifa kama vile mkataba wa UNESCO kuhusu hifadhi ya urithi wa dunia.

Vilevile, mara baada ya uhuru, serikali ya Tanzania ilitunga sheria ya uhifadhi wa urithi wa kiutamaduni mwaka 1964 inayojulikana kama Sheria ya Mambokale Tanzania (The Antiquities Act of Tanzania) ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 1979 na 1985. Hii ni sheria inayoweka msisitizo katika kusimamia, kulinda na kuhifadhi rasilimali za urithi wa kiutamaduni zinazohamishika na zisizohamishika. Kwa kufuata sheria na kanuni hizi, jamii inalinda urithi wao na haki ya kufaidika na rasilimali hizo kwa njia inayoheshimu maadili na maslahi ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Hii inasaidia kuleta maendeleo endelevu na kuhifadhi urithi kwa ustawi wa jamii na mazingira.

**Kazi ya kufanya 3.8**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya taarifa, ikiwamo mtandao, chambua vitendo vingine vya kimaadili vinavyoweza kukuza fursa zitokanazo na urithi.

**Zoezi 3.4**

1. Je, unafikiri ni kwa namna gani tabia ya uadilifu inachangia kuhifadhi na kusimamia rasilimali za urithi?
2. Eleza namna mapambano dhidi ya rushwa yanavyosaidia kusimamia rasilimali za urithi.
3. Eleza umuhimu wa uwazi na uwajibikaji katika utunzaji na usimamizi wa urithi wa taifa.
4. Kwa nini kuwa na dhamira thabiti ya kuheshimu fursa za urithi ni muhimu katika maendeleo endelevu ya jamii?
5. Toa mifano ya fursa za kiuchumi zinazotokana na kuhifadhi urithi wa kiutamaduni.
6. Je, unafikiri ni kwa namna gani elimu inaweza kusaidia katika kukuza fursa zinazotokana na urithi wa taifa?

## Vitendo visivyo vya kimaadili vinavyodumaza fursa zitokanazo na urithi

Fursa za urithi huathiriwa na ukiukwaji wa maadili. Ukiukwaji huu husababishwa na vitendo visivyo vya kimaadili ambavyo ni pamoja na:

### Rushwa na ufisadi

Rushwa ni zao la mmomonyoko wa kimaadili unaomsukuma mtu kufanya jambo lenye sura ya uhalifu. Pia, rushwa ni matumizi mabaya ya nafasi ya uongozi kwa manufaa binafsi au ya kikundi

FOR ONLINE READING ONLY

fulani, bila kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Rushwa na ufisadi ni miongoni mwa vitendo vya ukiukaji wa maadili unaosababisha upotevu wa rasilimali za umma. Pia, vitendo hivyo huchangia kudhoofisha ustawi wa uchumi na kukwamisha fursa za maendeleo endelevu ya nchi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba rushwa na ufisadi huweza kuchangia uharibifu wa mazingira na rasilimali za urithi (kama ubomoaji ovyo wa malikali) kutokana na ukiukaji wa mikataba ya uwekezaji. Vilevile, rushwa huchangia kupungua kwa pato la taifa kutokana na ubadhirifu. Serikali ya Tanzania imeendelea kujikita katika mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa na ufisadi kama mbinu ya kurekebisha ukiukwaji wa maadili katika sekta ya utalii na uhifadhi wa malikale ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma na kulinda maadili ya taifa. Hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa ikiwemo kutokomeza na kudhibiti mifumo ya rushwa na udanganyifu mahali pa kazi. Hatua hizo zimeendelea kukuza sekta ya utalii na mchango wake kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

**Uharibifu wa mazingira**

Uharibifu wa mazingira ni mojawapo ya vitendo visivyo vya kimaadili vinavyoathiri fursa zinazotokana na urithi katika maeneo mbalimbali nchini Tanzania. Uharibifu wa mazingira huathiri hata malikale (turathi). Kwa mfano, ulimaji na ukataji wa miti ovyo karibu na malikale husababisha uharibifu wa majengo, makaburi na mabaki mengine ya rasilimali malikale. Uharibifu huo unaweza kusababisha mmomonyoko wa udongo ambao husababisha madhara zaidi kwa malikale. Vilevile, uharibifu wa mazingira una athari hasi katika urithi asilia. Mathalani, ukataji ovyo wa miti huwa na athari hasi kama vile kupungua kwa maliasili za asilia kama misitu, wanyamapori, na vyanzo vya maji. Hii inaweza kusababisha kupungua kwa fursa za utalii wa utamaduni na asili, ambao ni chanzo kikubwa cha mapato kwa jamii zinazoishi karibu na maeneo hayo. Kwa hiyo, ni vema kila mmoja wetu achukue hatua za kuhifadhi mazingira ili kulinda fursa zinazotokana na urithi wetu.

**Uvunjifu wa sheria za kimataifa za uhifadhi**

Kuvunja sheria za kimataifa za uhifadhi za urithi ni kitendo hatari kwa taifa na kinaweza kusababisha madhara ya kupoteza rasilimali za kiutamaduni na asilia, kushuka kwa hadhi ya taifa kimataifa, na kuwekewa vikwazo vya kimataifa. Hii ni kutokana na ukiukaji wa mikataba, makubaliano au kanuni za kulinda urithi. Kwa mfano, *International Charter for the Conservation and Restoration of Monuments and Sites* ilitungwa mwaka 1964 katika mji wa Venice, Italia na kupitishwa na kuridhiwa na *International Council on Monuments and Sites (ICOMOS)* mwaka 1965. Mkataba huu ulikataza na kuzuia uharibifu wa majengo, makaburi au aina yoyote ya malikale za kihistoria zenye umuhimu kwenye jamii husika. Kila nchi ilitakiwa kuuridhia na kuufuata mkataba huu katika kuhifadhi, kutumia na kulinda malikale. Kuna mikataba kuhusu mali asilia kama vile mkataba wa *Convention on International Trade in Endangered Species of Wild Fauna and Flora (CITES)*. Mkataba huu

FOR ONLINE READING ONLY

ni miongoni mwa mikataba inayokataza uvunaji haramu wa faru na tembo. Ukiukaji wa mkataba huu huhatarisha kuwapo kwa wanyamapori kwenye mazingira yao na kupoteza urithi wa asili kwa vizazi vijavyo na taifa. Kwa kuwa nchi yetu si kisiwa, ni muhimu kuhakikisha kuwa sheria za uhifadhi za kimataifa zinazingatiwa na kutekelezwa. Lengo kuu ni kulinda na kusimamia rasilimali za urithi wetu kwa kushirikiana na jumuiya za kimataifa. Ushirikiano huu wa uhifadhi utakuza fursa za urithi endelevu na kukomesha vitendo visivyo vya kimaadili vya uharibifu wa urithi wa taifa.

### Kuharibu miundombinu ya kihistoria

Utunzaji wa miundombinu ya kihistoria ni muhimu sana kwa manufaa ya taifa. Kuharibu miundombinu ya kihistoria ni mojawapo ya vitendo visivyo vya kimaadili ambavyo vinaweza kusababisha madhara makubwa kwa urithi wa taifa. Vitendo hivi vinaweza kujumuisha kubomoa majengo ya kihistoria, kuharibu maeneo ya kale au kufuta alama za historia ambazo ni sehemu muhimu ya utambulisho wa kitaifa. Madhara ya vitendo hivi ni pamoja na kupoteza uhusiano wetu na historia yetu, kuharibu utalii wa kiutamaduni, na kupunguza fursa za elimu na utafiti. Kwa hiyo, ni muhimu kuhifadhi miundombinu ya kihistoria ili kulinda na kukuza urithi wa taifa. Jambo hili linahitaji juhudi za pamoja kutoka serikalini, asasi za kiraia na jamii kwa ujumla ili kuhakikisha kwamba maeneo ya kihistoria yanahifadhiwa na kutunzwa kwa ajili ya vizazi vijavyo. Vitendo hivi visivyo vya kimaadili vimeandikwa vizuri na Idara ya Malikale Tanzania. Idara hiyo inataja vitendo hivyo kuwa ni: uharibifu na wizi unaohusisha kubomoa majengo ya kale ili kupata mawe kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kisasa, kubomoa majengo na makaburi ya kihistoria ili kupata nafasi ya ujenzi wa nyumba za kisasa, na kubadilisha sura na usanifu wa asili wa majengo ya kihistoria kwa kutumia teknolojia za kisasa na kupoteza uasili wake. Kitendo kingine ni uharibifu katika michoro ya miambani kwa kuandika au kuigiza picha ama maandiko kwa kutumia kalamu, mkaa, masizi ama chaki.

### Ukosefu wa uwajibikaji

Kukosekana kwa uwajibikaji ni mojawapo ya vitendo visivyo vya kimaadili ambavyo vinaweza kuathiri sana fursa za urithi wa taifa. Uwajibikaji unahusisha wajibu wa kufuata sheria, kanuni, na maadili katika kuhifadhi na kusimamia rasilimali za kiutamaduni. Kukosekana kwa uwajibikaji kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya rasilimali hizo, uharibifu wa mazingira, na kupotea kwa urithi wa taifa. Serikali au taasisi za umma zinaweza kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kuhifadhi na kusimamia rasilimali za kihistoria na kiutamaduni kwa kukosa uwajibikaji, kama vile kukosa mipango ya kuzuia uharibifu wa maeneo yenye urithi wa utamaduni. Vilevile, kampuni ikikosa uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za kiutamaduni, kama vile uuzaji na ubomoaji holela wa majengo ya kale mijini ili kujenga majengo ya kisasa huharibu urithi wetu. Madhara yake ni pamoja na kupotea kwa utamaduni na historia pamoja na kupungua kwa fursa zitokanazo na urithi.

FOR ONLINE READING ONLY

### Zoezi 3.5

1. Eleza hatua ambazo serikali inaweza kuchukua ili kuhakikisha uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za urithi wa kiutamaduni.
2. Pendekeza mbinu zinazoweza kutumika kuelimisha jamii jinsi ya kusimamia uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za kiutamaduni.
3. Eleza hatua ambazo jamii inaweza kuchukua katika kuyahifadhi mazingira na kuzitunza rasilimali za urithi.
4. Je, unafikiri ni kwa namna gani mapambano dhidi ya rushwa yanaweza kuongeza uwajibikaji na kuuepusha uharibifu wa mazingira?
5. Pendekeza mbinu za kushirikisha jamii na jumuiya za kimataifa katika kuzuia uvunjifu wa sheria za kimataifa za uhifadhi.
6. Kwa nini ni muhimu kwa serikali kuchukua hatua madhubuti za kuhifadhi rasilimali za kihistoria?

### Zoezi la marudio

1. Eleza jinsi shughuli za uhifadhi wa mazingira zinavyochangia katika kukuza fursa za urithi.
2. Kwa nini ni muhimu kuelimisha jamii kuhusu fursa zitokanazo na urithi?
3. Eleza jinsi elimu ya utalii katika vivutio vya kihistoria na urithi inavyoweza kuwahamasisha wanafunzi kuhifadhi na kuendeleza utamaduni na historia ya maeneo yao.
4. Ni kwa nini serikali inaweka msisitizo katika mapambano dhidi ya rushwa katika uendelezaji wa vivutio vya kihistoria na urithi wa Tanzania?
5. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ina mchango gani katika uboreshaji, utunzaji na uendelezaji wa vivutio vya kihistoria na urithi wa Tanzania?
6. Kwa mtazamo wako, eleza namna jamii inavyoweza kushirikishwa katika juhudi za kuhifadhi na kuendeleza vivutio vya kihistoria na urithi wa Tanzania?
7. Pendekeza mbinu mbalimbali za kukabiliana na vitendo visivyo vya kimaadili vinavyoziathiri fursa zitokanazo na urithi.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Nne

# Jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni

## Utangulizi

*Kabla ya ujio wa ukoloni, jamii za Kitanzania zilikuwa zimepiga hatua za maendeleo katika sekta mbalimbali. Katika sura hii, utajifunza vichocheo vya maendeleo katika jamii za Kitanzania na jinsi maadili ya jamii za Kitanzania yalivyoyachochea maendeleo hayo kabla ya ukoloni. Vilevile, utajifunza mifumo ya kuyasimamia maadili katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuthamini maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania yalivyochangia maendeleo ya jamii hizo kabla ya ukoloni. Pia, utakuwezesha kuyadumisha maadili ambayo yatachochea maendeleo yako na ya jamii kwa ujumla.*

**Fikiri**

**Maendeleo ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni.**

FOR ONLINE READING ONLY

### Maana ya maendeleo ya jamii

Maendeleo ya jamii ni mchakato wa kuongeza uzalishaji mali na uwezo wa binadamu kuboresha maisha yake. Maendeleo yanahusisha ongezeko la uwezo wa jamii kubadilisha uhusiano wake na jamii nyingine na kushiriki vyema katika mchakato wa mabadiliko. Pia, yanahusisha ongezeko la uwezo wa jamii kuhusisha sekta mbalimbali za uzalishaji mali, kujiongoza kwa amani na kuhimili mabadiliko. Kimsingi, maendeleo ya jamii hubainishwa kwa kuangalia uwezo wa jamii katika stadi na maarifa ya kuyakabili mazingira yake. Hivyo, tunapoangalia maendeleo ya jamii, inatupasa kuangalia kama jamii inaweza kubaini na kujipatia mahitaji yake na kuwa na ziada. Viashiria vya maendeleo ya jamii ni kama vile amani, umoja, kuvumiliana, kuhusishwa kwa wananchi wote katika kufanya maamuzi, utawala bora, usawa wa jinsia na ustahimilivu wa kiuchumi.

### Vichocheo vya maendeleo katika jamii za Kitanzania

Maendeleo ya jamii za Kitanzania kabla ya ujio wa ukoloni yalichochewa na sababu mbalimbali za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni.

**Vichocheo vya maendeleo ya kijamii**

Maendeleo katika jamii za asili za Kitanzania yalichochewa na sababu mbalimbali za kijamii ikiwamo elimu ya jadi na huduma za afya zilizokuwa zinatolewa.

*Elimu*

Elimu ya jadi ilikuwa kichocheo kimojawapo kikubwa katika kufanikisha shughuli za maendeleo ya jamii husika. Elimu ilijikita katika kuwajengea watoto umahiri wa maarifa, stadi, maadili, utamaduni na utaratibu wa maisha yao ya kila siku. Walifundishwa kazi mbalimbali na mikakati madhubuti ya kujikinga na kujilinda dhidi ya majanga katika mazingira yao. Pia, watoto walifundishwa jinsi ya kukabiliana na njaa, magonjwa, mafuriko, tetemeko la ardhi pamoja na maadui wa jamii na mali zao.

Katika mfumo wa elimu ya jadi, ilikuwa vigumu kuitenganisha elimu ya jadi na kazi. Hii ni kutokana na elimu kutolewa kwa vitendo zaidi na nadharia kidogo sana. Elimu ya jadi katika jamii nyingi za Kitanzania ilitolewa kwa njia ya jando na unyago. Kwa mfano, jamii za Wazaramo, Wakurya, Wayao, Wamasai, Wadigo, Wapare, Wanyaturu na jamii za visiwani Zanzibar zilitumia jando na unyago kuwafundisha watoto wao mafunzo ya amali mbalimbali za jamii zinazohusika. Pia, elimu ilitolewa kulingana na mazingira husika. Katika jando, mafunzo yaliwaelekeza watoto wa kiume kujiamini, kufanya kazi kwa bidii, kuzingatia maadili, kuwaheshimu watu wengine, kuwa shupavu, uwajibikaji na majukumu ya kuilinda familia, ukoo na kabila. Hivyo, mafunzo ya jando yaliwawezesha watoto wa kiume kuwa baba bora kwa kuwajibika na kufanya kazi kwa bidii. jambo ambalo lilichochea maendeleo katika jamii iliyohusika.

Kwa upande wa watoto wa kike, elimu ilitolewa kupitia mafunzo ya unyago. Katika unyago ilitolewa elimu iliyowaandaa watoto wa kike kuwa tayari kuyakabili majukumu ya kiutu uzima. Baada ya mafunzo ya unyago kwa mtoto wa kike, mafunzo hayo yalilenga kumwandaa kuwa tayari kuolewa. Katika unyago alifundishwa namna bora ya kutunza nyumba yake, jinsi ya kumtunza mume, usafi wa nyumba, na malezi ya watoto ili kujenga usikivu ndani ya ndoa na familia. Vilevile, watoto wa kike walifundishwa kuandaa chakula cha familia, utii, kupenda ndugu na kufanya kazi kwa bidii. Mafunzo ya unyago yalitolewa na watu maalumu katika jamii kutokana na umuhimu na uzoefu wao katika kuwafunda watoto wa kike waliojulikana kwa jina la Kungwi.

Kwa kawaida muda wa mafunzo ya elimu ya jando na unyago ulitofautiana kulingana na jamii husika. Kwa wastani, elimu ya unyago ilidumu kwa miezi mitatu, ambapo mafunzo haya yalifanyika mara baada ya kipindi cha mavuno. Ama kwa hakika, jando na unyago ilikuwa shule ya malezi bora kwa vijana ambao walikuwa wanahama kutoka rika ya watoto kuwa watu wazima. Walifundishwa mambo mbalimbali kama vile ulinzi, ukakamavu na ushujaa, tabia ambazo zilikuwa muhimu kwa ajili ya maendeleo yao kama watu wazima na maendeleo ya jamii kwa ujumla. Jambo la kuzingatiwa katika hili

FOR ONLINE READING ONLY

ni kwamba elimu ya jadi ilifundisha malezi bora na kuwandaa vijana kujitegemea na kuthamini utu na kazi. Malengo ya elimu ya jadi ilikuwa kutengeneza jamii bora na kuongeza ubunifu katika sekta mbalimbali za uzalishaji mali, na hatimaye kuchochea maendeleo katika jamii iliyohusika.

*Huduma za afya*

Huduma za afya zilizokuwa zinatolewa zilikuwa kichocheo kikubwa sana katika kuzifanikisha shughuli za maendeleo za jamii husika. Tangu zamani ilikuwapo mifumo mbalimbali ya utoaji wa huduma za afya kutegemeana na jamii husika. Hakukuwa na hospitali au vituo vya afya vikubwa kama sasa lakini hii haimaanishi huduma za afya hazikuwapo. Kila jamii ilikuwa na mifumo yake ya utoaji wa tiba na njia zake za kufanya vipimo. Wataalamu wa afya wa jamii hizi walikuwa wabobezi katika tiba. Kwa sababu hawakuwa na vifaa vya kisasa lakini walitoa huduma bora na kwa wakati. Baadhi yao walifanya ramli ili kuangalia dalili za ugonjwa. Walifananisha dalili za mgonjwa na magonjwa wengine na hatimaye kugundua tiba ya tatizo. Hii ilikuwa na changamoto pale magonjwa tofauti yalipokuwa na dalili za kufanana.

Jamii mbalimbali zilikuwa na taratibu zao za utabibu. Tiba hizi ziliwafanya watu katika jamii zao wawe na afya njema na kushiriki katika shughuli za maendeleo. Kwa mfano, jamii za Wahehe, Wabena, Wakinga, Wapangwa na Wawanji kutoka mikoa ya Iringa na Njombe walikuwa na utaratibu wao wa utabibu. Kabla Mgonjwa hajatibiwa, alifanyiwa ramli kama ilivyo leo hii mgonjwa anapoenda maabara kupima ili kujua ukubwa wa tatizo la ugonjwa alionao. Baada ya kujua ugonjwa, mgonjwa alipatiwa dawa. Kwa wale wenye ugonjwa mkubwa walipelekwa hatua za juu kwa ajili ya huduma zaidi. Kwa mfano, katika jamii ya Wabena wagonjwa walipelekwa kwenye msitu wa Nyumbanitu kwa matibabu zaidi.

Kwa upande wa jamii za makabila ya Wasukuma, Wakerewe, Wahaya na Waha, ambayo yanapatikana Ukanda wa Maziwa Makuu katika mikoa ya Mwanza, Kagera na Kigoma, walikuwa wabobezi wa kuunga mifupa iliyovunjika. Maarifa haya ya kuunga mifupa ya binadamu iliyovunjika yapo katika jamii nyingi hadi sasa. Kuwapo kwa wataalamu wa tiba asili kumesaidia sana jamii kupata tiba mbadala za magonjwa mbalimbali. Pia, wapo wakunga wa jadi ambao hupatikana katika kila jamii na kazi yao kubwa ni kutoa huduma za afya kwa kina mama na watoto wadogo. Wataalamu hawa walikuwa msaada kwa mama wajawazito, hasa katika kipindi cha kujifungua. Maendeleo katika huduma za afya yaliziwezesha jamii hizi kuwa na afya bora na kuwafanya wanajamii washiriki vyema katika shughuli za maendeleo, hususani uzalishaji mali.

Aidha, jamii za makabila ya Wairaqw na Wadatoga, kama ilivyokuwa katika jamii nyingine, zilikuwa zimepiga hatua kubwa katika maendeleo ya elimu, afya na utamaduni kabla ya ukoloni. Kwa upande wa afya, Wairaqw walibobea sana katika tiba za matumbo na kuunga mifupa. Kwa sasa jamii hizi hutibu watu wao kwa dawa za asili. Kwa mfano, dawa ya tumbo ya mti unaojulikana kama *qarengei* ni tiba nzuri sana. Mtu aliyevunjika mguu alitibiwa

FOR ONLINE READING ONLY

kwa kupewa supu iliyokuwa ya mifupa na iliyochanganywa na magome ya miti ili kumfanya mgonjwa asikinai kula supu hiyo. Magome hayo yalitolewa kwenye mti maarufu kwa jina la *Mandoqasi.*

Mpaka hapo tunaona kwamba jamii za Kitanzania zilikwishapiga hatua kubwa katika huduma za afya ambayo ilisaidia kuchochea maendeleo kwenye sekta nyingine. Watanzania pia walikuwa wataalamu katika kutoa huduma za mama na mtoto wakati wa kujifungua. Kulikuwa na wataalamu waliobobea katika dawa mbalimbali za asili zenye kutibu magonjwa anuai. Historia inatuambia kuwa jamii za Kitanzania kwa ujumla zilikuwa na uwezo mkubwa sana wa tiba asilia. Hii inajidhihirisha wazi hadi leo ambapo kuna magonjwa yanayoshindikana kutibika hospitalini lakini yanawezekana kwa waganga wa tiba za asili. Tiba za asili si za kupuuzwa hata kidogo kwani wahenga walinena, "Mtu chake na jasiri haachi asili". Watanzania lazima wajivunie asili yao kwa kuenzi tiba za asili. Kuna haja ya wazee kuwarithisha watoto wao ujuzi wa aina mbalimbali za mitishamba inayotumika kama tiba kwa binadamu na wanyama wa kufugwa.

**Kazi ya kufanya 4.1**

Fanya uchunguzi kupitia vyanzo mbalimbali kuhusu jamii za asili za makabila mengine ambayo hayajaelezewa, kisha eleza jinsi elimu na huduma za afya zilivyochochea maendeleo ya jamii hizo kabla ya ukoloni.

**Zoezi 4.1**

1. Linganisha mchango wa elimu ya jadi na elimu ya sasa katika kuchochea maendeleo ya jamii.
2. Eleza ni kwa namna gani elimu za jando na unyago zinaweza kutumika katika mazingira ya sasa ili kuchangia maendeleo ya kijamii.
3. Jadili mambo yanayoweza kuigwa na kuendelezwa kutoka katika elimu ya jadi.
4. Eleza ni kwa namna gani baadhi ya tiba za jadi zinaweza kutumika katika kutoa huduma za afya katika jamii za sasa za Kitanzania.
5. Buni mikakati ya kuboresha huduma za afya kupitia tiba asilia.

## Vichocheo vya maendeleo ya kiuchumi

Jamii za Kitanzania zilikuwa na maendeleo chanya ya kiuchumi hata kabla ya ukoloni. Kiuchumi maendeleo hayo yalichochewa na matumizi ya chuma na kutumia maarifa ya sayansi na teknolojia ya wakati huo.

### *Matumizi ya zana za chuma*

Maendeleo katika jamii za Kiafrika kabla ya ukoloni yalipata msukumo mkubwa zaidi mara baada ya kuibuka kwa matumizi ya zana za chuma katika kipindi cha miaka 1000 katika zama za sasa. Katika kipindi hiki chuma ilikuwa bidhaa muhimu sana kutokana na faida zifuatazo: kuimarika kwa shughuli za viwanda, kilimo na ufugaji, kuanza kwa makazi ya kudumu, mgawanyo wa kazi, kuimarika kwa zana za ulinzi na uzalishaji pamoja na kuanza kwa

FOR ONLINE READING ONLY

biashara. Hivyo, kabla ya ukoloni, shughuli za kiuchumi zilichochea kwa kiwango kikubwa maendeleo ya kijamii kwa kuwa kulikuwa na mabadiliko makubwa ya uzalishaji kutokana na matumizi ya zana za chuma katika shughuli za kiuchumi. Miongoni mwa jamii zilizofua chuma zilikuwa Wapare, Wafipa, Wakinga na Wazinza. Pamoja na kufua chuma, jamii hizi zilitengeneza zana za chuma.

*Kuibuka kwa maarifa ya sayansi na teknolojia*

Kuibuka kwa sayansi na teknolojia kulisababisha maendeleo katika shughuli mbalimbali za uzalishaji kama vile kukua kwa viwanda vya asili vya mikono vilivyoanzishwa katika jamii za Kitanzania. Viwanda hivyo vilikuwa hasa katika fani ya ususi, ufinyanzi, uhunzi, uchimbaji wa madini na ufuaji wa chuma. Vilevile, viwanda vya kutengeneza zana za kilimo na bidhaa zitokanazo na kilimo na ufugaji vilitegemea zaidi upatikanaji wa malighafi katika eneo linalohusika. Katika hali hiyo, viwanda vilichochea maendeleo ya uchumi na uzalishaji wa bidhaa. Kukua kwa teknolojia kulisababisha pia kukua kwa sekta nyingine. Kwa mfano, matumizi ya zana za chuma katika kilimo kama vile majembe, mundu, mashoka na mapanga kulisaidia kuongezeka kwa uzalishaji katika kilimo. Hatimaye, kukawa na ongezeko la chakula ambalo lilileta ongezeko la watu na jamii yenye afya bora. Uzuri wa viwanda hivi ni kwamba vilishabihiana na kilichozalishwa na jamii husika. Viwanda viliziwezesha jamii kuwa na shughuli za kufanya na kupata mahitaji ya lazima, na hatimaye kuleta maendeleo katika jamii zilizohusika.

*Maendeleo kwenye shughuli za kilimo*

Kilimo kilikuwa ndiyo shughuli kuu ya uchumi miongoni mwa jamii nyingi za Tanganyika na Zanzibar kabla ya ukoloni. Kilimo katika kipindi hiki kilishamiri zaidi katika jamii zilizokuwa na matumizi ya teknolojia ya chuma tayari pamoja na maeneo yaliyokuwa na hali nzuri ya hewa na udongo wenye rutuba. Wakati huo, jamii ambazo hazikuwa na mvua za kutosha na udongo wenye rutuba zilifanya kilimo cha kuhamahama, kwa mfano, Wayao, Wasukuma, Wamwera na Wanyamwezi. Jamii ambazo zilikuwa na uhakika wa kuwa na mvua kwa kipindi kirefu cha mwaka na kuwa na ardhi yenye rutuba ziliendesha kilimo cha kudumu cha mazao ya muda mrefu kama vile ndizi. Kilimo hiki kiliwalazimu kuwa na makazi ya kudumu. Maeneo hayo ni kama Kagera na maeneo ya kuzunguka ziwa Viktoria, maeneo ya milima ya Kilimanjaro, Meru, Usambara na maeneo ya Tukuyu huko Mbeya. Vilevile, kulikuwa na jamii ambazo zilikuwa zinafuga na kulima kwa pamoja, mathalani, Wairaqw, Wachaga na Wameru. Maendeleo ya kilimo yalifikiwa baada ya jamii kutumia zana bora za uzalishaji. Maendeleo ya kilimo yalikuwa na matokeo mbalimbali katika jamii hizo kama vile kuwawezesha watu kupata chakula cha kutosha na kuifanya jamii izaliane na kuongezeka. Pia, yalichochea kukua kwa biashara kwani kilimo kilisababisha kufanyika kwa biashara ya mazao kati ya jamii moja na nyingine. Vilevile, biashara iliimarisha uhusiano baina ya jamii hizo.

FOR ONLINE READING ONLY

*Ufugaji*

Ufugaji ulichochea sana maendeleo ya Watanzania kabla ya ukoloni. Katika jamii za Kitanzania, ufugaji ulianza sambamba na maendeleo ya kilimo. Hatua hii ilianza mara tu baada ya jamii kuishi pamoja na kuanza kufuga wanyama tofauti tofauti. Aina ya ufugaji ulitegemea zaidi mazingira na hali ya hewa ya eneo husika kama vile mvua na hali ya joto. Mara nyingi wafugaji waliishi katika maeneo ya mbuga na nyanda zenye uoto wa nyasi nyingi na kuwa na maji ya kutosha. Katika zama hizo ufugaji katika jamii za Kitanzania ulikuwa na umuhimu na ilikuwa njia kuu ya jamii mbalimbali kuishi. Jamii kama za Wamasai na Wadatoga ziliishi kwa kutegemea ufugaji tu, na ilikuwa fahari kuwa na mifugo mingi. Pia, kuna jamii kama za Wasukuma, Wanyamwezi, Wazinza, Wagogo na nyinginezo ambazo zilifuga pamoja na kulima. Ufugaji uliimarika katika maeneo yaliyokuwa na malisho mazuri na ulidorora katika maeneo yenye ukame. Ufugaji katika maeneo ya ukame ulikuwa wa kuhamahama. Mathalani, maeneo ya Wamasai na Wadatoga yaliyopo katika mkoa wa Arusha, Manyara na Mara yalikuwa na ukame na kuwafanya wawe wanahamahama kulingana na majira ya mwaka na upatikanaji wa nyasi na maji.

Ufugaji nao ulichochea maendeleo katika jamii za Kitanzania kwa kuwa uliwezesha jamii kupata chakula kitokanacho na mifugo na kusaidia vyema jamii kufanikisha shughuli zao mbalimbali kama zile za mila na desturi kama vile jando, unyago, harusi, misiba na kutawazwa kwa viongozi wa kijamii. Chakula kilichotokana na mifugo kilikuwa nyama, maziwa na samuli. Pia, mifugo ilizalisha mbolea ya samadi iliyosaidia kustawisha mazao, hasa kwa zile jamii zilizofuga na kulima. Kwa hiyo, mazao yaliongezeka na kupata chakula zaidi. Aidha, ngozi za mifugo zilitumika kutengenezea vitu na bidhaa kama nguo, ngao, vitanda, ngoma na vitu vingine vya muhimu. Hivyo, bidhaa hizo zilisaidia kukua kwa biashara baina ya jamii za Kitanzania. Vilevile, mifugo, hasa ng'ombe, ilihesabika kama alama ya utajiri na shughuli zote za jamii zilitegemea kuwapo kwake. Mathalani, ng'ombe walitumika katika kutoa mahari, matambiko, sherehe mbalimbali, na sehemu ya adhabu au faini kwa wale waliofanya makosa mbalimbali katika jamii.

*Biashara*

Biashara pia ilikuwa kichocheo kikubwa sana katika maendeleo ya Watanzania kabla ya ukoloni. Jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni zilianza kufanya biashara mara tu baada ya kuwa na makazi ya kudumu katika eneo moja na kujiingiza kwenye shughuli za uzalishaji mali kama kilimo, uvuvi, ufugaji na viwanda. Mwanzoni biashara iliendeshwa kwa njia ya kubadilishana bidhaa kati ya jamii moja na jamii nyingine. Vilevile, wakulima walilima mazao tofauti kulingana na hali ya hewa ya mazingira walimoishi. Ili kupata bidhaa nyingine kama nyama au bidhaa za chuma, walilazimika kubadilishana mazao na jamii za wafugaji au wahunzi (wayeyushaji vyuma). Biashara ilikuwa kichocheo muhimu katika maendeleo kwa jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni kwani hakukuwa na jamii ambayo ilikuwa inajitosheleza kwa kila kitu. Biashara ilirahisisha upatikanaji wa

FOR ONLINE READING ONLY

bidhaa muhimu zilizowawezesha wanajamii kukidhi mahitaji yao ya chakula. Isitoshe, biashara ilisaidia pia katika kujenga mahusiano mema kati ya jamii moja na nyingine. Hali hii ilisaidia sana kuleta amani ambayo ni kigezo kikubwa sana cha maendeleo ya uchumi kwani bila amani shughuli zote za uchumi zingekufa. Mwisho, biashara ilisababisha kukua kwa miji katika jamii za Kitanzania. Vituo vya kubadilishia bidhaa viliendelea na baadaye kuwa miji. Hii ilisababishwa na kukutana pamoja kwa watu wengi kwa wakati mmoja. Hivyo, mahitaji ya vitu kama malazi, chakula, usimamizi, amani na utulivu yaliongezeka na kuvifanya vituo hivyo kuwa na maendeleo. Kwa njia hii, biashara ilisaidia kukua na kuimarika kwa zana za uzalishaji mali, kuongezeka kwa bidhaa, na kukua kwa kilimo, ufundi na sanaa kama vile uchongaji, uhunzi na ufinyanzi. Pia, biashara ilisababisha kuimarika kwa tawala na uongozi.

**Kazi ya kufanya 4.2**

Soma matini kutoka katika vyanzo mbalimbali vya taarifa halafu fafanua jinsi sayansi na teknolojia ilivyo muhimu kwa jamii katika kujiletea maendeleo.

**Vichocheo vya maendeleo ya kisiasa**

Maendeleo ya kisiasa katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni yalichochewa na sababu nyingi ikiwa ni pamoja na:

*Maisha ya pamoja*

Maendeleo ya kisiasa katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni yalianza kupamba moto baada ya watu wa aina ambalimbali kuishi pamoja. Maisha haya ya pamoja yalianza baada ya uvumbuzi wa moto na kuanza shughuli za kilimo, ufugaji na biashara. Kuishi huku kwa pamoja kulisababisha ushirikiano baina ya watu na wakati mwingine migongano na mifarakano katika koo na hata katika kabila husika. Hivyo, ili kupunguza migogoro na kutokuelewana ndani ya jamii, ilikuwa muhimu kuwa na uongozi ambao, pamoja na mambo mengine, ulikua na jukumu la kutatua migogoro kwa haki. Viongozi wa jadi walijulikana kwa majina ya vyeo vyao kama vile *Pazi* kwa Wazaramo, *Mangi* kwa Wachaga, *Omukama* kwa Wahaya, *Mtemi* kwa Wanyamwezi na Wasukuma, *Mtwa* kwa Wahehe na Wasangu na *Nkosi* kwa Wangoni. Wote hawa walikuwa na majukumu ya kulinda amani katika jamii kwa kutatua migogoro au mifarakano inayoweza kuhatarisha na kusambaratisha uhai wa jamii nzima.

*Mfumo wa uongozi wa ukoo*

Kisiasa, uongozi wa ukoo ulikuwa kichocheo kikubwa sana cha maendeleo. Uongozi huu ulitokana na familia kadhaa zenye undugu au zenye chimbuko moja. Katika ngazi ya ukoo, uongozi uliweka kanuni na taratibu za kuishi. Kwa mfano, kiongozi alisimamia mali zote za ukoo kama vile mashamba, mbuga, mifugo, na misitu. Pia, kiongozi wa ukoo alisimamia shughuli zote za utawala, sherehe za dini na kutatua migogoro miongoni mwa wanaukoo. Uongozi wa ukoo ulisimamia pia shughuli

FOR ONLINE READING ONLY

zote za ndoa katika ukoo. Mfumo huu wa uongozi ulichochea maendeleo ya jamii kupitia shughuli mbalimbali za uzalishaji mali kwani kiongozi wa ukoo ndiye alikuwa mwangalizi mkuu wa mali za jamii kama ardhi, misitu, na vyanzo vya maji. Viongozi walisimamia matumizi bora ya ardhi, walilinda vyanzo vya maji na walihakikisha usalama wa jamii yote kwa ujumla. Hata hivyo, usimamizi wa shughuli zote hizi za ukoo haukutoka kichwani mwa kiongozi mmoja. Kiongozi alikuwa hajiamulii tu cha kufanya bali alikuwa anasimamia sheria, mila na desturi za ukoo kwani alikuwa na washauri wake. Kuhusiana na masuala ya ndoa, alifuata sheria, kanuni, mila na desturi za ukoo. Kadhalika, katika masuala ya rasilimali za ukoo, alifuata, mila na desturi za umiliki wa rasilimali zilizowekwa na ukoo.

*Mfumo rika wa kiuongozi*

Matumizi ya mfumo wa uongozi wa rika ulileta maendeleo makubwa sana ya kisiasa katika jamii zilizokuwa zinatumia mfumo huu. Mgawanyo wa majukumu katika mfumo huu wa utawala uliegemea katika umri na jinsi. Utawala huu ulitumiwa na jamii za wafugaji kama vile Wamasai na Wadatoga na jamii nyingine ambazo hazikuwa za kifugaji kama Wanyakyusa na Wameru. Mathalani, katika jamii ya Wanyakyusa, mfumo huu ulizingatia umri ambapo watoto walio chini ya miaka 10 walifanya shughuli za kiuchumi kama kuchunga ng'ombe na kulima chini ya uangalizi wa wazazi. Walipofika umri wa ujana walikuwa wanaondoka na kwenda kuanzisha kijiji chao sehemu nyingine mbali na eneo walilokulia. Aidha, katika mfumo rika, kila rika lilikuwa na kazi maalumu katika mfumo wa uongozi. Muundo na wajibu wa kila rika ulitofautiana kulingana na jamii husika. Kwa mfano, rika la Morani katika jamii ya Wamasai lilikuwa ndiyo nguvukazi ya jamii. Miongoni mwa majukumu ya kundi hili ilikuwa kulinda mali, hasa mifugo na rasilimali nyingine za jamii, kuilinda jamii ya Kimasai dhidi ya maadui, kutafuta maji na malisho kwa ajili ya mifugo yao na kuongeza mifugo kwa kuvamia na kupora ng'ombe kwa jamii zingine kama Wasukuma na Wakurya. Rika la wazee lilikuwa na jukumu la kuongoza jamii kupitia kufanya uamuzi na kutatua migogoro. Wanawake walikuwa na jukumu kubwa la kuangalia familia na malezi ya watoto. Mfumo huu wa uongozi ulichochea maendeleo katika jamii hizo kwa kuwa kila mwanajamii alikuwa na majukumu yake; na hivyo, kuwezesha ongezeko la uzalishaji mali.

*Mfumo wa uongozi wa kitemi*

Kisiasa, kuibuka kwa mfumo wa uongozi wa kitemi katika karne ya 16 na 17 ilikuwa hatua kubwa sana ya maendeleo katika jamii husika. Jamii za Kitanzania ambazo zilitumia mfumo huu zilikuwa zile ambazo ziko katika maeneo ya Kaskazini Magharibi na Kusini Magharibi ya Tanzania. Maeneo haya waliishi zaidi watu wa jamii ya Wasukuma, Wakimbu na Wanyamwezi. Jamii hizi zilikuwa za wakulima pamoja na wafugaji ambao uongozi wao ulizingatia malimbikizo ya ziada ya mali. Viongozi katika jamii hizi waliitwa Watemi na walikuwa na majukumu muhimu sana katika jamii zao. Pamoja na kuwa watemi wengi walirithi uongozi kupitia wazazi

FOR ONLINE READING ONLY

wao, kulikuwa na taratibu za matambiko ambazo zilihusika kumthibitisha kiongozi. Hivyo, kiongozi alipatikana kwa urithi lakini urithi huo ulithibishwa na wazee wa ukoo. Viongozi waliwaomba mababu na mizimu ili kiongozi atakayepatikana awe na baraka kwa jamii. Kama mrithi akikataliwa na mizimu basi hawezi kuwa mtemi. Badhi ya shughuli za watemi zilikuwa kugawa mashamba, kuongoza shughuli za kufyeka mapori, kusimamia masuala yote ya kisiasa, kutatua migogoro iliyoibuka katika jamii pamoja na kugawa ardhi. Pia, watemi walisimamia masuala ya imani za jadi kama vile kutoa sadaka kwa mizimu na kusimamia miiko na desturi za ukoo. Aidha, watemi pia walikuwa na madaraka ya kukusanya kodi kutoka kwa wanajamii. Mfumo huu wa uongozi ulichochea maendeleo katika jamii kwa sababu ulidumisha na kulinda amani.

*Mfumo wa uongozi wa kidola*

Kisiasa, kuibuka kwa mfumo wa uongozi wa kitabaka ilikuwa hatua kubwa sana ya maendeleo. Kuanzia karne ya 11 jamii za Kitanzania zilianza kupata mabadiliko katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hii ilitokea zaidi katika jamii zilizokuwa zinajishughulisha na kilimo na zile zilizochanganya kilimo na ufugaji kuliko zile zilizojikita katika ufugaji tu. Kuanzia kipindi hiki jamii zilishuhudia kukua kwa jamii kisiasa. Mabadiliko haya yalisababisha kuongezeka kwa maingiliano baina ya watu wenye asili, lugha na tamaduni tofauti. Pia, kumiliki teknolojia ya chuma kulisababisha kukua kwa shughuli za kilimo na ufugaji. Shughuli hizi za kilimo zilisabibisha uzalishaji mkubwa wa chakula na ongezeko la watu na kusababisha kutokea kwa jamii kubwa zenye matabaka kijamii na kiuchumi. Haya matabaka yalisababisha kutokea kwa uongozi wa kisiasa wenye nguvu tofauti na ule wa koo. Aidha, matumizi ya chuma kilichotumika kutengeneza majembe, mapanga na mashoka ambayo yalitumika katika uzalishaji mali yalileta pia maendeleo. Uzalishaji kupitia zana hizo ulipoimarika matabaka yakazidi kuzuka katika jamii. Tabaka moja lenye nguvu lililotokea ni lile la wale waliomiliki ardhi au mifugo na tabaka jingine lisilo na nguvu lilikuwa la wale ambao hawamiliki chochote. Mahusiano kati ya matabaka haya mawili yalijulikana kama mahusiano ya kitabaka. Jamii ambazo msingi wake wa uhusiano wa uzalishaji mali uko katika umiliki wa ardhi huitwa jamii za kikabaila. Ukabaila ni itikadi au imani ambayo msingi wake mkubwa ni umiliki binafsi wa njia kuu za uzalishaji mali kama vile ardhi, viwanda, mifugo, taasisi za fedha, na biashara.

Waliokuwa wanamiliki njia kuu za uzalishaji mali walijulikana kama mabwana na wale ambao hawakuwa wanamiliki njia kuu za uzalishaji mali walijulikana kama watwana. Katika mfumo huu, madaraka ya uongozi yalikuwa mikononi mwa wenye mali, yaani mabwana. Mawazo ya matajiri ndiyo pia yalikuwa mawazo ya wana jamii. Kwa maneno mengine, mawazo na fikra za matajiri ndizo zilikuwa zinatawala. Mawazo ya watwana yalikuwa hayaheshimiki kwani yalikuwa yanadharauliwa. Kwa kuwa hawakuwa na mali, hawakusikilizwa. Isitoshe, katika mfumo huu wa kitabaka, viongozi walikuwa wale ambao walionekana wanatetea na

FOR ONLINE READING ONLY

kulinda maslahi ya matajiri. Kwa maneno mengine, uongozi ulitokana na tabaka la matajiri au washirika wao. Masikini au watwana walikuwa hawawezi kupata nafasi ya uongozi katika jamii zenye mfumo wa kitabaka.

Jamii za Kitanzania ambazo zilifuata mfumo huu zilipatikana katika sehemu za Kaskazini Magharibi mwa ziwa Viktoria kama vile Karagwe na mwambao wa Bahari ya Hindi pamoja na Zanzibar. Mfumo huu wa kitabaka katika maeneo ya pwani ulijulikana kama Umwinyi. Katika mfumo wa kimwinyi kulikuwa na tabaka la mamwinyi au mabwana waliokuwa wanamiliki njia kuu za uzalishaji na tabaka la watwana ambao hawakumiliki mali. Katika ukanda wa Magharibi wa ziwa Viktoria, mfumo huu wa kikabaila ulijulikana kwa jina la *Nyarubanja*. Huko Buha ambako ni Kigoma, Waha walikuwa na mfumo wa kikabaila ulioitwa *Ubugabire*. Tofauti na *Umwinyi* na *Nyarubanja*, *Ubugabire* uliegemea kwenye ng'ombe. Katika muktadha wa maendeleo, mifumo hii ya utawala ilikuwa hatua mojawapo ya maendeleo katika eneo la siasa ya jamii zetu za Kitanzania kabla ya ukoloni. Mifumo hii iliwawezesha watu katika jamii kuishi kwa kufuata mila na desturi za jamii husika, utaratibu ambao uliwasaidia watu kuishi kwa amani na usalama.

Kiutawala, mfumo wa uongozi wa kidola ni mfumo uliokuwa unaongoza watu kupitia wafalme au machifu ambao walikuwa wanarithi uongozi kutoka kwa wazazi wao. Viongozi hao walikuwa na mamlaka kamili na walikuwa na wawakilishi kuanzia ngazi ya chini hadi juu. Katika mfumo huu kulikuwa na matabaka yaliyojengeka kutokana na sababu mbalimbali. Kwa mfano, katika jamii za Karagwe mfumo wa *Nyarubanja* ulitokana na umiliki wa ardhi uliosababisha kujengeka kwa matabaka mawili. Tabaka moja lilimiliki ardhi na tabaka lingine halikumiliki kitu. Hivyo, uhusiano huu ulijulikana kuwa ni uhusiano wa kitabaka. Jamii ambazo msingi wake wa uhusiano wa uzalishaji mali uko katika umiliki wa ardhi ziliitwa jamii za kikabaila. Ukabaila ulikuwa mfumo wa uzalishaji ambao msingi mkuu wa uchumi wake ni umiliki wa ardhi. Jamii hizi zilikuwa na matabaka mawili, tabaka la wamiliki wa ardhi (mabwana) na pili ni tabaka la watu wasiomiliki ardhi (watwana).

Katika maeneo ya pwani na visiwa vya Zanzibar kulikuwa na mfumo wa *Umwinyi* ambao ulikuwa na matabaka ya kijamii ya walio na mali na wasio na mali. Walio na mali walijulikama kama mabwana na wasio na mali waliitwa watwana. Mamwinyi walimiliki ardhi na kuikodisha kwa watwana na kulipwa kwa njia mbalimbali kama vile riba, kufanyiwa kazi au pesa.

Kwenye mfumo wa kidola, viongozi walikuwa na mamlaka ya juu ya umiliki wa ardhi au mifugo au biashara iliyokuwa ikiendeshwa katika himaya zao. Mfumo wa kidola ulichochea maendeleo kwa njia mbalimbali kwani ardhi ilikuwa ndiyo msingi wa uzalishaji mali wa jamii. Aidha, kuongezeka kwa uzalishaji mali kulisababisha kukua kwa biashara na ongezeko la pato kwa serikali kupitia kodi.

FOR ONLINE READING ONLY

**Kazi ya kufanya 4.3**

Tafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali, kisha andika maelezo kwa kutumia mifano sahihi ni kwa namna gani mfumo wa kidola wa jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni ulifanana na mfumo wa sasa wa serikali.

**Vichocheo vya maendeleo ya kiutamaduni**

Vichocheo ni sababu au hali zilizopelekea kuwepo kwa maendeleo ya kiutamaduni katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. Maendeleo ni hali inayoashiria kuboreka kwa maisha ya binadamu na mazingira. Utamaduni, kwa upande wake, ni jumla ya mambo yote yaliyokubalika katika jamii ili kukidhi utashi na maendeleo ya watu wake. Kwa maneno mengine, utamaduni ni mtindo wa maisha ya watu katika jamii ambao unahusisha taratibu za kuendesha maisha. Kwa kifupi, utamaduni ni maisha ya watu wa jamii husika. Maisha ya watu yanajumuisha ujuzi, imani, sanaa, michezo, mavazi, sheria, mila na desturi ambazo zinamuongoza mtu katika maisha yake ndani ya jamii. Swali la kujiuliza hapa ni hili: Ni vitu gani vilichochea maendeleo ya kiutamaduni? Kwa maneno mengine, ni sababu zipi zilileta maendeleo ya kiutamaduni kwa jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni? Utamaduni wa Kitanzania kabla ya ukoloni ulikuwa unachochewa na maadili, ujuzi kulingana na mazingira, imani za dini, sanaa na mavazi.

*Maadili*

Maadili yana tabia moja ya muhimu na ya msingi. Kwa hulka yake, maadili lazima yasambazwe, yafundishwe na yaeleweke kwa mtu mmoja mmoja na kwa jamii nzima. Maadili yasiposambazwa katika jamii yanakuwa hayana umuhimu wowote kwani lengo kuu ni kuwafanya watu wayaishi na hatimaye kufanikisha maisha ya pamoja katika jamii. Kwa maneno mengine, maadili ni ya watu wote. Hakuna maadili ya mtu mmoja tu. Maadili yapo ili kuwezesha mahusiano yenye tija kati ya mtu na mtu, kati ya mtu na watu wengine katika jamii husika, na kati ya watu na mazingira.

Maadili yalirithishwa kwa kufundishwa katika ngazi ya familia. Ili kusambaza maadili kwa ufanisi mkubwa, mababu na mabibi wa zamani walitumia familia kutoa mafunzo ya maadili. Familia hizo hazikuhusisha baba, mama na watoto wao tu bali na ndugu na jamaa wengine walio hai, waliokufa, wanaotarajiwa kuzaliwa, na mazingira kwa ujumla. Hapa tunaona kwamba maadili ndiyo yalikuwa kichocheo cha familia pana. Kuibuka kwa familia hizo kulikuwa hatua ya maendeleo kwani familia ziliwawezesha watu kustahimili changamoto za maisha na hatimaye kuishi maisha bora zaidi kuliko yale waliyoishi kabla ya kuibuka kwa familia pana. Familia pana, pamoja na changamoto za usasa, ni sehemu ya utamaduni wetu kama Watanzania.

FOR ONLINE READING ONLY

Aidha, maadili yalirithishwa na kuenezwa kwa kutumia sanaa. Kwa kuwa wakati huo watu walikuwa hawajui kusoma na kuandika, vyombo pekee vilivyotumika kueneza ujumbe wenye maadili ni sanaa. Ili kufikisha ujumbe, wahenga walitunga nyimbo zinazohusiana na maadili ya hatua mbalimbali za maisha ya watu kama vile kuzaliwa, kuugua, kuoa, na kufa. Vilevile, walitunga nyimbo zinazohusiana na maadili ya shughuli za kilimo, ufugaji, uvuvi, na uwindaji. Kwa kifupi shughuli zote za maisha zilitungiwa nyimbo za maadili. Hii ina maana kwamba, bila kuwepo kwa maadili nyimbo, ngoma, simulizi za mdomo, methali, vitendawili, michoro, na sanaa nyingine zote zisingekuwa na maana wala umuhimu katika jamii. Hapa pia tunaona wazi kwamba maadili ndiyo yalipelekea kuibuka kwa aina mbalimbali za sanaa. Vilevile, kuibuka kwa sanaa hizo ilikuwa pia hatua ya maendeleo kwani hivi leo sanaa hizo ndizo zimekuwa miongoni mwa utambulisho wa utamaduni wetu pia.

Maadili pia yalikuwa kichocheo cha maendeleo kwani yaliwafanya wanajamii waheshimiane na kupendana. Hii iliwafanya wawe wamoja na wenye ushirikiano katika kila jambo kwenye jamii yao. Maadili yaliwafanya watu wapende kazi, jambo ambalo liliongeza hali ya kujibidiisha na kuongeza ufanisi wa kazi uliosababisha kuongeza uzalishaji na kipato kwa wanajamii. Ongezeko la kipato lilichochea moja kwa moja maendeleo ya jamii.

*Ujuzi kulingana na mazingira*

Jamii za Kitanzania zilikuwa na watu waliokuwa na ujuzi mbalimbali uliochangia katika maendeleo ya jamii hizo. Watu hao wenye ujuzi walitumia maarifa na uzoefu mkubwa katika kutekeleza majukumu yao kama vile ujenzi, ususi, uhunzi na mambo mengine mengi. Kwa mfano, watu hawa wenye ujuzi waliweza kujenga makazi au nyumba za kuishi kulingana na mazingira au hali ya hewa. Hali ya hewa ilichochea ujenzi wa nyumba ambazo hivi sasa ni utambulisho wa utamaduni wa jamii hizo. Kwa mfano, jamii zilizokuwa zinaishi katika maeneo yenye joto kama vile Singida na Dodoma zilijenga nyumba ambazo hazitunzi joto. Hivyo, walijenga zaidi kwa kutumia miti, udongo na nyasi. Jamii zilizoishi maeneo yenye mvua nyingi na baridi kama vile Moshi, baadhi ya maeneo ya Dodoma, Arusha, Iringa, Mbeya, Sumbawanga na Songea walijenga nyumba ambazo zinastahimili mvua na baridi kali. Ujenzi wa nyumba zinazoendana na hali ya hewa ilikuwa hatua muhimu sana ya maendeleo ya kiutamaduni. Maendeleo hayo yalizifanya jamiii hizo ziishi kwa raha mstarehe na kuwa tayari kwa shughuli zingine za uzalishaji mali. Vielelezo 4.1 na 4.2 vinaonesha nyumba za asili za kabila la Wahaya na Wagogo mtawalia.

FOR ONLINE READING ONLY



Kielelezo 4.1: *Nyumba za kabila la Wahaya*



Kielelezo 4.2: *Nyumba za kabila la Wagogo*

FOR ONLINE READING ONLY

*Imani za dini*

**Jamii za Kitanzania kabla ya kuja kwa dini za kigeni zilikuwa na imani zao ambazo siku hizi zinaitwa "Dini za Jadi". Msingi wa maadili ya dini za jadi ni utaratibu mzima wa maisha au kuishi. Hivyo, imani za jadi katika jamii zilizohusika, kwa njia moja au nyingine, kuwawezesha wanajamii kuthamini maisha na kutenda mambo mema ambayo pia yalichochea maendeleo. Imani za jadi zilisaidia katika kujenga umoja, upendo, amani, heshima na mshikamano kwa jamii nzima. Imani za jadi zilisaidia katika kuhimiza uwajibikaji na kumtaka kila mwanajamii afanye kazi za uzalishaji mali. Mila na desturi mbalimbali kama matambiko na miiko zilisadia katika kutengenezwa kwa sheria, taratibu na kanuni za kimaadili katika jamii husika. Kulikuwa na miiko na makatazo mbalimbali kama utunzaji wa mazingira na miiko ya kuzuia tabia mbaya kama uchoyo, wizi, uvivu na ubinafsi. Aidha, imani za dini zilitumika sambamba katika kutibu baadhi ya magonjwa kupitia matambiko sanjari na matumizi ya mitishamba. Hivyo, imani za jadi zilikuwa ndizo utaratibu mzima wa maisha na ilikuwa lazima kila mwanajamii afuate imani hizo. Vilevile, imani za jadi zilisaidia katika utunzaji wa mazingira**

na wanyama. Dawa za jadi pia zilitumika kukinga na kutibu magonjwa mbalimbali. Kwa hali hii, imani za jadi zilichangia kuhifadhi mazingira na kutoa tiba na kuzifanya jamii zenye afya bora ambayo na kushiriki vyema katika uzalishaji mali.

*Sanaa*

Sanaa kama vile ngoma, nyimbo, mashairi, tenzi, ngonjera, na michezo zilisaidia kueneza maadili na kuwahamasisha watu kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali. Kwa mfano, ngoma zilitumiwa katika sherehe za kijamii, ibada, na burudani na zilifundisha ushirikiano, nidhamu, na kufanya kazi kwa bidii. Jamii zilikuwa na ngoma mbalimbali ambazo zilikuwa zinahimiza kufanya kazi kwa bidii. Mathalani, Wasukuma walikuwa na ngoma ya *Gugobogobo*, Wangoni, ngoma ya *Lizombe*, Wasambaa, ngoma ya *Mdumange*, Wahehe, ngoma ya *Kiduo* na Wakinga ngoma ya Kivilila. Hivyo, pamoja na kuburudisha na kuelimisha, sanaa zilitumika kuwahamasisha wanajamii kushiriki ipasavyo kwenye shughuli za uzalishaji mali ambazo zilichochea maendeleo katika jamii kwa ujumla.

*Mavazi*

Jamii za Kitanzania zilibuni, zilitengeneza na kuvaa mavazi ya aina mbalimbali kulingana na mazingira na hali ya hewa ya maeneo walimoishi. Pamoja na mambo mangine, watu walivaa ili kujisitiri na kuficha sehemu za faragha za mwili, au kulingana na tukio na kazi fulani. Mavazi haya yalikuwa ya heshima na yaliendana na utamaduni wa jamii iliyohusika. Pia, mavazi katika jamii za Kitanzania yalibadilika kulingana na mazingira, tukio au kazi. Nguo zilitengenezwa kwa kutumia sufi, magome ya miti na ngozi za wanyama. Jamii zilizokuwa maarufu kwa utengenezaji wa nguo ni pamoja na Wafipa, Wahaya, Wanyakyusa na Waha. Nguo ziliwasaidia watu kukabiliana na hali ya hewa kama vile kujikinga dhidi ya baridi na kuwawezesha kuishi na kuwa na afya bora. Jamii hizi zilitengeneza nguo maalumu kwa viongozi (machifu) ili kuonesha alama ya mamlaka. Pia, kulikuwa na nguo za wanawake na wanaume. Afya bora iliyosababishwa na mavazi mazuri yanayoendana na hali ya hewa iliwawezesha wanajamii kushiriki ipasavyo kwenye shughuli za uzalishaji mali na ufanyaji wa biashara ya nguo na jamii nyingine, na hatimaye kuchangia maendeleo katika jamii hizo.

**Kazi ya kufanya 4.4**

Tafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali, kishaandika maelezo ya vichocheo vingine vya maendeleo ya kiutamaduni kabla ya ukoloni.

**Zoezi 4.2**

1. **Linganisha mifumo ya uongozi wa jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni na mifumo ya sasa ya uongozi nchini.**
2. **Jadili ni kwa namna gani mifumo ya kiuongozi iliyobuniwa na jamii za Kitanzania iliendana na shughuli za kiuchumi na kuchochea maendeleo katika jamii hizo.**
3. **Nini mchango wa utamaduni katika**

FOR ONLINE READING ONLY

kuleta maendeleo?

4. Tofautisha mchango wa imani za jadi kabla ya ukoloni na sasa katika kuchangia maendeleo ya jamii.
5. Eleza nafasi ya michezo katika kuchochea maendeleo ya jamii za sasa za Kitanzania.

## Jinsi maadili ya jamii za Kitanzania yalivyochochea maendeleo

Maadili ni miongozo inayotawala tabia na matendo ya mtu mmoja mmoja au jamii kwa ujumla. Ni miongozo au maelekezo ya kutenda matendo mema au kuwa na tabia njema. Maadili ya jamii za Kitanzania ni mengi na yamejengwa kupitia mila na desturi mbalimbali katika vipindi tofauti. Miongoni mwa mifano ya maadili ya jamii za Kitanzania ambayo yamekuwapo kutoka jamii za asili ni pamoja na: utu, undugu na upendo. kufanya kazi kwa bidii, heshima, ushirikiano, ukarimu, kusaidia wazee na wasiojiweza, malezi na makuzi bora kwa watoto, na kutii sheria. Kabla ya ukoloni, maadili yalichochea maendeleo ya kijamii katika jamii za Kitanzania. Maelezo kuhusu jinsi baadhi ya maadili yalivyochochea maendeleo ni haya yafuatayo:

### Utu, undugu na upendo

Utu ni hali ya kuthamini na kutambua kuwa mtu au watu wengine ni binadamu na wanastahili haki. Aidha, undugu na upendo ni hali ya kumpenda na kumchukulia binadamu mwenzako kama umezaliwa mtu uliyezaliwa naye katika familia moja. Utu, undugu na upendo ni tabia zinazowezesha jamii kujenga mshikamano, licha ya tofauti za utaifa, ukabila, rangi, mahali anapotoka mtu na hali ya uchumi ya mtu. Maadili ya utu, undugu na upendo yaliisaidia jamii kuishi kwa amani, kusaidiana na kuheshimiana. Utu, undugu na upendo vilisisitizwa na kuthaminiwa katika jamii kwa sababau maadili hayo yaliwasaidia pia watu kuishi na kufanya shughuli za uzalishaji mali kwa pamoja kama vile kilimo, uwindaji, ufugaji na urinaji asali. Kwa mfano, jamii za wawindaji kama Watindiga, Wasandawe na Wandorobo walishirikiana katika shughuli za uwindaji na mawindo yaliyopatikana yalitumiwa kwa pamoja. Vilevile, jamii zilizojihusisha na ufugaji na kilimo zilifanya shughuli mbalimbali kwa kushirikiana na kusaidiana kama matokeo ya kuthamini utu, undugu na upendo miongoni mwao. Ushirikiano huu miongoni mwa jamii za Kitanzania ndio uliokuwa chachu ya maendeleo. Bila kulinda maadili ya utu, undungu na upendo, ingekuwa vigumu kwa jamii za Kitanzania kupata maendeleo kabla ya ukoloni.

Maadili haya yalikuwa na mchango mkubwa katika kuleta maendeleo ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. Maadili haya yaliwawezesha wanajamii kuishi kwa kuthaminiana na kupendana, na hatimaye kuwawezesha kushirikiana katika shughuli mbalimbali za kijamii na uzalishaji mali. Aidha, maadili ya kuthamini utu, undugu na upendo uliwawezesha wanajamii kuwa wamoja na wenye kudumisha amani na mshikamano miongoni mwao.

### Umoja

Sheria na kanuni zilizoyajenga na kuyalinda maadili ya umoja zilichangia sana maendeleo ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. Umoja, ambao ni hali

FOR ONLINE READING ONLY

ya watu kukubaliana na kushirikiana kwa pamoja ili kutimiza lengo linalokusudiwa, ndio uliokuwa nguzo ya maendeleao ya jamii za Kitanzania. Ikumbukwe kwamba, jamii hizi ziliishi katika mazingira magumu kwani maradhi yalikuwa mengi, mazingira waliyokuwa wanaishi yalikuwa hatarishi pia kwani wanyama hatari walikuwa karibu. Vilevile, walikabiliwa na majanga ya asili kama vile matetemeko ya ardhi, maporomoko ya ardhi, mafuriko, upepo mkali, na moto ambayo yalitokea mara kwa mara. Pamoja na hali hiyo ngumu, bado mababu na mabibi zetu waliweza kuishi na kuturithisha maarifa tuliyo nayo sasa. Umoja ndio ilikuwa silaha yao. Walipotokea wanyama wakali wanaotishia maisha katika kijiji au ukoo, walitoka wote kwa pamoja kuwawinda wanyama hao hatarishi na kuwaua. Magonjwa yalipolipuka walishirikiana kutafuta suluhisho la mlipuko huo. Wenye utaalamu wa dawa walishirikiana kutafuta dawa, wapiga ramli nao walitafuta sababu za mlipuko, na wazee waliwashirikisha mizimu kujua namna ya kutoka katika mlipuko huo. Na majanga ya asili yalipotokea kila mmoja alishiriki kuwaokoa waathirika au kuwapatia msaada stahiki. Wenye chakula walitoa chakula na wenye dawa walitoa dawa. Isitoshe, kulikuwa na ushirikiano mkubwa sana katika matukio ya ugonjwa, misiba, harusi, jando, unyago, au mtoto kupewa jina. Haya yote yalikuwa matukio yaliyoigusa jamii nzima na kila mmoja alishiriki. Pamoja na hayo, watu walishirikiana katika kazi kama vile kilimo, uvuvi, uashi, na ufugaji. Kwa kushirikiana katika kazi hizi, waliweza kuzalisha rasilimali ambazo ziliwasaidia kuboresha maisha yao.

**Malezi bora kwa watoto**

Jamii za Kitanzania zilithamini maadili ya malezi na makuzi bora kwa watoto. Malezi yalitolewa kulingana na mila, desturi na maadili ya jamii zilizohusika. Malezi yalitolewa tangu mimba ilipotungwa, na mtoto alipozaliwa hadi alipofikisha umri wa kuvunja ungo au kubalehe na kutambulika kama mtu mzima. Malezi yalijikita katika kuwapatia watoto vyakula bora, tiba, elimu, miiko, maelekezo na miongozo ili kujenga tabia njema na kuwawezesha kuwa wanajamii wema, wanaojua wajibu wao na wenye bidii katika kazi. Kwa mfano, jamii zilizokuwa na elimu ya jando na unyago, walitumia mafunzo hayo kujenga malezi na makuzi bora kwa watoto.

Maadili ya malezi na makuzi bora kwa watoto yalikuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii za asili za Kitanzania. Kwanza, maadili haya yalikuwa chanzo cha kuandaa wanajamii wenye afya bora, maadili, na wenye kujua wajibu wao katika jamii. Maadili haya yalijenga kizazi bora ambacho kilikuwa tayari kupokea majukumu na kushiriki katika shughuli za jamii na uzalishaji mali ambazo zilileta maendeleo katika sekta mbalimbali. Pili, maadili haya yaliiwezesha jamii kuandaa nguvukazi muhimu kwa jamii. Kwa mfano, jamii zilizokuwa na mfumo wa rika kama Wamasai, rika la vijana au morani liliandaliwa kuwa nguvukazi na walinzi wa jamii. Walikuwa na majukumu ya kulinda mali, hasa mifugo, na rasilimali nyingine, kutafuta maji na malisho kwa ajili ya mifugo na kupeleleza maeneo jirani ili kujipatia malisho ya mifugo yao. Hivyo, maadili ya malezi na makuzi bora yaliiwezesha jamii kuwa na nguvukazi bora iliyoshiriki

FOR ONLINE READING ONLY

katika uzalishaji mali na ambayo ilichochea maendeleo ya jamii zilizohusika.

**Bidii ya kazi**

Kufanya kazi kwa bidii katika jamii nyingi za Kitanzania kabla ya ukoloni ilikuwa sehemu ya maadili muhimu. Kufanya kazi kwa bidii lilikuwa lengo la kuziwezesha familia au jamii kufanikisha uzalishaji wa chakula au bidhaa ili kukidhi mahitaji husika. Ili kujenga maadili ya kufanya kazi kwa bidii, ukakamavu, uhodari na ujasiri ulisisitizwa na uvivu na kudharau kazi vilikemewa vikali katika jamii zote. Kufanya kazi kwa bidii na kujituma kulichukuliwa kuwa ni heshima na fahari na ilikuwa ni msingi muhimu sana katika kuwawezesha wanajamii kuishi. Kwa mfano, katika jamii zilizojihusisha na kilimo, kila mwanajamii alihimizwa kufanya kazi kwa bidii ili kuiwezesha familia au jamii yake kukidhi mahitaji ya chakula.

Kufanya kazi kwa bidii kulichangia maendeleo ya jamii, hasa baada ya ugunduzi wa zana za chuma kwani kulisaidia kupatikana kwa chakula cha kutosha. Kama ilivyoelezwa hapo awali, maendeleo haya ya teknolojia ya chuma yalisababisha uanzishwaji wa makazi ya kudumu, kuwa na mgawanyo wa kazi ulioendelea, kuimarika kwa zana za ulinzi na uzalishaji pamoja na biashara. Maendeleo ya jamii yaliendana na umahiri wa matumizi sahihi ya zana za uzalishaji na kufanya kazi kwa bidii. Kadiri binadamu alivyoweza kuongeza bidii ya kazi na kumudu mazingira yake, ndivyo alivyozidi kupata maarifa mapya ya uzalishaji mali.

Kwa mfano, bidii ya kazi katika viwanda vya asili vya mikono vilivyoanzishwa katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni zilisababisha ongezeko la bidhaa za ususi, ufinyanzi, uhunzi, uchimbaji madini na ufuaji wa chuma. Katika hali hiyo, matumizi ya zana za chuma na bidii ya kazi katika viwanda vilisababisha kukua kwa uchumi na uzalishaji; na hatimaye, kuongeza maendeleo kwenye jamii za Kitanzania.

**Utii wa sheria**

Sheria ni mfumo wa kanuni na taratibu ambazo kwa kawaida hupaswa kutekelezwa na mtu mmoja mmoja na taasisi zilizoko kwenye jamii inayohusika. Mojawapo ya maadili muhimu ya jamii za Kitanzania ilikuwa utii wa sheria, kanuni na taratibu ambazo zilikuwa makatazo na miiko mbalimbali katika jamii. Kulikuwa na sheria au makatazo katika kila jamii ambayo iliwabidi wanajamii wayazingatie. Matokeo ya utii wa sheria yalikuwa kuwa na jamii iliyokuwa inafanya kazi kwa mujibu wa sheria, na kuwepo kwa amani na mshikamano, utatuzi wa migogoro pamoja na haki na usawa katika jamii. Kutii sheria lilikuwa jambo la muhimu sana katika kuleta maendeleo ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. Utii huo ulisaidia katika kujenga jamii iliyokuwa inaishi pamoja na kutumia rasilimali zake kwa usawa na kuepuka unyonyaji katika jamii hizo.

Kwa kufuata sheria, jamii zilikuwa salama na kujenga mazingira mazuri ya kufanya kazi na kuzalisha mali au bidhaa katika viwanda vya jadi. Pia, kutii sheria kuliimarisha utengamano na uongozi bora katika jamii. Wanajamii walipaswa kuelewa

FOR ONLINE READING ONLY

umuhimu wa kufuata sheria au makatazo na viongozi kuchukua hatua za kisheria pale mtu anapokiuka sheria au makatazo. Hii ilisaidia kujenga jamii yenye nidhamu, haki, na usawa kwa wote. Hivyo, utii wa sheria ulichochea maendeleo katika jamii za Kitanzania kwa kuwa ulisaidia kuleta amani na kuondoa uonevu baina ya wanajamii. Hii iliwawezesha watu kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli za uzalishaji mali na bidhaa. Kuwapo kwa amani na utengamano katika jamii kuliwawezesha wanajamii kushiriki vyema katika uzalishaji mali na kuchangia maendeleo ya jamii zilizohusika.

**Kazi ya kufanya 4.5**

Soma matini kutoka katika vyanzo mbalimbali vya taarifa, halafu eleza jinsi heshima na ushirikiano kama vipengele vya maadili vilivyosaidia kukuza maendeleo katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni.

**Changamoto za kimaadili katika kuleta maendeleo**

Pamoja na ukweli kuwa maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni yalichangia katika kuleta maendeleo, bado kulikuwa na changamoto za kimaadili. Baadhi ya changamoto hizo za kimaadili ni pamoja na:

(a) *Wizi*: Kama ilivyo katika jamii za sasa, katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni kulikuwa na watu ambao walikiuka maadili ya jamii zilizohusika. Kwa mfano, katika jamii za wafugaji, kulikuwa na wanajamii ambao walikuwa wanaiba mifugo kutoka katika jamii zingine. Hali hii ilidumaza maendeleo kwenye jamii zilizoibiwa mifugo. Changamoto hii ilishughulikiwa kwa wezi kupewa adhabu mbalimbali na jamii kama njia ya kuwarudisha kwenye maadili. Kwa mfano, katika jamii nyingi za Kitanzania watu au mtu aliyebobea kwenye wizi alifukuzwa kutoka kwenye kijiji au jamii yake na ilimlazimu kwenda sehemu nyingine asiyoijua kuendelea na maisha.

(b) *Uvivu na uzembe:* Katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni kulikuwa na baadhi ya watu ambao walikuwa wavivu na wasiofanya kazi kwa bidii. Watu hawa walihatarisha usalama wa familia, hasa kwa kusababisha ukosefu wa chakula na mahitaji mengine katika familia. Aidha, walidumaza maendeleo ya familia na jamii kwa kuwa hawakuwa na mazao au bidhaa za ziada ambazo zingeweza kubadilishwa au kuuzwa kwa jamii nyingine na kuleta maendeleo ya familia au jamii kwa ujumla. Kwa hiyo, jamii nyingi za Kitanzania hazikupenda wanajamii wavivu na wazembe kwani walikuwa kikwazo katika maendeleo ya jamii hizo. Hii ilikuwa changamoto mojawapo ya kimaadili iliyoenda kinyume na maadili ya kupenda na kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya maendeleo ya jamii.

(c) *Kuiga tabia au mila za jamii nyingine kiholela:* Kuwa na uhusiano na jamii zingine

FOR ONLINE READING ONLY

kulisababisha kuingiliwa na maadili kutoka katika jamii nyingine. Hali hii ilisababisha mwingiliano wa mila na desturi ambazo zilisababisha baadhi ya maadili ya jamii husika kuachwa au kutotekelezwa ipasavyo, mathalanimaadili ya dini za jadi. Hivyo, kuanza na kukua kwa biashara kati ya jamii za karibu na zile za mbali kulileta utamaduni mpya kama vile mavazi mapya, chakula na dini tofauti na kuathiri maadili ya jamii iliyohusika. Hii ilisababishwa na baadhi ya mila na desturi kutoka jamii nyingine kutoendana na mila na desturi za jamii iliyohusika nakusababisha mmomonyoko wa maadili.

(d) *Kukua kwa matabaka:* Kukua kwa maendeleo katika jamii, hasa zilizokuwa za mfumo wa kidola, kulisababisha kuibuka kwa tabaka la watu wasiofanya kazi (wale walionacho) na kuwategemea wale wasionacho kuzalisha kwa ajili yao. Mfumo wa uzalishaji mali katika jamii hizo ulikuwa wa kikabaila, ambapo msingi mkuu wa uchumi ulikuwa umiliki wa ardhi. Jamii hizi zilikuwa na matabaka mawili, tabaka la wamiliki wa ardhi (mabwana) na tabaka la wasiomiliki ardhi (watwana). Kwa hiyo, mabwana waliwanyonya watwana na kupata zaidi kutoka kwenye uzalishaji wa watwana. Mfumo huu uliondoa ile dhana ya usawa, upendo na ushirikiano baina ya wanajamii. Hali hii ilikuwa kinyume na maadili ya jamii za Kitanzania kwani jamii zetu zilisisitiza utu, undugu, upendo na kufanya kazi kwa kushirikiana.

**Kazi ya kufanya 4.6**

Fanya uchunguzi katika jamii unamoishi kisha tathmini mafanikio na changamoto zinazokabili nafasi ya maadili katika kuleta maendeleo ya jamii nchini Tanzania.

**Zoezi 4.3**

1. Eleza nafasi ya maadili ya jamii za Kitanzania katika kuchangia maendeleo ya jamii ya sasa.
2. Ainisha sababu za mmomonyoko wa maadili katika jamii.
3. Pendekeza mikakati ya kukuza maadili katika jamii za kisasa nchini Tanzania.
4. Jadili nafasi ya mavazi katika kuyalinda maadili ya taifa.
5. Eleza namna uzalendo unavyoweza kuchangia maendeleo ya jamii za Kitanzania katika mazingira ya sasa ya utandawazi.

### Mifumo ya kusimamia maadili kabla ya ukoloni

Kabla ya ukoloni, jamii za Kitanzania zilikuwa na mifumo mbalimbali ya usimamizi wa maadili. Mifumo ya usimamizi wa maadili ilikuwa pamoja na taasisi za familia, ukoo, kabila, dini

FOR ONLINE READING ONLY!

na jando na unyago. Mifumo hii ilifanya kazi kwa kuzingatia mila na desturi (yaani utamaduni) za jamii iliyohusika.

### Familia

Familia ndiyo ilikuwa taasisi ya kwanza katika usimamizi wa maadili katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. Wazazi au kiongozi wa familia waliwajibika katika hili na walikuwa walimu wa kwanza katika kuwafundisha watoto kuhusu maadili yanayopaswa kuzingatiwa katika familia na jamii kwa ujumla. Katika ngazi ya familia, watoto walifundishwa maadili kama vile kuwa na tabia njema, upendo, heshima, ushupavu, uhodari na kufanya kazi kwa bidii. Njia zilizotumika ni kutoa maelekezo kwa njia ya mdomo na kufanya kwa vitendo, wazazi kufanya kazi pamoja na watoto wao na kutumia simulizi za hadithi na matukio muhimu yaliopita ya kimaadili. Wazazi au kiongozi wa familia aliwajibika pia kutoa adhabu, maonyo au maelekezo kwa watoto pale walipoenda kinyume na maadili ya familia au jamii yao.

### Ukoo

Ukoo ulitokana na familia kadhaa zenye uhusiano wa damu moja. Ulihusisha mume, mke, watoto, babu na bibi na watu wengine wenye nasaba moja. Familia hizo zililazimika kumchagua mtu mmoja miongoni mwa wazee katika ukoo kuwa kiongozi ambaye alipewa majukumu ya kusimamia shughuli zote za utawala, sherehe za dini na kushauri au kutatua migogoro miongoni mwa wanaukoo. Kiongozi huyo alifanya kazi ya uongozi kwa kushirikiana na wazee wengine kwenye ukoo ambao ndio walikuwa washauri wake katika kufanya maamuzi. Aidha, kiongozi wa ukoo alikuwa na wajibu wa kusimamia shughuli zote za ndoa katika ukoo wake na kuhakikisha maadili ya jamii yanafuatwa. Iwapo maadili yamekiukwa, alisimamia utoaji wa adhabu kwa mhusika. Sifa za kuwa kiongozi wa ukoo ilikuwa ni pamoja na kuwa na ujuzi wa uganga, ushujaa, busara, hekima, uelewa mzuri wa historia ya ukoo pamoja na kujua mipaka ya ardhi ya ukoo na kufanya matambiko. Jamii zenye kufuata utawala wa kiukoo ziligawanyika katika makundi makuu mawili. Kundi la kwanza ni jamii zilizoishi kwa kufuata urithi kwa ukoo wa mama. Mfano wa jamii hizi ni zile zilizoishi Kusini na Mashariki ya Tanzania, ambazo ni Wamakonde, Wayao, Waluguru, Wapogoro, Wazaramo, Wamatumbi, Wakwere, Wamakua na Wangindo. Kundi la pili ni zile jamii zilizofuata urithi kwa ukoo wa baba kama vile Wanyakyusa, Wahehe, Wasukuma, Wagogo, Wachaga, Wahaya, Wanyamwezi, Wabena, Wakurya, Wairaqw na Wajaluo. Hivyo, ukoo katika jamii hizi ulikuwa taasisi kubwa baada ya familia katika kusimamia maadili ya jamii.

### Kabila

Katika jamii za Kitanzania, kabila lilikuwa taasisi kubwa zaidi ya ukoo. Vilevile, watu waliokuwa katika kabila moja walikuwa wanaongea lugha moja ambayo inaeleweka kwenye jamii nzima. Kila kabila lina mila na desturi zake ambazo zinaangalia masilahi ya koo zote na kuhakikisha koo zinafuata maadili. Katika jamii za asili, kabila lilikuwa na kanuni za kijamii ambazo zilitoa msingi wa maadili kama vile sheria, taratibu, miiko na miongozo mbalimbali kwa jamii. Hivyo basi, kabila lilitoa utambulisho wa kiutamaduni ambao, kwa namna moja au nyingine, ulisimamia matendo yote katika jamii yakiwamo yale ya kimaadili na matendo yasiyo ya kimaadili.

FOR ONLINE READING ONLY

Kwa mfano, katika kabila la Wamasai, rika la wazee lilikuwa kundi la juu kabisa katika jamii ya Wamasai ambalo lilianzia umri wa miaka 40 na kuendelea. Miongoni mwa kazi za wazee hawa wa Kimasai zilikuwa kufanya uamuzi muhimu kuhusu jamii yao, kusimamia maadili, kusuluhisha migogoro katika jamii, na kutoa amri ya jambo ili liweze kufanyika au lisifanyike. Kiongozi mkuu wa rika la wazee aliitwa *Olaiboni*. Huyu ndiye mwenye mamlaka makubwa ya jamii nzima ya Kimasai. Viongozi wa rika nyingine walilazimika kupata ushauri kutoka kwa kiongozi huyu kabla ya kufanya jambo lolote katika kundi lao.

**Dini**

Dini za jadi zilikuwa miongoni mwa mifumo ya kusimamia maadili katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. Dini ilikuwa sehemu muhimu ya maisha ya kiroho na kijamii katika jamii za asili na msingi wa maadili katika kuwafundisha watu kuhusu mema na mabaya. Kwa mfano, dini ziliwafundisha watu kuhusu upendo, uaminifu, huruma, haki, utunzaji wa mazingira na wajibu wa kuwasaidia wengine. Jamii hizo zilikuwa na utaratibu wake wa kufanya ibada ikiwamo kufanya matambiko. Matambiko hayo yaliongozwa na wazee wa koo. Mzee mmoja alichaguliwa kuwaongoza wenzake. Kwa mfano, katika jamii ya Wakushito, uongozi wa ukoo ulikuwa mikononi mwa baraza la wazee ambao walikuwa na jukumu kubwa katika kusuluhisha migogoro, kufanya matambiko na kusimamia maadili ya dini. Aidha, katika jamii nyingine, matambiko yalihusisha sherehe za kimila kwa lengo la kutimiza ibada na kuwafunza watu maadili ya jamii iliyohusika kama sehemu ya ibada. Kwa mfano, miti mikubwa ya asili na misitu minene ilitumika kwa matambiko na haikuruhusiwa mtu kuingia bila ruhusa maalumu. Lengo lilikuwa kutunza na kuhifadhi mazingira. Watu waliaswa na kuhimizwa kufuata taratibu za ibada ili kuepuka kupata mikosi na balaa.

**Mafunzo ya jando na unyago**

Elimu ya jando na unyago ilikuwa sehemu ya kukuza maadili na malezi ya vijana katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. Vijana walifundishwa mambo mbalimbali kuhusu majukumu ya kijinsia na kijamii kupitia jando na unyago. Shabaha kubwa ya elimu hii ilikuwa kuwarithisha ujuzi, mila, desturi, sheria, maarifa na maadili mbalimbali ya jamii ili mtoto aendane na mazingira ya jamii inayohusika. Kwa mfano, wavulana walifundishwa ujasiri, uaminifu na kutunza familia wakati wasichana walifundishwa ustadi wa kazi za nyumbani na majukumu ya familia. Mafunzo ya unyago yalitolewa na watu maalumu kutokana na umuhimu na uzoefu wao katika kuwafunda watoto wa kike, ambao walijulikana kwa jina la kungwi. Aidha, kwa zile jamii ambazo hazikuwa na sherehe za jando na unyago, elimu ilitolewa na wazee au wazazi kwa watoto kulingana na umri. Kwa wakati huo, hapakuwa na majengo rasmi ya madarasa kama sasa; hivyo, elimu ilitolewa mahali popote kama vile nyumbani, shambani, porini katika mawindo na katika mikusanyiko mbalimbali ya watu. Katika jamii ya Wahaya, vijana wa kiume waliofikisha umri wa balehe walipelekwa porini kufunzwa maadili na utamaduni wa Kihaya na mambo mangine kama ujasiri na ukakamavu. Mfumo huu wa kuelimisha vijana uliitwa *Omuteko*. Vijana katika jamii ya Wapare walipewa elimu ya maadili na mambo ya utamaduni

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Tano
# Uhusiano wa jamii za Kitanzania na jamii nyingine

## Utangulizi

*Kabla ya ukoloni, jamii za Kitanzania zilikuwa na uhusiano na jamii nyingine za Afrika na za mataifa mengine nje ya bara la Afrika. Katika sura hii, utajifunza kuhusu aina ya uhusiano ulioibuka kati ya jamii za Kitanzania na jamii nyingine za Afrika na za mataifa mengine nje ya Afrika kama vile Mashariki ya Kati, Mashariki ya Mbali na Ulaya. Pia, utajifunza kuhusu uhusiano wa mifumo ya maadili ya jamii nyingine duniani na jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. Umahiri utakaoujenga, utakuwezesha kuthamini na kuboresha uhusiano wa jamii yako na jamii nyingine.*

**Fikiri**

**Uhusiano uliokuwapo kati ya jamii za Kitanzania na jamii nyingine kabla ya ukoloni.**

FOR ONLINE READING ONLY

### Uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na jamii nyingine za Afrika

Kabla ya ukoloni, jamii za Kitanzania zilikuwa na uhusiano na jamii mbalimbali kulingana na maeneo yao ya kijiografia.

Aidha, uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na jamii nyingine za Afrika ulitokana na sababu mbalimbali. Mojawapo ya sababu hizo ni kuongezeka kwa uzalishaji mali ambako kulifanya jamii hizo kuwa na mali za ziada. Ongezeko la uzalishaji lilichochea ubadilishanaji wa bidhaa (biashara) ambao nao ukawa mwanzo wa uhusiano kati ya jamii moja na jamii nyingine. Pia, uhusiano wa jamii za Kiafrika, kati ya jamii moja na nyingine, ulitokana na uhamaji na kubadilishana uzoefu na mbinu za uzalishaji mali. Pia, uhusiano huo ulitegemea aina ya bidhaa zilizopatikana au kuzalishwa eneo moja lakini hazipatikani au hazizalishwi katika eneo lingine. Mfano wa bidhaa hizo ni chumvi, chuma na dawa ambazo hazikupatikana wala kuzalishwa na kila jamii.

Mwanzoni, biashara kati ya jamii za Kitanzania na jamii nyingine za Afrika ilihusisha kubadilishana bidhaa miongoni mwa wahunzi, wakulima, wasusi, wachongaji, wafinyanzi na wafugaji. Lengo la biashara hii lilikuwa kupata bidhaa kutoka jamii nyingine kwa ajili ya matumizi ya kila siku kama chakula, zana

za kazi kama majembe na shoka pamoja na silaha kama mishale na mikuki kwa ajili ya ulinzi. Uhusiano wa kibiashara kati ya jamii za Kitanzania na jamii za nchi nyingine za Afrika ulihusisha biashara za masafa marefu. Biashara hii ilikuwa maarufu katika karne za 18 na 19 za zama hizi. Biashara ya masafa marefu ilianza baada ya watu kuzalisha ziada au kuwa na mahitaji ambayo yangepatikana kwa njia ya kufanya biashara. Biashara hii ilifanyika ili kuzipata bidhaa ambazo jamii haikuweza kuzizalisha katika mazingira yao au kuzipata kutoka katika jamii za karibu. Kielelezo 5.1 kinaonesha njia za biashara ya masafa marefu kati ya jamii za Kitanzania na jamii jirani.




**Kielelezo 5.1:** *Njia za biashara ya masafa marefu katika Afrika Mashariki*

### Kazi ya kufanya 5.1

Soma matini kutoka vyanzo mbalimbali vya taarifa ili kupata taarifa zaidi kuhusu uhusiano uliokuwapo kati ya jamii za Kitanzania na jamii za nchi jirani hapa barani Afrika.

Katika ukanda wa pwani ya Tanzania, biashara ilifanyika ili kuunganisha watu wa maeneo ya bara na mwambao wa pwani ya Bahari ya Hindi na visiwa vya Zanzibar na Pemba. Misafara ya biashara kutoka Zanzibar kwenda bara, hasa maeneo ya Unyanyembe, Ujiji, Buganda, Katanga, Uyao na Malawi ilipitia katika maeneo ya Bagamoyo, Pangani, Saadani na Kilwa Kivinje. Uhusiano wa kibiashara kati ya jamii hizi ulisaidia jamii za wakati huo kupata mahitaji yao kwa urahisi, kuboresha maeneo ambayo baadaye yalitumiwa kama njia za usafiri na kuibua vituo vya biashara ambavyo vilisababisha miji kukua. Biashara kati ya jamii za Tanganyika na Zanzibar ni matokeo ya ongezeko la uzalishaji kutoka katika sekta mbalimbali zikiwamo kilimo, viwanda, uvuvi, ufugaji na uwindaji. Pia, kuibuka kwa wataalamu mbalimbali katika sekta za uhunzi, ufinyanzi na ususi kulichangia kukuza biashara kati ya jamii za Kitanzania na jamii zingine. Biashara kati ya jamii za Tanganyika na Zanzibar zilitofautiana kati ya jamii moja na nyingine kulingana na mazingira na aina ya shughuli za kiuchumi zilizofanyika katika maeneo hayo.

Biashara hii ilikuwa na umuhimu mkubwa kwa jamii za pwani ya Tanganyika na Zanzibar. Kwanza, ilirahisisha upatikanaji wa bidhaa muhimu kama zana za chuma na

FOR ONLINE READING ONLY

chumvi zilizowawezesha wanajamii kukidhi mahitaji yao ya chakula. Aidha, biashara ilileta maendeleo mbalimbali katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, na kijamii katika jamii hizi. Kwa njia hii, biashara ilisaidia kukua na kuimarika kwa uzalishaji wa zana za uzalishaji mali na bidhaa katika sekta za kilimo na ufundi kama vile uchongaji, uhunzi na ufinyanzi. Vilevile, biashara ilikuza na kuimarisha tawala na kusababisha kuibuka kwa matabaka kama vile ya wafanyabiashara ya masafa mafupi na wale wa masafa marefu ndani ya jamii za Kitanzania.

Aidha, jamii zilizoishi kusini mwa Tanzania zilifanya biashara na jamii mbalimbali za Msumbiji, Malawi na Zambia. Katika upande huu, biashara ya masafa marefu ilipitia njia ya kusini ambayo iliongozwa na Wayao. Misafara ya biashara hii ilianzia miji ya Kilwa Kivinje na Mikindani kuelekea ukanda ya ziwa Nyasa na Msumbiji. Vilevile, Wayao walifanya biashara ya bidhaa kutoka pwani ya Tanzania kama vile mapambo, shanga, nguo, vioo, bunduki, risasi, baruti na bidhaa nyingine za viwandani. Bidhaa zilizosafirishwa kutoka bara kwenda pwani ni pamoja na dhahabu, pembe za ndovu, ngozi za wanyama, nta na asali.

Katika upande wa kusini magharibi mwa Tanganyika, jamii za Wanyakyusa na Wakisi walibobea katika biashara ya vyungu, mikeka na vikapu. Jamii za Wafipa na Wakinga walikuwa maarufu kwa uhunzi wa vyuma. Hivyo, waliwauzia Wanyakyusa na Wakisi zana za chuma kama majembe, mishale na mikuki. Wakisi ambao walikuwa wafinyanzi hodari waliwauzia vyungu Wanyakyusa, Wakinga na Wafipa. Ubora wa vyungu vya Wakisi uliwafanya wavushe bidhaa zao kwa mitumbwi hadi Malawi. Katika upande wa kaskazini-mashariki mwa Tanganyika, jamii za Wapare, Wachaga, Wasambaa na Wamasai zilihusiana katika biashara. Jamii hizi pia zilikuwa na uhusiano wa kibiashara na jamii za Kenya kama Wakamba na Wataita. Misafara ya biashara ilianzia Kilimanjaro kuelekea Mombasa, Malindi, Baringo, Mlima Kenya, Mlima Elgon na maeneo ya ziwa Viktoria.

Aidha, katika upande wa magharibi na kaskazini-magharibi mwa Tanganyika, jamii za Wanyamwezi na Wasumbwa zilifanya biashara na jamii za Burundi, Rwanda, Bunyoro, Buganda na Katanga. Misafara ya biashara ilianzia Tabora na Urambo kupitia Uvinza, na Ujiji kuelekea Katanga. Aidha, misafara mingine ilielekea kaskazini na kupitia Karagwe, Buganda, na Bunyoro hadi Sudani. Bidhaa katika biashara hii zilikuwa chumvi kutoka Uvinza, chuma na zana za chuma kutoka Karagwe na Bunyoro, shaba kutoka Katanga, kahawa kutoka Buhaya, na nguo za miwale kutoka Kongo.

**Kazi ya kufanya 5.2**

Tafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali kisha onesha maeneo mengine ya Afrika yaliyokuwa na uhusiano na jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni.

### Matokeo ya uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na jamii nyingine za Afrika

Matokeo ya uhusiano wa kibiashara kati ya jamii za Kitanzania na jamii za nchi jirani

FOR ONLINE READING ONLY

ulisaidia ubadilishanaji wa bidhaa kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania na ulileta matokeo chanya na hasi. Hii ilitokana na namna jamii husika zilivyoshiriki katika biashara hiyo. Baadhi ya matokeo ya uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na jamii nyingine Afrika ni pamoja na:

(a) Baadhi ya wafanyabiashara wa asili kama vile Chifu Machemba, Mtemi Mirambo na Mtemi Isike wa Tabora walipata utajiri. Viongozi hawa walijipatia mali kutokana na kushiriki kwao katika biashara ya masafa marefu na pia walitoza ushuru misafara ya wafanyabiashara waliopita katika maeneo yao.

(b) Jamii zilifanikiwa kupata bidhaa mbalimbali za kigeni kama vile bunduki, nguo za hariri, shanga pamoja na vyombo vya udongo.

(c) Kuibuka na kukua kwa vituo vya biashara kama vile Zanzibar, Saadani, Pangani, Bagamoyo, Kilwa, Kilimatinde, Tabora na Ujiji. Miji hii ilikuwa vituo vikubwa vya biashara na hatimaye kuwa miji mikubwa. Wafanyabiashara wa Kiarabu waliweka makazi katika miji hii.

(d) Kuibuka kwa dola zenye nguvu katika baadhi ya jamii za Kitanzania kama vile Wahehe na Wanyamwezi. Dola zilizoongozwa na Mtwa Mkwawa na Mtemi Mirambo mtawalia zilinufaika sana na biashara ya masafa marefu. Hii ilitokana na kukusanya ushuru na kujipatia bidhaa muhimu na za thamani kubwa.

(e) Biashara ya masafa marefu ilichangia kuingia kwa aina mpya ya mazao ya biashara na chakula kama vile karafuu, mahindi, mpunga na mihogo. Mazao haya yalianza kulimwa na jamii za Kitanzania na yameendelea kulimwa hadi sasa.

(f) Biashara ilisababisha kuingia na kuenea kwa tamaduni mpya za mavazi. Kwa mfano, mtindo wa uvaaji wa kanzu na baraghashia uliingia katika miji kama Zanzibar, Bagamoyo, Kilwa, Tabora na Ujiji. Katika miji hii utamaduni wa Kiarabu umeshamiri sana mpaka sasa.

(g) Biashara ilichangia kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili. Kiswahili kilikua kwa kasi katika miji mbalimbali kama lugha ya kibiashara. Lugha hii ilikuwa muhimu sana katika kuwaunganisha watu katika harakati za kudai uhuru. Kiswahili pia kilitumika katika majeshi ya kikoloni na mahakama katika kuamua mashtaka ya Waafrika.

Hali kadhalika, biashara hii kwa upande wa pili ilisababisha madhara katika jamii. Miongoni mwa matokeo hasi ya biashara ya masafa marefu ni kama vile kuibuka kwa vita vya makabila, uwindaji wa tembo ili kupata pembe za ndovu, kupungua kwa idadi ya watu kutokana na biashara ya utumwa na kupata maendeleo duni. Vilevile, kutoweka kwa amani katika jamii, kudunishwa kwa maadili na ustaarabu wa Watanzania, kudhoofika kwa baadhi ya viwanda vya jadi na unyonyaji wa rasilimali za Tanzania zilikuwa athari hasi kwa Watanzania zilizotokana na biashara ya masafa marefu.

FOR ONLINE READING ONLY

### Zoezi 5.1

1. Linganisha sababu za kuzuka kwa uhusiano kati jamii za Kitanzania na jamii nyingine kabla ya ukoloni na jamii za sasa.
2. Jadili mafanikio na changamoto za uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na jamii nyingine za Afrika kabla ya ukoloni.
3. Linganisha uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na jamii nyingine za Afrika kabla ya ukoloni na wakati wa sasa.
4. Eleza uhusiano wa sasa kati ya jamii za Kitanzania na jamii zingine za Afrika.
5. Pendekeza mikakati ya kuimarisha uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na jamii nyingine za Afrika.

### Ujio wa Wangoni

Pamoja na uhusiano wa jamii za Kitanzania na jamii nyingine za Afrika kupitia biashara, jamii hizi pia zilishuhudia ujio wa Wangoni waliotokea Afrika Kusini katika miaka ya 1840. Kabila la Wangoni lilikuwa mojawapo ya makabila ya Wanguni wa sehemu ya Uzulu huko Natal. Waliondoka Afrika Kusini mwaka 1820 chini ya uongozi wa Zwangendaba wakikimbia utawala wa kijeshi wa Mfalme Shaka. Wangoni walikuwa na ustadi mkubwa katika masuala ya vita ambapo walijifunza vizuri mbinu za kivita kutoka kwa Shaka aliyekuwa kiongozi shupavu wa Wazulu. Walifanikiwa kuvuka mto Zambezi mwaka 1835 wakiwa wanaelekea upande wa kaskazini mpaka walifika uwanda wa Ufipa, magharibi mwa Tanzania miaka ya 1840. Wangoni hawa, wakiwa njiani, walipata watu wengine wengi kutoka katika jamii mbalimbali walizokutana nazo na kuwa sehemu ya Wangoni. Katika kipindi hiki, kundi la Wangoni lilikuwa kubwa na kuwa na wapiganaji wengi.

Wangoni walibaki katika maeneo ya uwanda wa Ufipa mpaka Zwangendaba alipofariki mwaka 1848. Baada ya kifo chake, kundi hili la Wangoni liliingia kwenye mgogoro wa nani arithi madaraka kwani watoto wake Mpezeni na Mombera walikuwa wadogo sana kiumri kurithi madaraka hayo. Kwa hiyo, mdogo wake Ntabeni alichukua madaraka na kumtangaza Mpezeni kama mrithi halali wa Zwangendaba. Lakini naye alifariki baada ya kipindi kifupi tu. Madaraka yakatwaliwa na binamu wa Zwangendaba aliyeitwa Mgayi, ambaye naye alimtangaza Mombera kama kiongozi ajaye. Kutokana na hizi tofauti za warithi wa Zwangedaba, jamii ya Wangoni iligawanyika katika makundi matano. Makundi hayo yalikuwa Watuta, Wagwangara, Wampezeni, Wamombera na Wasiwere. Watuta na Wagwangara walibaki Tanzania na makundi matatu, yaani Wampezeni, Wamombera na Wasiwere walienda Malawi na Zambia.

**Kazi ya kufanya 5.3**

Soma matini kutoka vyanzo mbalimbali vya taarifa, kisha bainisha makundi matano ya Wangoni baada ya kifo cha Zwangendaba na chambua kwa kina historia ya kila kundi.

FOR ONLINE READING ONLY

### Athari za ujio wa Wangoni nchini Tanzania

Athari za ujio wa Wangoni ni pamoja na:

(a) Kuundwa kwa jamii mpya ya Wangoni hapa nchini. Ujio wa Wangoni ulisababisha kutokea kwa jamii mpya hapa nchini, jamii ya Wangoni waliotokana na muunganiko wa kundi dogo la Wanguni kutoka Afrika Kusini na wenyeji wengine wengi waliojiunga njiani wakati wapiganaji wa Kingoni wakija Tanzania.

(b) Kuanzishwa kwa mbinu mpya za vita za Kingoni. Mbinu hizi ziliigwa na jamii mbalimbali za Tanzania katika kujilinda dhidi ya Wangoni wenyewe au kupanua himaya zao za utawala. Viongozi kama Merere wa Wasangu, Mirambo wa Wanyamwezi na Nyungu-ya-Mawe wa Wakimbu walifaidika na mbinu hizi mpya za Wangoni katika kujenga utawala wao.

(c) Kutokea kwa migogoro katika jamii ambazo hapo mwanzo zilikuwa na hali ya amani. Sehemu walizopita hawa Wangoni walisababisha migogoro. Kwa mfano, migogoro ilitokea katika maeneo ya Uheheni na Unyamwezini na Ufipani ikihusisha upanuzi wa himaya za Wahehe na Wanyamwezi.

(d) Kusababisha baa la njaa kwa baadhi ya jamii za Kitanzania. Ujio huu ulienda sambamba na Wangoni kuharibu mashamba na mazao, kupora chakula, kuharibu nyumba, mali na maghala ya chakula ya jamii za Kitanzania walizozivamia.

(e) Kusababisha kutokea kwa ndoa baina ya Wangoni na jamii nyingine za Kitanzania. Wanaume wa Kingoni waliwaoa wanawake wa maeneo waliyopita na wale wa wenyeji waliowakuta katika eneo waliloweka makazi, ambalo ni Songea ya leo. Kwa mfano, wanaume wa Kingoni waliwaoa wanawake wengi wa Kindendeule.

(f) Kusababisha baadhi ya jamii dhaifu kuhama kutoka katika maeneo yao ya asili na kwenda maeneo mengine. Mfano mzuri ni Wandendeule waliohama kutoka eneo lao la asili, Songea, na kwenda Namtumbo ambako walianzisha makao yao mapya, na

(g) Kusababisha uzalishaji mali kupungua kwa sababu kuna maeneo amani ilikosekana na watu wengi walitumia muda mwingi kujificha na kuukimbia uvamizi huu.

Wangoni walihamia Tanzania kabla ya kuja kwa ukoloni. Kwa hiyo, jamii hii ni miongoni mwa jamii za Kitanzania zilizokuja kuunda koloni la Ujerumani ya Afrika Mashariki wakati wa utawala wa Wajerumani, Tanganyika wakati wa ukoloni wa Waingereza, na nchi ya Tanzania baada ya uhuru. Kwa maana hiyo, kabla ya ukoloni hakukuwa na nchi bali kulikuwa na jamii moja moja yenye utawala wake.

#### Zoezi 5.2

1. Jadili faida na hasara za ujio wa Wangoni katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni.
2. Kwa nini Wangoni walifanikiwa kuzishinda jamii nyingi walizozikuta na kuanzisha makazi yao ya kudumu Tanzania?

FOR ONLINE READING ONLY

3. Eleza athari za ujio wa Wangoni katika maadili ya jamii za Kitanzania.

## Uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na za Mashariki ya Kati na Mbali

Uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na zile za Mashariki ya Kati na Mashariki ya Mbali ulianza mapema sana, takribani miaka 2000 iliyopita. Jamii za mwanzo zilizotembelea pwani ya Tanzania zilikuwa za watu kutoka Asia katika nchi kama Syria, Saudia Arabia, Oman, India, Singapore, Malaysia, Burma, Thailand na China. Jamii hizi zilifanya biashara kwa mtindo wa kubadilishana bidhaa. Upatikanaji wa bidhaa kama vile meno ya tembo, dhahabu, ngozi za wanyama na watumwa ni mojawapo ya sababu zilizowavutia wafanyabiashara hao kutembelea pwani ya Afrika Mashariki. Kabla ya jamii hizi za Asia, wafanyabiashara kutoka Ugiriki, Urumi na Misri walikuja pwani ya Afrika Mashariki, hususani Tanzania wakileta bidhaa zao na kubadilishana na bidhaa kutoka kwa jamii za pwani.

Ushahidi kupitia uchunguzi wa akiolojia unaonesha kuwa jamii hizi zilianza uhusiano na jamii za Kitanzania mnamo miaka ya 2000 kabla ya zama za sasa. Ushahidi huu unatokana na kugunduliwa kwa mabaki ya vyombo vya udongo, majagi, sarafu, shanga na makaburi katika pwani ya Afrika Mashariki ambayo yanaaminika kuwa yanatoka Mashariki ya Kati na Mbali. Ushahidi mwingine kutoka katika kitabu cha "Periplus of the Ertythrean Sea" au "Kitabu cha Mwongozo kwa Bahari ya Hindi", kilichoandikwa na wafanyabiashara wa awali wa Ugiriki. Kitabu hiki kina maelezo kuhusu pwani ya Afrika Mashariki. Mawasiliano ya mara kwa mara yaliongezeka zaidi kupitia biashara mnamo karne ya 8. Wafanyabiashara wengi walitoka China, Indonesia, na India. Baadaye, katika karne ya 10 ya zama za sasa, wafanyabiashara pia walikuja kutoka Arabia, Uajemi (Iran), Syria na Misri. Shughuli zao za kibiashara zilisambaa pwani yote ya mashariki mwa Afrika kati ya Mogadishu na Sofala.

**Kazi ya kufanya 5.4**

Soma vyanzo mbalimbali vya taarifa, kisha chunguza kwa undani sababu za uhusiano wa kibiashara kati ya jamii za Mashariki ya Kati, ya Mbali na Ulaya na jamii za Kitanzania kuwa za njia ya uelekeo mmoja tu, yaani wageni kuja Tanzania na si jamii za Kitanzania kwenda huko.

### Shughuli zilizowakutanisha

Watu kutoka Mashariki ya Mbali, Waarabu na Waajemi walikuja pwani ya Tanzania kipindi kirefu huko nyuma hata kabla ya zama za sasa. Vichocheo vikubwa vilivyosababisha Waarabu na Waajemi kutoka Mashariki ya Kati kuja pwani ya Tanzania vilikuwa biashara na ushawishi wa kuieneza dini ya Kiislamu. Wafanyabiashara wa Kiarabu walikuja pwani ya Tanzania kupitia Bahari Nyekundu kisha Bahari ya Hindi. Hawa walikaa pwani ya Tanzania wakifanya biashara na kuieneza dini ya Kiislamu katika maeneo yote ya mwambao wa Bahari ya Hindi. Usafiri kutoka

FOR ONLINE READING ONLY

Mashariki ya Kati hadi pwani ya Tanzania ulitegemea majahazi yaliyosaidiwa na upepo uliojulikana kama pepo za kusi na kaskazi. Wageni hawa waliweza kuweka makazi na hatimaye kuchangamana na wenyeji wa pwani ya Tanzania mapema zaidi kuliko jamii zingine za bara.

Biashara ndiyo ilikuwa shughuli na kichocheo kikuu cha uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na watu kutoka Mashariki ya Kati. Wafanyabiashara kutoka Mashariki ya Kati katika mataifa ya Oman, Saudia Arabia, Yemen, Syria, na Lebanon walifika pwani ya Afrika Mashariki kwa lengo la kufanya biashara na kujipatia faida zaidi kwani waliona fursa iliyotokana na hazina kubwa ya utajiri nchini Tanzania. Kuwapo kwa utajiri mkubwa wa rasilimali kama dhahabu, pembe za ndovu, ngozi, pembe za wanyama pori, magamba ya kobe na kakakuona pamoja na mazao ya misitu kama mikoko, asali, nta, na gundi kuliwavutia wafanyabiashara hao. Biashara hii ilifanyika kwa njia ya kubadilishana bidhaa kwa bidhaa. Baadaye, biashara hii ilianza kutumia fedha kama njia ya kuuziana bidhaa. Biashara hii ilifanyika mwaka mzima. Katika kutaka kufaidi zaidi biashara hii, wafanyabiashara wa kiarabu na kiajemi, ambao walikuwa Waislamu, walihamia kwa wingi pwani ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kufanya biashara na shughuli za uzalishaji mali. Baadhi ya koo za Kiarabu zilihamia katika miji ya Kilwa, Bagamoyo, Mikindani, Zanzibar na Pemba.

Kwa mfano, ukoo maarufu uliotawala Kilwa ulikuwa ukoo wa Shirazi. Kilwa ilianzishwa katika karne ya 10 na Ali ibn al-Hassan Shirazi, mwana wa mfalme wa Shiraz. Ukoo wa Shirazi ulisimika utawala wao Kilwa takribani karne ya 12. Ushawishi wao ulienea kote katika pwani ya Tanganyika. Vilevile, Zanzibar ilianza kutawaliwa na ukoo wa Al Said kutoka Mascat, Oman baada ya kuanguka kwa utawala wa Wareno katika Afrika Mashariki, mwaka 1698. Kwa hiyo, Zanzibar sasa ikawa rasmi chini ya utawala wa Oman kuanzia mwaka 1698. Idadi ya Waislamu wahamiaji kutoka Uarabuni ikazidi kuongezeka baada ya mwaka 1698. Hawa walichangia sana kuenea kwa Uislamu katika pwani ya Afrika Mashariki. Kufikia mwanzoni mwa karne ya 19, pwani ya Afrika Mashariki ilikuwa chini ya Usultani wa Oman. Sultani Seyyid Said aliyeanza kuitawala Oman mwaka 1804 alihamishia makao makuu Zanzibar mwaka 1840. Utawala huu ulichukua nafasi muhimu katika maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii, na kiutamaduni ya Afrika Mashariki kupitia biashara na utawala. Waarabu wa Oman walianzisha biashara ya misafara na ushuru wa forodha. Sultani Seyyid Said aliwaalika Wahindi kuja Zanzibar miaka ya 1840 na 1850. Wahindi hawa wakawa tabaka la wafanyabiashara muhimu waliotoa mikopo kwa wafanyabiashara wa Kiarabu waliofanya biashara ya masafa marefu kwenda bara kupitia Bagamoyo, Kilwa Kivinje na Pangani. Pia, Wahindi hawa waliajiriwa bandarini Zanzibar wakiwa makarani na wakusanya ushuru. Kufikia mwaka 1860 walikuwapo Wahindi 6000 wakiweka makazi yao katika miji ya Zanzibar, Bagamoyo, Kilwa, Pemba na Pangani. Pia, Sultani aliwaalika Waarabu kutoka Oman kuja Zanzibar kuwekeza kwenye kilimo cha mashamba makubwa ya minazi na mikarafuu. Utamaduni wa

FOR ONLINE READING ONLY

Kiarabu na matumizi ya lugha ya Kiswahili yalipanuka kutokana mwingiliano huu wa kibiashara.

**Kazi ya kufanya 5.5**

Kupitia vyanzo mbalimbali vya taarifa, tumia ushahidi wa kihistoria na kiutamaduni kuthibitisha kuwapo kwa uhusiano kati ya Tanzania na jamii za Mashariki ya Kati tangu karne ya 8.

**Njia na vyombo vya usafiri vilivyotumiwa**

Waarabu na Waajemi walitumia njia ya baharini iliyowezeshwa na pepo za kusi na kaskazi kama njia ya usafiri kufikia pwani ya Afrika Mashariki. Pepo hizi zilirahisisha usafiri na kukuza shughuli za kibiashara kati ya pwani ya Afrika Mashariki na nchi za Mashariki ya Kati na Mbali. Safari hizi ziliwezesha mwingiliano wa kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni kati ya nchi hizi. Kielelezo 5.2 kinaonesha ramani na njia iliyokuwa inatumiwa na Waarabu na Waajemi kutoka bara la Asia hadi kufika pwani ya Tanzania katika miaka ya 1250 ya zama hizi.




**Kielelezo 5.2:** *Njia ya Waajemi na Waarabu kutoka bara la Asia hadi Tanzania*

FOR ONLINE READING ONLY

**Kazi ya kufanya 5.6**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya taarifa, soma matini kuhusu uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na jamii za Mashariki ya Kati, kisha bainisha vyombo vya usafiri vilivyotumika kubebea bidhaa majini na nchi kavu.

Zoezi 5.3

1. Eleza chimbuko la biashara kati ya jamii za Mashariki ya Kati na Mbali na jamii za Kitanzania.
2. Ni kwa namna gani usafiri wa baharini ulifanikisha biashara kati ya jamii za Kitanzania na jamii za Mashariki ya Kati na ya Mbali?
3. Fafanua sababu zilizofanya jamii za Mashariki ya Kati na ya Mbali kufanya biashara na mwambao wa Tanzania zaidi na si maeneo mengine ya bara.
4. Ni kwa namna gani faida za kijiografia zilivyosaidia kukua kwa biashara kati ya jamii za Kitanzania na zile za Mashariki ya Kati?
5. Fafanua changamoto zilizokuwapo katika biashara kati ya jamii za Kitanzania na jamii za Mashariki ya Kati na ya Mbali.

### Vituo na miji ya kibiashara

Mawasiliano ya kibiashara kati ya Uarabuni na pwani ya Afrika Mashariki yalisababisha kuanzishwa kwa makazi ya kudumu na vituo vya kibiashara vya Waasia na Waarabu katika maeneo ya mwambao wa pwani, na baadaye walielekea ndani ya nchi ambayo kwa sasa inaitwa Tanzania Bara. Vituo vya biashara vya pwani kama Bagamoyo, Dar es Salaam, Tanga, Kilwa na Mikindani vilitawaliwa zaidi na Waarabu pamoja na Waajemi. Uhusiano kati ya Waarabu na majirani zao Waafrika ulikuwa wa kirafiki. Kutokana na kukua kwa biashara, wafanyabiashara wa Kiarabu walianza kupenya ndani zaidi kuelekea bara. Baadhi ya wafanyabiashara hawa walianza misafara yao Kilwa Kivinje kuelekea Ziwa Nyasa. Wafanyabiashara wengine walipita njia ya kati, iliyoanzia Bagamoyo hadi kufika Unyanyembe (Tabora) kwa Wanyamwezi. Tabora ilikuwa njia panda ya njia iliyoelekea magharibi hadi Ujiji, Katanga, Burundi na Umanyema huko Kongo Mashariki. Tabora na Ujiji vilikuwa vituo muhimu vya kibiashara. Waarabu kadhaa waliongozwa na Mohamed Murjebi (Tip Tip) walifanya makao yao huko. Kutoka Tabora, njia nyingine ilielekea upande wa kaskazini hadi maeneo ya ziwa Viktoria, hasa katika falme za Uhaya (Karagwe, Kyamtwara na Isingiro) hadi falme za Buganda na Bunyoro huko Uganda. Katika njia hii, bidhaa maarufu zilikuwa pembe za ndovu na ngozi za wanyama pori, asali, nta, na gundi. Watumwa wengi walitoka katika maeneo haya pamoja na njia ya kusini iliyofika Msumbiji na Malawi.

Kutokana na fursa hizi, Sultan Seyyid Said alijenga himaya kubwa ya kibiashara akiwateua wawakilishi wake katika miji yote iliyopita misafara hii ya kibiashara, hasa njia za kati na kusini mwa Tanzania. Kwa mfano, Mohamedi Murjebi, maarufu kama Tip Tip alikuwa gavana wa Waarabu wa Katanga huko Kongo Kusini

FOR ONLINE READING ONLY

akimuwakilisha Sultani wa Zanzibar. Sultani aliidhibiti biashara hii ambayo ilimletea faida kubwa.

Bidhaa zilizoletwa kutoka kwa Waarabu na Waajemi hadi kwa watu wa Tanzania kabla ya ukoloni zilikuwa shanga, nguo, sime, jambia, visu, bakuli, birika na majagi. Vitu hivi vilikuwa sehemu ya biashara ya kubadilishana bidhaa kati ya wafanyabiashara wa Kiarabu na Kiajemi na watu wa pwani ya Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla wake. Waarabu na Waajemi walichukua kutoka katika jamii za Kitanzania bidhaa kama dhahabu, pembe za ndovu, ngozi, pembe za wanyama pori, bidhaa za misitu na watumwa. Pia, uvumbuzi wa akiolojia kando ya pwani ya Tanzania umegundua vitu kama vyungu, vito vya kioo, sarafu, na vyombo vya udongo ambavyo vinafanana na vile vilivyopatikana Mashariki ya Kati na ya Mbali. Uvumbuzi huu unaashiria biashara na mwingiliano wa utamaduni moja kwa moja kati ya maeneo haya mawili. Ushahidi mwingine unaonekana katika usanifu wa majengo na mpangilio wa miji. Ujenzi na upangaji wa miji ya pwani ya Tanzania, kama vile mji wa Zanzibar, unashabihiana na ujenzi wa nyumba zilizopo Mashariki ya Kati, hususan mitindo ya Kiarabu na Kiajemi ambapo miundo ya nyumba za kuishi na misikiti inafanana.

Lugha na utamaduni ni uthibitisho mwingine unaoonesha uhusiano wa maeneo haya. Lugha ya Kiswahili, inayozungumzwa Tanzania, ina maneno mengi yenye asili ya Kiarabu. Hii inaonesha kuwapo kwa mwingiliano mkubwa na wa karibu wa lugha na kuwa ushahidi dhahiri wa uhusiano kati ya sehemu hizi mbili. Aidha, mila na desturi au utamaduni vimekuwa ushahidi mkubwa wa uhusiano huu. Mila na desturi kama za mapishi, mitindo ya mavazi na imani za kidini katika maeneo mengi katika jamii za Kitanzania, hasa kwenye vituo vya kibiashara katika pwani, ni mifano halisi inayoonesha mwingiliano wa jamii hizi za Mashariki ya Kati na mbali na jamii za Tanzania.

FOR ONLINE READING ONLY

**Athari**

Uhusiano wa jamii hizi ulileta athari mbalimbali za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa kwa jamii za Kitanzania.

*Athari za kiuchumi*

Uhusiano wa jamii za Kitanzania na Mashariki ya Kati na ya Mbali ulikuwa na athari mbalimbali za kiuchumi. Baadhi ya athari hizo ni:

(a) Kukua kwa biashara: Chanzo kikuu cha uhusiano kati ya jamii za Tanzania na za Mashariki ya Kati na Mashariki ya Mbali ni biashara, hasa iliyokuwa inafanyika kwenye mwambao wa Tanzania. Biashara hizi zilisababisha kuanzishwa kwa makazi ya wageni ambao waliamua kulowea nchini Tanzania na kuchangamana na wakazi wa mwambao kupitia kuwaoa wanawake wa mwambao wa pwani. Biashara hii ilifanyika kupitia misafara ya watumwa kwenye njia za kanda za kusini, kati na kaskazini. Watumwa walitumika kubeba bidhaa kama dhahabu, pembe za ndovu, ngozi za wanyama pori pamoja na bidhaa nyingine.

(b) **Kukua kwa shughuli za kilimo:** Uhusiano kati ya Waarabu na jamii za Tanzania ulichochea pia maendeleo ya kilimo kwa njia mbalimbali. Shughuli za biashara zilisababisha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao kutokana na mahitaji makubwa ya vyakula, mazao ya biashara na mifugo katika miji ambako misafara ya biashara ilipita kutoka na kuelekea Zanzibar. Mahitaji haya yalihimiza jamii za Kitanzania kuimarisha mbinu zao za kilimo. Zaidi ya hayo, upatikanaji wa ardhi yenye rutuba na mvua za uhakika katika baadhi ya maeneo viliwavutia wageni kutoka ughaibuni kuanzisha mashamba makubwa ya chakula na mengine kwa ajili ya biashara. Kwa mfano, Sultan Seyyid Said alihamia Zanzibar mwaka 1840 kwa lengo la kuanzisha mashamba makubwa ya mikarafuu na minazi huko Unguja na Pemba. Pia, kulikwa na mazao mengine yaliyolimwa kama ndizi na viungo.

(c) **Kukua kwa ufundi na ujuzi pamoja na mawazo mapya:** Kutokana na uhusiano kati ya jamii za Tanzania na jamii nyingine kutoka Mashariki ya Kati na Mashariki ya Mbali, ujuzi na ufundi kutoka mataifa mbalimbali uliingia nchini Tanzania na kusaidia uboreshaji wa shughuli za kilimo, biashara, uwindaji na uvuvi.

**Kazi ya kufanya 5.7**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya taarifa, chunguza athari nyingine zilizotokea kutokana na uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na jamii za Mashariki ya Kati na ya Mbali.

(d) **Unyonyaji mkubwa wa rasilimali za Kitanzania:** Uhusiano kati ya jamii za Tanzania na Mashariki ya Kati na ya Mbali ulisababisha unyonyaji kupita kiasi wa rasilimali za Kitanzania kupitia biashara ambayo haikuwa sawa kimapato. Jamii za Kitanzania walitoa bidhaa zenye thamani kubwa kama vile watumwa, pembe za ndovu, ngozi za wanyama pori na magamba ya kobe wakati wageni walileta bidhaa zenye thamani ndogo kama vile vioo, shanga, jambia na vyombo vya ndani. Kwa mantiki hiyo, wageni walinufaika zaidi kimapato kuliko jamii za Kitanzania.

(e) **Kujulikana kwa Tanzania sehemu nyingine duniani:** Kutokana na uhusiano huu, utajiri wa Tanzania ulianza kujulikana kwa mataifa mengine duniani. Hivyo, mataifa na jamii nyingi zaidi za Uarabuni na Mashariki ya Kati zilivutiwa na utajiri huu na kuanzisha uhusiano na ukanda huu wa Afrika, hasa jamii za Kitanzania. Uhusiano huu ulisababisha rasilimali za Tanzania kuanza kuvunwa zaidi na kuuzwa kwenye mataifa hayo. Vilevile, ulisababisha madhara mengine kama migogoro, utumwa na mengineyo.

(f) **Kupungua kwa uzalishaji mali kutokana na utumwa:** Kupitia uhusiano wa jamii za Kitanzania na jamii kutoka Mashariki ya Kati na ya Mbali, vijana wengi wenye nguvu walichukuliwa kutoka jamii mbalimbali za Kitanzania na kupelekwa nchi za Uarabuni kufanya kazi za majumbani. Watumwa wengine walipelekwa kufanya kazi katika

FOR ONLINE READING ONLY

mashamba ya walowezi wa kizungu huko Amerika. Hii ilisababisha uhaba wa nguvukazi, hasa kwenye maeneo ya jamii hizo walikotoka ambako walikuwa wazalishaji wakubwa wa mazao ya chakula na kufanya shughuli zingine za kujipatia riziki.

*Athari za kijamii*

Uhusiano huu pia ulisababisha matokeo hasi na chanya ya kijamii katika jamii za Kitanzania kama inavyoelezwa hapa chini.

(a) Kukua kwa miji: Uhusiano miongoni mwa jamii za Kitanzania na wageni kutoka nchi za Mashariki ya Kati na ya Mbali ulisababisha kukua na kuendelea kwa miji ya pwani na vituo vya kibiashara vilivyoibuka huko bara. Miji ilikua kutokana na biashara ya misafara ya masafa marefu. Miji iliyoanza kukua ilikuwa ya maeneo ya pwani ya Tanzania kama vile Bagamoyo, Pangani, Kilwa, Unguja na Pemba. Kadiri biashara ilivyoendelea kukua na kupanuka, ndivyo maeneo ya bara kama miji ya Mpwapwa, Kilimatinde, Itigi, Tabora, Ujiji, Mamboya, Puge na Msene ilivyozidi kukua. Watu kutoka vijijini walipeleka bidhaa zao kama nta, asali na gundi ili kuziuza kwa wafanyabiashara waliokaa katika miji hii.

(b) Kuenea kwa dini ya Kiislamu: Ujio wa Waarabu na Waajemi ulisababisha kuja kwa utamaduni wao kama mavazi, chakula na dini. Hii ilisababisha kuenea kwa dini ya Kiislamu maeneo yote ambayo wageni kutoka Mashariki ya Kati walipita na kuishi. Maeneo hayo ni ukanda wote wa mwambao wa pwani ya Tanzania, kwenye vituo vya kibiashara na kukusanyia watumwa na miji iliyokuwa na walowezi wa Kiarabu na Kiajemi. Watanzania walianza kuiga ustaarabu wa Kiarabu na Uislamu katika miji iliyopita misafara ya kibiashara.

(c) Ndoa: Ndoa inaheshimika sana na kupewa kipaumbele na umuhimu mkubwa katika utamaduni wa jamii za Kitanzania. Kutokana na uhusiano wa muda mrefu kati ya jamii hizi, Waarabu na Waajemi pamoja na wanajamii wa Kitanzania walianza kuoana na kufanikiwa kujenga familia zao. Watoto waliozaliwa walikuwa machotara. Ushahidi huu upo, hasa kwenye jamii zilizopo maeneo ya pwani, visiwa wa Pemba, Unguja, Kilwa na Mafia. Kwa mfano, licha ya asili yake kama koloni la Uajemi, ndoa nyingi baina ya wanawake wenyeji wa Kibantu wa pwani ya Tanzania na wanaume wa Kiarabu na Kiajemi zíligeuza Usultani wa Kilwa kuwa na mchanganyiko wa tamaduni za Kiajemi-Kiarabu na Kibantu unaosifiwa kwa kujenga utamaduni na kuzidi kuikuza lugha ya Kiswahili na utamaduni wa Kiswahili.

(d) Kukua kwa lugha ya Kiswahili: Kukua na kuenea kwa lugha adhimu ya Kiswahili ni moja ya matokeo ya uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na jamii kutoka Mashariki ya Kati na ya Mbali. Lugha ya Kiswahili ilizidi kukuzwa na mchanganyiko wa lugha za asili ya Kitanzania, hasa zile za Kibantu, lugha ya Kiarabu na lugha

FOR ONLINE READING ONLY

nyinginezo. Hivyo, Kiswahili kilikua kutokana na kutumika katika shughuli mbalimbali kama biashara, sherehe na nyinginezo. Kiswahili kilizidi kukua na kuenea katika mwambao wa Afrika Mashariki mara tu uhusiano kati ya jamii hizi uliposhika kasi. Baadaye kiliendelea kuenea hadi maeneo ya bara kwa kadiri misafara ya kibiashara ilivyokuwa inazidi kupanuka.

(e) Kuletwa kwa elimu na maarifa mapya: Mbali na dini ya Kiislamu, elimu, ujuzi na maarifa mapya mbalimbali yaliletwa na wageni kutoka Mashariki ya Kati na ya Mbali. Ujuzi wa namna ya kupanda miti ya miembe na mitende uliingizwa pia. Pia, walileta kilimo cha mpunga. Aidha, Waarabu walileta ujuzi wa uvuvi, utengenezaji wa majahazi pamoja na mapishi mbalimbali ya vyakula. Ujuzi huu ulienea katika maeneo ya pwani ya Tanzania na maeneo mengine ya bara. Elimu ya Kiarabu, lugha ya Kiarabu, tarakimu za Kiarabu, hasa dhana ya sifuri, elimu ya unajimu na kalenda ya Kiislamu vilianza kutumika katika Tanzania.

(f) Dawa: Aina mbalimbali za dawa za asili kutoka Uarabuni ziliIetwa katika maeneo ya Tanzania. Dawa hizo zilikuwa katika mfumo wa mitishamba na nyingine chakula. Jamii za Kitanzania zilipata maarifa mapya katika kupambana na magonjwa mbalimbali ya binadamu pamoja na wanyama wa kufugwa. Pia, jamii za Tanzania zilipata namna mpya ya kutibu mazao yao pale yanaposhambuliwa na wadudu waharibifu. Mimea tiba iliyoletwa na Waarabu kwa ajili ya kutibu magonjwa ya binadamu ilikuwa karafuu, mdalasini na viungo vingine.

(g) Uhamiaji: Kutokana na utajiri mkubwa ambao jamii za Mashariki ya Kati na ya Mbali ziliukuta katika maeneo ya Tanzania, jamii hizi ziliamua kuhamia kabisa katika nchi hii. Pamoja na mambo mengine, jamii hizo zilianzisha makazi ya kudumu na kuchukua ardhi yenye rutuba kwa ajili ya kilimo cha mazao ya kudumu kama karafuu na nazi. Baadhi wa wanajamii wa Kitanzania walitumika kama vibarua na watumwa katika mashamba haya. Vilevile, aina hii ya uchumi wa mashamba makubwa ilisababisha migogoro na hatimaye vita kwa baadhi ya jamii za Kitanzania. Wahamiaji hawa walisababisha miji kukua na kuwa masoko ya bidhaa kutoka nje ya Tanzania. Maeneo ya Kilwa, Zanzibar, Bagamoyo, Tabora na Dar es Salaam yalikaliwa na maelfu ya wahamiaji na kuanzisha makazi ya kudumu pamoja na familia zao. Idadi ya wahamiaji katika pwani ya Tanzania iliongezeka zaidi katika karne ya 19 ambapo Waarabu na Waasia, hasa Wahindi, walipokuja Zanzibar kufanya biashara. Uhamiaji huu uliambatana na ujio wa utamaduni wa Kiarabu na Kihindi.

(h) Kudhoofishwa kwa mila na desturi za jamii za Kitanzania: Madhara mengine ni kudhoofishwa kwa mila na desturi za jamii za Kitanzania na kuingia kwa utamaduni mpya kama vile dini ya Kiislamu, mavazi ya kanzu na kofia, chakula na ngoma. Vilevile, maeneo ambayo wageni

FOR ONLINE READING ONLY

hawa waliyatawala waliwalazimisha wazawa kufuata mila na desturi zao. Mila na desturi za Kiarabu na Kihindi zilianza kuenea pwani ya Tanzania na katika miji ya bara walikoenda kwa ajili ya biashara. Mila na desturi za kigeni zilianza kuonekana ni bora kuliko za jamii za Kitanzania. Hata hivyo, kiuhalisia hakuna utamaduni, mila na desturi za jamii moja zilizo bora kuliko nyingine.

(i) **Kuibuka kwa matabaka:** Kuzaliwa kwa matabaka katika jamii za Kitanzania ni athari nyingine iliyotokea kutokana na kuwa na uhusiano na jamii kutoka Mashariki ya Kati na ya Mbali. Jamii nyingi za Kitanzania kabla ya uhusiano na wageni kutoka Mashariki ya Kati na ya Mbali ziliishi kwa kumiliki mali kama ardhi na mifugo kwa pamoja. Pia, jamii hizi zilifanya kazi kwa kushirikiana. Baada ya kuja kwa wageni, yalianza kuibuka matabaka kati ya walionacho na wasionacho yaliyosababishwa na utofauti wa vipato vya wanajamii. Kulikuwa na matabaka ya watawala ambao walianza kumiliki ardhi kubwa na yenye rutuba na kuikodisha kwa watawaliwa. Wakodishaji wa ardhi walilipa kwa njia tofauti kama mazao, kazi na baadaye kwa pesa. Hii iliondoa umoja na mshikamano ambao ulikuwepo kabla ya ujio wa wageni kutoka Mashariki ya Kati na ya Mbali.

**Kazi ya kufanya 5.8**

Fanya utafiti mdogo kuhusu utamaduni wa Tanzania, kisha bainisha athari za kiutamaduni zinazoonekana kutokana na uhusiano wa sasa baina ya Tanzania na nchi za Mashariki ya Kati na ya Mbali.

*Athari za kisiasa*

(a) **Kukua kwa baadhi ya dola:** Jamii nyingine zilifanikiwa sana na kuendelea kutokana na kukua na kuendelea kwa biashara ya misafara katika maeneo yao. Kwa mfano, dola ya Kilwa ilifanikiwa kuwa dola kubwa sana barani Afrika na duniani kwa ujumla. Katika karne ya 13 na 14, Kilwa ilikuwa imeendelea sana kutokana na kuwa kituo kikubwa zaidi cha biashara katika ukanda wa bahari ya Hindi. Kilwa ilitengeneza sarafu yake kurahisisha biashara na jamii nyingine duniani. Katika karne ya 19, dola za Shambaa, Uhehe, Unyanyembe na Karagwe ziliibuka na kuwa dola zenye nguvu huko bara. Biashara ya dhahabu, pembe za ndovu, watumwa na bidhaa za wanyama na misitu ilishamiri sana katika kipindi hicho. Dola hizi zilikuwa na utawala imara ambao ulihakikisha kuna amani katika misafara ya kibiashara. Maeneo mengine yaliyoendelea ni Zanzibar, Bagamoyo na Pangani.

(b) **Kuanguka kwa baadhi ya tawala za jadi:** Kukua kwa dola mbalimbali kulisababisha pia dola zingine

FOR ONLINE READING ONLY

kuanguka. Katika kipindi hicho, jamii za Kitanzania zilikuwa katika tawala za kiukoo na kichifu. Pia, wageni wa Kiarabu walipofika katika sehemu za pwani na bara walianzisha utawala wao na kuwaondoa Watanzania katika utawala katika maeneo ya pwani ya Tanzania na Zanzibar. Hii ilisababisha baadhi ya tawala za Kitanzania kupotea kabisa. Katika maeneo ya bara kuna jamii nyingi ambazo tawala zao zilianguka, hasa kutokana na madhara ya biashara ya utumwa. Tawala hizo ni kama vile tawala za Waha na Wazinza. Aidha, tawala katika maeneo ya Pangani, Upareni na Kilimanjaro zilivunjika na kuwa tawala ndogo ndogo zisizo na nguvu kubwa. Pamoja na wageni kuleta athari hiyo, Waafrika nao walianza kutanua dola zao ili kufaidi biashara ya misafara. Kupanuka kwa dola kubwa kuliambatana na kuchukua maeneo kutoka kwa jamii za Kitanzania ambazo hazikuwa na nguvu za kujilinda kutokana na uvamizi huo. Dola ya Uhehe ilipanuka hadi Mpwapwa ilikopita misafara ya biashara kutoka pwani hadi bara na kinyume chake. Dola za Unyanyembe na Urambo nazo zilipanuka zikimeza tawala za kijadi walizozishinda katika vita vya upanuzi. Lengo la upanuzi lilikuwa kutawala njia za misafara ya biashara ili kutoza ushuru.

(c) Vita: Kutokana na ujio wa wageni na hatimaye kujimilikisha mali za jamii za Kitanzania kama ardhi, misitu na njia za usafirishaji, kulitokea migogoro ya mara kwa mara kati ya wahamiaji na jamii hizo katika kushindania rasilimali. Pia, wahamiaji walianzisha utawala wao na kutishia tawala za jadi zilizokuwapo katika kipindi hicho. Jamii za Kitanzania zilipinga mambo mbalimbali ya wageni kama mila na desturi na viongozi waligoma kuachia nafasi zao za uongozi. Pia, vita zilikuwa nyingi kama njia mojawapo ya kuwapata watumwa katika maeneo mengi ya jamii za Kitanzania.

(d) Kubadili mfumo wa jinsi ya kupata viongozi: Ujio wa biashara za masafa marefu chini ya Waarabu ulisababisha kubadili mfumo wa jinsi ya kupata viongozi kwa baadhi ya jamii za Kitanzania kutoka katika kurithi hadi nguvu za uchumi. Biashara hii iliwafaidisha baadhi ya watu waliopata nguvu si za kiuchumi tu bali hata za kisiasa baada ya kupata pesa au mali nyingi. Mfano mzuri ni mtemi Mirambo aliyepata utawala kwa sababu alikuwa tajiri na nguvu kubwa kiuchumi iliyomfanya aweze kuongoza dola kubwa na yenye nguvu ya Unyamwezi. Chifu Machemba pia alijenga dola kubwa ya Wayao.

### Zoezi 5.4

1. Kwa kutumia mifano sahihi, bainisha mila na desturi za jamii yako inayokuzunguka zenye asili ya Mashariki ya Kati na ya Mbali.
2. Ni kwa namna gani sababu za kijiografia zilisababisha kuanza na kukua kwa uhusiano wa kibiashara kati ya Tanzania na nchi za Mashariki ya Kati na ya Mbali?

FOR ONLINE READING ONLY

3. **Je, unafikiri lugha ya Kiswahili isingekuwapo kungeathiri kwa namna gani kukua kwa biashara baina ya jamii za Kitanzania na za Mashariki ya Kati na ya Mbali.**
4. **Eleza jinsi unyonyaji wa rasilimali za Kitanzania uliotokana na uhusiano wa jamii za Kitanzania na wageni ulivyoathiri maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika jamii za Kitanzania.**

## Uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na jamii za Ulaya

Pamoja na kuwa na uhusiano na watu wa Mashariki ya Kati na ya Mbali na jamii zingine za Afrika, jamii za Kitanzania zilihusiana na jamii za Ulaya pia. Miongoni mwa nchi za kwanza za Ulaya kuwa na uhusiano na nchi za Afrika Mashariki, ikiwamo Tanzania, ni Ureno. Uhusiano huu ulikuwa kati ya karne ya 15 na 17. Kipindi hicho taifa la Ureno lilikuwa chini ya uongozi wa Mfalme John wa Kwanza. Zama hizo zilitambulika kama enzi ya ugunduzi. Pamoja na mambo mengine, Wareno waliongoza misafara ya kutafuta njia ya baharini kufika India, hasa baada ya ile njia inayopita Mashariki ya Kati kufungwa katika karne ya 13. Miongoni mwa Wareno waliotumwa ni Vasco da Gama ambaye kutoka mwaka 1497 hadi 1499 alifanya safari ya kuelekea India kupitia Rasi ya Tumaini Jema (Cape of Good Hope), ambayo kwa sasa inajulikana kama Cape Town akitokea Ureno. Alifika pwani ya Afrika Mashariki mwaka 1498. Katika safari yake aliona na kushuhudia utajiri na biashara yenye thamani kubwa kwenye mwambao wa pwani ya Bahari ya Hindi. Hivyo, alivutiwa na baadaye Ureno iliyavamia na kuyatawala maeneo hayo. Wareno walistaajabu kukuta biashara yenye thamani na faida kubwa katika pwani ya Afrika Mashariki, hasa Kilwa, Sofala na Mombasa iliyokuwa inahusisha dhahabu, pembe za ndovu na watumwa.

Uvamizi wa Wareno, hasa Kilwa mwaka 1503, ulikuwa na lengo la kuzipata rasilimali hizo na kupata faida za kiuchumi na kujiimarisha kimkakati na kiulinzi katika maeneo yote waliyokuwa wanayatawala. Zaidi ya hayo, Wareno walisukumwa na tamaa yao ya kutawala maeneo ya Bahari ya Hindi ili kuwa na mamlaka na kuzidhibiti rasilimali pamoja na vituo vya biashara katika pwani ya Afrika Mashariki. Baadhi ya bidhaa zilizotumika kwenye biashara kati ya jamii za Kitanzania na zile za Ulaya zilikuwa nguo, bunduki, pombe, manukato, na shanga. Jamii za Kitanzania zilitoa bidhaa kama dhahabu, pembe za ndovu, watumwa, ngozi na bidhaa za msituni kama asali na nta. Kuanzia wakati huo, Wareno waliitawala pwani ya Afrika Mashariki kiuchumi na kisiasa. Kwa ajili ya kuona njia zilizotumika, angalia Kielelezo 5.3 ambacho kinaonesha jinsi Wareno walivyofika pwani ya Afrika Mashariki.

FOR ONLINE READING ONLY




Kielelezo 5.3. *Njia ya Wareno kutoka bara la Ulaya hadi Tanzania*

**Kazi ya kufanya 5.9**

**Kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya taarifa, bainisha sababu mbalimbali zilizosababisha Wareno kuja pwani ya Afrika Mashariki wakati wa zama za ugunduzi.**

Sababu za Wareno kuvamia pwani ya Tanzania

Kama ambavyo imeelezwa hapo awali kwa ufupi, sababu za Wareno kuivamia pwani ya Afrika Mashariki mwanzoni mwa karne ya 16 kwa upana ni masilahi ya kiuchumi. Sababu hizo ni kutafuta dhahabu na kupanua njia za biashara, kuilinda misafara yao ya kibiashara kutoka India kwenda Ulaya na utafutaji wa maeneo ya masoko. Pia, Wareno walitaka kuendeleza vita vya Wakristo dhidi ya Uislamu vilivyokuwa vinaendelea huko barani Ulaya kwa kipindi hicho na kwa hiyo kueneza Ukristo Tanzania na Afrika kwa ujumla. Vilevile, Wareno waliona kuivamia Tanzania kungepanua nguvu na fahari ya kiuchumi kwa Ureno iliyokuwa inashindana na Hispania katika kutafuta makoloni katika zama hizo. Kwa kutumia nguvu za kijeshi, waliona kuwa safari za ng'ambo ni fursa ya kuupata umaarufu na utajiri kwa taifa lao. Kama ilivyoelezwa hapo awali, viungo na kutafuta njia ya baharini kuelekea India ilikuwa sababu kubwa sana ya ujio wao. Pia, uanzishwaji wa vituo katika pwani ya Afrika ulikuwa muhimu katika juhudi zao za kutawala njia za biashara, kufikia rasilimali za thamani kama dhahabu, pembe

FOR ONLINE READING ONLY

za ndovu, watumwa, viungo vya vyakula na kupanua ushawishi wao duniani kote.

**Sababu za kuanguka kwa utawala wa Kireno**

Utawala wa Wareno katika pwani ya Afrika Mashariki ulichukua takribani miaka mia mbili (200). Utawala huu wa kimabavu ulifanya mabadiliko mengi katika nyanja zote, yaani uchumi, siasa na utamaduni. Pamoja na matumizi yake ya mabavu, ulifika wakati utawala huu ukaanguka katika maeneo haya. Utawala wa Kireno ulikoma pwani ya Tanzania mwaka 1698, baada ya Wareno kushindwa vitani na kuanguka kwa *Fort Jesus* ya Mombasa yaliyokuwa makao makuu yao. Sababu zifuatazo zilichangia kuanguka kwa utawala huu katika pwani ya Afrika Mashariki:

(a) Upinzani kutoka jamii za Kitanzania: Upinzani na mashambulizi kutoka kwa jamii za Kitanzania ambazo zilichukizwa na utawala wa Kireno kulichangia katika kuanguka kwa utawala huu. Wareno walikuwa wakatili, wanyang'anyi na wauaji kwani walikuwa wanawaua wanajamii wa Kitanzania pindi walipokataa kutii amri zao. Pia, wanajeshi wa Kireno walifanya vitendo vya udhalilishaji dhidi ya wanawake, kitu ambacho Watanzania hawakukikubali. Hivyo, walianzisha mapigano ya mara kwa mara kati yao na Wareno. Baadhi ya jamii hizo ni zile za Kilwa na Pemba, na jamii zingine za maeneo ya jirani katika pwani ya Afrika Mashariki.

(b) Upinzani na ushindani: Kulikuwa na ushindani mkubwa kutoka kwa mataifa pinzani ya Ulaya kuhusiana na umiliki wa biashara katika Bahari za Hindi na Atlantiki. Ushindani ulitoka katika mataifa kama Uhispania, Uholanzi, Uingereza na Ufaransa. Ushindani mkubwa ulikuwa unatoka kwao barani Ulaya. Ushindani huu wa nje ya Afrika uliuathiri uwezo wa Wareno katika kupambana na jamii za Kitanzania ambazo zilikuwa zinasaidiwa na Waarabu kutoka Oman, Uajemi, na Yemen. Uingereza iliwasaidia Waarabu wa Oman kumng'oa Mreno katika pwani ya Tanzania. Lengo la Uingereza lilikuwa kuwadhoofisha Wareno na hatimaye kuwaondoa katika umiliki wa biashara katika Bahari ya Hindi. Waarabu walikuwa na lengo la kuurudisha umiliki wao wa kibiashara wa pwani ya Tanzania waliokuwa nao kabla ya kunyang'anywa na Wareno katika karne ya 16. Muungano wa Waarabu na wenyeji uliuondoa utawala wa Kireno na kuweza kuirudisha biashara iliyofungwa na kudorora sana kati ya jamii za Kitanzania na ile ya Mashariki ya Kati na ya Mbali.

(c) Udhaifu wa Wareno: Wareno waliwadharau wenyeji katika utawala; hivyo, walitumia mabavu badala ya kuzishirikisha jamii za Tanzania katika shughuli zao. Wareno walilazimisha mifumo yao ya utawala na kibishara itawale jamiii za pwani ya Tanzanaia. Ureno pia haikuweza kuwa na watu wenye uwezo mkubwa wa kutawala maeneo yao yaliyokuwapo schemu mbalimbali duniani ikiwemo pwani ya Tanzania. Udhaifu huu wa kukosa watu wenye weledi ulisababisha kuwa na changamoto nyingi za kiutawala

FOR ONLINE READING ONLY

na upinzani kutoka kwa watawaliwa. Walikusanya mali mbalimbali kwa wenyeji kwa kutumia mabavu hali iliyosababisha kupata upinzani karibu katika kila eneo walilokuwa wanalitawala.

(d) Magonjwa ya kitropiki: Hali ya hewa pamoja na magonjwa ya sehemu za joto ilikuwa kikwazo kikubwa kwa Wareno kuishi kwenye maeneo ya jamii nyingi za Kitanzania. Waliugua magonjwa kama vile malaria, magonjwa ya tumbo na malale. Hii ilisababisha Wareno wengi kufa na wengine kuwa dhaifu na kurudi kwao.

(e) Kupungua kwa misafara ya biashara: Kulikuwa na kupungua kwa misafara ya biashara katika njia za mwanzo zilizokuwa zinatumika kutoka ndani ya Afrika Mashariki na wale waliokuwa wanakuja kutokea Mashariki ya Kati. Kupungua kwa misafara hii kulisababishwa na unyonyaji wa Wareno ambao ndiyo walikuwa wanadhibiti ukanda wote wa pwani ya Afrika Mashariki. Unyang'anyi wa bidhaa kwenye misafara, matumizi ya nguvu na ushuru mkubwa vilisababisha wafanyabiashara waache kutumia bandari ya Kilwa katika usafirishaji wa bidhaa. Hii ilichangia shughuli za kibiashara kudorora kwani hata wafanyabiashara kutoka Mashariki ya Kati nao walisitisha shughuli zao za kibiashara. Hii ilikuwa na madhara makubwa katika utawala wa Wareno na kuwa moja ya sababu za anguko la utawala huo.

**Kazi ya kufanya 5.10**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya taarifa, bainisha sababu zilizofanya jamii za Kitanzania kuungana na Waarabu kupinga utawala wa wareno.

### Athari za uvamizi wa Wareno

Uvamizi wa Wareno katika jamii za Kitanzania ulikuwa na athari mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Athari hizi zilitokana na mabadiliko makubwa yaliyofanywa na utawala wa Wareno katika maeneo ya pwani ya Tanzania. Jamii za Kitanzania zilishuhudia athari katika maeneo yote ya maisha kama inavyoelezwa hapa chini.

(a) Kudorora na hatimaye kuanguka kwa biashara: Lengo kubwa la Wareno kuvamia na hatimaye kutawala jamii za pwani ya Tanzania, lilikuwa ni kuidhibiti na kuiendesha biashara iliyokuwa inafanyika katika mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki. Walitaka kuthibiti biashara ya dhahabu iliyokuwa inafanyika Kilwa hadi kwenye dola ya Mwanamutapa, ambayo ni Zimbabwe ya sasa, ambako ndiko dhahabu ilikuwa ikitoka. Baada ya udhibiti wa Wareno, misafara hiyo ilianza kudhoofika kwa sababu mbalimbali zikiwamo ukatili na ukosefu wa uungwana. Matokeo yake, biashara hiyo ilizidi kuzorota na hatimaye kuanguka.

(b) Udhibiti wa biashara: Baada ya kuvamia na hatimaye kuidhibiti na

FOR ONLINE READING ONLY

kuihodhi biashara katika pwani ya Afrika Mashariki, Wareno walitawala pwani hiyo kwa takribani miaka 200. Katika kipindi chote hiki wao ndio walikuwa wanaendesha biashara na kuudhibiti usalama wa Bahari ya Hindi kuanzia Mogadishu hadi Sofala. Hii ilisababisha Wareno kudhibiti makusanyo ya kodi na biashara ya pembe za ndovu, dhahabu na watumwa katika mwambao wa pwani. Waliimarisha usalama wa kijeshi kwa kuweka vituo vya kijeshi (ngome) kwenye maeneo mbalimbali kama vile Mombasa ambako kulikuwa na kituo kikubwa kilichoitwa *Fort Jesus*. Pia, kulikuwa na vituo vya kijeshi katika maeneo mengine kama vile Unguja, Pemba, Kilwa na Bagamoyo. Ngome hizi ziliwawezesha kujilinda na kudhihirisha kuwa lengo la Wareno halikuwa kutawala tu bali pia kudhibiti biashara katika maeneo ya bahari ya Hindi.

(c) Vita: Kutokana na watawala wa Kireno kutumia njia ya nguvu nyingi kutawala maeneo ya mwambao wa Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla wake, walisababisha machafuko ya mara kwa mara kati ya jamii za Kitanzania na wao. Hii ilisababisha maeneo mengi kukosa utulivu na kuwa na mapambano kati ya jamii za pwani ya Tanzania dhidi ya Wareno. Pia, jamii za pwani ya Tanzania zilishirikiana na jamii nyingine kama wafanyabiashara Waarabu na Waajemi kupambana dhidi ya Wareno. Katika mapambano haya yote, watu wengi walifariki, walipotea na wengine kujeruhiwa na kupata ulemavu wa kudumu.

(d) Kuenea kwa dini ya Kikristo: Matokeo mengine ya kuwapo kwa Wareno katika pwani ya Afrika Mashariki ni kusambazwa kwa dini ya Ukristo katika maeneo yote ambayo Wareno walifanikiwa kutawala. Wareno walisambaza dini ya Kikristo kama sehemu ya kupambana na Waarabu ambao nao walikuwa wanaieneza dini ya Kiislamu. Changamoto kubwa ilikuwa kwamba, katika maeneo ya mwambao wa pwani ambako Wareno walikuwa wanatawala Uislamu ulikuwa tayari umeshika mizizi kwa takribani karne 8. Pamoja na ugumu huu, Wareno walijenga makanisa Zanzibar na Pemba. Kwa hiyo, kuenea kwa Ukristo kulikuwa polepole sana kati ya karne ya 16 na 17. Mafanikio zaidi ya uinjilishaji wa Ukristo yalikuja baadaye wakati walipokuja wamisionari na ukoloni kutoka Ulaya Magharibi katika karne ya 19.

(e) Kuingizwa kwa mazao mapya: Ujio wa Wareno ulileta baadhi ya mazao ambayo hapo awali hayakuwepo katika maeneo ya Tanzania. Mbali ya Wareno kutegemea vyakula kama matunda na mboga za majani, walileta pia vyakula ambavyo walikuwa wamevizoea na kupanda kwenye ardhi ya Watanzania. Waliamua kuzalisha mazao hayo ili yatumiwe na wanajeshi pamoja na wafanyakazi

FOR ONLINE READING ONLY

wengine ambao walikuwa wanaishi katika pwani ya Afrika Mashariki. Baadhi ya mazao hayo ni kama vile mihogo na mahindi.

(f) **Msamiati wa Kireno kuingia kwenye Lugha ya Kiswahili:** Kutokana na mwingiliano kati ya jamii za Kitanzania na Wareno, kulitokea uingizaji wa baadhi ya maneno ya lugha ya Kireno katika lugha ya Kiswahili. Maneno kama *gereza, meza, bendera* na *pesa* yametoholewa kutoka katika lugha ya Kireno, ambayo hadi sasa yanatumika katika lugha ya Kiswahili.

(g) **Uharibifu wa mali kama vile majengo:** Kuingia kwa utawala wa Kireno kuliambatana na matumizi ya nguvu za kijeshi baada ya watawala wengi wa pwani ya Tanzania na Afrika Mashariki kukataa kuingia makubaliano yoyote ya kibiashara na utawala na Wareno. Jamii za pwani ya Tanzania zilizokataa kuwa chini ya utawala wa Wareno ziliingiliwa kijeshi. Kwa mfano, Sultani wa Kilwa alipokataa kutii amri ya Wareno ya kujisalimisha kwa utawala wa Kireno, wanajeshi wa Kireno chini ya Fransisco de Almeida walivamia Kilwa mwaka 1505. Katika uvamizi huu, sehemu kubwa ya mji wa Kilwa ikawa imeharibiwa vibaya na kugeuka magofu kutokana na mashambulizi ya Wareno. Hali hii ya uharibifu ilikuwa wazi pia katika maeneo mengi ambako Wareno walienda kutawala kama Unguja na Pemba. Walitumia nguvu na vita na kusababisha uharibifu mkubwa wa mali kama vile majengo na mazao.

(h) **Kubadili uelekeo wa biashara:** Wareno waliubadili uelekeo wa biashara uliokuwa umezoeleka katika pwani ya Tanzania na kusababisha mdororo wa biashara katika maeneo haya. Wareno walibadilisha uelekeo wa biashara kwenda Mashariki ya Kati na ya Mbali na kuielekeza Ulaya na Amerika kupitia Bahari ya Atlantiki. Kitendo hiki kiliathiri sana biashara katika Bahari ya Hindi na kusababisha kushuka kwa biashara katika pwani ya Tanzania.

FOR ONLINE READING ONLY

## Uhusiano wa mifumo ya maadili ya Kitanzania na jamii zingine

Mifumo ya maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni iliundwa kutokana na malengo ya jamii iliyohusika kwa madhumuni ya kuondoa changamoto za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa zilizokuwapo katika jamii hizo. Mifumo hii iliyajenga, iliyalinda na kuyatunza maadili ya Kitanzania kwa njia mbalimbali kama vile utoaji wa elimu, mila na desturi, miiko, sheria, utaratibu, sanaa na mengineyo. Baada ya ujio wa jamii zingine kama Waarabu, Waajemi, Wazungu na jamii zingine kutoka maeneo mbalimbali, mifumo ya usimamizi wa maadili ya Kitanzania iliathirika kwa namna moja au nyingine. Mifumo iliyoletwa na jamii nyingine haikufanana kwa falsafa, malengo na mbinu za mifumo ya jamii za Kitanzania kwa namna mbalimbali.

Imani za kidini

Ujio wa dini za kigeni uliambatana na kuingia kwa imani mbalimbali za kigeni. Waarabu walikuja na dini ya Kiislamu na Wazungu walikuja na dini ya Kikristo. Imani ya dini hizi kwa kiasi kikubwa zilitofautiana na imani za dini za jadi za jamii za Kitanzania. Maisha katika jamii za pwani ya Tanzania kwa kiasi kikubwa yalihusishwa na imani ya dini. Imani za dini zilihusika na matambiko, sherehe, misiba, ulinzi wa jamii, mazingira, rasilimali na kadhalika. Hapakuwapo na muda maalumu wa kuabudu kwani imani za dini zilifanyika muda wote. Shughuli zote zilizofanyika katika jamii zilihusishwa na kutafsiriwa kwa uwapo wa nguvu za mizimu na miungu. Kwa kiasi kikubwa, ujio wa wageni uliziathiri imani hizi za dini na namna mbalimbali za kimuundo, kimaudhui na utekelezaji wake. Imani za dini zilizoletwa na Waarabu na Wazungu zilikuwa na utaratibu maalumu wa namna ya kuabudu imani hizo. Kwa mfano, katika Uislamu, ibada ilifanyika msikitini na kwa upande wa Ukristo ibada ilifanyika kanisani. Pia, suala la imani lilibaki kuwa uamuzi wa mtu mmoja mmoja wakati katika dini za jadi imani ya dini ni suala la lazima na ni kwa jamii nzima. Vilevile, mafundisho ya dini za kigeni yalikataza mila na desturi mbalimbali za Kitanzania kama vile upigaji ramli, matambiko, dawa za asili na suala la kuoa wake wengi kwa wale walioongokea dini ya Ukristo.

Mfumo wa elimu

Mfumo wa elimu wa jamii za Kitanzania kabla ya ujio wa wageni ulikuwa mfumo wa utoaji elimu usiokuwa rasmi. Elimu ilitolewa kupitia njia mbalimbali za asili. Mfumo huu ulizingatia mafundisho kwa watoto na vijana kukua kwa kuzingatia mila na desturi za Kitanzania. Mafundisho haya yalikuwa ya kivitendo zaidi kuliko nadharia na yalitolewa kupitia masimulizi ya mdomo, miiko, muziki na ngoma. Mafundisho haya yalizingatia zaidi rika kuliko umri na yalitolewa katika familia, ukoo na jamii yote kwa ujumla. Vilevile, ilikuwa lazima kwa kila mwanajamii kupitia elimu hizo. Pia, elimu iliyotolewa iliendana na mazingira halisi yaliyowazunguka. Vijana walifundishwa mila na desturi kama heshima, utii, ukarimu, upendo na shughuli za kiuchumi kama kilimo, biashara, ufugaji na uwindaji. Mfumo huu wa elimu ulitumika kutoka kizazi kimoja hadi kingine na ulikuwa njia pekee ya kuhamisha ujuzi na maarifa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Walipokuja wageni, hasa Waarabu na Wazungu, walileta mifumo mipya ya elimu ambayo ilitofautiana na mifumo ya awali ya Kitanzania kwa kiasi kikubwa. Mifumo hiyo ilikuwa tofauti kimuundo kwani ilitolewa kwenye majengo maalumu, yaani madrasa kwa Waislamu na shule kwa wamisionari wa Kizungu. Shule zilijengwa na wamisionari walioingia Tanzania katika maeneo mbalimbali na kuanzisha elimu ya kimagharibi wakiwa na lengo la kueneza dini na kuchunguza maeneo mbalimbali ya nchi ya Tanzania. Shule hizo zilifundisha elimu kwa mfumo wa nadharia na kwa kipindi maalumu. Wale waliofaulu

FOR ONLINE READING ONLY

waliendelea na wasiofaulu waliachwa. Pia, suala la elimu halikuwa la jamii nzima ila la mtu binafsi. Aidha, maudhui yaliyotolewa hayakuendana na mazingira ya Kitanzania kwa kiasi kikubwa.

**Mfumo wa kijamii**

Jamii za Kitanzania zilithaminiana sana na kuishi kwa kushirikiana, kwa usawa na kuheshimiana. Kulikuwa na maadili kwa jumuiya nzima na kila mtu alikuwa na thamani na nafasi sawa katika jamii. Mfumo wa maadili ya kijamii ulikuwa ndio dira iliyoonesha namna ya kushirikiana kufikia lengo la jamii katika kutimiza mipango iliyohusika. Kuelewana kwa wanajamii kulienda zaidi ya uhusiano wa kindugu au kibiolojia katika kutekeleza maadili katika jamii. Jamii za Kitanzania zilishirikiana, zilijaliana, zilitegemeana na ziliungana katika kutekeleza mambo mbalimbali. Chochote kilichotokea kwa mtu kilitokea kwa jamii nzima. Kwa mfano, furaha au huzuni ya mtu mmoja ilienea kwa wanajamii wengine wote. Kulikuwa na utayari wa kuwasaidia wengine kwa maendeleo ya jamii yenye usawa. Hii ilipingana na ubinafsi ulioletwa na Waarabu na Wazungu ambao mafundisho yao, kupitia elimu, yalisababisha kujenga haiba ya mtu mmojammoja zaidi kuliko haiba ya jamii nzima. Mifumo ya elimu ya kigeni ilifundisha umuhimu wa mtu binafsi kupambana ili ajiletee maendeleo kama kujilimbikizia mali kupitia kumiliki mashamba makubwa na watumwa pamoja na kuhodhi biashara. Hii ilisababisha kuibuka kwa matabaka na kuudhoofisha umoja na mshikamano uliokuwapo hapo awali kabla mifumo ya kimaadili ya wageni haijaingia katika jamii za Kitanzania.

**Mfumo wa uchumi**

Mfumo wa uchumi ni eneo lingine ambalo lilikuwa muhimu katika kuathiri maadili ya jamii za Kitanzania. Katika jamii za Kitanzania, mali zilimilikiwa na jamii nzima na hakukuwa na mali binafsi. Ardhi kama njia kuu ya uzalishaji mali ilikuwa mali ya jamii nzima na iligawanywa kwa wote. Hapakuwa na mtu binafsi aliyekuwa anamiliki ardhi. Vilevile, shughuli za uzalishaji mali kama kilimo, uvuvi, uwindaji na biashara zilifanywa na jamii yote kwa pamoja. Aidha, kilichopatikana kiligawanywa kwa usawa kwa wanajamii wote. Maadili ya jamii hizi yalisisitiza umoja, mshikamano, upendo na usawa katika kufanya shughuli mbalimbali. Hii ilikuwa tofauti kwa mifumo ya uzalishaji mali iliyoletwa na wageni wa Kiarabu na Kizungu ambayo iliruhusu umiliki wa mali kwa watu binafsi katika jamii.

Mifumo ya kimaadili ya wageni ilisisitiza ufanyaji kazi kwa bidii kwa mtu mmoja mmoja wakati mifumo ya kijamii ya Kitanzania ilisisitiza ufanyaji kazi kwa bidii kwa jumuiya nzima ili kinachopatikana kigawanywe sawa kwa wote. Ufanyaji kazi ulipewa kipaumbele kikubwa sana katika jamii, na wale wachapakazi walipewa heshima na kuthaminiwa katika familia na jamii. Kwa ujumla, watu ambao si wachapakazi walidharaulika sana, na ndio wengi waliokuwa wahanga wa

FOR ONLINE READING ONLY

utumwa katika mfumo mpya wa kitabaka ulioletwa na wageni. Utamaduni wa wageni ulianza kuruhusu watu wanyonyaji kuanza kujiingizia kipato bila kufanya kazi, kinyume na mila na desturi za Kitanzania.

**Mifumo ya kiutawala**

Mifumo ya utawala ya jamii za Kitanzania ilikuwa na muundo wa kiungozi ambao ulitokana na asili za jamii iliyohusika, ambapo mpangilio wake ulitokana na ukoo au kabila. Mpangilio huo uliendana na mgawanyo wa madaraka na umiliki wa ardhi wa jamii iliyohusika. Kiongozi ndiye alikuwa na jukumu la kutoa maelekezo mbalimbali kuhusiana na masuala kama vile kugawa ardhi, kutatua migogoro, kutangaza msimu wa kuanza kilimo na kuanza kuvuna na sherehe mbalimbali. Vilevile, jukumu la kuyasimamia na kuyalinda maadili lilikuwa la viongozi wa jadi. Kulikuwa na mahakama na vyombo vingine vya kulinda maadili na kuhakikisha utoaji wa haki. Muundo wa serikali ulishuka hadi ngazi ya chini kutegemea na ngazi husika, hii ilifanywa mahususi ili kuzuia rushwa, upendeleo, na kulinda maadili. Watawala pia ndiyo waliokuwa wanasimamia ulinzi wa jamii kwa kuhakikisha usalama wa jamii na kushirikisha jamii kwa kufanya matambiko mbalimbali ili kujilinda na majanga. Tofauti na mfumo wa jamii za Kitanzania, mifumo iliyoletwa na wageni ilihodhiwa na watu wachache na madaraka makubwa yalikuwa katika vyeo vya juu, ambao walikuwa na uamuzi wa mwisho pia. Mifumo ya Wazungu, kwa mfano, ilitofautiana na mifumo ya jamii za Kitanzania kwani ilitenganishwa na dini. Aidha, jukumu la uangalizi wa sheria, mgawanyo wa madaraka, ulinzi wa jamii, na kulinda maadili lilikuwa jukumu la vyombo vya utawala.

**Mifumo ya kiutamaduni**

Mila na desturi, afya, michezo, vyakula na mavazi vilikuwa sehemu ya utamaduni katika jamii za Kitanzania. Mila na desturi zilihusisha taratibu, sheria, kanuni, miiko na matambiko ambayo ni ibada za kutolea sadaka kwa mizimu na miungu ya kijadi. Huduma za afya kwa kiasi kikubwa zilihusisha mitishamba, matambiko na waganga wa jadi ambapo, kwa mfano, huduma za afya na mtoto kwa kinamama zilitolewa na wakunga wa jadi. Katika utoaji wa huduma za afya kulikuwa na huduma za ushauri nasaha, hasa kwa kinamama kuhusu masuala ya ndoa. Huduma hii ilitolewa na watu wazima wenye uzoefu na masuala ya ndoa ambao waliitwa kungwi. Hakukuwa na eneo maalumu la kutolea huduma za afya kwani huduma ilitolewa eneo lolote kutegemeana na mahali alipo mgonjwa.

Pia, kulikuwa na michezo mbalimbali kama kuvuta kamba, kuruka kamba, kucheza ngoma, kuogelea katika mabwawa na mito, mieleka, riadha, na kulenga shabaha, ikiwa na lengo la kujifurahisha na kujiimarisha kiafya na ukakamavu wa mwili. Aidha, kulikuwa na mitindo mbalimbali ya mapishi kama vile kuchemsha, kukaanga, kuoka na kubanika vyakula. Aina ya mapishi ilitegemea aina ya chakula, tukio na majira husika. Kulikuwa na mitindo ya kunyoa

FOR ONLINE READING ONLY

na kusuka nywele pia. Vilevile, chakula kilitumika kama sehemu ya kuonesha ukarimu na heshima kwa wageni na jamii. Sanjari na hayo, mavazi yalitengenezwa kutokana na rasilimali zilizopatikana kwenye jamii husika. Kwa mfano, mavazi yalitokana na ngozi za wanyama, sufi na magome ya miti ambapo mavazi hayo yalitumika kujisitiri na kujikinga na baridi au jua.

Kwa upande wa utamaduni, wageni walileta tamaduni zao ambazo kwa kiasi kikubwa zilikuwa zinapingana na baadhi ya mambo katika tamaduni za Kitanzania. Aidha, mfumo wao wa matibabu ulikuwa tofauti na wa jamii za Kitanzania, kwa mfano, mfumo wao wa matibabu haukuhusisha matambiko na walipiga marufuku matumizi ya ramli kwa sababu waliona kuwa ni imani potofu. Vilevile, walitumia vituo maalumu vya kutolea huduma ambazo ni hospitali. Michezo, vyakula, mavazi na muziki vilivyoletwa na wageni havikuwa na uhusiano wowote na jamii za Kitanzania. Lengo lake lilikuwa kueneza kasumba kuwa imani na tamaduni za kigeni ni bora kuliko za Watanzania.

**Sayansi na teknolojia**

Ujio wa wageni kutoka Mashariki ya Kati, Mbali na Ulaya uliambatana na kuletwa kwa teknolojia mpya katika jamii za Kitanzania. Maendeleo ya sayansi na teknolojia kwa jamii za Kitanzania yalitegemea zaidi mazingira yaliyowazunguka. Kwa mfano, katika maeneo yenye mito, maziwa na bahari walikuwa wameendelea sana katika teknolojia ya uvuvi na, hivyo hivyo katika maeneo yenye kilimo, ufugaji na uwindaji. Uzalishaji wa mazao ya chakula, utengenezaji wa mavazi, nyumba na shughuli zote za kiuchumi na kiutamaduni ulitegemea teknolojia katika jamii iliyohusika. Teknolojia hizi zilijitosheleza na zilikua kulingana na wakati. Pia, zilikuwa rafiki katika mazingira kwa kuwa ziliwezesha uzalishaji wa bidhaa ambazo hazikuwa na madhara kwa jamii. Ujio wa wageni ulisababisha kuingia kwa bidhaa mbalimbali kutoka kwa wageni ambapo baadhi yake zilikuwa na faida na nyingine zilikuwa na madhara. Bidhaa kama sime, jambia, bunduki, pombe, na sigara hazikuendana na maadili ya Kitanzania kwa kiasi kikubwa kwani zilisababisha uvunjaji wa maadili na kuleta tabia zisizo za kimaadili kama ulevi, uzinzi, vita na mauaji katika jamii za Kitanzania.

FOR ONLINE READING ONLY

**Zoezi 5.5**

1. Eleza athari za utawala wa Kireno katika maadili ya Kitanzania.
2. Ni kwa nini jamii za Mashariki ya Kati zilishirikiana na jamii za Kitanzania kupambana na Utawala wa Kireno?
3. Kwa nini Wareno walitawala eneo la pwani ya Tanzania tu na hawakujishughulisha sana na maeneo ya ndani ya Tanzania bara?
4. Ni namna gani teknolojia ya bahari iliwasaidia Wareno kutawala pwani ya Tanzania.
5. Kwa nini Wareno walibadilisha

uelekeo wa biashara kutoka kwenda Mashariki ya Mbali na Kati hadi kuelekea Ulaya na Amerika kupitia bahari ya Atlantiki?

## Zoezi la marudio

1. Eleza uhusiano uliopo kati ya matambiko na mizimu katika kujenga maadili ya jamii.
2. Ni kwa jinsi gani uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na jamii nyingine duniani kabla ya ukoloni ulichangia mabadiliko ya maadili ya jamii za Kitanzania?
3. Jadili namna dini za asili zilivyoathiriwa na ujio wa dini za Kiislamu na Kikristo.
4. Ni kwa namna gani ngoma, muziki na sanaa viliathiriwa na ujio wa wageni?
5. Kwa nini pamoja na ujio wa dini kutoka kwa wageni bado imani za dini za asili ziliendelea kuwapo katika jamii?
6. Ni taratibu zipi za kimaadili zilizopo leo ambazo zimetokana na jamii za Kitanzania kuwa na uhusiano na jamii za Waarabu na Wazungu?
7. Ni kwa namna gani kuibuka kwa matabaka kulisababisha tofauti za kiuchumi miongoni mwa wanajamii wa Kitanzania baada ya kuja kwa wageni kutoka Mashariki ya Kati?

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Sita
# Mifumo ya kihistoria na maadili kabla ya ukoloni

## Utangulizi

*Kuelewa mifumo ya kihistoria na maadili ya Kitanzania kabla ya ukoloni ni msingi muhimu katika kudumisha utambulisho wa taifa na kuendeleza maadili yetu katika ulimwengu wa leo. Katika sura hii, utajifunza mabadiliko katika historia ya maadili yaliyotokana na uhusiano wa kihistoria kati ya jamii za Kitanzania na jamii nyingine. Pia, utajifunza matokeo ya mapokeo ya mifumo ya kihistoria na maadili ya Kitanzania kabla ya ukoloni na mapokeo ya kidini na namna yalivyochangia katika kuyajenga maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. Umahiri utakaoujenga utakusaidia kuthamini historia na maadili ya Kitanzania na kuyaishi.*

**Fikiri**

**Historia ya maadili ya jamii za Kitanzania.**

FOR ONLINE READING ONLY

### Mabadiliko ya kihistoria na maadili Tanzania

Tanzania, kama jamii zingine duniani, ina mifumo yake ya maadili ambayo ina mizizi ya kihistoria kutoka zama za mababu na mabibi zetu. Kuwapo kwa maadili ya Kitanzania ya sasa ni matokeo ya uhusiano kati ya mifumo ya maadili iliyowekwa na mababu na mabibi zetu kupitia mila na desturi pamoja na uhusiano na jamii nyingine na ushawishi wa kisiasa. Maadili ya Kitanzania yamepitia hatua mbalimbali hadi sasa. Hii ilitokana na matukio ya kihistoria ambayo yamesababisha mabadiliko ya kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi ambayo jamii yetu ya Tanzania imeyapitia. Matukio hayo ya kihistoria ni pamoja na uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na za mataifa ya nje kama yale ya bara la Asia katika nchi za India, China, Indonesia, Oman, Uajemi, Saudi Arabia na Yemen. Kwa upande wa Ulaya kuna nchi kama vile Ureno, Ufaransa, Uingereza na Ujerumani. Hivyo, mwingiliano katika kipindi chote cha uhusiano na mataifa hayo kulichangia kwa namna moja au nyingine kubadilika kwa mifumo ya maadili ya jamii za Kitanzania.

Zaidi ya hapo, Tanzania, kama nchi

nyingine za Afrika, imeathiriwa na mila na desturi za jamii zingine kutokana na mwingiliano na jamii za mataifa jirani. Mila na desturi hizo mara nyingi zilikita mizizi katika maadili ya jumuiya, mifumo ya utawala na utamaduni ambao ulitawala uhusiano wa ndani wa jamii na kati ya jamii moja na nyingine.

**Chimbuko la maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni**

Asili ya maadili katika jamii inatokana na mfumo wa pamoja wa imani, mila na desturi, sheria, na kanuni ambazo zimekuwapo kwa muda mrefu. Katika historia kuna vyanzo mbalimbali ambavyo vimechangia mabadiliko ya maadili katika jamii za Kitanzania. Miongoni mwa vyanzo hivyo ni pamoja na:

*Masimulizi ya mdomo:* Jamii ya watu wengi wa kale wa Tanzania walitumia hekaya na hadithi kueleza chanzo cha maadili katika jamii za Kitanzania. Masimulizi ya mdomo yalikuwa na dhima kubwa katika kutafsiri mila na desturi, kusambaza maarifa, kuelezea sanaa mbalimbali za asili na kuzitunza na kuzikusanya kumbukumbu kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia maongezi au nyimbo. Njia hii ya masimulizi ya mdomo ilihusisha hadithi, mashairi, ngonjera na utani ambavyo vilisaidia sana katika kujenga maadili katika jamii za Kitanzania.

*Tafakuri ya kifalsafa na kisanii:* Wanafalsafa mbalimbali na watu wenye busara katika jamii walisaidia katika kujenga maadili katika jamii. Viongozi wa jamii walikuwa na dhima kubwa ya kuangalia mustakabali wa jamii. Hii ilisababisha wafanye tafakuri mbalimbali za kifalsafa. Maelekezo ya kifalsafa yalikuwa na dhima kubwa katika kuonya, kuelimisha na kuleta hamasa katika jamii. Kwa mfano, misemo ya wahenga kama, "Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu" au "Mchuma janga hula na wa kwao", iliwafanya watu wawe watiifu kwenye jamii. Kulikuwa na wanafalsafa na washairi wa Kitanzania ambao waliandika kuhusu utamaduni wa jamii mbalimbali, kwa mfano, "Mwanakupona Binti Mshamu aliyeishi huko Pate ambaye alitunga utenzi unaojulikana kwa jina la "Mwanakupona" kwa ajili ya binti yake Mwana Hashima Binti Mataka mwaka 1275. Alitunga ili kumuasa binti huyu kuhusu kuheshimu mila na desturi za jamii.

*Mageuzi:* Hakuna jamii isiyobadilika. Jamii za Kitanzania zilipiga hatua mbalimbali za kimaendeleo kutoka kipindi kimoja kwenda kingine, jambo ambalo lilisababisha mageuzi katika sekta mbalimbali kama vile uchumi, utamaduni, na siasa. Hali ilikuwa vivyo hivyo kwenye maadili kwani maendeleo yalisababisha mabadiliko kwenye kanuni, sheria, taratibu na miiko katika jamii. Mabadiliko katika maadili yalisababishwa na matokeo ya changamoto na utatuzi mbalimbali vilivyojitokeza katika vipindi tofauti.

*Mila na desturi:* Chanzo kingine cha maadili ni kuwapo kwa mila na desturi ambazo zilidumu kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mapokeo hayo ya mila na desturi yalijenga mtindo wa maisha ambao jamii nzima iliufuata kama mwongozo na mwelekeo wa jamii nzima. Kwa hiyo, matambiko, sherehe, sheria, taratibu na

FOR ONLINE READING ONLY

kanuni za kijamii ni matokeo ya kihistoria. Mila na desturi zilikusanya mambo yote mazuri yaliyotakiwa kufuatwa kwenye jamii inayohusika kama vile utu, uungwana, uhodari, uchapa kazi, uzalendo, uadilifu na ukweli. Mila na desturi zilirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia mbalimbali kama vile masimulizi, utoaji wa elimu na kuiga kwa vitendo.

*Matukio ya kihistoria:* Matukio ya kihistoria kama magonjwa, vita, mafuriko, matetemeko, njaa, uhamaji na shughuli za kiuchumi kama biashara, kilimo, uwindaji na uvuvi, vyote kwa pamoja, ni chanzo cha maadili ya jamii za Tanzania. Matukio haya yalisababisha jamii kuunda utaratibu, sheria, kanuni na miongozo ya namna bora ya kuishi katika jamii ili kujikinga na changamoto hizo.

## Mambo yaliyochangia mabadiliko ya maadili kutokana na uhusiano wa kihistoria

Kulikuwa na matukio mbalimbali ya kihistoria ambayo yalichangia mabadiliko ya maadili katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. Miongoni mwa matukio hayo ni pamoja na:

*(a) Mwingiliano wa utamaduni*

Mabadiliko ya maadili ya jamii za Kitanzania yaliathiriwa na mwingiliano wa utamaduni na uhusiano wa jamii mbalimbali za kigeni kutoka katika mataifa ya mabara ya Asia na Ulaya. Uhusiano huu ulisababishwa na shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii, hasa biashara ambayo iliwaleta watu pamoja kutoka katika sehemu mbalimbali. Hii ilisababisha utamaduni wa sehemu nyingine kuingia katika jamii za Kitanzania kama vile imani za dini, mavazi, chakula na muziki na michezo. Utamaduni mpya ulisababisha kuibuka kwa maadili mbalimbali kutokana na mtindo mpya wa maadili kutoka jamii zingine.

*(b) Athari za kibiashara*

Biashara ilikuwa ndiyo shughuli kuu iliyozikutanisha jamii mbalimbali pamoja. Katika uhusiano huo kulihitajika utaratibu maalumu wa jinsi ya kuongoza biashara, ubadilishanaji wa bidhaa, uhifadhi na usafirishaji. Biashara ilihitaji uaminifu, ushirikiano, upendo na kuwasiliana. Kabla ya ujio wa wageni, biashara ilifanyika kwa kuzingatia maadili ya Kitanzania ambayo ni kubadilishana bidhaa kwa bidhaa lakini baada ya kuingia kwa Waarabu na Waajemi, biashara ilianza kufanyika kwa misingi na miongozo ya kanuni za Uislamu. Wafanyabiashara hawakuruhusiwa kutoza bei kubwa kwa bidhaa zao. Aidha, biashara ilisababisha kukua kwa miji, kuongezeka kwa watu na kubadili mtindo wa maisha. Hivyo, mwingiliano wa jamii mbalimbali ulichangia kuleta mabadiliko ya maadili ya jamii ya wenyeji.

*(c) Uhamaji*

Uhamaji wa watu kutoka eneo moja na kwenda kuishi eneo lingine kulichangia kwa kiasi kikubwa mwingiliano wa mila na desturi kwa jamii za Kitanzania. Kwa mfano, kuhamia kwa Waarabu na Waajemi katika pwani ya Tanzania kulisababisha jamii za Kitanzania kuiga mila na desturi zao na kusababisha mila hizo kuwa sehemu ya maadili ya Watanzania hadi sasa. Mwingiliano wa tamaduni ulichangia kutokea kwa utamdaduni chotara. Kwa mfano, mwingiliano wa Wabantu, Waarabu

FOR ONLINE READING ONLY

na Waajemi ulioenda pamoja na ndoa na biashara huko Kilwa, Bagamoyo na Zanzibar ulitengeneza utamaduni chotara unaoitwa Uajemi-Uarabu. Vilevile, jamii za Kitanzania zilikuwa zinahama eneo moja kwenda jingine kutafuta maeneo mapya ya kilimo, mifugo na ardhi yenye rutuba. Kuhama huko kulisababisha kukutana na jamii zingine na hivyo maadili kubadilika kulingana na mazingira mapya.

*(d) Kukua kwa miji*

Ukuaji wa miji ulichangiwa zaidi na uhusiano wa kibiashara kati ya jamii moja na nyingine kupitia shughuli mbalimbali za kibiashara. Kukua kwa miji kama Unguja, Pangani, Kilwa na Pemba kulisababisha mabadiliko ya kimaadili yaliyotokana na mfumo mpya wa maisha ya mjini. Miji hii ilikusanya watu wa jamii tofautitofauti wenye matabaka yao, historia yao na shughuli zao za kiuchumi. Kuwapo kwa miji kulisababisha kuibuka kwa mila na desturi ambazo hazikuwapo hapo awali. Ukuaji wa miji ya pwani ulibadilisha mtindo wa maisha na uhusiano wa kijamii na maadili. Hali hii ilisababisha muundo mpya wa mfumo wa maadili ili kuweza kuimarisha umoja, amani na mshikamano katika jamii.

*(e) Mabadiliko katika mifumo ya utawala*

Mabadiliko ya maadili katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni yaliathiriwa pia na kubadilika kwa mifumo ya kiutawala. Katika maeneo mengine zilipoishi jamii za Kitanzania wahamiaji kutoka Uarabuni, Uajemi na Ulaya walitawala. Katika utawala wao walibadilisha taratibu na sheria mbalimbali na kuendesha utawala kulingana na mila na desturi za kwao. Kwa mfano, Kilwa ilitawaliwa na Ali Bin Al-Hassan Shiraz kutoka Uajemi wakati Zanzibar ilitawaliwa na Sultan Seyyid Said kutoka Oman. Viongozi hawa kwa kiasi kikubwa walishiriki katika kubadilisha mifumo ya maadili ya jamii za Kitanzania na kuleta ya kwao kama vile imani ya dini, na utaratibu wa utoaji elimu na afya; na hivyo, kuzuia mila na desturi ambazo zilikuwa zinapingana na utamaduni wao.

*(f) Imani za kidini*

Kuenea kwa dini za Uislamu na Ukristo nchini Tanzania kulichangia kubadilisha mfumo wa maadili katika jamii zilizokuwa katika maeneo yenye Uislamu na Ukristo. Mafunzo ya imani za kidini yalizalisha misingi, miongozo na kanuni ambazo ziliongoza mwenendo wa mtu binafsi na jamii kwa ujumla. Taratibu mbalimbali za kidini zilizoletwa na wageni zilijipenyeza kwenye utaratibu mzima wa jamii za Kitanzania na kusababisha baadhi ya maadili ya jamii za Kitanzania kuachwa au kubadilika kulingana na maadili yaliyoletwa na dini iliyohusika.

*(g) Migogoro na majanga*

Matukio mbalimbali ya kihistoria katika jamii kama vile migogoro na vita yalichangia kwa kiasi kikubwa katika kuibadilisha jamii kimtazamo na kifikra. Jamii ililazimika kubuni mfumo mpya wa maadili ili kupambana na changamoto zilizojitokeza kama vile vita, migogoro na majanga ya asili kama njaa, ukame, na mafuriko. Jamii ilianza kujenga maadili kama ukakamavu, ujasiri, na uhodari ili kutatua changamoto hizo. Wale wote ambao walionesha ari na nia katika mapambano ili kulinda jamii yao walionekana ni mfano bora katika jamii inayohusika.

FOR ONLINE READING ONLY

**Kazi ya kufanya 6.1**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, ikiwamo mtandao, fanya utafiti kuhusu maadili halafu eleza kwa nini mabadiliko katika maadili ni jambo lisiloepukika.

**Zoezi 6.1**

1. Kwa kutumia mifano, eleza kwa nini maadili hubadilika kutoka kipindi kimoja hadi kingine.
2. Eleza uhusiano uliopo kati ya dini na kukua kwa maadili ya Kitanzania.
3. Kwa nini uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na Wareno haukuwa na athari kubwa katika mabadiliko ya kimaadili?
4. Je, unafikiri ni kwa nini lugha ya Kiswahili ina mchango katika ujenzi wa maadili katika jamii za Kitanzania?

## Matokeo ya mapokeo ya mifumo ya kihistoria na maadili

Matokeo ya mapokeo ya mifumo ya kihistoria na maadili ya Kitanzania kutokana na uhusiano wa jamii mbalimbali za Kitanzania na zile za Mashariki ya Kati, Mbali na Ulaya yalikuwa na athari nyingi kwa jamii za Kitanzania kabla ya kuingia kwa ukoloni. Athari hizi zilibadili mwelekeo wa mfumo wa maadili ya Kitanzania kwa kuongeza au kubadili vipengele kadhaa vya kimapokeo vya kijamii na vile vipya vilivyoletwa na wageni kama Waarabu, Waajemi, Washihiri, Wahindi na Wazungu.

Matokeo ya mapokeo ya uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na zile za kigeni yalikuwa na athari hasi na chanya kama ifuatavyo:

### Kufifia kwa baadhi ya mila na desturi

Uhusiano wa Tanzania na jamii nyingine ulileta desturi mpya za kiutamaduni na kiimani katika jamii za Kitanzania. Hali hii ilisababisha kudhoofika kwa baadhi ya mila na desturi za Kitanzania ambazo zilifunikwa na mila na desturi za wageni. Baadhi ya mila na desturi ambazo ziliathiriwa ni pamoja na dini za jadi, matambiko ya asili, jando na unyago, mavazi pamoja na matumizi ya baadhi ya vyakula na vinywaji vya asili.

### Kuibuka kwa imani mpya za kidini

Athari nyingine ilikuwa kuibuka kwa dini zingine zilizoletwa na wageni kutoka Mashariki ya Kati, ya Mbali na Ulaya ambazo zilikuwa ni Uislamu na Ukristo mtawalia. Kwa kiasi kikubwa imani hizi zilikinzana na dini za jadi zilizokuwapo katika jamii za Kitanzania. Baadhi ya watu katika jamii za Kitanzania walijiunga katika dini hizo kwa kushawishiwa au kulazimishwa na wahamiaji au utawala wao. Katika kipindi hicho cha kabla ya kuja kwa ukoloni, jamii nyingi zilizokuwapo katika mwambao wa pwani ya Tanzania ziliathiriwa na uhusiano na dini ya Kiislamu. Pia, jamii nyingine za, maeneo kama vile ya Zanzibar, Bagamoyo, Unyanyembe (Tabora), Kilimanjaro, Songea, na Kagera zilijiunga na dini ya Kikristo. Hii ilisababisha jamii za Tanzania kufuata mapokeo mengine ya maadili ikiwemo chakula, mavazi, mitindo ya maisha kama ndoa, malezi ya familia na muziki au sanaa.

FOR ONLINE READING ONLY

### Athari za kijamii

Mwingiliano na jamii zingine kutoka Mashariki ya Kati na ya Mbali uliathiri kanuni mbalimbali za kijamii na kimaadili. Hali hii ilisababisha athari baina ya watu ndani ya jamii za Kitanzania na kusababisha mabadiliko ya miundo ya elimu, malezi, mavazi na chakula katika jamii. Mtindo wa ujenzi wa nyumba, michezo, muziki na mila na desturi za miliki zilibadilika pia. Kabla ya ujio wa wageni, mali zote kama vile ardhi, mifugo na misitu zilimilikiwa na jamii nzima. Baada ya ujio wa wageni, mali zilianza kumilikiwa na mtu binafsi au kikundi fulani cha watu. Hii ilisababisha kujengeka kwa matabaka mbalimbali katika jamii za Kitanzania, mfumo ambao hapo mwanzo haukuwapo.

### Athari katika mifumo ya kiutawala

Mifumo ya utawala kabla ya ujio ya wageni ilikuwa kwenye ngazi ya familia na ukoo. Familia na koo ziliweka msingi wa uongozi kwa kuzingatia mamlaka na sheria za kimila. Ujio wa wageni ulihamisha mfumo na muundo huo na kuweka mfumo mpya wa utawala ambao uliegemea zaidi katika muundo wa kiserikali. Mfumo mpya wa kisiasa ulisababisha kupungua kwa mamlaka za asili za kiutawala ambazo kwa kiasi kikubwa zilichukuliwa na mifumo mipya ya kigeni. Kwa mfano, utawala wa usultani ulikuwa na viongozi walioitwa maakida, maliwali, majumbe na wakuu wa vijiji. Mfumo huu wa uongozi ulififisha uwezo wa viongozi wa familia, ukoo na kabila katika jamii zilizohusika katika kusimamia shughuli za kiuchumi na maadili katika jamii.

### Uharibifu wa mazingira

Uhusiano wa jamii za Kitanzania na jamii zingine ulisababisha kutangazwa kwa utajiri wake katika nchi za nje. Wageni wengi kutoka sehemu mbalimbali duniani walianza kufika kwa wingi kwa lengo la kuvuna rasilimali na utajiri. Wageni walifungua mashamba makubwa ya kilimo na uvunaji wa mazao ya misitu bila kuzingatia uhifadhi wa mazingira. Wageni wengine walijishughulisha pia na uwindaji wa wanyamapori. Uvunaji wa mazao ya misitu, kufyeka misitu kwa ajili ya mashamba na shughuli nyingine ulianza kuenea kwa Watanzania. Hali hii ilisababisha kuingia katika mfumo mpya wa maisha ambao haukuzingatia maadili ya matumizi endelevu ya mazingira. Kuibuka na kukua kwa miji kulikohitaji nishati ya kuni na mkaa kulichangia sana uvunaji wa misitu ambao si endelevu kwa misitu na rasilimali nyingine.

### Kuibuka kwa migogoro na vita

Uhusiano kati ya jamii za kigeni na wenyeji wa jamii za Kitanzania haukuwa rahisi kwani uligubikwa na migogoro iliyotokea mara kwa mara. Hii ilichangiwa na mambo mengi ikiwamo kunyang'anya na kugombania rasilimali, kugombania utawala, kulinda mila na desturi za Kitanzania na kukataa kufuata imani za dini nyingine. Hali hii ilizijenga jamii za Kitanzania kuwa na ujasiri, uzalendo na umoja katika kulinda mali na utamaduni wa Kitanzania. Kwa mfano, ujio na utawala wa Wareno katika pwani ya Tanzania ulisababisha vita dhidi ya jamii za Kitanzania ambazo zilikuwa zikipinga utawala wa Wareno. Pia, ujio wa Wangoni

FOR ONLINE READING ONLY

kutoka Afrika ya Kusini ulisababisha vita katika maeneo walimopita na katika jamii za Kitanzania, hususani katika maeneo ya kusini magharibi na kusini mwa Tanzania.

**Kazi ya kufanya 6.2**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya taarifa, fanya uchunguzi, kisha linganisha mapokeo ya kijamii kabla ya kuja kwa ukoloni na mapokeo ya kijamii wakati wa sasa.

**Zoezi 6.2**

1. Eleza mabadiliko yaliyotokea katika maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni.
2. Je, unafikiri ni kwa namna gani uhusiano wa Tanzania na jamii zingine uliathiri umoja na mshikamano wa jamii za Kitanzania kabla ya ujio wa wakoloni?
3. Jadili uhusiano uliopo kati ya mmomonyoko wa maadili na ujio wa wageni katika jamii za Kitanzania.
4. Kwa kutumia mifano, eleza jinsi uhusiano na wageni kutoka nje kabla ya ukoloni ulivyobadili mtindo wa maisha, hasa kuhusiana na imani za dini na mifumo ya utawala.
5. Je, unafikiri ni mabadiliko gani yanatokea katika maadili yanayotokana na uhusiano uliopo kati ya jamii za Kitanzania na jamii za mataifa mengine wakati wa sasa?
6. Ni kwa namna gani athari hasi katika mfumo wa maadili wa jamii za Kitanzania ulisababishwa na wahamiaji kutoka jamii za mabara mengine?

## Mapokeo ya kidini yalivyochangia kujenga maadili

Mapokeo ya imani mbalimbali za dini yalisaidia kuyakuza maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ujio wa wakoloni. Kabla ya kuja kwa wakoloni nchini Tanzania, kulikuwa na aina mbalimbali za dini, ambazo ni dini za jadi, Uislamu na Ukristo. Dini hizi zilikuwa na jukumu kubwa katika kuyasimamia na kuyatunza maadili ya jamii. Kwa mfano, katika kabila la Wamasai, waliweza kutunza imani zao kupitia imani za jadi chini ya mungu wao *Engai*. Utamaduni wa Wamasai ulitoa mwongozo na utaratibu wa namna ya kuishi, muundo wa kazi za jamii, matambiko, na usimamizi wa kazi chini ya Olaiboni. Dini ilitumika kama msingi mkuu wa jamii na iliongoza shughuli za jamii nzima kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa. Mapokeo ya kidini yalichangia kwa namna moja au nyingine katika kujenga maadili ya jamii za Kitanzania.

### Dini za jadi

Imani za jadi zilikuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya maadili ya Kitanzania kabla ya ujio wa wakoloni katika kujenga utamaduni, jamii na kuijenga jamii kiroho. Baadhi ya mchango wa imani za jadi ni kama ifuatavyo:

(a) *Umoja:* Dini za jadi zilikuwa sehemu muhimu za utambulisho wa utamaduni wa makabila mbalimbali ya Kitanzania. Dini hizo zilisaidia katika kuleta umoja wa jamii kupitia

FOR ONLINE READING ONLY

matambiko na sherehe za kuanza mwaka, kupanda na kuanza kuvuna mazao na shughuli nyingine katika jamii iliyohusika. Aidha, zilichangia kujenga umoja, undugu, uzalendo na muendelezo wa urithi wa mila na desturi za jamii iliyohusika. Dini ilitumika kama sehemu ya kuwaunganisha watu, kusuluhisha migogoro, kujenga uzalendo, uadilifu na kuthaminiana.

(b) *Ujuzi na tiba:* Katika jamii nyingi za Kitanzania, mifumo ya elimu pamoja na afya iliambatana na dini iliyohusika. Kuna baadhi ya magonjwa yalitibiwa kwa kutumia imani za jadi ambapo matibabu yake yaliambatana na matambiko mbalimbali. Katika jamii za Kitanzania, mfumo wa tiba uliunganishwa na uwepo wa mizimu au miungu. Hivyo, dini ilikuwa si suala la mtu mmoja au hiari bali lilikuwa jambo la lazima na la jamii yote.

(c) *Mshikamano na upendo:* Dini za jadi zilichangia katika kukua kwa mshikamano na kuheshimu maadili ya jamii na kuzisimamia sheria, kanuni, taratibu na matendo ya wanajamii. Hii ilisaidia katika kujenga uhusiano kati ya mtu na mtu, mwenendo wa viongozi na uhusiano kati ya jamii moja na nyingine. Dini za jadi mara zote zilisisitiza umuhimu wa umoja, heshima kwa wakubwa na viongozi na upendo katika jamii.

(d) *Maadili ya kiroho:* Imani katika dini za jadi zilitoa muundo mzima na muunganiko wa kiroho na nguvu za kimungu na maisha baada ya kifo. Hii ilikuwa ni pamoja na asili ya binadamu, mizimu na miungu ya jamii iliyohusika. Matendo ya kuamini mizimu, kuheshimu matambiko, na kuthamini matendo ya kiroho na sherehe za jadi katika maisha yalichangia zaidi katika kumjenga Mtanzania katika ulimwengu wa kiroho. Maadili haya yalijengwa katika matukio ya kijamii kama vile sherehe za matambiko wakati mtoto anapozaliwa, harusi na kifo, ambapo yote haya yaliunganishwa na ulimwengu wa kiroho. Matendo haya yalichangia katika kumjenga na kumlinda mwanajamii pamoja na kukua na kuenenda kulingana na maadili ya jamii iliyohusika.

(e) *Utii:* Dini za jadi zinahusisha kuwaheshimu, kuwathamini, kuwapenda na kuwatendea mema binadamu wengine. Pia, dini za jadi zilihusisha utoaji wa nasaha za umuhimu wa watu kuwathamini watu wengine na kuepuka tabia zinazoharibu utu wa watu wengine. Kulikuwa na watu mahususi katika kuyasimamia maadili hayo pamoja na ustawi wa jamii nzima katika kutatua migogoro kupitia njia za kiroho. Viongozi hao waliheshimiwa sana na kila mwanajamii na walifuata walichoelekezwa na viongozi hao.

(f) *Kuheshimu, kutunza na kulinda mazingira:* Dini za jadi ziliwaandaa wanajamii kuyajali na kuyapenda mazingira. Dini hizi ziliwahimiza

FOR ONLINE READING ONLY

wanajamii kulinda na kutunza mazingira kwa kuweka sheria na miiko mbalimbali ya kimaadili. Dini za jadi ziliweka msisitizo mkubwa katika kutunza na kuwaunganisha watu na mazingira yao. Pia, zilisisitiza kutunza na kuendeleza matumizi bora ya mazingira. Dini zilitoa utaratibu wa matumizi ya rasilimali kama misitu, maji na ardhi. Kwa ujumla, mapokeo ya imani ya dini za jadi yalijenga msingi imara katika matumizi ya mazingira na rasilimali zake katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni.

(g) *Haki na usawa:* Dini za jadi zilisaidia katika utoaji haki katika jamii za Kitanzania kwa kukuza misingi, kanuni na maadili yaliyochangia haki za kijamii. Upendo, amani, utu, usawa, uadilifu, uhuru, haki na maelewano ya kijamii yalikuwa msingi wa jamii yenye uadilifu. Katika jamii za Kitanzania, mfumo wa dini za jadi uliweka miiko kwa viongozi kama njia mojawapo ya kutenda haki. Msisitizo huu wa haki na maadili kupitia dini za jadi ulisaidia kukuza ustawi wa jamii za Kitanzania na kuhakikisha kwamba haki inakuwa msingi thabiti wa uhusiano wa jamii.

**Kazi ya kufanya 6.3**

Soma matini kutoka katika vyanzo mbalimbali kuhusu dini za jadi katika jamii za Kitanzania, kisha eleza miiko ya dini hizo katika utunzaji wa mazingira.

**Zoezi 6.3**

1. Kwa kutumia mifano, eleza miiko mbalimbali iliyosisitizwa na dini za jadi katika jamii za Kitanzania kabla ya kuingia kwa ukoloni.
2. Tathmini hali ya dini za jadi katika jamii za Kitanzania kwa sasa.
3. Eleza ni kwa namna gani dini za jadi zilikuza maadili ya kiroho.
4. Fafanua jinsi dini za jadi zilivyochangia mapambano dhidi ya rushwa na unyonyaji.
5. Unafikiri ni kwa namna gani dini za jadi zinaweza kukuza maadili ya jamii za Kitanzania kwa sasa?

**Dini ya Kiislamu**

Kuingia kwa dini ya Kiislamu katika pwani ya Afrika Mashariki kulisukumwa zaidi na wafanyabiashara kutoka bara la Asia, hasa Waarabu na Waajemi ambao walifika pwani ya Afrika Mashariki kupitia Bahari ya Shamu (Bahari Nyekundu) na Hindi. Waarabu walipofika pwani ya Afrika Mashariki katika kipindi cha karne ya 8, walijiimarisha pembezoni mwa mwambao wa pwani na waliendelea kuingia bara kadiri miaka ilivyokuwa inaenda mbele. Uingiaji huo ulifanikiwa kwa sababu mfumo wa kisiasa na kijamii uliokuwapo katika jamii za Kitanzania haukuwa wa kiserikali. Katika kipindi hicho, jamii hizo zilikuwa zinaongozwa na mfumo wa kifamilia na kiukoo. Hii iliwasaidia Waarabu na Waajemi kuingia nchini bila upinzani wowote na kuanzisha makazi kwenye maeneo ya pwani ya Bahari ya Hindi.

FOR ONLINE READING ONLY

Dini ya Kiislamu ilichangia katika ujenzi wa maadili ya jamii ya Kitanzania kwa kuleta mabadiliko katika mifumo mbalimbali za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kitamaduni katika jamii za Kitanzania. Matokeo ya mabadiliko haya ni kama ifuatayo:

(a) *Utamaduni mseto:* Uislamu ulichangamana na utamaduni wa wenyeji. Hii ilisababisha muunganiko na tamaduni za kigeni na ule wa Kitanzania na kuunda mfumo mpya wa maadili. Mwingiliano huu ulisababisha mchanganyiko wa mila na desturi za Kiarabu, Kiajemi na za kiasili na kuunda mchanganyiko wa kiutamaduni kati ya Uislamu na jamii za Kitanzania. Mifano ya utamaduni mseto ilishamiri zaidi Zanzibar, Bagamoyo na Kilwa. Msingi mkubwa wa Uislamu ulikuwa uungwana, haki, usawa, kujitolea, uvumilivu na ujasiri. Jamii hizi za Tanzania zilipokea pia mapokeo mengine mengi kama umoja, mshikamano na upendo kupitia dini ya Kiislamu.

(b) *Kukua kwa miji:* Kuenea kwa Uislamu kulienda sambamba na kukua kwa lugha ya Kiswahili na miji iliyokuwa na utamaduni uliojulikana kama uswahili, ambao baadaye ulikuwa na mchanganyiko wa Kiarabu na mila na desturi za Kitanzania na ulienea katika miji yote ya pwani ya Tanzania. Utamaduni huu wa mjini si tu kwamba ulifafanua maadili ya mtu binafsi bali uliongoza pia jamii katika mambo ambayo yalisababisha kuimarishwa kwa maadili na kuzuia mambo yote ambayo yalikuwa hayakubaliki kwa mujibu wa dini ya Kiislamu kama rushwa, wizi, uzinzi, utengano na husuda. Mtazamo huu wa pande mbili wa maadili ya mtu binafsi na ya jumuiya uliimarisha muundo wa maadili wa jamii za Waswahili. Kwa mantiki hiyo, miji hii ilikuwa na utamaduni wake na uliongozwa kwa kiasi kikubwa na imani ya dini ya Kiislamu. Misingi ya uhusiano wa Kiislamu ilikuwa ni undugu uliohakikisha kwamba maendeleo ya kimaadili hayakuwa tu kwa matendo ya kibinafsi bali yanaenea kwa mwingiliano wa kijamii nzima.

Vilevile, kukua kwa miji kulienda sambamba na kujengwa kwa misikiti na madrasa. Kuwapo kwa misikiti kulikuwa jambo muhimu katika kujenga maadili. Hii ni kwa sababu mafundisho ya dini ya Kiislamu yalilenga katika kuhimiza undugu, upendo na mshikamano miongoni mwa Waislamu. Imani ya Kiislamu ilisisitiza kwamba Waislamu wote ni ndugu bila kujali rangi, kabila wala kipato. Utaratibu wa Waislamu kusaali mara tano kwa siku katika misikiti kulitoa fursa adhimu ya watu kukusanyika, hasa Watanzania na Waarabu bila kubaguana.

(c) *Elimu:* Matokeo mengine ya kimapokeo kwenye maendeleo ya maadili nchini Tanzania ni maendeleo katika sekta ya elimu. Elimu ya Kiislamu ilichangia katika kukuza mshikamano katika jamii ya Waislamu bila kujali tofauti za rangi au kabila.

FOR ONLINE READING ONLY

Kuanzishwa kwa elimu ya Kiislamu na kuandika lugha za Kiafrika kwa kutumia maandishi na tarakimu za Kiarabu kuliwezesha kuenea kwa imani, maadili na desturi za Kiarabu katika makabila na lugha mbalimbali katika maeneo ya pwani na yale ambayo waliishi jamii ya Waarabu na watu kutoka Mashariki ya Kati. Elimu ya Kiislamu ilitoa maarifa na mafunzo kwa misingi ya kidini ambayo ni muhimu kwa watu binafsi kujitambua na hivyo, kuendeleza mfumo wa maadili na utambulisho. Elimu ya Kiislamu ilichukua nafasi katika jamii na iliathiri maadili katika mfumo wa utawala, sheria na tiba za magonjwa mbalimbali, malezi na uhusiano katika ndoa. Katika maeneo ya mjini kulianzishwa shule na vyuo ambavyo vilivyofundisha dini ya Kiislamu iliyokuza maadili kama utii wa sheria, uaminifu, upendo na kusaidia maskini na wasiojiweza. Kielelezo 6.1 kinaonesha msikiti mmojawapo uliojengwa katika mji wa kale wa Kilwa.



**Kielelezo 6.1:** *Msikiti mmojawapo uliojengwa katika mji wa kale wa Kilwa*

FOR ONLINE READING ONLY

**Kazi ya kufanya 6.4**

Uliza watu mbalimbali katika jamii unamoishi kuhusu mchango wa dini ya Kiislamu katika mapambano dhidi ya rushwa au ufisadi.

(d) *Mabadiliko ya kijamii:* Uislamu uliathiri baadhi ya miundo na kanuni za kijamii za Kitanzania. Kwa mfano, watu walitakiwa kuwa waumini watiifu wa dini ya Kiislamu katika mfumo wa maisha, na hivyo kuathiri dini za jadi za jamii za Kitanzania. Dini za jadi zilisisitiza ujenzi wa maadili ulioendana na jamii za Kitanzania. Kuenea kwa Uislamu kulianzisha mfumo mpana wa kimaadili uliotegemea Kuran na mafundisho ya Mtume Muhammad. Mfumo huu ulisisitiza fadhila kama vile uaminifu, haki, hisani, na ujasiri pamoja na kukuza msingi thabiti wa maadili katika jamii. Mafundisho ya Kiislamu yaliwahimiza watu binafsi kuendeleza sifa njema kama vile shukurani, subira, na ujasiri, huku wakionya dhidi ya kiburi na kupenda anasa za dunia kupita kiasi. Kukazia huku kwa maadili kulichangia kustawi kwa jamii yenye uadilifu kwa kuzingatia maadili ya mtu binafsi na jamii. Aidha, Uislamu haukufafanua tu maadili ya mtu binafsi bali pia uliiongoza jamii juu ya mambo ambayo yanasababisha kuimarika kwa maadili na kuzuia ufisadi. Uislamu ulikataza wafanyabiashara kuuza bidhaa kwa bei ya juu ili kujipatia faida nono. Lengo ni kuwalinda watu wa kipato cha chini ili nao waweze kununua bidhaa muhimu. Mtazamo huu wa pande mbili juu ya maadili ya mtu binafsi na ya pamoja uliimarisha muundo wa maadili wa jamii na utumiaji wa maadili ya Kiislamu kwa wote. Kanuni za maadili za Uislamu zilishughulikia kila kipengele cha maisha ya mwislamu, kuanzia mwenendo wake kibinafsi hadi uhusiano na jamii zingine. Ushirikiano huu ulihakikisha kwamba maendeleo ya kimaadili hayakuwa tu kwa matendo ya kibinafsi bali yanaenea kwa mwingiliano wa kijamii pia.

**Zoezi 6.4**

1. Husianisha maendeleo ya miji ya pwani na kukua kwa maadili ya Kitanzania.
2. Ni kwa namna gani teknolojia ilisababisha mabadiliko katika maadili.
3. Jadili nafasi ya dini ya Kiislamu katika kukuza mshikamano wa jamii za Kitanzania.
4. Je, unafikiri ni kwa nini dini ni muhimu katika kuleta haki na usawa?
5. Eleza chimbuko la kukua kwa miji ya pwani ya Afrika Mashariki.

### Dini ya Kikristo

Dini ya kikristo ina historia ndefu nchini Tanzania, ikianzia karne ya 15 pale Wareno walipoingia katika pwani ya Afrika Mashariki wakiongozwa na Vasco da Gama. Lengo la kuja kwao lilikuwa kufanya biashara na kusambaza dini ya

FOR ONLINE READING ONLY

Kikristo. Wareno hawakuweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa sana kutokana na kukuta tayari dini ya Kiislamu ilishaenea katika mwambao wa pwani na wao hawakujishughulisha kwenda bara kueneza dini ya Ukristo. Awamu ya pili ya kuingia kwa dini ya Kikristo ni katikati ya karne ya 19 pale ambapo Wamisionari wa Kikatoliki walianza kujiimarisha katika mwambao wa Bahari ya Hindi. Kielelezo 6.2 kinaonesha kanisa la kwanza kujengwa nchini lililoko mjini Bagamoyo.



**Kielelezo 6.2**: *Kanisa la kwanza kujengwa Tanzania*

FOR ONLINE READING ONLY

Kuingia kwa dini ya Kikristo nchini Tanzania mwaka 1860 kuanzia Zanzibar kulikuwa na athari kubwa katika mfumo wa maadili nchini Tanzania. Wakati dini ya Kikristo ikienea nchini Tanzania ilisababisha pia mabadiliko kadhaa kwenye mila na desturi za Kitanzania. Imani ya dini ya Kikristo ina mchango mkubwa katika mfumo wa maadili ya Kitanzania kwani ilichangia kwa kiasi kikubwa kutoa muundo ambao uliboresha utaratibu na misingi ya kuendesha maisha ya kila siku. Mchanganyiko wa dini ya Kikristo na mapokeo ya Kitanzania umesababisha uhusiano mwema katika jamii, heshima kwa wakubwa na kujenga utambulisho kwa mwanajamii. Ingawa dini za jadi za Tanzania zilikuwa na nguvu kama vile kuthamini maisha ya binadamu na jamii, dini ya Kikristo ilileta mambo mengi ya ziada kama vile dhana ya wokovu, kushinda hofu ya athari za mababu, na uhusiano wa moja kwa moja na Mungu. Dini ya Kikristo ilichangia zaidi katika kuleta amani, upendo, heshima umoja na maridhiano katika jamii.

Mapokeo ya dini ya Kikristo katika maadili ya Kitanzania ni makubwa, na kwa kiasi fulani Ukristo umechukua nafasi kubwa katika mfumo wa maadili ya Kitanzania. Mapokeo ya dini ya Kikristo katika ujenzi wa maadili ni kama ifuatavyo:

(a) *Elimu:* Kuingizwa kwa mfumo wa elimu ya Magharibi nchini katika jamii za Kitanzania kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na dini ya Kikristo. Kuanzishwa kwa mifumo ya elimu ya Magharibi na wamisionari wa Kikristo kulisababisha pia kuingizwa kwa maadili ya Kikristo katika jamii za Kitanzania. Mtindo mpya wa elimu ulioletwa na wamisionari ulisababisha kuanzishwa kwa shule ambazo zilijumuisha taratibu za masomo ya kitaaluma na mafunzo ya ufundi stadi. Mfumo mpya wa elimu ulioletwa na dini ya Kikristo ulichangia kwa kiasi kikubwa katika kubadili imani za watu, kujenga jamii yenye utii, heshima, mshikamano, huruma na upendo. Elimu hii ya dini ilitolewa shuleni na kanisani kupitia mahubiri. Watoto walifundishwa dini katika shule za jumapili.

(b) *Kukua kwa sanaa na usanii:* Kwa namna mbalimbali, kuingia kwa dini ya Kikristo Tanzania kulisababisha mabadiliko makubwa katika shughuli za sanaa pamoja za utamaduni. Ukristo ulileta aina mpya za sanaa, kama vile usanifu wa ujenzi, uchongaji na uimbaji. Pia, mwelekeo wa kulinda, kujenga na kuendeleza maadili ya jamii ulijengwa katika shughuli za kisanii na sanaa. Nyimbo, maigizo na mafundisho yaliyosisitiza upendo, huruma, umoja, utu na mengineyo yaliwasilishwa kupitia shughuli za sanaa na usanii. Wamisionari walileta zana za muziki kama kinanda na gitaa ambazo walizitumia katika nyimbo za ibada. Mwanzoni ngoma za asili kama vile njuga, zeze na marimba zilikatazwa katika nyumba za ibada za Kikristo.

(c) *Uwajibikaji:* Suala la uwajibikaji limejielekeza katika kuhimiza umuhimu wa watu kufanya kazi ili kulinda utu wao katika jamii. Ni wazi kwamba katika jamii zilizostarabika, utu wa mtu unapimwa kwa namna anavyowajibika binafsi na kwa jamii anamoishi. Mafundisho ya dini ya Kikristo yalisaidia katika maadili ya Kitanzania kwa kusisitiza kila mwanajamii afanye kazi. Kwa mfano, katika mafundisho ya dini Kikristo "*2 Wathesalonike 3:10*" inasema, "*... ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi asile chakula*". Hii inaendana na baadhi ya mila na desturi za Kitanzania ambazo zinasema kuwa "Kazi ni kipimo cha utu". Imani ya Kikristo inahimiza mtu kupata hadhi na heshima kutokana na kazi yake anayoifanya.

(d) *Uadilifu:* Ujio wa dini ya Kikristo katika jamii za Kitanzania ulisaidia katika kuyajenga maadili kupitia mafundisho yake yaliyo kwenye kitabu kitakatifu cha Biblia, ambacho kimesisitiza sana uadilifu. Dini ya Kikristo pia imesisitiza umuhimu wa watu kuwa waungwana na kufanya

FOR ONLINE READING ONLY

shughuli mbalimbali kwa kuzingatia mwenendo mwema na kufuata misingi ya maadili. Vilevile, mafunzo ya dini ya Kikristo yanasisitiza matendo mema, upendo kwa watu wote, uvumilivu, msamaha, uhusiano mwema kati ya mtu na mtu au mtu na jamii yake. Katika mtazamo wa Kikristo, uadilifu unachukuliwa kuwa ni ile hali ya kuaminika, kuwa mkweli na kutimiza ahadi, kutenda matendo mema muda wote na kuwa mtu mwenye imani na kujithamini. Waumini wanatakiwa kuwa wakweli muda wote na kuonesha uaminifu wao kwa kanisa na serikali, kwa matendo na si kwa maneno tu.

(e) *Mabadiliko ya kijamii:* Imani ya Kikristo imesaidia kuongeza kasi ya mabadiliko katika maadili ya jamii za Kitanzania kwa kutoa mfumo mzuri unaokuza kanuni, taratibu na misingi ya maadili kwa maendeleo ya jamii. Imani ya Kikristo inasisitiza maadili kama vile uaminifu, uadilifu, uwazi, ukweli, na uvumilivu, ambayo ni msingi kwa maendeleo ya mifumo mizuri ya kiuchumi na kidemokrasia. Maadili haya yalipojumuishwa katika maadili ya kiutamaduni ya Kitanzania yalichangia katika kukuza jamii yenye uadilifu zaidi na yenye usawa.

(f) *Mabadiliko ya kiuchumi:* Imani ya dini ya Kikristo imesaidia katika mabadiliko ya kiuchumi kwa kushawishi kujenga maadili ya mtu binafsi, tabia, na njia ya kufanya uamuzi katika njia mbalimbali za kiuchumi. Kanuni na mafundisho ya Kikristo ya kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa kusisitiza maelekezo ya kimaadili na ambayo huongoza uhusiano wa watu katika kufanya shughuli za kiuchumi vilisaidia kukuza uchumi. Kwa kuweka shughuli za kiuchumi katika kanuni za kikristo, jamii ziliweza kujitahidi kuelekea mfumo endelevu zaidi na shirikishi wa kiuchumi ambao unashughulikia ukosefu wa usawa wa kijamii na kukuza na kulinda manufaa ya wote.

(g) *Utii:* Imani ya Kikristo iliweka mkazo kwa watu kutii mamlaka za utawala wa dini na wa kiserikali. Wamisionari waliamini viongozi wa kiserikali waliwekwa na Mungu. Viongozi hawa waliwatawala watu kwa niaba ya Mungu, hivyo walisisitiza waheshimiwe. Waumini walitakiwa kutii mamlaka ya kikoloni na ya viongozi wa dini zao.

**Kazi ya kufanya 6.5**

Soma matini kutoka katika nyanzo mbalimbali vya taarifa vinayoelezea dini ya Kikristo, kisha eleza mchango wa dini hiyo katika mapambano dhidi ya rushwa au ufisadi.

**Zoezi 6.5**

1. Elezea mchango wa elimu katika ujenzi wa maadili nchini Tanzania.
2. Dini zina mchango gani katika mapambano dhidi ya rushwa hapa nchini?

FOR ONLINE READING ONLY

3. Fafanua jinsi mapokeo ya dini ya Kikristo yalivyosaidia katika kuhimiza umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii.
4. Andika insha kuhusu mchango wa dini ya Kikristo katika kujenga maadili katika jamii za Kitanzania wakati wa sasa.
5. "Hakuna jamii bora bila ya maadili" Jadili kauli hii.

**Zoezi la marudio**

1. Eleza mchango wa dini ya Kiislamu katika kujenga umoja na mshikamano katika jamii za Kitanzania.
2. Ni kwa namna gani maadili yaliyoletwa na dini za Kiislamu na Kikristo yamechangia ujenzi wa maadili ya jamii za Kitanzania zilizopo sasa?
3. Eleza mbinu mbalimbali zilizotumika katika ujenzi wa maadili katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni.
4. Je, dini za jadi zina nafasi gani katika kujenga maadili katika mazingira ya sasa?
5. Elezea mchango wa dini ya Kikristo katika kujenga umoja na mshikamano katika jamii za Kitanzania.
6. Tanzania ni taifa lenye watu wenye imani mbalimbali za kidini, eleza ni kwa namna gani limefanikiwa kuujenga umoja na mshikamano wa kitaifa.
7. Kwa nini viongozi wakuu wa nchi wakipewa madaraka huapishwa kwa kutumia imani zao?
8. Kwa nini hadi sasa viongozi wa jadi ni wadau muhimu katika kuyasimamia maadili ya jamii za Kitanzania?

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Saba
# Nguvu ya ukoloni katika kujenga mwelekeo mpya wa jamii

## Utangulizi

*Watawala wa kikoloni walitumia mbinu mbalimbali kuzitawala jamii za Kitanzania. Wakoloni walitumia ushawishi (nguvu laini) na mabavu (nguvu ngumu) katika juhudi za kutawala jamii za Kitanzania. Katika sura hii, utajifunza kuhusu maana ya ukoloni, uhusiano wake na kukua kwa ubepari, chimbuko la ukoloni na jinsi ulivyoenea nchini Tanzania. Pia, utajifunza athari za ukoloni kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kimaadili. Vilevile,, utajifunza ujasiri na uzalendo wa Watanzania katika kupambana na ukoloni. Umahiri utakaoujenga, utakuwezesha kujilinda na kuilinda jamii yako dhidi ya uvamizi wa aina mbalimbali.*

**Fikiri**

**Sababu za taifa moja kulitawala taifa lingine.**

### Dhana ya ukoloni, nguvu laini na nguvu ngumu

**Ukoloni ni hali ya taifa moja kwenda nje ya mipaka yake na kutawala kwa mabavu taifa lingine katika nyanja zote, yaani uchumi, utamaduni, siasa na jamii. Kumekuwa na nadharia mbili zilizojadiliwa na wasomi mbalimbali kuhusu sababu za kutawaliwa kwa bara la Afrika. Nadharia ya kwanza ni ile inayosema kuwa bara la Afrika lilitawaliwa kwa sababu za kibinadamu kama vile kuleta ustaarabu wa Ulaya Magharibi. Madai yaliyoletwa na kundi hili la wasomi ni kwamba, wakoloni walikusudia kuwaokoa Waafrika dhidi ya biashara haramu ya utumwa na vita vya kikabila. Pia, kundi hili lilidai kwamba Afrika ilitawaliwa ili kuleta ustaarabu kwa njia ya dini ya Ukristo na biashara halali za mazao ya kilimo. Kwa ujumla, nadharia hii imejikita katika kuutetea ukoloni na kuona kama "mkombozi" wa Waafrika ambao walikuwa nyuma sana kimaendeleo na kiustaarabu ukilinganisha na maendeleo ya Ulaya Magharibi.**

**Nadharia ya pili ni ile ya kiuchumi ambayo inahusisha kutawaliwa kwa bara la Afrika na kukua kwa ubepari katika bara la Ulaya mnamo robo ya mwisho ya karne ya 19.**

FOR ONLINE READING ONLY

Hoja yao ni kwamba kukua huko kwa ubepari kulisababishwa na mabadiliko makubwa ya kiuchumi na mapinduzi ya viwanda. Mahitaji ya viwanda vya kibepari yalitia msukumo wa kuligawa bara la Afrika yaliyoambatana na malengo kama kupata malighafi, masoko ya bidhaa za viwandani, maeneo ya uwekezaji, mitaji na vibarua katika vitega uchumi vya kikoloni. Kwa mujibu wa tafiti mbalimbali zilizofanyika, nadharia ya pili ndiyo iliyobeba ukweli halisi kuhusu madhumuni ya ukoloni mkongwe katika bara la Afrika.

Bara la Afrika lilianza kutawaliwa rasmi na wakoloni kutoka bara la Ulaya baada ya kuhitimishwa kwa Mkutano wa Berlin ulioitishwa na Kansela Otto von Bismarck wa Ujerumani mwaka 1884 – 1885. Mkutano wa Berlin ndio ulioamua makoloni ya Afrika yagawiwe kwa nchi za Ulaya ili kuepuka umwagaji damu baina ya mataifa hayo ambayo yalikuwa yakigombea baadhi ya maeneo yenye utajiri mwingi. Hata hivyo, kuna maeneo kama vile Afrika Mashariki ambayo hayakugawanywa katika Mkutano wa Berlin. Maelezo zaidi kuhusu ugawaji wa maeneo mengine yatajadiliwa zaidi hapo baadaye kwenye sura hii.

Uanzishwaji wa ukoloni na baadaye utawala wake ulihitaji mbinu mbalimbali ili kuwahadaa au kuwavamia Waafrika. Mbinu au njia hizi ziligawika katika makundi mawili makuu, yaani nguvu laini (ushawishi) na nguvu ngumu (mabavu) kama zinavyodadavuliwa katika sehemu zinazofata.

**Nguvu laini**

Katika utekelezaji wa malengo ya kuitawala Tanganyika na Zanzibar, wakoloni walitumia nguvu laini. Nguvu laini ni ule uwezo wa upande mmoja kutumia ushawishi na mbinu za kidiplomasia kutimiza malengo maalumu dhidi ya upande wa pili. Nguvu laini haitumii mabavu bali inatumia ushawishi wa kiutamaduni, miiko na maadili ya kisiasa na siasa za kimataifa kufanya mabadiliko. Pia, ni uwezo wa taifa moja kuishawishi na kuibadilisha tabia ya mataifa mengine ili kupata kile ambacho taifa hilo linakitafuta. Mfano wa nguvu laini zilizotumiwa na wakoloni ni kama mikataba, dini, elimu na utamaduni. Jambo muhimu hapa ni kwamba nchi inayopanga kutumia nguvu laini huwa na ajenda inayoweza kuishawishi nchi nyingine bila kutumia vitisho au nguvu za kijeshi au vikwazo vya kiuchumi na kisiasa. Zifuatazo ni njia mbalimbali za nguvu laini zilizotumiwa na wakoloni.

*Mikataba ya kilaghai*

Moja ya nguvu laini iliyotumiwa na watawala wa Kijerumani ili kuzitawala jamii za Kitanzania ni kusaini mikataba ya kilaghai na jamii hizo. Mkataba maarufu ulikuwa ule uliosainiwa kati ya Karl Peters na Chifu Mangungo wa Msovero, Usagara mwaka 1884 katika wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro. Mkataba huu ulisomeka kwamba Chifu Mangungo alikubali kuikabidhi ardhi yake pamoja na watu wake kwa Wajerumani na wao kugeuzwa kuwa watawaliwa. Karl Peters alifanikisha mkataba huu wa kilaghai kwa kutumia lugha ngeni ambayo Chifu Mangungo alikuwa haifahamu. Pia, Mangungo hakufahamu

FOR ONLINE READING ONLY

kanuni za mikataba ya kimataifa. Ni kupitia mkataba huu ardhi ya watu wa Msovero na Ujerumani ya Afrika Mashariki kwa ujumla ilikabidhiwa kwa utawala wa Wajerumani mwaka1885. Baada tu ya mikataba ya aina hii, Karl Peters na kampuni ya Kijerumani alipewa mamlaka na serikali ya Kijerumani ya kuanzisha utawala katika ardhi ya Ujerumani ya Afrika Mashariki. Karl Peters alipewa jina la "mkono wa damu" kwa tabia yake ya ukatili. Kwa hiyo, kupitia mikataba ya kilaghai jamii nyingi za Kitanzania zilijikuta zinatawaliwa bila kujua na kuwa chini ya Wajerumani.

**Kazi ya kufanya 7.1**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya taarifa, tafuta mkataba kati ya Chifu Mangungo na Karl Peters, kisha uchambue mkataba huo kwa kuzingatia maadili ya Kitanzania.

*Imani ya dini*

Dini ilitumika kama nguvu laini ya kueneza ukoloni katika jamii za Kitanzania kupitia wamisionari kwa kukuza maadili ya utamaduni wa magharibi na imani ya dini ya Kikristo. Imani ya dini ilidhoofisha imani, mila na desturi za jadi za jamii za Kitanzania kwa kiasi kikubwa. Wamisionari waliitumia dini ya Kikristo kuziandaa jamii za Kitanzania kuwa waumini wazuri wa Ukristo, dini mpya kutoka Ulaya. Kwa maana hiyo, pamoja na kumtangaza Mungu, dini ilitumika kuzibadilisha jamii za Kitanzania kuamini na kuheshimu maadili, utamaduni na matakwa ya watu wa Ulaya Magharibi. Ukristo, pamoja na mambo mengine, uliwafundisha wanajamii wa Kitanzania kuwa wanyenyekevu kwa wageni na watu wote, pamoja na kutii na kuheshimu mamlaka za kanisa na serikali. Hali hii, kwa kiasi fulani, ilifanya uvamizi wa wakoloni kuwa rahisi na kukubalika haraka. Wamisionari walihubiri na kutangaza kuwa utamaduni, mila na desturi za jamii za Kitanzania zimepitwa na wakati, ni ovu, na za kipagani. Mahubiri hayo si tu yalisaidia kuwaondolea watu wa jamii za Kitanzania kujiamini bali pia ilizidi kudhoofisha maadili na utamaduni wa jamii hizo. Haya yote yalirahisisha upandikizaji wa utamaduni na maadili ya kimagharibi na kufanya kuwa rahisi kuzitawala jamii zilizoamini katika Ukristo. Kwa hivyo, jamii hizi zilianza kutawaliwa kiimani na kifikra. Nguvu laini hii ilisaidia utawala wa kikoloni kwa kiasi fulani.

*Elimu*

Elimu ya kikoloni ilitumika kama nguvu laini katika kutawala jamii za Kitanzania. Kama ilivyokuwa kwa Ukristo, elimu pia ilitumika katika kupandikiza utamaduni wa kimagharibi, yaani utamaduni wa Kizungu, ambao uliathiri mtazamo, kujiamini, uzalendo na tabia za jamii za Kitanzania. Elimu ya kikoloni ilitumia mitaala ya kikoloni iliyoandaliwa ili kuwaandaa wanafunzi wa jamii za Kitanzania kurithi utamaduni wa kimagharibi na kuachana na utamaduni wao. Njia hii iliwasaidia wakoloni si tu kutangaza na kueneza mila na desturi zao, bali pia kuwalainisha Watanzania kueneza na kutekeleza itikadi zao na kufanikisha masilahi yao katika kutawala kiurahisi koloni lao hapa Tanzania.

FOR ONLINE READING ONLY

*Ushirikishwaji*

Ushirikishwaji nao ni njia mojawapo iliyotumiwa na wakoloni kama nguvu laini. Katika njia hii wakoloni walitumia migogoro, uhasama na uadui uliokuwepo katika jamii za Kitanzania baina yao kama mtaji wa kuwatawala wote kirahisi kwa njia ya kuungana na mmoja au wawili kuishinda jamii yenye nguvu zaidi. Wakoloni walivyoingia Tanganyika waliyakuta baadhi ya makabila kama Wabena na Wasangu wakiwa na uhasama na Wahehe. Vilevile, miongoni mwa Wachaga walikutwa wana uhasama kati ya Mangi Sina wa Kibosho na Mangi Mandara (Mangi Rindi) wa Old Moshi na pia Mangi Marreale wa Marangu na Vunjo dhidi ya Mangi Meli wa Old Moshi. Kwa kutumia migogoro hii, Wajerumani waliamua kuungana na kushirikiana na Wasangu na Wabena kupigana na kabila shupavu la Wahehe chini ya Mtwa Mkwawa. Kule Uchagani, Wajerumani waliamua kuungana na Mangi Rindi kumpiga kiongozi shupavu Mangi Sina wa Kibosho aliyepinga kwa nguvu zote uvamizi wa Kijerumani. Wajerumani pia waliungana na Mangi Marreale dhidi ya Mangi Meli. Kama ilivyoandikwa hapo awali, wakoloni waliamua kutoa ushirikiano kwa kusaidia upande uliokuwa dhaifu katika uhasama huo ili kutimiza malengo yao ya kuingiza utawala wao katika jamii ya Wachaga na nyinginezo Tanzania.

Machifu hawa wa jamii za Kitanzania waliingia katika mtego huu bila kujua kuwa wakoloni walikuwa na nia ya kuwagawa na kuwatawala wote. Sababu zilizowafanya viongozi wa jamii za Kitanzania kuingia katika mtego huu ni pamoja na udhaifu wao wa kijeshi, kiu ya kuwashinda maadui wao, ambao ni Waafrika wenzao, kupata amani kutokana na vita vya muda mrefu baina yao, kupata fursa mbalimbali za kibiashara kutoka kwa wakoloni, na uelewa mdogo dhidi ya malengo ya wakoloni. Baada tu ya kusaidia kuwashinda hao maadui wao wa siku nyingi, viongozi hawa walijikuta nao chini ya utawala wa wakoloni. Hakuna walilopata katika ahadi zote walizoahidiwa na wakajikuta wamewarahisishia wakoloni kutawala jamii zote za Kitanzania.

**Kazi ya kufanya 7.2**

Soma vyanzo mbalimbali vya taarifa ili kuchunguza jinsi ubaguzi wa rangi ulivyokuwa nguvu laini iliyotumiwa na ukoloni.

**Nguvu ngumu**

Nguvu ngumu ni matumizi ya nguvu za kijeshi au mabavu au nguvu za kiuchumi kushawishi na kubadilisha tabia au mtazamo au masilahi ya nchi au jamii zingine. Masilahi haya yanaweza kuwa ya kisiasa, kijamii, kiutamaduni au kiuchumi. Mara nyingi mfumo huu unatumia mabavu na hufanikiwa pale unapotumiwa na upande wenye nguvu ya kiuchumi na kijeshi dhidi ya upande dhaifu. Kwa hiyo, nguvu ngumu inahusisha matumizi makubwa ya nguvu za kijeshi na vikwazo vya kiuchumi. Aidha, nguvu ngumu katika muktadha wa ukoloni inahusishwa pia na uwezo wa nchi kujenga au kuanzisha mabadiliko katika utawala wa kisiasa dhidi ya nchi nyingine. Kuna mifano mbalimbali ya nguvu ngumu iliyowahi kutumiwa na nchi zenye nguvu za kijeshi

FOR ONLINE READING ONLY

dhidi ya jamii dhaifu, kwa mfano, uvamizi wa Wajerumani kwa jamii za Kitanzania. Pamoja na uvamizi, nguvu ngumu hii iliambatana na kunyongwa kwa viongozi waliongoza mapambano dhidi ya uvamizi huo. Sehemu ifuatayo inaeleza matumizi ya nguvu ngumu au mabavu ya ukoloni dhidi ya jamii za Kitanzania wakati wa uvamizi na utawala wa kikoloni.

**Uvamizi wa kikoloni na mapambano ya jamii za Kitanzania**

Uvamizi na uanzishaji wa ukoloni katika bara la Afrika kwa kiasi kikubwa ulitumia nguvu ngumu kwa sababu jamii nyingi za Kiafrika hazikuwa tayari kuupoteza uhuru wao. Ujerumani, kama mataifa mengine ya Ulaya, ilitumia nguvu ngumu wakati ikiivamia Ujerumani ya Afrika Mashariki (Tanganyika) kwa sababu uvamizi huo ulikutana na upinzani mkali kutoka kwa baadhi ya jamii za Kitanzania. Jamii hizo zilipambana dhidi ya Wajerumani ili kuulinda uhuru wao, kulinda maadili, mila na desturi zao, kuzuia kuporwa kwa ardhi yao, na kulinda biashara na usalama wao. Jamii hizi, chini ya machifu wao shupavu, zilitumia zaidi silaha za jadi kuonesha ukakamavu, ujasiri, mshikamano na uzalendo katika kupambana dhidi ya wavamizi wa Kijerumani. Lakini, kwa kuwa wavamizi wa Kijerumani walikuwa madhubuti kijeshi na kiuchumi, matumizi yao ya nguvu ngumu yaliwadhibiti na kuzishinda jamii za Kitanzania zilizopinga uvamizi wao. Viongozi wa Kitanzania walioongoza mapambano dhidi ya uvamizi wa Kijerumani walikamatwa na kunyongwa.

Wakoloni walitumia mabavu katika maeneo mbalimbali ya Tanzania, hususani ukanda wa pwani, kusini mwa nchi, nyanda za juu kusini, kanda ya magharibi na kanda ya kaskazini. Kwa upande wa pwani, wakoloni wa Kijerumani walitumia nguvu kubwa dhidi ya watu wa Pangani wakiongozwa na Abushiri bin Salum na Bwana Heri aliyeongoza mapambano huko Saadani kati ya mwaka 1888 na 1889. Jamii za pwani zilisimama kidete pale watawala wa Kijerumani walipōsimika bendera yao kuashiria kuanza kwa utawala wao mwaka 1888. Vita hivyo vilisambaa maeneo mengi ya pwani kama Tanga, Pangani, Bagamoyo, na Dar es Salaam. Kwa kuwa Wajerumani, chini ya kiongozi wake wa kijeshi Von Weismann, walikuwa na silaha za kisasa, walifanikiwa kushinda vita hivyo na kuchukua utawala wa ukanda wa pwani mwaka wa 1889. Wajerumani walimkamata Abushiri na kumnyonga baada kusalitiwa na Jumbe Magaya wa Usagara mwaka 1889. Huko Kilwa wananchi walipambana na Wajerumani chini ya kiongozi wao Hassan bin Omari Makunganya mwaka wa 1889. Vita hiyo haikudumu kwa muda mrefu baada Makunganya kukamatwa na kunyongwa mwaka 1895 kwenye mwembe maarufu kama "Mwembe Kinyonga" huko Kilwa Kivinje.

Maeneo mengine ambayo wakoloni walitumia nguvu ngumu ni nyanda za juu kusini. Wajerumani walitumia mabavu ili kuingiza utawala wao wa kikoloni huko Iringa. Jamii ya Wahehe chini ya kiongozi wao jasiri Mtwa Mkwawa walipambana dhidi ya utawala dhalimu wa Kijerumani

FOR ONLINE READING ONLY

kuanzia mwaka 1891 hadi 1898. Vita vya Wahehe ndiyo mapambano dhidi ya Wajerumani yaliyopiganwa kwa kipindi kirefu. Mkwawa alipigana na jeshi la kikoloni ili kuulinda uhuru wa kisiasa na wa kiuchumi wa jamii yake. Mtwa Mkwawa alizuia misafara ya kibiashara isipite katika eneo lake bila kulipa ushuru. Wajerumani walipinga zuio hili na wakajiandaa kwa uvamizi dhidi yake. Katika mapambano dhidi ya Wajerumani, jeshi la Mkwawa lilimuua kamanda wa Kijerumani Emil von Zelewski na wafuasi wake. Wajerumani walishindwa katika mapigano hayo huko Lugalo mwaka 1891. Hata hivyo, Wajerumani walijipanga upya kwa kuishambulia na kuiteka ngome ya Mkwawa huko Kalenga mwaka 1894. Ngome ya Kalenga ilikuwa makao makuu ya serikali ya Mtwa Mkwawa. Pamoja na kuikamata ngome yake Mtwa Mkwawa hakukubali kuitambua serikali ya Wajerumani katika himaya yake. Hivyo, aliendesha vita ya msituni kuanzia mwaka 1894 hadi mwaka 1898 ambapo ardhi ya Wahehe iliangukia mikononi mwa Wajerumani. Mkwawa hakukubali dhihaka na aibu ya kukamatwa hivyo, alijiua kwa kujipiga risasi kichwani. Wajerumani waliukuta mwili wa Mkwawa na wakaamua kumkata kichwa na kukipeleka Ujerumani.

Kwa upande wa magharibi mwa Tanzania, Wajerumani pia walitumia nguvu ngumu katika kupenya katika ardhi ya Tanzania. Wajerumani walivamia ardhi ya Wanyamwezi na kuingia katika mapigano na Wanyamwezi mwaka 1891 hadi1893. Wanyamwezi chini ya kiongozi wao mahiri Mtemi Isike walipambana dhidi ya Wajerumani kulinda uhuru wao, hasa biashara za masafa marefu ambazo zilikuwa uti wa mgongo wa uchumi wa himaya ya Kinyamwezi. Pamoja na mapambano ya muda mrefu, Wajerumani walifanikiwa kulishinda jeshi la Isike na kuiweka himaya ya Kinyamwezi chini ya utawala wa Kijerumani mwaka 1893.

Eneo lingine ambalo watawala wa kikoloni walitumia mabavu ni katika ardhi ya Wayao kusini mwa Tanzania. Wajerumani walianzisha kodi ya kichwa kusini mwa Tanzania, jambo ambalo lilitafsiriwa na Wayao kuwa ni la kupoteza uhuru na la kinyonyaji. Chini ya kiongozi wao Chifu Machemba, Wayao walipambana na majeshi ya Kijerumani kuanzia mwaka 1890 hadi 1899. Pamoja na mashambulizi ya Wajerumani, Machemba alishinda vita hivyo katika hatua ya awali. Wajerumani walitangaza hali ya hatari kwa Chifu Machemba lakini alikataa na kuendelea kupigana. Mwishoni mwaka 1899, Wajerumani walitumia nguvu kubwa za kijeshi na kufanikiwa kumshinda Machemba ambaye alitoroka na kukimbilia Msumbiji.

Katika maeneo ya Umatumbi huko Kilwa, jamii za Kitanzania pia zilishuhudia matumizi makubwa ya nguvu kutoka kwa wakoloni wa Kijerumani. Katika eneo hili, pamoja na malalamiko mengi dhidi ya ukoloni wa Kijerumani, jamii za Umatumbi zilipinga kulazimishwa kwa nguvu kulima na kufanya kazi kwenye mashamba ya pamba yaliyoanzishwa na serikali ya kikoloni ya Kijerumani. Jamii hizi, chini ya kiongozi mahiri Kinjekitile Ngwale, walipigana dhidi ya Wajerumani katika vita vya Maji Maji kuanzia mwaka 1905

FOR ONLINE READING ONLY

hadi 1907 wakipinga kulazimishwa kulima pamba, kulipa kodi na unyanyasaji katika mazingira ya kazi. Vita hivyo vilienea katika makabila mengi ya kusini mwa Tanzania na viliyagharimu maisha ya Watanzania wengi. Huu ulikuwa upinzani mkali uliowahi kuukumba utawala wa kikoloni kuliko vita zilizopita nchini. Imani za kidini zilitumika kupata ujasiri na kuondoa tofauti za kikabila kwa wapiganaji wa Kitanzania. Kinjekitile aliwaaminisha watu kutumia maji wakati wa mapambano ili kupunguza madhara yatokanayo na mashambulizi ya silaha za moto.

Vita ya Maji Maji inaendelea kukumbukwa kama msingi wa mapambano dhidi ya ukoloni dhalimu wa Kijerumani. Kaulimbiu ya Kinjekitile ilikuwa ni uhuru na umoja ndiyo nguzo muhimu ya ushindi dhidi ya uvamizi wa wakoloni. Pamoja na mbinu hizi za Kinjekitile, risasi hazikuweza kubadilika kuwa maji na hakukuwa na msaada wa mizimu wakati wa vita kinyume na alivyowaaminisha wapiganaji wake. Wajerumani walifanikiwa kuwashinda wapiganaji wa Kinjekitile na Watanzania wengi waliuawa na viongozi wao walinyongwa. Vita ya Maji Maji ndiyo vita kubwa katika historia ya kupigania uhuru wa Tanzania. Vita hivi vilipiganwa katika eneo kubwa la kusini mwa nchi na kufanikiwa kuleta upinzani mkali kwa jeshi la Kijerumani. Vita hivyo viliwafanya Wajerumani wasimamishe mradi wa kilimo cha pamba katika maeneo ya Umatumbi na hata kubadilisha kidogo mfumo wao wa utawala katika koloni hili. Wajerumani walipunguza ukatili dhidi ya wananchi katika kukusanya kodi na kutafuta nguvu kazi katika kuijenga miundombinu ya serikali kama barabara, reli na maboma ya utawala.

Kwa upande wa Zanzibar, wakoloni wa Kiingereza pia walitumia nguvu ngumu kupenyeza ajenda zao za kuwarahisishia utawala wao. Mfano, Mwaka 1944 kulizuka ugonjwa wa ng'ombe wa kimeta. Kutokana na ugonjwa huo, Idara ya Mifugo ilianza kuwapa chanjo ng'ombe wote na kuuliwa ng'ombe wenye maradhi. Vilevile, ng'ombe wasiokuwa na maradhi waliogeshwa kwenye maji ya dawa ili kuwakinga na maradhi. Wazanzibari walioipinga amri hiyo walipata adhabu kali. Jambo hili halikuwapendeza wananchi kwa kuhofia kwamba wakoloni walitaka kuwaua ng'ombe wao ili wayachukue maeneo yao ya malisho na kuwapa walowezi wa Kiarabu. Walijua lengo ni kuwapa walowezi wa Kiarabu ili wapanue mashamba ya karafuu kwa nia ya kufaidi bei ya juu ya karafuu iliyopanda maradufu katika soko la dunia kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya karafuu katika viwanda baada ya Vita Kuu ya Pili ya dunia. Mwaka 1951 wananchi wengi waligoma kuwapa chanjo ng'ombe wao. Msako mkali ulifanyika kote Zanzibar. Watu zaidi ya kumi walikamatwa wakapelekwa rumande katika jela ya Kiinua Miguu Zanzibar kwa kupinga chanjo. Waandamanaji wakaivamia jela ili kuwakomboa viongozi wao. Mapambano yakaanzia hapo. Hii ndiyo sababu ya mgogoro huu kuitwa vita vya ng'ombe.

Vilevile, kuna maeneo ambayo wakoloni walitumia njia zote mbili, yaani nguvu ngumu na laini katika kuhakikisha wanafikia malengo yao. Njia hii ilijulikana kama njia ya diplomasia na vita au mabavu.

FOR ONLINE READING ONLY

**Kazi ya kufanya 7.3**

Tumia vyanzo mbalimbali vya taarifa kubainisha maeneo mengine ambayo nguvu ngumu na laini ilitumika na wakoloni wa Kijerumani katika kutawala jamii za Kitanzania.

Zoezi 7.1

1. Kwa kutumia mifano sahihi, fafanua jinsi elimu ilivyotumiwa kama nguvu laini wakati wa ukoloni nchini Tanzania.
2. Ushirikishwaji ni miongoni mwa njia zilizotumiwa na wakoloni katika kutawala na kuibadili mifumo ya maisha ya jamii za Kitanzania. Jadili dhana ya usaliti iliyojitokeza katika njia hiyo.
3. Jadili madhara ya matumizi ya nguvu ngumu.
4. Je, ni kwa namna gani viongozi wa jamii za Kitanzania walipambana ili kuyalinda maadili ya taifa?
5. Eleza kwa mifano sahihi namna elimu ilivyotumika katika kueneza utamaduni wa kikoloni.

## Chimbuko la ukoloni na kuenea kwake Tanzania

Chimbuko la ukoloni nchini Tanzania ni matokeo ya kukua kwa ubepari huko Ulaya Magharibi katika nusu ya pili ya karne ya 19. Ukuaji huu wa ubepari umepitia hatua mbalimbali kama vile ubepari-uchwara kati ya karne ya 15 na ya 18, Ubepari-shindani (au ubepari wa viwanda) kati ya karne 18 na katikati ya karne ya19 na ubepari-hodhi kuanzia robo ya mwisho ya karne ya 19. Ukoloni ulioletwa Tanzania na Afrika kwa ujumla una uhusiano zaidi na hatua ya mwisho ya ubepari-hodhi. Katika hatua hii, ubepari ulikuwa umekua sana na hata hatua ya mapinduzi ya viwanda ilikuwa juu zaidi.

Kama ilivyo ada, ubepari unahitaji kupata si tu faida bali faida kubwa. Kupata faida kubwa kulionekana kuwa kugumu katika hatua ya ubepari-shindani kwa kuwa makampuni mbalimbali yalishindana katika aina moja ya masoko huku wakizalisha na kuuza bidhaa zilizofanana. Hali hii ilisababisha masoko kujaa sana; na kwa hiyo, kuuza bidhaa kwa bei za chini na kupata faida kidogo au kukosa kabisa faida. Hii ilisababisha kutokea kwa mdororo wa uchumi huko Ulaya mwaka 1873. Mdororo huo ulijirudia tena mwaka 1895. Mdororo huu wa uchumi ulisababisha ubepari kubadilika na kukua kwenda hatua ya ubepari-hodhi ulioleta ubeberu mwishoni mwa karne ya 19. Pamoja na mdororo wa uchumi, kukua kwa teknolojia na mitaji kulikuwa pia sababu zilizosababisha kukua kwa ubepari katika hatua hii.

Ubepari katika hatua hii ulihitaji kupata faida kubwa na wakati huo huo ubepari na mapinduzi ya viwanda vilikuwa vimeenea Ulaya Magharibi yote. Hali hii ilizidi kutengeneza matatizo ya uchumi yaliyozuia kupata faida kubwa na migogoro ya wafanyakazi waliodai masilahi zaidi kutoka kwa wamiliki wa viwanda. Kwa hiyo, nchi za kibepari zilianza kutafuta maeneo mengine nje ya Ulaya ambayo yanaweza kuwasaidia kupata suluhisho la

FOR ONLINE READING ONLY

matatizo hayo. Suluhisho la kwanza lilikuwa kupata faida kubwa na pili kutatua mahitaji makubwa yaliyoletwa na mapinduzi ya viwanda, yaani masoko, maeneo ya kuwekeza mitaji mikubwa, kupata malighafi za kitropiki na kupata vibarua au nguvu kazi rahisi ya kufanikisha uzalishaji mali katika sekta tofauti. Hapa ndipo Afrika, ikiwemo Tanzania, ilipoonekana kuwa suluhisho sahihi kwa ajili ya ustawi wa ubepari na viwanda vya Ulaya. Hapo ndipo ukoloni ulipochipukia na kuwa njia ya ubepari kusaidia kupata mahitaji ya viwanda na kuwezesha ubepari kupata faida kubwa kama ilivyokusudiwa.

Kwa hiyo, mataifa ya Ulaya Magharibi kama vile Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Ubelgiji, Hispania, Ureno, na mengineyo yalianza kutafuta makoloni barani Afrika ili kupata maeneo yatakayosaidia kupatikana kwa mahitaji ya viwanda vyao. Katika kutafuta hayo maeneo, mataifa haya ya Ulaya yalijikuta yakigongana katika maeneo waliyowavutia wote. Hali hii ilisababisha migogoro miongoni mwao na tishio la kuibuka kwa vita miongoni mwa mataifa haya kuwa dhahiri. Kama ilivyoelezwa hapo awali, kwa kuogopa kutokea kwa vita, kiongozi wa Ujerumani na mwanadiplomasia, Kansela Otto von Bismack, aliitisha mkutano ili kuligawa bara la Afrika kwa amani. Mnamo mwaka 1884-1885, kiongozi huyo wa Ujerumani aliitisha mkutano mjini Berlin ambapo mataifa ya Ulaya yaliyokuwa yanapigania kuwa na makoloni barani Afrika yalihudhuria pamoja na mataifa machache yalialikwa kama vile Marekani. Pamoja na mambo mengine, mkutano huu uliligawa na kuchora mipaka ya bara la Afrika. Lakini Mkutano huu ulijikita zaidi kuigawa Afrika Magharibi na kuacha maeneo mengine kama Afrika Mashariki kugawanywa baadaye. Afrika Mashariki iligawanywa kupitia makubaliano ya mataifa mawili, yaani Ujerumani na Uingereza mwaka 1886 na yale ya 1890 (*Delimitation and Heligoland Treaties*) mtawalia. Ujerumani ya Afrika Mashariki (Tanganyika, Rwanda na Burundi) ilichukuliwa na Ujerumani huku Kenya, Zanzibar na Uganda zikiangukia mikononi mwa Uingereza. Mpaka wa Ujerumani ya Afrika Mashariki na Ureno ya Afrika Mashariki (Msumbiji) uliweka mto Ruvuma kuwa mpaka mwaka 1891. Wajerumani na Wabelgiji walikubaliana kuwa mpaka wa Ujerumani ya Afrika Mashariki na Kongo ya Kibelgiji uwe katikati ya Ziwa Tanganyika mwaka 1894.

**Kazi ya kufanya 7.4**

Soma matini kutoka vyanzo mbalimbali vya taarifa, kisha uchambue sababu za kiuchumi zilizosababishwa na mapinduzi ya viwanda huko Ulaya hivyo kusababisha kutawaliwa kwa jamii za Kitanzania.

### Watangulizi wa ukoloni

Suala la ukoloni halikuwa tukio la siku moja bali ni mchakato uliochukua muda mrefu na kuwashirikisha watu wengi wa aina tofauti tofauti. Miongoni mwa makundi muhimu katika ujio wa ukoloni Tanzania lilikuwa kundi la watangulizi wa ukoloni, kama inavyojadiliwa hapa chini.

*(a) Wapelelezi*

Kulikuwa na makundi mawili ya wapelelezi, Wajerumani na Waingereza. Miongoni mwa wapelelezi wa Kijerumani ni Karl Peters,

FOR ONLINE READING ONLY

Johann Krapf, Johannes Rebman, Karl von Decken, Albretch Roscher na von Schoeler. Wapelelezi wa Kiingereza walikuwa Richard Francis Burton, John Hanning Speke, John Morton Livingstone, Henry Morton Stanley na wengineo. Wapelelezi hawa walichunguza maeneo mbalimbali na kupeleka taarifa katika nchi zao kuhusu maeneo yaliyokuwa yanafaa kwa kilimo, uchimbaji madini, mito, maziwa na ardhi yenye rutuba. Wapelelezi walitumia nguvu laini kushawishi jamii za Kitanzania kukubali kutoa ardhi zao kwa wakoloni.

*(b) Wamisionari*

Hawa walikuwa waenezaji wa dini ya Kikristo. Walikuja Tanzania katika makundi mbalimbali yaliyoitwa madhehebu. Wamisionari walikuwa na lengo kuu la kueneza dini ya Kikristo na kutoa elimu kwa jamii za Kitanzania na Afrika kwa ujumla. Hivyo, katika kutimiza kazi zao walijenga makanisa, shule na hospitali. Wamisionari walitumika kuzishawishi jamii za Kitanzania kuwakubali wakoloni ili wapate maendeleo. Mfano wa mashirika ya wamisionari yaliyokuja Tanzania ni Holy Ghost Fathers, White Fathers (Missionaries of Africa), Church Missionary Society (CMS), Universities Mission to Central Africa (UMCA), na London Missionary Society (LMS). Wamisionari walipewa mafunzo rasmi kwa ajili ya kutumika katika makoloni. Vilevile, safari za wamisionari kuja Afrika zilifadhiliwa na serikali za wakoloni. Aidha, wapelelezi walipumzika katika kambi maalumu za wamisionari zilizokuwapo pwani na bara.

*(c) Wafanyabiashara*

Kulikuwa na wafanyabiashara wa kizungu walioingia nchini kibinafsi au kwa kampuni. Hawa wote walikuwa na lengo la kufanya biashara na kukusanya taarifa kwa ajili ya kuzipeleka kwenye serikali zao huko Ulaya na Marekani. Kwa upande wa kampuni, kulikuwa na kampuni mbalimbali kutoka nchi za Uingereza na Ujerumani. Kampuni hizo ni kama Imperial British East Africa Company iliyokuwa chini ya Harry Johnson na German East Africa Company iliyokuwa chini ya Karl Peters.

Matokeo ya safari za watangulizi wa ukoloni

Watangulizi wa ukoloni waliingia Tanzania kwa madhumuni mbalimbali lakini lengo lao kubwa ilikuwa kukusanya taarifa mbalimbali kuhusu uzuri na utajiri wa jamii za Kitanzania na kuzipeleka katika mataifa yao. Kwa kuwa walificha shabaha yao hiyo, jamii za Kitanzania ziliwapokea kwa ukarimu mkubwa na kuwapa kila ushirikiano waliouhitaji. Baada ya kupata taarifa kuhusu maeneo mbalimbali ya jamii za Kitanzania, mataifa ya Ulaya yaliaanza kugombania maeneo hayo. Hatimaye, Tanzania bara (ikiwa sehemu ya Ujerumani ya Afrika Mashariki) iliangukia katika utawala wa kikoloni wa Wajerumani wakati Zanzibar ilitawaliwa na Uingereza kupitia Waarabu walioongoza kwa niaba yao.

**Kazi ya kufanya 7.5**

Fanya utafiti na andika kuhusu dola ya kikoloni na sekta zake na jinsi kila sekta ilivyofanya majukumu yake katika makoloni ya Tanganyika na Zanzibar kati ya mwaka 1890 na miaka ya mwanzoni mwa 1960.

FOR ONLINE READING ONLY

### Kutawaliwa kwa Tanganyika na Zanzibar

Mkataba uliosainiwa baina ya Ujerumani na Uingereza mwaka 1890 ulihitimisha mgawanyo wa taifa la Tanganyika lililokabidhiwa kwa wakoloni wa Kijerumani. Baada ya mgawanyo huo, Tanganyika, Rwanda na Burundi zilianza kujulikana kwa jina la Ujerumani ya Afrika Mashariki. Mgawanyo huu pia ulihusisha pwani ya Tanganyika ambayo pia ilikabidhiwa kwa wakoloni wa Kijerumani baada ya kulipa fidia kwa Sultani wa Zanzibar. Mkataba wa Heligoland ulirasimisha kisiwa cha Zanzibar kuwa chini ya himaya ya utawala wa Waingereza na kufanya visiwa vyote viwili vya Unguja na Pemba kuwa chini ya uangalizi wa Uingereza. Moja ya ajenda ya utawala wa Waingereza ilikuwa kukomesha kabisa biashara ya utumwa na kuimarisha masilahi ya kiuchumi ya Uingereza visiwani Zanzibar. Ili kutekeleza hilo, serikali ya Uingereza ilimteua Gavana wa Zanzibar mwaka 1913.

Kwa upande wa Tanzania bara, Ujerumani ilitawala kuanzia mwaka 1885 hadi 1918 ambapo utawala wao ulikoma baada ya kushindwa katika Vita Kuu ya Kwanza vya Dunia. Eneo hili lilikabidhiwa rasmi mwaka 1919 kwa Uingereza likiwa chini ya mamlaka ya Shirikisho la Mataifa (*League of Nations*) kama Eneo Lililo Chini ya Uangalizi/Udhamini wa Uingereza (*Mandate Territory*). Eneo hili lilibadilishwa jina kutoka Ujerumani ya Afrika Mashariki na kuwa Tanganyika mwaka 1920. Ubelgiji ilikabidhiwa Rwanda na Burundi izitawale kwa niaba ya mamlaka ya Shirikisho la Mataifa (*League of Nations*) kama Eneo Lililo Chini ya Uangalizi/Udhamini wa Ubelgiji (*Mandate Territory*).

#### Zoezi 7.2

1. Jadili msukumo uliosababisha wakoloni kutawala jamii za Kitanzania.
2. Eleza ni kwa namna gani maendeleo ya ubepari wa Ulaya ya Magharibi uliathiri maendeleo katika jamii za Kitanzania.
3. Jadili kwa kina jinsi wakoloni walivyochangia kumomonyoka kwa maadili ya jamii za Kitanzania.
4. Kwa nini wakoloni walitumia mikataba ya kilaghai ili kuzitawala jamii za Kitanzania?
5. Fafanua ni kwa namna gani Tanzania kama taifa tunaweza kujifunza kutokana na mikataba ya kilaghai iliyosainiwa kati ya wakoloni na machifu wa jamii za Kitanzania.
6. Kwa kutumia mifano sahihi, eleza dhana ya uzalendo kama ilivyooneshwa na viongozi wa jadi wa jamii za Kitanzania katika kupinga utawala wa kikoloni.
7. Jadili umuhimu wa vita vya Maji Maji katika historia ya Tanzania.

### Athari za ukoloni

Ukoloni ulidumu kwa miaka zaidi ya sabini (70) nchini Tanzania. Kwa minajili hii, ukoloni umedumu kwa muda mrefu zaidi ya vizazi viwili na kufanya mambo mengi kama vile kuleta mambo mapya, kufanya mabadiliko katika sekta mbalimbali na hata

FOR ONLINE READING ONLY

kuyaendeleza yale waliyoyakuta. Hivyo, ukoloni ulikuwa na athari mbalimbali katika jamii za Kitanzania katika nyanja zote, yaani nyanja za kiuchumi, kisiasa, kijamii, kiutamaduni na kimaadili. Athari hizo zinajadiliwa hapa chini.

### Athari za kisiasa

Kama tulivyoona hapo awali, wakoloni walitumia mbinu mbalimbali kuingia na kutawala katika jamii za Kitanzania. Matokeo ya utawala huo yalikuwa na athari katika siasa za jamii za Kitanzania kama ifuatavyo:

*(a) Kuanguka kwa tawala za jadi*

Ujio wa wakoloni uliendana sambamba na kuanguka kwa tawala za jadi za jamii za Kitanzania. Ikumbukwe kuwa katika maeneo mengi , ambako wakoloni waliimarisha utawala wao, jamii za Kitanzania ziliupinga utawala wa kikoloni. Baada ya ukoloni kuingia mnamo mwaka 1885, kulikuwa na jitihada mbalimbali za kuhakikisha wanasimika utawala wao nchini Tanzania. Hivyo, kwa kutumia mbinu mbalimbali kama nguvu laini, nguvu ngumu na ushirikishaji walifanikiwa kuziangusha tawala hizo na kuanzisha utawala wao ambao ulikuwa chini ya gavana. Dola zote za kijadi ziliangushwa na kuundwa dola moja ya kikoloni iliyosimamia koloni lote.

*(b) Kuibuka kwa mfumo wa utawala wa kikoloni*

Baada ya kuzishinda jamii katika maeneo yote ya Tanganyika na Zanzibar, wakoloni walianzisha mfumo mpya wa utawala ambao ulikuwa tofauti na ule wa jamii za Kitanzania. Kwa Wajerumani, utawala ulikuwa chini ya Gavana ambaye alisaidiwa na Wakuu wa Wilaya, Akida, Liwali, Jumbe na mkuu wa kijiji (Headman). Kwa upande wa mfumo wa utawala wa Uingereza, kulikuwa na Gavana, Wakuu wa Majimbo, Wakuu wa Wilaya, na Viongozi wa Jadi ambao walikuwa wanafanya kazi kwa niaba ya serikali ya kikoloni ya Kiingereza. Mfumo huu wa utawala ulikuwa wa kiserikali na ulikuwa unaratibiwa kutokea katika ngazi za chini hadi za juu.

*(c) Kuibuka kwa viongozi vibaraka*

Kutokana na mfumo wa utawala wa kikoloni kutumia viongozi wa jamii za Kitanzania kama sehemu ya utawala wao, viongozi hao wa jamii za Kitanzania, ambao wengi wao walikuwa machifu, walianza kufanya kazi kwa niaba na masilahi ya wakoloni na si kwa manufaa ya jamii zao. Hii iliambatana na kufanya kazi za nguvu zisizo na malipo au malipo kidogo. Kazi hizo zilikuwa kama vile kulima mazao ya biashara kwa manufaa ya wakoloni na ujenzi wa miundombinu kama barabara, shule na zahanati. Wale ambao walikiuka utaratibu na sheria za kikoloni walipewa adhabu kali ikiwamo adhabu ya viboko na kifungo.

*(d) Kuanzishwa kwa taasisi mpya za kimagharibi katika utawala*

Ukoloni ulianzisha taasisi mpya za kimagharibi katika utawala. Kuna taasisi mpya kama mahakama, bunge, jeshi au polisi zilizoundwa kusaidia utawala kutekeleza wajibu na matakwa ya ukoloni. Pia, mikoa, wilaya na idara mbalimbali zilianzishwa na hata kurithiwa na serikali baada ya uhuru hata leo.

FOR ONLINE READING ONLY

**Athari za kiuchumi**

Dhumuni kubwa la ujio wa wakoloni hapa nchini lilikuwa kuzinyonya rasilimali za jamii za Kitanzania kadri iwezekanavyo. Hivyo, ujio wa ukoloni ulileta athari mbalimbali za kiuchumi katika jamii za Kitanzania kama ifuatavyo:

*(a) Kuletwa kwa mazao ya biashara*

Wakoloni walipokuja waliweka mkazo katika uzalishaji wa mazao ya biashara kama mkonge, kahawa, pamba, chai na pareto. Mkazo huu ulilenga kuzalisha malighafi kwa ajili ya kulisha viwanda vya Ulaya. Kwa hiyo, mashamba makubwa yalianzishwa kulima mazao hayo. Wakulima wadogo nao walisisitizwa kujikita katika kulima mazao hayo mapya, hasa pamba na kahawa. Mazao haya yanalimwa hapa nchini hadi leo.

*(b) Uchumi fedha*

Athari zingine zilizoletwa na wakoloni ni kuubadilisha mfumo wa uchumi kwa kuuleta mfumo wa matumizi ya fedha. Kabla ya ujio wa ukoloni, jamii za Kitanzania zilijihusisha na biashara kwa kubadilishana bidhaa kwa bidhaa, kwani fedha haikuwa muhimu sana katika biashara na mabadilishano ya bidhaa. Ujio wa uchumi wa kifedha ulileta aina nyingine ya uchumi ambao ulizilazimu jamii za Kitanzania kufanya kazi kwenye mashamba ya kikoloni na kulima mazao ya biashara ili kupata fedha kwa ajili ya kulipa kodi na kupata mahitaji, hasa kununua bidhaa kutoka Ulaya. Ili kurahisisha biashara kati ya koloni na Ujerumani au Uingereza, taasisi za kifedha kama benki za kibiashara zilianzishwa ili kurahisisha biashara ya kusafirisha bidhaa nje na kuingiza bidhaa Tanzania. Baadhi ya benki hizo ni Deutsche Bank, Barclays na Standard Bank.

*(c) Manamba*

Utawala wa kikoloni ulianzisha mfumo wa kutumia manamba. Hawa walikuwa vibarua ambao walitolewa eneo moja la nchi kwenda kufanya kazi katika eneo lingine. Utaratibu huu wa manamba ulibuniwa na wazungu ili kuhakikisha wanapata vibarua wa kazi katika mashamba yao muda wote. Hii iliwasaidia wakoloni kwani waliwalipa ujira mdogo wafanyakazi hao. Pia, waliwadhibiti katika mashamba yao kwa sheria kali ya kuwazuia wasihamehame shamba moja hadi jingine. Mbinu mojawapo ilikuwa kuwauzia bidhaa zao ili mwisho wa wiki au mwezi walipe madeni yao na kujikuta wakiendelea kutegemea kufanya kazi mashambani na migodini. Mfumo huu wa manamba ulileta madhara makubwa kwa jamii kwani manamba walichukuliwa eneo moja na kusafirishwa eneo jingine. Hali hii ilisababisha utengano wa kifamilia na baadhi yao kufa kutokana na hali ya hewa na magonjwa. Manamba wengi walichukuliwa kutoka Jimbo la Kati (Dodoma na Singida), Jimbo la Magharibi (Kigoma, Tabora na Rukwa). Jimbo la Kusini (Lindi na Ruvuma) na Jimbo la Ziwa (Mwanza na Shinyanga) kwenda kufanya kazi katika mashamba ya katani huko Tanga na Morogoro na mashamba ya chai na kahawa huko Moshi, Arusha na Usambara.

*(d) Unyang'anyi wa ardhi*

Moja ya lengo kuu la wakoloni ilikuwa kuzalisha malighafi kwa ajili ya viwanda vyao huko Ulaya. Hivyo, walipofika nchini walihakikisha kila sehemu iliyo na ardhi

FOR ONLINE READING ONLY

yenye rutuba inachukuliwa kwa nguvu kwa ajili ya kulima mazao ya kibiashara. Hii ilisababisha maeneo mengi ya wenyeji kuchukuliwa na wakoloni kwa ajili kuanzisha mashamba makubwa ya kilimo. Watanzania walioathirika na unyakuzi huu wa ardhi walibaki kwenye ardhi isiyokuwa na rutuba. Maeneo yaliyoathiriwa zaidi ni yale ambayo wakoloni walianzisha mashamba makubwa ya kilimo kama vile Arusha, Tanga, Morogoro, na Pwani.

*(e) Kazi za lazima*

Katika kuhakikisha kuwa wanapata nguvukazi ya uhakika na kwa gharama nafuu, wakoloni walianzisha utaratibu wa kufanya kazi kwa lazima kwenye mashamba na maeneo mengine ya uzalishaji mali. Kulikuwa na aina nyingi za kufanya kazi kwa lazima. Kwa mfano, walitenga siku moja kwa wiki kwa ajili ya kufanya kazi kwenye mashamba ya kikoloni au saa kadhaa kutumika kwa ajili ya kujenga barabara, kuponda mawe na kazi nyinginezo. Watanzania hawakulipwa chochote bali waliambiwa ni kazi za kujitolea, jambo ambalolilikuwa unyonyaji mkubwa.

*(f) Kunyonywa kwa rasilimali za jamii za Kitanzania*

Ukoloni ulishiriki moja kwa moja katika unyonyaji na usafirishaji wa rasilimali za jamii za Kitanzania. Rasilimali kama pembe za ndovu, madini, wanyama, ngozi na nyinginezo zilivunwa na kuchukuliwa na wakoloni na kusafirishwa Ulaya kwa faida yao. Wakoloni walikuwa na meli kubwa za kibiashara zilizosafirisha mazao hayo hadi Ulaya Magharibi. Kampuni kubwa za kibiashara za Kijerumani na baadaye za Kiingereza zilitawala biashara wakati wa ukoloni Tanganyika na Zanzibar. Rasilimali hazikuwafaidisha Watanzania kwani ziliuzwa kwa faida ya mataifa ya Ulaya Magharibi.

**Kazi ya kufanya 7.6**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, ikiwemo mitandao, tathimini athari hasi na chanya za kijamii za ukoloni nchini Tanzania.

**Athari za kijamii**

Ujio wa wakoloni nchini Tanzania ulisababisha athari za kijamii kama ifuatavyo:

*(a) Ubaguzi*

Utoaji wa huduma za kijamii uliangalia zaidi rangi ya wale waliopelekewa huduma hizo. Kulikuwa na shule za Wazungu, Waarabu, Wahindi na Waafrika. Zaidi ya hilo, utoaji wa huduma hizo na ubora wa shule hizo ulitegemea rangi ya wahusika. Kulikuwa na sheria mbalimbali zilizowekwa na wakoloni ili kuhakikisha kuwa watu wote wanazifuata. Kwenye huduma za usafiri kama mabasi ya umma na hotelini kulikuwa na mabasi kwa ajili ya Wazungu ambapo Waafrika kamwe hawakuruhusiwa kuchangamana. Ubaguzi ulikuwapo katika maeneo yote, katika elimu, afya, uongozi na makazi. Wazungu walikuwa raia wa daraja la kwanza walipata huduma nzuri za kila aina huku Waafrika wakipata huduma za kiwango cha chini kuliko wote.

Athari nyingine za kijamii wakati wa ukoloni zilikuwa katika huduma za ujenzi

FOR ONLINE READING ONLY

na makazi ya watu ambayo ilitolewa kutegemeana na rangi za watu. Kulikuwa na makazi ya Wazungu ambayo yalikuwa na huduma zote za msingi kama maji safi na mfumo wa maji taka. Vilevile, kulikuwa na makazi ya Wahindi, Waarabu na jamii yote ya watu kutokea bara la Asia. Hawa nao walikaa kwenye maeneo ya mijini na walikuwa na huduma bora za makazi kama nyumba, maji na umeme kama raia wa daraja la pili. Watanzania walikuwa daraja la tatu na walikaa kwenye makazi duni yasiyokuwa na miundombinu yoyote. Katika mpangilio huo, ilikuwa marufuku kwa mtu mweusi kwenda au kuishi kwenye makazi ya Wazungu au jamii ya Kiasia. Huduma za maji safi na maji taka zilitolewa kwenye makazi ya Wazungu na Waasia.

Huduma hizi hazikutolewa kwenye makazi ya Watanzania. Kwa ujumla, maeneo mengi waliyokuwa wanaishi Watanzania yalikuwa hayajapimwa; hivyo, ilikuwa vigumu kufikisha huduma hizo. Vilevile, haikuwa kipaumbele cha wakoloni kutoa huduma hizo kwa jamii ya Watanzania.

*(b) Kuharibiwa kwa mifumo ya jadi ya afya*

Katika jamii ya Kitanzania kulikuwa na namna ya kupambana na magonjwa kabla ya ujio wa wakoloni. Jamii za Kitanzania ziliyagawa magonjwa katika maeneo mawili, magonjwa yatokanayo na uwezo wa Mungu (magonjwa ya asili) na magonjwa yatokanayo na uwezo wa mwanadamu. Magonjwa yaliyotokana na uwezo wa Mungu yalitibiwa kwa kutumia mizizi, majani na matunda pori. Magonjwa yaliyosababishwa na uwezo wa mwanadamu yalitibiwa na waaguzi na waganga wa jadi. Baada ya ujio wa wakoloni barani Afrika, serikali ya kikoloni ilijikita kwanza kuwahudumia wanajeshi wake, watawala na walowezi ambao walikuwa katika hatari ya kushambuliwa na magonjwa ya kitropiki kwa kujenga hospitali. Serikali ya kikoloni ilianza kutoa huduma kwa Waafrika, hasa manamba na wafanyakazi wa mijini ambao idadi yao ilikuwa ikiongezeka katika miaka ya 1900. Huduma ya afya pia ilitumika kama mkakati wa kuthibitisha uhalali wa serikali ya kikoloni barani Afrika. Baada ya Vita ya Kwanza ya Dunia, huduma za afya zilipanuka kutoka kuhudumia watu wachache na kuanza kuhudumia watu wengi zaidi. Wakati wa ukoloni, huduma za afya za serikali zilikuwa chache zikijikita zaidi mijini wakati wamisionari walijenga huduma hizi, hasa maeneo ya vijijini kulikokuwa na watu wengi.

Nchini Tanzania hospitali zilijengwa kimkakati kwa kuzingatia mahitaji ya serikali ya kikoloni. Hospitali na vituo vingi vya afya vilijengwa katika maeneo yenye tija ya kama vile kilimo cha mazao ya biashara. Maeneo hayo ni Bukoba, Kilimanjaro na Mbeya kwa ajili ya kuimarisha kilimo cha kahawa, Tanga kilimo cha mkonge na Mwanza kwa ajili ya kilimo cha pamba. Huduma za kijamii eneo la Dar es Salaam ziliwahudumia watawala wa kikoloni. Katika maeneo ya Majimbo ya Kati na Magharibi mwa Tanzania yaliyotengwa kwa ajili ya kutoa manamba, huduma za afya zilikuwa chache mno, na maeneo mengine hazikuwepo kabisa. Hospitali zilizojengwa ni pamoja na *Kilimanjaro Christian Medical Centre* (KCMC) huko Kilimanjaro, Bugando huko Mwanza, Peramiho huko Songea,

FOR ONLINE READING ONLY

na Ndanda huko Mtwara. Huduma za afya, zilikuwa na athari hasi katika jamii na maadili ya Kitanzania. Athari hizo ni pamoja na:

(i) Huduma zilikuwa za kibaguzi kinyume na maadili ya Kitanzania. Maadili ya Kitanzania yamejikita katika haki na usawa. Ubaguzi wa rangi, ulitawala huduma za kiafya. Raia wa kigeni walitibiwa katika hospitali bora zaidi nchini au nje ya nchi na Watanzania walipata huduma duni za afya;

(ii) Huduma za afya zilitolewa kwa kuangalia maeneo muhimu kwa uchumi wa kikoloni. Serikali ya kikoloni ilipendelea kujenga huduma za afya katika maeneo yenye kiwango kikubwa cha uzalishaji wa malighafi kama Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Bukoba, Mbinga, na Morogoro huku wakiweka mkazo mdogo katika maeneo yasiyo na uzalishaji mkubwa kama ya magharibi na katikati ya nchi, na

(iii) Huduma za afya zilizoanzishwa na wakoloni zilisababisha Watanzania kudharau tiba za asili zenye uwezo wa kutibu magonjwa mbalimbali. Baadhi ya dawa hizo zilikuwa zikitumika kutibu magonjwa mengi katika jamii ya Kitanzania.

**Zoezi 7.3**

1. **"Huduma za afya zilitumika kama mbinu ya kiutawala na ya kinyonyaji dhidi ya jamii za Kitanzania." Jadili uhalali wa hoja hii.**
2. **Fafanua matokeo hasi ya huduma za afya zilizotolewa wakati wa ukoloni.**
3. **Eleza ni kwa namna gani huduma za afya zilizoanzishwa na wakoloni ziliwanufaisha Watanzania.**
4. **Ni vigezo gani vilivyozingatiwa wakati wa uanzishwaji wa taasisi za afya wakati wa ukoloni?**
5. **Kwa kuzingatia taasisi za afya zilizojengwa wakati wa ukoloni, eleza namna Watanzania wanavyoendelea kunufaika na huduma hizo baada ya uhuru.**

*(c) Ujio wa elimu ya kikoloni*

Kabla ya ujio wa wakoloni, jamii za Kitanzania zilikuwa na mfumo wake wa elimu ambao ulitofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Elimu hiyo ilijikita katika ujuzi, mila, desturi, sheria na maadili ya jamii. Elimu hii ilisaidia kujenga jamii ya Kitanzania kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Wakoloni walipoingia waliiona elimu ya jadi kama ya kijinga na iliyopitwa na wakati. Kama ilivyokuwa sekta ya afya, elimu ya kikoloni pia ilianzishwa kimkakati ili kukuza uchumi wa kibepari barani Ulaya. Elimu ilikuwa nguvu laini iliyotumiwa na wakoloni katika kupenyeza ajenda yao ya kuinyonya Tanganyika. Elimu ya kikoloni kwa Watanzania ililenga katika kuendeleza masilahi ya kibepari kwa mataifa ya Ulaya na si kukidhi haja na matakwa ya wananchi. Waingereza walijikita katika kuelekeza mbinu bora za kilimo na kuimarisha viwanda vya kuchakata malighafi ya hapa nchini. Kielelezo 7.1 kinaonesha shule ya kwanza ya serikali ya kikoloni iliyojengwa huko Tanga, iitwayo Shule ya Sekondari Old Tanga.

FOR ONLINE READING ONLY




Kielelezo 7.1: *Shule ya kwanza ya serikali ya kikoloni (Shule ya Old Tanga)*

FOR ONLINE READING ONLY

**Elimu ya kikoloni ilileta matokeo hasi yaliyoathiri jamii za Kitanzania kutokana na sababu zifuatazo:**

(i) **Kwa sehemu kubwa, ilitumika kama mkakati wa kuimarisha utawala wa kikoloni na uyonyaji katika Tanzania. Waafrika walijifunza ualimu wa dini, ualimu, ukarani na fani nyinginezo ili waajiriwe serikalini kwa lengo la kuimarisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa faida ya wakoloni. Hii ilikuwa kinyume na maadili ya Kitanzania yaliyojengwa katika elimu ya jadi iliyosimamia usawa kwa watu wote bila kujali jinsia, umri na hali ya mtu;**

(ii) **Ilitumika kama chombo cha kurahisisha utawala wa wakoloni,** kuwadhibiti Waafrika kifikra na **kuendelea kuwadunisha katika nyanja mbalimbali. Waafrika walioipata elimu ya kikoloni walishindwa kutumikia na kuendeleza jamii zao kwa sababu elimu walioyopata iliwaandaa kufanya kazi ya kuimarisha utawala wa kikoloni;**

(iii) **Iliathiri maadili ya jamii yaliyojengwa katika usawa na mshikamano. Kwa kuzigawa jamii za Kitanzania katika matabaka, ilisababisha baadhi ya wanajamii walioipata elimu hiyo kujiona bora kuliko wale wasioipata elimu ya kikoloni. Pia, walitaka kuishi maisha sawa na watawala wa kikoloni kinyume na mila, desturi na utamaduni wa maadili ya Kitanzania, ambayo yalihimiza usawa, mshikamano na upendo;**

(iv) **Ilitolewa kwa ubaguzi wa rangi. Watoto wa Wazungu, Kihindi na Kiarabu walisoma katika shule bora na kupata elimu bora. Jambo hili lilipandikiza dhana ya ubaguzi wa rangi kinyume na miiko, utamaduni na maadili ya Mtanzania yaliyojengwa katika usawa;**

(v) **Ilitolewa kwa nadharia kwa Waafrika na ilijenga hulka ya kudharau shughuli za mikono kama kilimo, ufugaji, uvuvi na ususi. Watanzania walianza kuwa na hulka ya kupenda** kazi za ofisini zaidi kuliko kazi

za kilimo, uvuvi na ufundi asilia. Jambo hili liliendelea kuwaathiri Watanzania hata baada ya uhuru kwani kazi za mikono zilitafsiriwa kama kazi za wasio wasomi. Hii iliathiri ukuaji wa sekta ya kilimo, uvuvi, ufugaji na ufundi;

(vi) Iliondoa dhana ya kujiamini na ujasiri miongoni mwa Watanzania. Utamaduni na maadili ya Kitanzania yaliyokuwapo kabla ya ukoloni yaliwafundisha vijana kujiamini na kuwa jasiri katika kuilinda jamii na nchi yao. Elimu ya kikoloni iliwafanya Watanzania wauone utamaduni na maadili yao kuwa ni duni. Pia, iliwafanya wajione kuwa watu duni, wanyonge na wasiofaa kulinganishwa na wakoloni. Hali hii iliwarahisishia wakoloni kuwatawala kirahisi na kufanikisha malengo yao ya kinyonyaji, na

(vii) Matumizi ya lugha za kigeni katika elimu ya kikoloni kama njia ya mawasiliano ilileta changamoto mbalimbali kwa Watanzania, ikiwamo ugumu wa kuelewa dhima ya elimu ya kikoloni. Tena ilifanya wazidharau lugha za asili na kuona kuwa lugha za kigeni ni bora zaidi. Hii pia iliathiri utamaduni na maadili ya Kitanzania ambapo lugha ni nguzo muhimu.

*(d) Kutokea kwa njaa katika jamii za Kitanzania*

Sera za kikoloni zilipuuza uzalishaji wa chakula cha ndani nchini katika jamii za Kitanzania. Hali hii ilisababisha kuibuka kwa njaa kwenye maeneo mengine ya Tanzania kwani waliacha kulima mazao ya chakula na kujielekeza kwenye mazao ya biashara. Hali hii ilisababisha utapiamlo na magonjwa ya kudumu yanayohusiana na lishe duni. Upuuziaji huu ulihusishwa moja kwa moja na matakwa ya uchumi wa kibepari uliouvuruga muundo wa mfumo wa uzalishaji mali uliokuwapo katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni.

**Kazi ya kufanya 7.7**

Fanya utafiti mdogo kupitia kusoma matini mbalimbali na kuwauliza watu katika jamii unayoishi kuhusu tofauti ya huduma za afya zilizotolewa wakati wa ukoloni na sasa.

FOR ONLINE READING ONLY

**Athari za kiutamaduni na maadili**

Kulikuwa na athari mchanganyiko zilizoletwa na ukoloni katika mfumo mzima wa maadili ya jamii. Ukoloni ulileta mfumo wa utamaduni wao wa kimagharibi, ambao ndiyo ulitakiwa kufuatwa na jamii za Kitanzania na kuacha mfumo wao wa jadi. Athari hizo zilikuwa katika maeneo mbalimbali ya kiutamaduni kama dini, sanaa, michezo na mila na desturi.

Ujio wa wakoloni ulienda sambamba na uenezaji wa dini ya Ukristo ambayo ilisambazwa na wamisionari na kuleta athari mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) Ukristo ulichangia kudunisha maadili na utamaduni wa jamii za Kitanzania kwa kufundisha kuwa imani zetu ni za kizamani na za "kipagani". Mfano wa mila hizo ni haki ya kuoa mke zaidi ya mmoja, kuzuia kula baadhi ya vyakula, na uhuru wa kufanya

kazi kwa baadhi ya siku za juma. Hii ilikuwa chanzo cha kuathirika kwa utambulisho wa utaifa wetu. Watanzania walianza kukataa dini zao za asili na hii ikawa chanzo cha migogoro kati ya tamaduni mbili, yaani zile za kimagharibi na za Kitanzania.

(b) Kuibuka kwa migogoro ndani ya jamii za Kitanzania iliyosababishwa na mgongano kati ya mila na tamaduni za kiasili na ile ya Kikristo. Kanisa lililowafundisha watoto kuwaheshimu wazazi wao ili siku zao za kuishi zipate kuwa nyingi, liliwafundisha pia waumini kutoheshimu maadili na sheria za kijamii kwa madai kwamba si za Kimungu. Walishauriwa kuachana na njia za asili za maisha kama kuamudu mizimu na miungu. Kwa mantiki hiyo wamisionari na viongozi wa kigeni wakageuka kuwa walezi na wazazi wa watoto wa jamii za Kitanzania waliobatizwa badala ya kulelewa na wazazi au walezi wao kwa misingi ya mila na desturi za asili.

(c) Ukristo pia uliathiri taratibu za mazishi katika jamii ya Kitanzania. Utaratibu wa misiba ulikuwa sehemu muhimu katika kutekeleza mila na desturi za jamii ya Kitanzania. Matukio haya yaliongozwa na maadili, kanuni, mila na utamaduni za jamii iliyohusika. Ujio wa Ukristo ulileta utaratibu mpya wa kuzika uliozingatia maelekezo ya kanisa kinyume na utamaduni wa jamii za Kitanzania. Pia, kulitokea utengano wakati wa msiba baina ya familia zilizokubali Ukristo na zile zilizobaki na dini zao za asili.

(d) Kukua kwa utamaduni wa magharibi katika jamii ya Kitanzania. Wamisionari wengi walifanya kazi ya kutukuza utamaduni wa nchi zao na kuwahamasisha Waafrika kuupokea na kuuamini. Wamisionari walibadilisha mfumo mzima wa maisha wa jamii za Kitanzania. Jamii za Kitanzania zilibadilishwa katika utaratibu wa kimagharibi na kuambiwa kuwa mila na desturi za Kitanzania hazijastarabika. Hivyo, ili wastaarabike walipaswa kuuiga utaratibu wa Ulaya. Kuliibuka kasumba ya kudharau kila kitu cha Mtanzania na kuthamini vitu na mawazo kutoka Ulaya. Watanzania walianza kuvaa mavazi kama ya Wazungu. Pia, walianza kudharau mila na desturi za Kiafrika kama vyakula, sanaa, ngoma na matambiko.

**Kazi ya kufanya 7.8**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, ikiwamo mitandao, chunguza athari za dini ya Kikristo katika mfumo wa ndoa katika jamii za Kitanzania.

**Zoezi 7.4**

1. Ni kwa namna gani mfumo wa kikoloni uliathiri umoja katika jamii za Kitanzania?
2. Tofautisha mfumo wa afya wa kikoloni na ule wa jamii za Kitanzania kabla ya ujio wa ukoloni.
3. Eleza jinsi mfumo wa kiuchumi

FOR ONLINE READING ONLY

wa kikoloni ulivyochangia katika kudunisha maadili ya jamii za Kitanzania.

4. Jadili jinsi viongozi wa jadi wa jamii za Kitanzania walivyogeuka kuwa mawakala wa mfumo wa kikoloni.
5. Fafanua namna elimu ya kikoloni ilivyofanikiwa kuyajenga matabaka katika jamii za Kitanzania.

### Uzalendo na ujasiri wa Watanzania dhidi ya ukoloni

Ili kupata uelewa mzuri ni muhimu kuainisha kwanza dhana ya uzalendo na ujasiri. Hizi ni dhana zinazopaswa kueleweka vizuri katika jitihada za kufahamu historia na utamaduni wa jamii za Kitanzania. Hizi ni fadhila au karama zinazoonesha hali ya juu ya maadili, ambayo mababu na mabibi zetu walionyesha ili kulinda na kutetea ustawi wa maadili na utamaduni wa jamii zao.

#### Uzalendo

Uzalendo ni tabia ya upendo na uaminifu wa mtu au watu kwa taifa lao. Uzalendo umetokana na hisia ambazo watu wengi wamezikuza kwa miaka mingi katika harakati za kuleta maendeleo ya nchi yao na uhuru wa eneo ambalo wanaishi. Mzalendo wa kweli anafahamika au kutambulika kwa tabia zifuatazo: kuwa na upendo au mapenzi ya pekee na ya dhati kwa nchi yake, kujitambulisha yeye mwenyewe na nchi yake na si nchi za watu wengine, kupenda sana ustawi wa nchi yake, na kuwa tayari kuyatoa maisha yake kwa ajili ya kuendeleza mema katika nchi yake. Zaidi ya hayo, mzalendo anafahamika pia kwa kujali nchi yake na anajivunia utamaduni wake na historia ya maendeleo ya nchi yake. Mzalendo ni mtu mwenye uaminifu kwa nchi na viongozi wake. Hushiriki katika shughuli za kitaifa na kusaidia kudumisha amani na utulivu; hujitolea kwa ajili ya maendeleo ya nchi yake kwa kushiriki katika shughuli za kijamii, kisiasa, au kiuchumi ili kuleta mabadiliko chanya; huwajibika kama raia na kuheshimu sheria na taratibu za nchi yake na kuwa raia mwema; na huunga mkono maendeleo ya nchi yake kwa kujitolea, kusaidia katika miradi ya maendeleo au kuanzisha miradi yao wenyewe. Mzalendo anajua umuhimu wa kushirikiana na wenzake katika kuleta mabadiliko chanya. Pia, ni mtu mwenye fikra za ubunifu na uyakinifu katika mambo yote ya kulijenga taifa lake na huitangaza nchi yake na rasilimali zake vizuri ndani na nje ya nchi.

#### Uzalendo wa Watanzania enzi za ukoloni

Pamoja na ukoloni kuja na matumizi makubwa ya nguvu ngumu au mabavu, bado kuna watu wa jamii za Kitanzania walisimama kidete kuupinga uvamizi na utawala huo. Katika kipindi cha ukoloni, wananchi walionesha uzalendo wao kwa kufanya haya yafuatayo:

(a) *Kupigana vita:* Watanzania walionesha uzalendo wao pale walipopinga kuingia kwa utawala wa kikoloni kwa kupambana kivita na wavamizi wa Kijerumani na baadaye wa Kiingereza. Baadhi ya mababu na mabibi zetu waliopinga kabisa ardhi yao kuchukuliwa na kutawaliwa ni Abushiri bin Salim al-Harthi wa Pangani, Mangi Meli wa Old Moshi, Mtemi Isike wa Unyanyembe, Mtwa Mkwawa wa Iringa, Nkosi

FOR ONLINE READING ONLY

(chifu) Songea Mbano wa Wangoni, Kinjikitile Ngwale wa Umatumbi huko Kilwa-Lindi, Liti Kidanka wa Unyaturu huko Singida na Hadija Mkomanile ambaye ni mwanamke shujaa aliyepigana na Wajerumani katika vita vya Maji Maji. Mashujaa hawa walisimama kidete kupinga uvamizi na utawala wa Kijerumani nchini Tanzania mwishoni mwa karne ya 19. Mababu na mabibi zetu hawakuwa tayari kuziachia ardhi zao kuchukuliwa na Wajerumani. Hali hii ilisababisha baadhi yao kunyongwa na Wajerumani. Wananchi wao walionesha uzalendo wa hali ya juu pale walipojitoa kushiriki katika vita na ulinzi wa jamii yao. Wanajamii waliweka rehani maisha yao na kujitokeza kwa wingi kushiriki katika vita dhidi ya wavamizi au maadui wa ndani na nje ili kulinda utu na uhuru wao. Vifo vyao vilipanda mbegu ya ukombozi katika jamii ya Kitanzania.

(b) *Kudumisha utamaduni:* Uzalendo ulionekana kwa kudumisha utamaduni, mila na desturi za jamii zilizo husika. Pamoja na wakoloni kuzuia na kupinga utamaduni, mila na desturi za jamii za Kitanzania, bado wananchi walisimama imara katika kudumisha na kuendeleza utamaduni wao kama ishara ya kujenga umoja na mshikamano katika kupinga ukoloni. Hata hivyo, wakoloni walidhoofisha baadhi ya mila na desturi za jamii za Kitanzania kama vile dini, lugha, mavazi, majina, matambiko ya kuzaliwa, ndoa, kuugua, na kufariki. Maadili mengi haya ya jamii hizo yaliendelea kufuatwa kisirisiri, hali ambayo imewezesha kuwapo hadi leo. Licha ya kufuatwa kisirisiri, wananchi walibuni pia mbinu za kuyatunza maadili kwa ajili ya vizazi vya baadaye. Baadhi ya mbinu zilizotumika ni kuwapa watoto majina ya kimaadili, kuipa miaka majina ya kimaadili, kutumia masimulizi na sanaa kama nyimbo, michoro, vinyago, hadithi, vitendawili, na methali ili kuyahifadhi maadili ya jamii kwa ajili ya vizazi vijavyo.

(c) *Kupinga ubaguzi:* Katika kipindi cha ukoloni, wananchi walidhihirisha uzalendo wao kwa kupinga waziwazi sera za ubaguzi wa rangi na unyonyaji uliokuwa ukifanywa na watawala wa kikoloni dhidi yao. Kwa mfano, wananchi walijiunga na TANU kwa wingi na kushiriki katika maandamano na mikutano ya kisiasa kama harakati za kupinga ubaguzi wa kikoloni. Pia, baadhi ya wananchi walisusia bidhaa za kikoloni kama njia ya kupinga utawala wa kibaguzi na kidhalimu wa kikoloni.

**Kazi ya kufanya 7.9**

**Soma vyanzo mbalimbali vya taarifa kuhusu ujasiri na uzalendo wa Watanzania na kutafuta mchango wake katika kuyalinda maadili ya jamii za Kitanzania.**

### Ujasiri

Ujasiri ni uwezo wa kutenda jambo bila woga au hali ya kukabiliana na jambo bila

FOR ONLINE READING ONLY

hofu. Katika muktadha huu, watu hutumia neno ujasiri au ushujaa kwa maana sawa. Hata hivyo, kihistoria, dhana ya ujasiri ilihusiana zaidi na vita. Vijana wapiganaji waliofariki wakiwa vitani wakiitetea nchi yao ndiyo walikuwa wanastahili kuitwa jasiri au mashujaa. Kwa ufupi, ujasiri ni hali ya kujitolea kwa hali na mali bila woga hata kufa ili kujisaidia au kuisaidia jamii. Pia, dhana ya ujasiri haihusishi tu wale wanaokufa vitani bali pia wale wanaokufa kwa kutetea maadili. Watu kama Nduna Songea Mbano, kiongozi wa Wangoni, Mangi Meli wa Wachaga, Mtwa Mkwawa wa Wahehe, Mtemi Isike wa Wanyamwezi na Linti Kidanka wa Unyaturu huko Singida, kwa kutaja wachache, ni watu jasiri kwa sababu walipoteza maisha yao kwa kupinga ukoloni. Walikufa kwa kutetea uhuru na utu wa Watanzania. Kwa hiyo, mtu jasiri anatambulika kwa kujitoa, uhodari na kujiamini kwake katika kutenda jambo kwa hamasa na bila woga wala kukata tamaa, hata katika mazingira magumu au hatarishi. Jasiri ni mtu anayeamini katika uwezo wake katika kukabiliana na hatari na vikwazo mbalimbali vinavyojitokeza katika harakati za kufikia malengo yake. Tunaweza kusema kuwa mtu jasiri ni yule anayewawezesha watu kuchukua hatua stahiki ili kufikia malengo yao au kulinda masilahi yao, hata kama kufanya hivyo kuna changamoto au hatari kwake.

**Kazi ya kufanya 7.10**

**Fanya uchunguzi kupitia vyanzo mbalimbali kuhusu Watanzania walioonesha uzalendo katika kuipigania nchi yao, kisha bainisha sifa nyingine walizokuwa nazo.**

**Ujasiri wa Watanzania enzi za ukoloni**

Katika kipindi cha ukoloni, wananchi walionesha ujasiri wa hali ya juu katika kuupinga mfumo na maadili ya kikoloni. Hii ni kutokana na mfumo na maadili hayo kutotokana na matakwa na mazingira yao. Hivyo, waliyapinga kwa nguvu zao zote. Kulikuwa na namna nyingi, lakini hapa zitaelezwa namna tatu: nguvu na moyo wa kuukabili unyonyaji, uvumilvu wa shida, na matatizo ya kubaguliwa na kunyanyaswa.

(a) *Kukabili unyonyaji:* Mfumo wa kikoloni ulikuwa wa kinyanyasaji, kibaguzi na kinyonyaji. Watanzania walibaguliwa katika nchi yao wenyewe. Walifanya kazi bila kupata ujira unaostahili, na katika sehemu nyingine za nchi, mfumo ulikuwa unawalazimisha wananchi kulima mazao yaliyoletwa na wakoloni kwa ajili ya viwanda vyao vilivyopo Ulaya. Ingawa mfumo wa kikoloni ulikuwa umekomaa, huku ukilindwa kwa vitisho na silaha za kisasa, yaani bunduki na mizinga, wananchi hawakuogopa bali waliamua kupambana nao ili kukomesha maisha ya kunyanyaswa na kunyonywa. Miongoni mwa vitendo vya ujasiri vilivyooneshwa na Watanzania ni ushiriki wao katika vita vya kupinga kuingizwa kwa ukoloni miaka ya 1890. Kwa mfano, wananchi wa kusini mwa Tanzania waliungana katika vita ya Maji Maji katika harakati za kupinga ukoloni na unyonyaji wa utawala wa Kijerumani.

(b) *Uvumilivu:* Ujasiri wa Watanzania katika enzi za ukoloni unaonekana

FOR ONLINE READING ONLY

wazi katika maisha yao ya uvumilivu. Ikumbukwe kwamba Wajerumani waliingia nchini mwishoni mwa karne ya 19. Walipofika walianza kupora ardhi nzuri ya uzalishaji, wakawa wanawatoza watu kodi kwa nguvu na kuwafanyisha kazi wananchi katika mashamba yao kwa ujira kidogo na wakati mwingine bure kabisa. Katika sehemu nyingine, Watanzania walilazimishwa kujenga reli ya kati na Tanga kwa viboko. Watu walilazimika kufanya kazi hata pale walipoonekana wamechoka. Isitoshe, wakishirikiana na wamisionari, wakoloni walipiga marufuku mila na desturi za Kiafrika. Majina ya Kiafrika yalionekana ni ya "kishenzi", dini za jadi zilionekana pia ni za "kishenzi", baadhi ya vyakula, nguo, lugha, na sanaa; vyote, vilipigwa marufuku. Wakatilia mkazo matumizi ya utamaduni wa Kizungu. Haya yote yaliendelea kwa zaidi ya miaka sabini (70) ambayo Tanzania ilikua chini ya ukoloni mkongwe. Ingawa wananchi walisikitika kulazimishwa kuacha mila na desturi zao, walivumilia mpaka wakati wa kupigania uhuru. Uvumilivu huu wa manyanyaso na mateso kwa miaka sabini ni ishara tosha ya ujasiri wa Watanzania.

(c) *Uthubutu wa kupigania uhuru:* Hakuna wakati ambao ulihitaji ujasiri kama wakati wa harakati za kudai uhuru. Ifahamike kwamba wakoloni walitaka kutawala Tanzania kwa muda mrefu. Ingawa Umoja wa Mataifa uliwapa Waingereza jukumu la kusimamia tu na kuiandaa Tanganyika kujitawala, ukweli ni kuwa hawakuwa na mpango wa kuondoka na kutoa uhuru kwa Watanganyika. Walikuwa wamejiimarisha kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni na walikuwa hawaoni kama Watanganyika wameendelea vya kutosha kuweza kujitawala. Kwa muktadha huu, juhudi za kudai Watanganyika wajitawale zilikuwa za hatari kubwa, hasa kwa viongozi waliokuwa mstari wa mbele kudai au kupigania uhuru pamoja na wafuasi wao. Wapigania uhuru walikumbana na kadhia kadhaa. Kwa mfano, baadhi yao walifungwa magerezani bila sababu za msingi baada ya kukamatwa kwa kupanga na kuongoza maandamano dhidi ya wakoloni. Kwa mfano, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, katika harakati za kupigania uhuru, alihukumiwa kwenda gerezani mwaka 1958 kwa hila kwa kosa la uchochezi la kusingiziwa. Mwalimu alilipa faini. Hii yote inadhihirisha kwamba harakati za uhuru hazikuwa lelemama bali zilikuwa hatarishi kwa usalama wa viongozi na wafuasi wao. Kuingia katika siasa za wakati huo lilikuwa suala lililohitaji ujasiri mkubwa.

(d) *Kuunganisha makabila:* Kabla ya ukoloni, jamii za Kitanzania zilikuwa zimegawanyika katika makabila. Kila kabila lilikuwa na utaratibu wake wa maisha, yaani mila na desturi zake. Kwa maana hiyo, kila kabila lilijitegemea. Kitendo cha viongozi kama Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuyaunganisha makabila haya na kuwa jamii moja ya Watanganyika hata ikawa himaya yenye nguvu kukabili changamoto

FOR ONLINE READING ONLY

za kupigania uhuru ni kitendo cha kishujaa. Kilikuwa kitendo cha ujasiri mkubwa kwani ilikuwa ni kazi ngumu kuwaunganisha watu ambao hawakuwa na uhusiano wa damu au wa kiukoo. Kila kabila lilijiona kama linajitosheleza; na hivyo, haikuwa rahisi kujiunga na kushirikiana na makabila mengine.

### Zoezi 7.5

1. Eleza ni kwa namna gani kama taifa tunaweza kujenga jamii ya watu wenye uzalendo.
2. Fafanua njia mbalimbali zilizotumiwa na jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni katika kuujenga ujasiri.
3. Husianisha dhana ya ujasiri na dhana ya uzalendo.
4. Ni kwa nini kiongozi bora lazima awe na sifa ya ujasiri na uzalendo?
5. Je, unafikiri ni kwa namna gani uzalendo na ujasiri vinaweza kujengwa wakati wa sasa wa utandawazi?

### Mashujaa walioupinga mfumo na maadili ya kikoloni

Jamii za Kitanzania zilionesha ujasiri mkubwa katika kuupinga mfumo na maadili ya ukoloni kwa kujitolea na kujituma katika harakati za kudai haki, heshima, uhuru na utamaduni wao. Ujasiri wao ndiyo uliochangia kwa sehemu kubwa kupatikana kwa uhuru na ujenzi wa taifa lenye msingi imara wa umoja na mshikamano hapo baadaye. Mashujaa wa taifa letu ni raia na viongozi mbalimbali waliojitolea kwa moyo na ujasiri mkubwa kupigania utamaduni wao, ardhi, uhuru na haki za watu wa taifa letu dhidi ya unyonyaji wa kikoloni. Mashujaa hao walikuwa tayari kupoteza maisha yao kwa masilahi mapana ya jamii zao. Katika muktadha huu, tutaangazia uzalendo na ujasiri wa mashujaa wetu mbalimbali waliopambana kupinga mfumo na maadili ya utamaduni wa kikoloni. Baadhi ya mashujaa hao ni hawa wafuatao: Mtwa Mkwawa wa Wahehe huko Iringa, Mangi Meli wa Wachaga wa Old Moshi, Mtemi Mirambo wa Unyamwezi, Kinjekitile Ngwale wa Ngarambe huko Kilwa, na Liti Kidanka wa Unyaturu huko Singida.

#### *Mtwa Mkwawa*

Mzalendo na shujaa huyu alizaliwa mwaka 1855 na kufariki mwaka 1898. Alikuwa mtoto wa Mtwa Munyigumba wa kabila la Wahehe huko Iringa. Alipokuwa anakua alifuata nyayo za baba yake na kuwa shujaa pale alipomuokoa baba yake katika vita na Wangoni. Baada ya kufanikiwa kumwokoa katika vita, baba yake akampa jina jipya, Mukwavinyika. Maana ya jina hilo ni "Mtwaa nchi kubwa" (*conqueror of many lands*). Hicho ni kipindi cha upanuzi wa dola. Mkwawa alikuwa na ari ya kupanua dola ya Wahehe na kuchukua ardhi ya Wasangu, Wagogo na hata Wangoni.

Wajerumani walivamia eneo lake, na hapo ndipo alipoudhihirisha ujasiri na uzalendo wake. Mkwawa alionesha ujasiri wake pale alipopigana na Wajerumani na kuweza kumuua kamanda mkuu wa Wajerumani, Emil von Zelewski katika eneo la Lugalo, Iringa mwaka 1891. Mwaka 1894 Wajerumani waliongeza wanajeshi na kupelekea mapigano makali kwa miaka

FOR ONLINE READING ONLY

4 kuanzia mwaka1894 hadi mwaka1898. Hatimaye, Mtwa Mkwawa alishindwa na Wajerumani ambao walitamani kumkamata akiwa hai ili wautumie mwili wake kumdhalilisha na kuwakatisha tamaa wengine ambao walikuwa na ari ya kuendeleza mapambano. Mkwawa alilibaini hili na akaamua kujipiga risasi na kufa kuliko kukamatwa na Wajerumani mwaka 1898. Wajerumani walikata kichwa chake na kukipeleka kwao. Fuvu lake lilirejeshwa nchini Tanzania ambapo limehifadhiwa katika Makumbusho ya Mkwawa yaliyopo Kalenga iliyokuwa ngome yake kuu.

Harakati za Mkwawa zinatufundisha mengi kuhusu ujasiri na ushujaa. Kwanza, tumeona jinsi alivyowaunganisha watu na kupata nguvu. Pia, upanuzi wa dola ulikuwa unaonesha ujasiri wa kuunganisha koo ndogondogo na makabila madogo na kuunda himaya kubwa kuanzia Uhehe hadi Mpwapwa. Aidha, tunajifunza maana ya ujasiri kwani Mkwawa alionesha mfano wa kuwa tayari kufa kwa ajili ya masilahi ya nchi yake. Kukataa kutekwa na kutoa maisha yake mwenyewe ni mfano halisi wa hatua kubwa katika uzalendo. Kielelezo 7.2 kinaonesha picha ya Mtwa Mkwawa.



Kielelezo 7.2: *Mtwa Mkwawa*

*Mangi Meli wa Old Moshi*

Mangi Meli alizaliwa mwaka 1866 na kufariki mwaka 1900. Alikuwa mtoto wa Mangi Rindi Mandara aliyekuwa kiongozi katika kabila la Wachaga huko Old Moshi. Meli alirithi madaraka ya umangi baada ya baba yake, Mangi Mandara kufariki mwaka 1890. Mangi Meli alikuwa shujaa na jasiri kwani alipinga ukoloni wa Wajerumani katika eneo la Kilimanjaro. Shujaa huyu alipigana na Wajerumani mwaka 1892 na kuwashinda kutokana na ujasiri wake ambapo aliweza kumuua kamanda wa kikosi cha Wajerumani, Von Bullow katika vita. Mangi meli alikuwa mzalendo kwani aliwapinga Wajerumani na kufanya utawala wao kuwa mgumu sana. Hakuwaogopa Wajerumani, pamoja na nguvu za kivita walizokuwa nazo. Mangi Meli alidhihirisha uzalendo wake kwani aliipigania jamii yake hadi mwisho wa maisha yake. Mangi Meli alinyongwa na Wajerumani mwezi Machi mwaka 1900. Kielelezo 7.3 kinaonesha picha ya Mangi Meli wa Old Moshi



Kielelezo 7.3: *Mangi Meli wa Old Moshi*

FOR ONLINE READING ONLY

**Kazi ya kufanya 7.11**

Fanya uchunguzi kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya taarifa, kisha waelezee Watanzania wengine walioonesha ujasiri na uzalendo kwa kuwapinga wakoloni.

*Mtemi Isike*

Mtemi Isike Kiyungi wa Unyanyembe alikuwa kiongozi mahiri na jasiri wakati wa utawala wa Ujerumani. Mtemi Isike alianza kuongoza dola ya Wanyamwezi mwaka 1885. Mpaka kufika mwaka huo, Isike alikuwa amejenga jeshi imara sana na lenye nguvu lililomsaidia kukusanya kodi kutoka kwa wafanyabiashara waliopita katika eneo lake kwenda Ujiji na Katanga na eneo la ziwa Viktoria hadi Buganda. Mwaka 1886, jeshi la Isike lilimuua mfanyabiashara wa Kijerumani aliyeitwa Giesecke kwa kosa la ulaghai katika biashara na kumnyang'anya mali zake zote. Baadaye mwaka 1890, Emin Pasha aliingia Tabora na wanajeshi wapatao 1000 na kusaini makubaliano na Waarabu kuhusu biashara na kumtaka Mtemi Isike kurudisha mali za Giesecke na kulipa pembe za ndovu kama fidia.

Aprili 1892, Wajerumani walivamia ikulu ya Mtemi Isike, huko Itetemya. Askari wa Mtemi Isike waliwashinda askari wa Kijerumani. Juni 1892 Wajerumani waliivamia tena ikulu ya Itetemya lakini wakashindwa tena. Na ilipofika Agosti 1892, Mtemi Isike aliamuru misafara yote ya kibiashara katika himaya yake ifungwe kutokana na mapigano makali sana kati yake na Wajerumani. Januari 1893 Ngome yake kuu ya Itetemya iliharibiwa na majeshi ya Wajerumani. Baada ya Mtemi Isike kuona kazidiwa na majeshi ya Kijerumani aliamua kujiua yeye mwenyewe na familia yake kwa baruti kuliko kukamatwa na Wajerumani. Na huu ukawa mwisho wa utawala wake.

*Kinjekitile Ngwale*

Kinjekitile Ngwale wa Umatumbi alikuwa mtaalamu wa dawa za jadi aliyeishi katika Kijiji cha Ngarambe wilayani Kilwa, Lindi. Alikuwa Mmatumbi kwa kabila. Mnamo mwaka 1905, Kinjekitile aliibuka kuwa shujaa kwa kuongoza mapambano dhidi ya Wajerumani katika vita ya Maji Maji. Kwa ujasiri mkubwa aliwaongoza Wamatumbi kupinga utawala wa Kijerumani. Wamatumbi walikuwa wanatumikishwa katika kilimo cha pamba ambayo hawakuona faida yake. Watu walichoka na manyanyaso na mwishoni waliamua kuing'oa miche ya pamba katika mashamba ya Wajerumani yaliyokuwepo katika eneo liitwalo Nandete. Tukio hili lilikuwa chanzo cha vita ya Maji Maji ambayo ilianza mwaka 1905 na kumalizika mwaka 1907. Kinjekitile aliwaaminisha wafuasi wake kuwa risasi za mkoloni zingegeuka kuwa maji. Hii ilisababisha jamii nyingi ya watu wa mikoa ya kusini mwa Tanzania kupambana ili kupinga kutawaliwa na wageni.

Huu ulikuwa ushahidi kwamba Kinjekitile alikuwa jasiri na mzalendo kwa jinsi alivyokuwa na shauku ya kuupinga ukoloni wa Mjerumani. Ingawa Wajerumani walimkamata Kinjekitile na kumnyonga mwaka 1905, lakini huo ndio ulikuwa mwanzo wa kuenea kwa vita ya Maji Maji. Watu wa jamii za kusini walionesha uzalendo na ujasiri, na kamwe hawakukata

FOR ONLINE READING ONLY

tamaa katika mapambano dhidi ya ukoloni. Pamoja na Wajerumani kuwakamata na kuwanyonga mashujaa hao, jamii nyingi za Kitanzania ziliendelea kupambana na Wajerumani hadi vita ilipoisha mwaka 1907.

Kupitia Kinjekitile, tunajifunza ujasiri na ushujaa wake na kuona kuwa imani ina nguvu kubwa na ni kielelezo cha uzalendo. Pia, pamoja na Wajerumani kuwa na jeshi kubwa na silaha nzito lakini kwa ujasiri wao jamii za Kitanzania ziliweza kupambana nao bila woga. Sambamba na Kinjekitile, wapo wengi waliojitolea maisha yao kwa ajili ya kurejesha uhuru wao kama kipimo cha uzalendo, mathalani mwanamke shujaa Hadija Mkomanile.

*Liti Kidanka*

Shujaa huyu mwanamke wa Kinyaturu alikuwa mzaliwa wa Singida, Tanzania. Aliishi kati ya miaka ya 1860 na mwaka 1907. Wazazi wa Liti walikuwa waganga wa tiba asilia. Hivyo, Liti naye alirithi utaalamu huo kutoka kwa wazazi wake. Tunajifunza kuwa ushujaa wake ulijitokeza mwaka 1903 pale alipopinga vitendo viovu vya wakoloni wa Kijerumani waliokuwa wanapora ng'ombe, mtama na kuwakamata watu kwa ajili ya kuwatumikisha kwenye shughuli za kiuchumi. Wanyaturu waliokataa kutoa mifugo au mtama walikabiliwa na adhabu kali kama kuchapwa viboko hadharani. Liti alikuwa jasiri kwani aliyaongoza mapambano dhidi ya uonevu wa Wajerumani kwa kutumia mbinu ya nyuki, ambapo kila walipofika kwenye maeneo yao ya Singida walishambuliwa kwa kuumwa na nyuki. Ujasiri wa Litti ulimwezesha kupambana na Wajerumani kuanzia mwaka 1903. Aliendesha mapambano hayo mpaka mwaka 1907, hadi pale aliposalitiwa na watu wake wa karibu na kuwawezesha Wajerumani kumkamata na baadaye kumnyonga. Tunajifunza kuwa sayansi ya vita si lazima iwe ya silaha zinazoundwa viwandani tu, bali elimu, sayansi na teknolojia ya jadi inaweza pia kuwa ya manufaa katika nchi yetu. Hii pia inatuonesha kuwa Liti alikuwa shujaa, mzalendo na mtu aliyepinga uvamizi na dhuluma pale alipotumia mbinu za kimiujiza za utaalamu wa kuwatuma nyuki wawaume askari wa Kijerumani tu. Kielelzo 7.4 kinamwonesha mwanamke shujaa Liti kidaka wa Singida.



**Kielelezo 7.4:** *Liti Kidanka*

**Zoezi 7.6**

1. Eleza kwa nini uzalendo ulikuwa nyenzo muhimu kwa jamii za Kitanzania katika kipindi cha ukoloni.
2. **Chagua** jina la shujaa mmoja ambaye aliongoza harakati za kupinga ukoloni, kisha eleza mbinu alizozitumia katika kupigania uhuru wa nchi ya Tanzania.

FOR ONLINE READING ONLY

3. Fafanua njia zilizotumiwa na jamii za Kitanzania katika kuendeleza harakati za kujikomboa na kudhihirisha uzalendo wao dhidi ya ukoloni.
4. Ni mafunzo gani tunayapata kupitia uzalendo na ujasiri uliooneshwa na mashujaa wa Kitanzania katika harakati zao dhidi ya mfumo wa ukoloni?
5. Jadili sababu zilizowafanya vingozi wazalendo na jasiri wa Tanzania kuupinga ukoloni.

## Zoezi la marudio

1. Husianisha maendeleo ya ubepari na kutawaliwa kwa Tanzania mwishoni mwa karne ya 19.
2. "Ushirikishwaji ulitumiwa na wakoloni kama mbinu laini ya kuzitawala jamii za Kitanzania kirahisi." Unafikiri ni kwa nini jamii za Kitanzania ziliingia kwenye mtego huu?
3. Jadili athari zitokanazo na utawala wa kikoloni katika maadili na utamaduni wa jamii za Kitanzania.
4. Eleza sababu zilizozifanya jamii za Kitanzania zipigane dhidi ya uvamizi na utawala wa kikoloni.
5. Vita vya Maji Maji vimeacha somo gani kwa Watanzania wa leo?
6. Kupitia uanzishwaji wa elimu, wakoloni walipanda mbegu ya kujiangamiza wenyewe. Jadili ukweli wa hoja hii.
7. "Uanzishwaji wa Ukristo na huduma ya afya wakati wa ukoloni ulikuwa mkakati wa kuitawala Tanzania." Jadili.
8. Jadili uhusiano wa maadili ya sasa na ukoloni hapa nchini Tanzania.
9. Jadili sababu zilizowafanya Watanzania wapambane na uvamizi wa wakoloni mwishoni mwa karne ya 19.
10. "Mmomonyoko wa maadili unaoshamiri katika jamii ya Watanzania wa sasa ni matokeo ya sera ya maendeleo ya kikoloni" Jadili ukweli wa hoja hii.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Nane
# Mchango wa ukoloni katika mfumo wa maadili ya Kitanzania

## Utangulizi

*Ukoloni ulikuwa na athari mbalimbali katika mifumo ya maadili ya jamii za Kitanzania. Katika sura hii, utajifunza maadili na mifumo ya usimamizi iliyojengwa wakati wa ukoloni. Pia, utajifunza uhusiano kati ya maadili yaliyojengwa kabla ya ukoloni na yale ya wakati wa ukoloni na athari za ukoloni katika maadili ya Kitanzania. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuyathamini na kuyalinda maadili ya jamii yako.*

**Fikiri**

**Athari za ukoloni katika mabadiliko ya kimaadili katika jamii za Kitanzania.**

## Maadili na mfumo wa usimamizi kabla na wakati wa ukoloni

**Wakoloni walileta mifumo yao ya maadili na usimamizi wake katika maeneo waliyoyatawala. Mifumo hii ilitofautiana na mifumo ya maadili na usimamizi wake katika jamii za Kitanzania iliyokuwapo kabla ya ukoloni. Hivyo, kwa sehemu kubwa mifumo hii iliujenga msingi wa maadili na usimamizi uliousaidia ukoloni kutimiza matakwa ya ubepari ili kupata faida nono. Mifumo hiyo iliathiri sana jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni, na ambayo bado inaendelea kuathiri mfumo na usimamizi wa maadili katika jamii nyingi za leo nchini Tanzania.**

**Mfumo wa usimamizi wa maadili ni muundo wa kanuni na taratibu zinazowekwa na kutekelezwa na jamii au taasisi fulani kwa lengo la kudumisha maadili na tabia zinazokubalika katika jamii au taasisi hiyo. Mfumo huu huwasaidia watu kufuata sheria, kanuni, miiko, taratibu, na miongozo katika maisha yao ya kila siku na, hatimaye, kukuza tabia njema na kuzuia ukiukaji wa maadili na haki katika jamii. Kabla ya ukoloni, jamii za Kitanzania zilikuwa na mfumo wake imara wa usimamizi wa maadili uliotokana na mila na desturi za kila kabila au jamii husika. Usimamizi wa maadili ulihusisha utungaji wa kanuni na taratibu za maadili zilizolenga kudumisha amani, umoja, heshima na mshikamano miongoni mwa wanajamii. Katika mfumo**

FOR ONLINE READING ONLY

huo, familia, ukoo, kabila, imani za dini na elimu ya jadi vilitumika kama taasisi muhimu za kuyajenga na kuyasimamia maadili katika jamii.

### Maadili na mfumo wa usimamizi wake kabla ya ukoloni

Kabla ya ukoloni, familia ilikuwa kitovu cha maadili katika jamii. Pia, ilikuwa na jukumu kubwa la kulea watoto na kuwafundisha kanuni, taratibu, maadili na tamaduni za jamii yao. Miongoni mwa maadili yaliyofundishwa katika ngazi ya familia ni pamoja na kuwaheshimu wazazi, na upendo wa kusaidiana na kushirikiana katika nyakati za shida na raha. Pia, ndani ya familia, watoto walifundishwa kuwaheshimu na kuwasaidia wazee ambao walichukuliwa kama nguzo muhimu katika kutoa ushauri na mwongozo kwa vijana.

Ukoo ulikuwa na jukumu la kuzisimamia sheria na taratibu za jadi za jamii iliyohusika. Aidha, koo zilikuwa na viongozi ambao walisimamia taratibu za maisha za kila siku za ukoo. Kwa mfano, viongozi hao walikuwa na jukumu la kutatua migogoro iliyotokea katika jamii kwa njia ya majadiliano kupitia vikao vya kijadi ambavyo vilikuwa na mamlaka ya kutatua migogoro. Katika kutatua migogoro na kudumisha nidhamu, koo zilikuwa na mifumo ya adhabu mbalimbali kwa wale waliokiuka maadili. Kwa mfano, katika jamii nyingi za Kitanzania, watu waliotukana matusi hadharani, walioiba na hata kulewa kupita kiasi, waliadhibiwa kwa kuchapwa viboko kadhaa mbele ya hadhara ya ukoo kama onyo kwa vitendo hivyo visivyo vya kimaadili. Vilevile, koo katika jamii nyingi zilikuwa na mamlaka ya kuzisimamia shughuli mbalimbali katika jamii. Baadhi ya shughuli hizo ni pamoja na kuziandaa na kuzisimamia ibada za jadi, sherehe, ndoa na urithi na shughuli nyingine mbalimbali za kiutamaduni.

Kwa upande mwingine, mifumo ya usimamizi wa maadili kabla ya ukoloni ilitegemea kabila moja hadi lingine. Kabila lilikuwa na taratibu, mila na desturi ambazo zililenga kuyadumisha maadili na nidhamu katika jamii. Pia, kabila lilikuwa msingi wa utambulisho wa mtu na nguzo ya umoja na mshikamano miongoni mwa wanajamii. Kupitia shughuli za kijamii kama vile sherehe za kimila na matamasha, kabila liliweza kuujenga upendo na uhusiano mzuri miongoni mwa wanajamii. Viongozi wa kabila walikuwa na jukumu la kutatua mizozo na kuyasimamia maadili ya jamii. Hadi sasa makabila yanaweza kutofautishwa kutokana na misingi ya maadili inayosimamiwa na kabila lililohusika. Pia, kila kabila lilikuwa na mfumo wake wa kutoa mafunzo ya maadili kwa vijana na watoto kupitia mila na desturi, kama vile jando na unyago. Vijana walifundishwa heshima, ukarimu, uaminifu, huruma, ushirikiano na utii kulingana na taratibu za makabila yao. Pia, wanajamii walifundishwa athari za usaliti, visasi, dharau, ukatili na ulaghai.

Dini za jadi zilikuwa sehemu muhimu ya maisha ya jamii nyingi za Kitanzania hata kabla ya ukoloni. Mara nyingi, maadili ya kidini yanaonekana katika maisha ya kila

FOR ONLINE READING ONLY

siku kupitia ibada, mila, desturi na miiko. Jamii zilikuwa na sehemu muhimu za ibada na matambiko. Ibada hizo zilifanyika kama sadaka ili kuombea jamii, kwa mfano, wakati wa ukame walifanya ibada kuomba mvua au pale jamii inapopatwa na majanga mbalimbali kama uvamizi wa wadudu waharibifu wa mazao, mafuriko au magonjwa. Viongozi wa dini za jadi walikuwa na jukumu la kuyafundisha maadili na kuusimamia utekelezaji wa taratibu za kidini.

Pia, elimu ya jadi ilikuwa njia ya kujifunza maadili na tamaduni za jamii. Kupitia hadithi, methali, na mafundisho ya wazee, vijana walifundishwa kujituma katika kazi, kuwaheshimu wengine, kuwathamini wageni na kudumisha amani na umoja katika jamii. Elimu hii vilevile ilihusu jinsi ya kutunza mazingira, ufugaji, uwindaji, kilimo na mila na desturi za jamii husika. Katika jamii nyingi za Kitanzania, jando na unyago pia vilitumika kama nyenzo muhimu ya kielimu katika kuwaelimisha vijana wa kiume na wa kike mtawalia, waliofika rika ya ujana. Lengo lilikuwa kuwaanda vijana hao kuwa wanajamii bora kimaadili na kijamii. Vijana walifundishwa kuijua miiko ya koo zao, kuheshimiana na kuepuka tabia zisizofaa.

Mfumo huu wa usimamizi wa maadili ulikuwa na nguvu na uliweza kuidumisha amani na utulivu katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. Hata baada ya ukoloni, baadhi ya mila na desturi hizi zimeendelea kuwepo na kuchangia katika kuyadumisha maadili na utamaduni wa Kitanzania.

**Maadili yaliyojengwa wakati wa ukoloni**

Ujenzi wa maadili umepitia vipindi tofauti tofauti. Kila kipindi kilijenga maadili yake yaliyoendana na wakati na jamii husika. Kwa hiyo, jamii za Kitanzania zimeshuhudia baadhi ya maadili yakibadilika, hasa wakati wa kipindi cha ukoloni. Pamoja na mabadiliko hayo, bado maadili ya wakati wa kabla ya ukoloni yaliendelea kuwapo na watu waliyaishi kwa sababu mbalimbali. Ukoloni ulileta utamaduni wa Ulaya magharibi ukiwa na misingi yake ya maadili. Ukoloni ulilazimisha jamii za Kitanzania ziendane na matakwa ya ubepari.

Utawala wa kikoloni ulileta mabadiliko makubwa katika mifumo ya usimamizi wa maadili. Mabadiliko haya yalijikita katika kuhakikisha kuwa Watanzania wanaendana na maadili ya kimagharibi ili waweze kuwa wazalishaji wa malighafi wazuri kwa ajili ya viwanda vya Ulaya Magharibi. Pia, yalilenga kuwafanya kuwa soko la bidhaa za viwanda vya Ulaya, wafanyakazi wanaolipwa kidogo na maeneo yao yanakuwa ya uwekezaji wa Wazungu yenye kuleta faida kubwa.

Wakoloni wa Kijerumani na Kiingereza walikuja na mifumo yao ya maadili. Kwa maana hii hawakuithamini mifumo ya maadili iliyoheshimiwa na kufuatwa kabla ya ujio wao. Wakoloni hawa walidai kuwa mifumo hiyo haikuendana na utamaduni na matakwa yao ya kibepari. Waliidharau mifumo ya maadili ya jadi kwani waliiona kuwa ni ya kizamani, haijaendelea na si ya kistaarabu. Kwa hiyo, walipofika tu kitu cha kwanza ilikuwa kuibadilisha mifumo hii na

FOR ONLINE READING ONLY

kuleta dhana zao za kimaadili, kiutamaduni na kiutawala. Maadili yaliyojengwa wakati wa ukoloni yalilenga kudumisha utawala wa kikoloni na kudhibiti jamii za Kitanzania. Jamii zilifundishwa na nyakati nyingine kulazimishwa kufuata na kutii mila na desturi za kikoloni zilizokuwa kinyume na zile za jamii zao. Hii ililenga kudhoofisha utambulisho wa kitamaduni wa jamii za Kitanzania, ikiwa ni pamoja na umoja na mshikamano wao.

Aidha, jamii ilifundishwa kuheshimu na kutii mamlaka za kikoloni kwa lengo la kuzuia upinzani na kudumisha utawala wa kikoloni. Vilevile, jamii ilifundishwa na kulazimishwa kufanya kazi kwa bidii ili kuutumikia uchumi wa kikoloni. Wakoloni walijenga taasisi zao za kuyasimamia maadili ya kikoloni kama mahakama, polisi, shule na mabaraza ya nidhamu kwa Watanzania. Kwa ujumla, maadili ya kikoloni yalijenga mfumo wa utawala uliodhibiti na kuendeleza maslahi ya wakoloni na kupuuza maadili na utamaduni wa jamii za Kitanzania. Hii ilisababisha migongano na kuvuruga mifumo ya asili ya maadili na utambulisho katika jamii nyingi za Kitanzania.

**Kazi ya kufanya 8.1**

Fanya utafiti mdogo kubaini taasisi na aina za adhabu walizopewa wanajamii waliotenda vitendo visivyo vya kimaadili katika jamii zao kabla ya ukoloni.

Wakoloni walikuja Tanzania wakiwa na malengo yao ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Walibuni njia mbalimbali za kuwasaidia kuyajenga maadili ya kikoloni yaliyokuwa yanafuata utamaduni wa kimagharibi. Kwa hiyo, njia mbalimbali zilitumika kujenga maadili ya kikoloni katika jamii za Kitanzania. Miongoni mwa njia hizo ni pamoja na:

*Dini:* Dini ya Kikristo iliingia Tanzania miaka ya 1840 ikianza na shirika la *Church Missionary Society.* Katika miaka ya 1860 hadi 1890 mashirika mengi ya dini ya Kikristo kama *Universities Mission to Central Africa, Holy Ghost Fathers, London Missionaries Society* na *Missionaries of Africa* yaliongezeka. Mashirika haya yalifungua misheni zao sehemu mbalimbali za nchi. Dini hii iligawanyika katika madhehebu mbalimbali kama vile dhehebu la Wakatoliki, Walutheri, Waanglikana na madhehebu mengine. Wakoloni waliotawala Tanzania walitumia dini ya Kikristo kujenga maadili ya kikoloni. Kama ilivyokuwa wakati wa kutafuta taarifa kuhusu jamii za Kitanzania na utajiri wao kabla ya ukoloni, hata wakati wa ukoloni dini ilitumika kufundisha maadili na utamaduni wa kimagharibi. Dini ya Ukristo ilileta imani hii na kuihubiri kama dini pekee ya Mungu. Mafundisho haya yalilenga kuzidhoofisha, kuzidunisha na kuzikana dini za jadi. Mafundisho yake yalilenga kueneza utamaduni wa Ulaya Magharibi kama ndoa ya mke mmoja; maarifa yanatoka kwenye Biblia tu; Mungu mmoja tu na mambo kama hayo. Vilevile, walianzisha shule za dini na za kawaida ambazo zilisisitiza katika kufundisha maadili na utamaduni wa magharibi. Kwa ujumla, dini ilitumika kufundisha maadili na mwenendo wa utii kwa mamlaka kulingana na matakwa ya wakoloni.

FOR ONLINE READING ONLY

*Elimu:* Wakoloni walileta mfumo wa elimu ya kikoloni ambao uliundwa kwa kufuata falsafa na mawazo ya Ulaya Magharibi na kutolewa shuleni. Elimu hii ilikazia katika kujifunza maadili na utamaduni wa Ulaya Magharibi. Wakoloni walisisitiza sana ustaarabu wa Ulaya kama historia ya ujenzi wa himaya za Kijerumani au Kiingereza, mapinduzi ya viwanda, maadili ya Ulaya yalivyo bora kuliko ya Kitanzania na mengineyo. Wakoloni waliwafundisha wanafunzi historia ya Ulaya wakiwa na lengo la kuwapandikizia maadili na utamaduni wa Ulaya Magharibi. Wanafunzi walifundishwa kwa kutumia muhtasari mmoja nchi yote bila kujali utofauti wao wa kimazingira au kiutamaduni. Elimu ya kikoloni ililenga kufundisha maadili ya kikoloni kwa vijana wa Kitanzania. Elimu hii ilikuwa ya nadharia zaidi kuliko vitendo.

Kwa upande mwingine, shule za kimisionari zilifundisha elimu ya dini na masomo kama usafi wa mtu binafsi na kutunza nyumba. Elimu hiyo ilibadilisha fikra, mtazamo na mwenendo wa vijana wengi walioipata na kuona utamaduni wa kikoloni ni bora kuliko utamaduni wao wa Kitanzania. Hii ilichangia kwa kiasi kikubwa kuuharibu umoja na mshikamano miongoni mwa jamii za Kitanzania na kumomonyoka kwa maadili ya jamii za Kitanzania kwa kiasi kikubwa.

*Utawala wa kikoloni:* Ukoloni ulikuja na aina mpya ya utawala uliotofautiana kimuundo na kifalsafa na ule wa jamii nyingi za Kitanzania. Kwanza, walianzisha dola ya kikoloni ambayo ilisimamia mambo yote katika nchi. Jamii zote za Tanzania ziligeuzwa kuwa jamii moja kiutawala. Dola ya kikoloni ilitumia utawala wake kuyadhibiti na kuyasimamia maadili ya koloni lote. Watawala wa kikoloni walitunga sheria na kanuni zilizopiga marufuku tamaduni na maadili ya jamii za Kitanzania ili kudumisha maadili yao ya kikoloni. Njia hizi zilichangia kwa kiasi kikubwa katika kubadilisha mtazamo na mwenendo wa watu na kujenga maadili ya kikoloni katika jamii hizo. Dola hii ya kikoloni ilijikita katika kuhakikisha matakwa na mahitaji ya mapinduzi ya viwanda na ubepari huko Ulaya Magharibi yanatekelezwa hapa nchini. Kwa hiyo, dola hii haikuwa na wajibu wowote wa kuyadumisha na kuyastawisha maadili bora kwa jamii za Kitanzania.

Kabla ya ukoloni na elimu ya kikoloni, familia ilikuwa taasisi ya msingi katika kuyalinda na kuyaenzi maadili katika jamii. Wakoloni walijaribu kuleta mabadiliko katika muundo wa familia kwa kukuza maadili mapya ya kikoloni kama vile utii kwa mamlaka ya kikoloni na kufuata mfumo wa familia unaofanana na ule wa Ulaya Magharibi. Mfumo huo ulipunguza mamlaka ya malezi ya watoto ambayo yalikuwa jukumu la jamii iliyohusika katika kurithisha maadili kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Hii ilisababisha mabadiliko katika namna ya uendeshaji wa familia kutokana na kuingia kwa maadili mapya katika jamii za Kitanzania.

Wakoloni waliingilia masuala ya kikabila kwa kusababisha migawanyiko kwa kuwatumia baadhi ya viongozi wa makabila kama vibaraka wao ili kudumisha utawala wao. Hii ilikuwa na athari kubwa kwa maadili ya jamii kwani mara nyingi

FOR ONLINE READING ONLY

walijaribu kuudhoofisha utambulisho wa kikabila ili kurahisisha utawala wao. Kwa kufanya hivyo, maadili ya jamii za Kitanzania yaliyojengwa katika mila na desturi za makabila yaliathirika.

Kama ilivyoelezwa hapo awali, wakoloni walileta dini ya Kikristo na kuitumia kueneza imani ambayo ilikuwa kama taasisi ya kudhibiti na kuleta mabadiliko ya kiutamaduni hasa katika suala la imani katika jamii za Kitanzania. Kwa kufanya hivyo, walifundisha imani na maadili ambayo kwa kiasi kikubwa yalikinzana na utamaduni na maadili ya dini za jadi zilizokuwepo. Kwa mfano, dhana za utawala wa kikoloni ziliendana na mafundisho ya dini ambayo yalikuwa na athari kwa maadili na mtazamo wa jamii. Jamii za Kitanzania ziliaminishwa kuwa mfumo wa dini za jadi haukufaa, na walipaswa kukubaliana na maadili yatokanayo na mafundisho ya imani ya dini zilizoletwa na wakoloni, ambao walioona imani au dini za jadi kuwa hazifai. Wanafunzi walitakiwa kuutukuza ustaarabu wa Ulaya Magharibi huku wakidunisha ustaarabu na maadili ya Kitanzania.

Kwa upande mwingine, elimu ya jadi ilikuwa sehemu muhimu katika ujenzi wa maadili katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. Wakoloni walipokuja waliingilia kati na kuanzisha mfumo wa elimu ambao ulilenga kubadilisha maadili na mtazamo wa watu kuelekea utawala wa kikoloni. Hii ilisababisha kubadilika kwa maadili ya kijadi ili kuendana na matakwa ya dini zilizoletwa na wakoloni na matakwa ya ukoloni. Kwa mfano, elimu ya jadi ilizingatia kuwaandaa vijana ili waweze kukabiliana na mazingira wanamoishi lakini elimu ya kikoloni ililenga kuwaandaa watu wa kada za chini watakaoweza kuwatumikia wakoloni katika utawala wao wa kinyonyaji. Elimu hiyo ililenga kuwabagua watu na kuwafanya wadharau tamaduni zao na kuzikumbatia tamaduni za kikoloni. Kwa hiyo, ukoloni ulikuwa na athari hasi katika mifumo ya maadili ya jamii za Kitanzania kupitia njia mbalimbali, na matokeo yake yanaonekana katika jamii hadi leo.

FOR ONLINE READING ONLY

### Zoezi 8.1

1. Ni kwa jinsi gani koo zilizokuwapo kabla ya ukoloni katika jamii za Kitanzania ziliweza kusimamia maadili ya jamii za Kitanzania?
2. Eleza kwa mifano mabadiliko ya maadili wakati wa ukoloni katika nyanja za kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni.
3. Fafanua ni kwa namna gani maadili ya Kitanzania baada ya uhuru yameendelea kuathiriwa na historia ya ukoloni?
4. Je, ni mambo gani ya kimaadili ya dini za jadi yameendelea kuwa muhimu katika kudumisha maadili ya jamii ya sasa ya Kitanzania?
5. Kama kijana mzalendo wa Kitanzania, unafikiri nini kifanyike ili kulinda maadili ya Kitanzania dhidi ya madhara ya utandawazi?

### Uhusiano wa maadili kabla na wakati ya ukoloni

Maadili ya jamii za Kitanzania yamepitia mabadiliko ambayo yaliathiri maisha ya kila siku ya Watanzania. Kabla ya ukoloni, utamaduni na maadili ya jamii za Kitanzania

vilikuwa vinaundwa na mila, desturi, na imani za jadi. Hizi zilijumuisha mifumo ya maadili ambayo iliongozwa na kanuni za kimaadili, heshima kwa wazee, utunzaji wa mazingira, na ushirikiano katika jamii.

Kwa mfano, katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni, kulikuwa na mfumo wa maadili unaoheshimu na kuthamini uongozi wa kijamii. Viongozi waliheshimiwa na kupewa mamlaka kwa sababu ya hekima zao na uwezo wa kusuluhisha mizozo na migogoro. Maadili kama vile ushirikiano, utunzaji wa familia, na kuheshimu wazazi yalisisitizwa sana. Mifano mingine ni pamoja na uhifadhi wa mazingira kama vile misitu na vyanzo vya maji, vitu ambavyo vilikuwa sehemu muhimu ili kuziwezesha jamii kuendeleza maisha yao ya kila siku.

Mazingira ya kijamii na kiutamaduni yalibadilika kwa kiasi kikubwa wakati wa ukoloni. Ukoloni ulileta mabadiliko makubwa katika muundo wa kijamii na kiuchumi. Pia, mtazamo wa watu kuhusu maadili na utamaduni wao wenyewe vilibadilishwa. Ukoloni na dini za kigeni vilileta mfumo mpya wa elimu, mavazi, chakula na muziki.

Kwa mfano, dini ya Kikristo iliyoletwa na wakoloni iliathiri sana maadili na imani za watu. Hata hivyo, pamoja na kusisitiza watu washike dini ya Kikristo, mara nyingi kulitokea watu ambao walirithi dini za kigeni lakini waliendelea kushika tamaduni zao na dini za jadi kwa pamoja. Hii ilisababisha mseto wa maadili na imani ambao unaweza kuuona nchini Tanzania hadi sasa. Kwa upande mwingine, mfumo wa maadili ya kikoloni ulileta utaratibu wa watu binafsi kumiliki mali badala ya jamii. Mali ilitoka katika kumilikiwa na jamii nzima hadi kuwa mali ya watu wachache. Ingawa kulikuwa na jamii chache za Kitanzania ambazo watu wachache walimiliki mali kama ardhi, mifugo na mali nyingine, bado katika jamii nyingi za Kitanzania mali hizo ziliendelea kumilikiwa na jamii, hasa ukoo. Viongozi walimiliki tu kwa niaba na kwa faida ya ukoo au jamii nzima.

Vilevile, kuhusiana na suala la dini, jamii nzima iliamini katika imani inayofanana ambayo ilikuwa inaendana moja kwa moja na utamaduni wa jamii husika. Kwa minajili hiyo, dini ilikuwa sehemu ya maisha ya watu na ilikuwa vigumu sana kuitofautisha na maisha ya jamii. Wakati wa ukoloni, dini ilianza kuonekana ni imani ya mtu mmoja mmoja na ni suala la hiari. Dini hii ilifanana na utamaduni na matakwa ya wakoloni kinyume na maadili na urithi wa jamii za Kitanzania.

Uhusiano wa maadili kabla na wakati wa ukoloni pia unaweza kuzungumziwa au kujadiliwa katika namna mbalimbali. Katika nyakati zote mbili, maadili yamekuwa zao la utamaduni unaotawala jamii. Kabla ya ukoloni, utamaduni wa jamii iliyohusika ndiyo ulioyazaa maadili ya jamii hiyo. Misingi kama familia, ukoo, kabila, elimu na dini viliathiri maadili moja kwa moja. Umoja, upendo, heshima, busara, kupenda kazi, ukarimu na uwajibikaji yalikuwa mazao ya misingi hiyo. Hili pia halikuwa jambo jipya wakati wa ukoloni ambapo dola ya kikoloni, elimu, dini na vitu kama hivyo vilisimamia kuzalisha maadili ya Ulaya Magharibi ili kufanikisha matakwa ya ukoloni.

FOR ONLINE READING ONLY

Kwa hiyo, kitaasisi, maadili ya kabla ya ukoloni na yale ya wakati wa ukoloni yamepitia katika aina moja ya mfumo. Tofauti ni kwamba, maadili wakati wa ukoloni yalihusu koloni (Tanganyika au Zanzibar) kama jamii moja. Makabila yote yalitakiwa kuwa na aina sawa za maadili zinazotakiwa na dola ya kikoloni. Maadili ya kabla ya ukoloni yalihusu zaidi jamii moja, yaani kabila au ukoo, ingawa kuna baadhi ya maadili yaliyofanana kutoka jamii moja na jamii nyingine.

Kitu cha muhimu kukijua hapa ni kwamba, pamoja na ukatili wa ukoloni na nia ya kudhoofisha na kuingiza utamaduni na maadili yake kwa jamii ya Kitanzania, bado kuna maadili na tamaduni za jamii zilizokuwapo kabla ya ukoloni ziliendelea kuwapo hata baada ya ukoloni. Taasisi za msingi katika maadili kama familia, ukoo na kabila zimeishi na kuweza kuendelea kuwepo hata baada ya ukoloni. Mila na desturi na baadhi ya taratibu na kanuni za jamii nyingi za Kitanzania nazo pia zimeendelea kuwapo. Umoja, upendo, ukarimu, mshikamano, na uzalendo ni baadhi ya mambo ambayo yameishi kwa jamii za Kitanzania hata baada ya ukoloni.

Pamoja na hayo, hii haina maana kuwa ukoloni haukuwa na athari kwa jamii za Kitanzania kimaadili. Kwa kuleta mabadiliko katika mifumo ya kiuchumi, kiutamaduni, kisiasa na kijamii, ukoloni umeathiri maadili kwa kuleta mambo mapya ambayo hayakuwapo kabla ya ukoloni. Kwa mfano elimu, utawala na mambo mengine ya kikoloni kama haya yameathiri maadili kwa kuleta utamaduni mpya wa Ulaya Magharibi uliochangia katika kuleta mmomonyoko wa maadili nchini, kupunguza ushirikiano kwa kuleta matabaka, na kuongeza na kukuza unyonyaji na ukandamizaji (kupunguza upendo). Kwa kuweka msisitizo, maadili yaliyojengwa kabla ya ukoloni yalikuwa maadili yaliyotokana na watu na jamii iliyohusika; kwa hiyo, yalikuwa sehemu ya utamaduni wa jamii husika. Kwa maana hiyo, wanajamii waliyaishi maadili yao yaliyokuwa sehemu ya maisha yao.

Hivyo, maadili hayo yalikuwa na faida katika jamii iliyohusika. Maadili yaliyojengwa wakati wa ukoloni yalijengwa kutokana na matakwa na falsafa ya ukoloni. Kwa hiyo, yalikuwa maadili yaliyotoka nje na kuletwa kwa jamii ambayo haikuhusika kuyatengeneza. Maadili ya Ulaya Magharibi hayakuwa sehemu ya utamaduni wa jamii za Kitanzania. Maadili haya hayakuwa na lengo la kulinda umoja na ushirikiano wa jamii za Kitanzania bali yalijikita katika kuhakiksha kuna ukandamizaji, unyonyaji, matabaka na uharibifu wa utamaduni wa jamii za Kitanzania kwa faida ya ukoloni na ubepari. Hii ilipingana na maadili ya usawa na haki, utu, upendo, uzalendo, umoja, usawa na mshikamano katika jamii. Ukoloni ulikandamiza maadili ya jamii za Kitanzania.

**Kazi ya kufanya 8.2**

Fanya uchunguzi kutoka katika vyanzo mbalimbali, kisha eleza namna mifumo ya kimaadili katika familia, ukoo na kabila ilivyoathirika wakati wa ukoloni.

FOR ONLINE READING ONLY

### Changamoto katika kusimamia maadili wakati wa ukoloni

Wakati wa ukoloni, jamii za Kitanzania zilipitia changamoto kubwa katika kuyasimamia maadili kutokana na athari za utawala wa kigeni. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:

*(a) Kuanzishwa kwa miundo mipya ya kusimamia maadili*

Ukoloni uliletea mabadiliko makubwa katika miundo ya jamii za Kitanzania iliyotokana na dola ya kikoloni. Miundo imara ya kijamii iliyokuwapo kabla ya ukoloni ilivurugwa na kusababisha changamoto katika kuyasimamia maadili ya jamii. Aidha, sera za ukoloni zilizokuwa na athari ya kuvuruga utamaduni wa asili zilidhoofisha mamlaka ya wazazi au familia katika malezi ya watoto kulingana na mila na desturi za Kitanzania. Hii ilisababisha changamoto katika usimamizi wa maadili kwa kupungua kwa nguvu ya familia na ukoo. Hali hii ilifanya baadhi ya jamii kuwa katika hatari ya kupoteza utambulisho wake kimaadili. Shule zilizofundisha elimu ya kikoloni ziliathiri maadili ambayo yalijengwa kwenye misingi ya heshima kwa wazazi, ndugu wa familia, wanaukoo na kabila. Maadili ya kizungu yalipewa kipaumbele kuliko kuendeleza utamaduni wa Kitanzania.

*(b) Kuingiliwa na utamaduni wa kigeni*

Utamaduni wa Kitanzania ulipambana na changamoto ya utamaduni wa kigeni ulioletwa na wakoloni kuvuruga maadili ya jamii za Kitanzania. Baadhi ya tamaduni za kigeni zilipingana na maadili ya asili au jadi ya jamii za Kitanzania. Mfano mzuri ni suala la heshima kati ya mdogo na mkubwa. Wakoloni walijiona wao ndio watu pekee wanaostahili heshima na waliudharau utamaduni wa Kitanzania. Mkoloni alijiona anastahili kupewa heshima na watu wote hata kama anayekutana naye anamzidi umri. Hii ilisababisha kuwapo kwa matabaka ya waliostahili kuheshimiwa, ambao walikuwa ni wazungu, na wanaostahili kutoa heshima hiyo, ambao walikuwa ni Watanzania.

*(c) Kupotea kwa nguvu ya mamlaka ya kijamii*

Baadhi ya mamlaka za jamii za Kitanzania zilipotea au kudhoofika kutokana na ushawishi wa utamaduni wa kigeni. Hii ilisababisha changamoto katika kuyasimamia maadili ya jamii. Kwa mfano, katika kipindi cha ukoloni, iliwekwa mifumo ya kudhibiti mamlaka za kijamii zilizowekwa na wanajamii wenyewe. Kudhibitiwa kwa mamlaka ya ukoo au uchifu kulivuruga miundo yake na kupunguza uwezo wake wa kuyasimamia maadili. Kwa mfano, katika baadhi ya maeneo, wakoloni walipendelea kuanzisha mfumo wa utawala wa kisheria ambao ulileta changamoto katika nafasi ya mamlaka ya viongozi wa kiukoo au kichifu katika kuyalinda na kuyaenzi maadili ya jamii. Wakoloni waliweka utawala wa kisheria wa kikoloni ambao haukuzingatia nafasi ya viongozi wa ukoo au kabila katika ujenzi wa maadili na ustawi wa jamii.

Kwa upande mwingine, usimamizi wa maadili ulikabiliwa na kikwazo kutoka katika sera za ukoloni zilizolenga kuyatenganisha makabila na kuidhoofisha miundo yao ya kijamii na kisiasa na kusababisha kuvurugika kwa mfumo wa maadili ya jamii zetu. Aidha, sera za ukoloni za kuzidhibiti rasilimali za asili na

FOR ONLINE READING ONLY

ardhi zilisababisha migogoro ya kikabila ambayo ilidhoofisha umoja wa kabila na kudhoofisha pia mfumo wao wa kuyalinda na kuyaenzi maadili mema kwa jamii.

**Kazi ya kufanya 8.3**

Fanya utafiti mdogo kubaini njia zilizotumiwa na jamii za Kitanzania katika kudumisha maadili wakati wa ukoloni, ambazo zinaweza kutumika katika kukabiliana na tatizo la mmomonyoko wa maadili katika jamii za Kitanzania za sasa.

### *(d) Kudharauliwa kwa imani na dini za jadi*

Kabla ya ukoloni, jamii za Kitanzania zilikuwa na imani ya Mungu, miungu na mizimu. Kulikuwa na mafundisho yaliyopatikana katika dini hizi. Mafunzo ya dini yaliheshimiwa katika kuyadumisha maadili ya jamii kabla ya ukoloni. Kuyalinda, kuyaenzi na kuyaendeleza maadili ya jamii kupitia dini za jadi kulikabiliwa na changamoto ya kuingia kwa dini za kigeni na ukoloni. Wakati wa ukoloni dini ya Kikristo ilitumiwa kama chombo cha kueneza utawala wa kikoloni. Kwa mfano, walitumia misheni na madhehebu ya dini ili kueneza imani ya Kikristo ambayo ilipingana na imani za kijadi ambazo zilikuwa muhimili muhimu sana katika kukuza na kuendeleza maadili. Hii iliathiri ukuaji wa maadili katika kipindi hiki cha ukoloni.

### *(e) Kutoheshimu elimu ya jadi*

Elimu ya jadi iliwawezesha wanajamii kuyafundisha maadili na utamaduni wa jamii. Zaidi ya hayo, elimu ya jadi iliziwezesha jamii kukabiliana na mazingira yao na kuleta ustawi wa jamii hizo. Elimu ya jadi katika kipindi cha ukoloni ilikutana na changamoto mbalimbali ikiwemo kupuuzwa au kupingwa na wakoloni ambao waliingiza elimu ya kikoloni iliyozingatia maslahi ya wakoloni. Hii ilisababisha kupotea kwa baadhi ya maarifa na mafundisho ya elimu ya jadi, ambayo yalikuwa muhimu sana katika kuyaenzi na kuyadumisha maadili ya jamii.

Kwa ujumla, mfumo wa usimamizi wa maadili ya jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni ulipitia changamoto nyingi sana zilizotokana na athari za utawala wa kikoloni ulioleta mifumo mipya ya kuyasimamia na kuyaendeleza maadili na utamaduni wa jamii. Mifumo hii mipya iliidhoofisha au kubadilisha kabisa mifumo ya jadi iliyokuwa ikiyasimamia, kuyaenzi na kuyadumisha maadili kabla ya ujio wa ukoloni. Athari zake zilikuwa dhahiri kwenye maadili, ingawa kwa sababu ya uimara wake bado ziliendelea kudumu, lakini si kwa kiwango na haiba ileile ya wakati wa kabla ya ukoloni.

**Zoezi 8.2**

1. Chambua athari za kimaadili zilizosababishwa na mgongano kati ya maadili ya utamaduni wa Kitanzania na mifumo ya kiserikali iliyowekwa na wakoloni.
2. Je, ni kwa jinsi gani ukoloni ulichangia katika kuvuruga mifumo ya kiuchumi na kiutamaduni hata kudhoofisha maadili ya Kitanzania?

FOR ONLINE READING ONLY

3. Je, ni njia zipi za upinzani zilichukuliwa na jamii za Kitanzania dhidi ya mfumo wa ukoloni ili kuyalinda au kuyarejesha maadili yao ya jamii?
4. Eleza kwa mifano vitendo vya ukoloni ambavyo vilipingana moja kwa moja na maadili ya jamii za Kitanzania.
5. Ni changamoto gani za kipekee zilizojitokeza katika kusimamia na kuilinda elimu ya jadi?

## Athari za ukoloni katika mfumo wa maadili ya Kitanzania

Ukoloni ulikuwepo katika jamii za Tanzania kwa zaidi ya miaka sabini (70) na kuacha athari nyingi sana ambazo ni zao lake. Baadhi ya athari za ukoloni ni kama hizi zifuatazo:

### Kupotea kwa falsafa ya Kiafrika ya jamii na kuukumbatia ubinafsi

Mojawapo ya adhari za ukoloni katika mfumo wa maadili ya Kitanzania ilikuwa kupotea kwa falsafa ya Kiafrika ya jamii na kuibuka kwa falsafa ya ubinafsi. Falsafa au mtindo wa maisha uliokuwa umezoeleka katika jamii za Kitanzania ulikuwa ule wa maisha katika jamii. Katika utamaduni wa Kiafrika, neno jamii lina maana pana sana. Hii ni kwa sababu linahusisha watu walio hai, waliokufa na ambao hawajazaliwa. Vilevile, neno jamii linahusisha wanyama, miti, ndege, wadudu, na mazingira yote kwa ujumla wake. Kwa hiyo, Waafrika wanapotumia neno jamii wana maana ya viumbe wote, walio hai, waliokufa na wanaotarajiwa kuzaliwa. Utaratibu wa kuielewa jamii kama mjumuiko tu wa watu walio hai ni uelewa wa kisasa ambao umetokana na ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo.

Uelewa wa jamii kama mjumuiko wa viumbe hai, vilivyokufa na vinavyotarajiwa kuzaliwa ndiyo ulikuwa msingi wa maadili ya Kitanzania. Kwa maneno mengine, uelewa huu ndio ulikuwa unajenga mfumo wa maadili ya Watanzania. Kwa upande mmoja, mfumo wa maadili ulianzia katika familia na kuendelea hadi kabila. Pamoja na hayo, familia haikuwa tu muungano wa baba na mama na watoto, kama wakoloni walivyotulazimisha kuamini, bali ilikuwa muungano wa baba na mama, watoto na ndugu wa pande zote mbili pamoja na viumbe hai, vilivyotangulia mbele ya haki, na vinavyotazamiwa kuzaliwa.

Kwa mfano, karibu kila familia kuna mnyama au mdudu au mti ambao ni ndugu wa familia. Ikiwa ni mnyama, basi familia inakuwa inamheshimu, inamtunza na kwa vyovyote vile haiwezi kumuua. Kwa familia ambazo aina fulani ya nyoka ni ndugu yao, huyo nyoka anaweza kuishi na familia hiyo. Kama asipopigwa au kuchokozwa, nyoka wa familia hawezi kumuuma au kumdhuru mwanafamilia yeyote. Tabia ya kuua nyoka au wanyama na kuyaharibu mazingira kwa ajili ya kutafuta faida binafsi imeletwa na ukoloni ambao kila kitu ni bidhaa. Ngozi za wanyama, na sumu za nyoka, wadudu na mamba zilihitajika kama malighafi kwa ajili ya tiba za kizungu na kutengeza bidhaa nyingine. Tabia ya kuona mazingira kama adui na si kama ndugu wa familia, ukoo au kabila ndiyo imezaa tabia ya kuharibu mazingira. Kwa upande mwingine, ukoo

FOR ONLINE READING ONLY

au kabila haukuwa mjumuiko wa watu tu bali ulihusisha pia viumbe hai, waliokufa na wanaotarajiwa kuja duniani.

Familia, kwa maana ya mjumuiko wa walio hai, waliokufa na watakaozaliwa, ndiyo ilikuwa taasisi ya mwanzo ya maadili. Watoto katika familia walilelewa kulingana na sheria na kanuni za maisha zilizokuwa zinakubalika katika ukoo. Katika malezi, wazazi waliwafundisha watoto wao kumjua baba na mama na ndugu zao, ikiwa ni pamoja na ndugu hai wa pande zote mbili na ndugu waliotangulia mbele ya haki. Mafundisho hayo hayakushughulika tu na kuwajua kwa majina bali kuwajua kwa tabia zao na namna ya kuwaheshimu katika maisha yao. Wazazi waliwaeleza watoto maana ya majina ya wanyama au viumbe ambavyo ni sehemu ya familia, tabia zao na namna ya kuviheshimu. Kwa mfano, waliwaeleza watoto jina la msitu, tabia ya huo msitu na namna ya kuishi nao kwa amani. Tabia ya kufikiri kwamba hakuna viumbe hai vyenye tabia za maadili imeletwa na wakoloni ambao waliamini wanyama na viumbe hai vingine vipo kwa matumizi ya binadamu na malighafi na si kwa ajili ya shughuli nyingine.

Mtoto alipokosa maadili na ikaonekana familia imemshindwa, wazee wa ukoo walikuwa wanaitwa kuisadia familia kumrekebisha mtoto huyo. Ilipoonekana imeshindikana kiukoo, wazee wa kabila walihusishwa. Hii ina maana kwamba masuala ya maadili yalikuwa ya jamii na si ya mtu mmoja. Hakuna mtu hata mmoja aliyekuwa na uwezo wa kuamua kilicho kizuri na kibaya pekee yake. Vigezo vya uamuzi juu ya mema na mabaya pamoja na mazuri na yasiyo mazuri ulikuwa mikononi mwa wazee wa jamii nzima. Mtu aliyekosa maadili alikuwa hajikosei mwenyewe au familia yake au ukoo wake tu bali alikuwa anaikosea jamii nzima. Tabia ya kufikiri mtu akifanya kosa la maadili ni la kwake mwenyewe imekuja na usasa ambao uliletwa na wakoloni.

Wakoloni walipokuja waliidhoofisha na kuidharau falsafa ya Kiafrika ya jumuiya na wakapandikiza falsafa yao ya ubinafsi. Falsafa hii ya ubinafsi imejengeka katika imani kwamba uhuru wa matendo ya mtu mmoja mmoja ni bora zaidi kuliko uhuru wa jamii. Kwa sababu hiyo, falsafa ya ubinafsi ilisisitiza zaidi uwekezaji wa watu binafsi kwa malengo ya faida kwa watu binafsi, na si jamii. Vilevile, ubinafsi ni tabia ya mtu kuwa huru na kujitemegema bila kuwashirikisha watu wengine. Athari za falsafa hii ya kikoloni ilikuwa kwamba, kimaadili, mtu binafsi alikuwa na uhuru kamili wa kuamua ubaya na uzuri wa matendo yake au wema na uovu wa matendo yake. Kwa maana nyingine, maadili yanakuwa hayatoki katika jamii kama utamaduni wa Kitanzania ulivyokuwa bali yanatoka kwa mtu binafsi. Kwa mantiki hii, mtu alikuwa na uwezo wa kufanya chochote anachokitaka ilimradi kwa kufanya hivyo hakuvunja sheria za nchi. Mawazo haya yalivuruga sana maadili ya Kitanzania kwani yalifanya familia, koo na makabila visiwe na madaraka yoyote juu ya maadili ya watu wao. Mtu binafsi akawa ndiye chanzo cha maadili yake na mwamuzi wa kilicho chema na kibaya. Kilio cha maadili kushuka katika jamii kinatokana na falsafa hizi za kikoloni. Kwa hiyo, ni sahihi kusema ukoloni ulidhoofisha

FOR ONLINE READING ONLY

maisha ya jumuiya katika muktadha wa jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni na kupandikiza maisha ya ubinafsi.

**Kudhoofika kwa dini za jadi na kushamiri kwa Ukristo**

Athari nyingine kubwa iliyoharibu mfumo wa maadili ya Kitanzania ni kuathirika kwa imani au dini ya jadi, ambayo ndiyo ilikuwa chimbuko kubwa la maadili ya jamii za Kitanzamia. Dini za jadi zilikuwa na mtazamo wake kuhusu dunia na nafasi ya binadamu ndani yake. Pia, zilikuwa zinajua kabisa lengo la kuwapo kwa binadamu duniani na hatima yake. Kwa waumini wa dini za jadi, maadili yamo ndani ya utamaduni na yalitoka kwa Mungu kupitia kwa mababu. Mungu na mababu ndiyo walituwezesha kujua matendo mema, ambayo yanalinda maisha ya binadamu na matendo mabaya, yaani yale yanayodhoofisha, kuhatarisha na hatimaye kutoa maisha ya binadamu. Kwa waumini wa dini za jadi, maadili yalitokana na jinsi watu walivyomuelewa Mungu au miungu yao. Waliamini kwamba jinsi Mungu alivyo na anavyofanya ndivyo pia wanadamu wanapaswa kutenda. Kama miungu ni waaminifu, basi na wanajamii walipaswa kuwa waaminifu na kama Mungu alitenda kwa haki basi na watu walipaswa kutenda matendo ya haki. Kwa maneno mengine, maadili ya dini ya jadi yalikuwa ya kuifuata miungu walivyofanya na walivyotaka.

Mungu wa Waafrika ana sifa nyingi. Kulingana na imani za jadi, miungu ina nguvu za kuadhibu, ina huruma, wema, inajali, inasaidia katika matatizo, inaponya, inafariji, inalinda, ina ukweli, ina uaminifu, inatawala, na inatoa riziki. Waumini wa dini za jadi hawakuwa na tabia ya kuwajadili miungu kwa kujiuliza kwa nini wanafanya hayo wanayoyafanya. Kwao, matendo na matakwa ya miungu hayajadiliwi.

Ujio wa wakoloni ulienda sambamba na ujio wa dini ya Kikristo. Dini hii ilikuwa tofauti kabisa na dini za jadi. Kwanza, wamisionari walipiga marufuku dini za jadi, marufuku ambayo ilidhoofisha maadili ya Watanzania, na katika baadhi ya maeneo kuyapoteza kabisa. Pili, walipiga marufuku kabisa mila na desturi zilizokuwa zinasimamiwa na dini za jadi. Kwa mfano, walipiga marufuku mila na desturi za ndoa za mitala, na mila na desturi za kuzaliwa mtoto na kupewa jina na, kulazimisha wanaobatizwa kuchukua majina ya Kizungu na si ya Kiafrika. Aidha, walipiga marufuku matambiko kwa mababu na mizimu kwa misingi kwamba ni ya kishenzi. Vilevile, waliwafundisha na kuwalazimisha watu kuongea lugha yao badala ya Kiswahili au lugha ya makabila yao huku wanawake wakitengwa zaidi katika shughuli za kisiasa, kijamii (kama vile elimu) na kiuchumi zilizoletwa na wakoloni.

Kwa kifupi, Mungu wa wakoloni alikuwa tofauti na Mungu wa jamii za Kitanzania kwani ni Mungu aliyekuwa anachukia utamaduni wa jamii za Kitanzania na maisha yao. Alikuwa Mungu asiyewaheshimu Watanzania wala mila na desturi zao na aliyetaka Wazungu wawatawale Watanzania na kuwakandamiza. Pia, alikuwa Mungu aliyekuwa analeta ukombozi kwa mtu mmoja mmoja na si kwa jamii nzima.

FOR ONLINE READING ONLY

Baada ya muda mrefu wa kuipokea dini ya Kikristo, maadili ya Kitanzania yakaanza kudhoofika na kupotea kwa watu wengi kwani walianza kufuata maadili ya wakoloni. Kwa hiyo, athari mojawapo kubwa ya ukoloni ilikuwa ni kupoteza maadili ya Kiafrika yaliyokuwa yanatokana na imani katika miungu yao ya jadi.

**Kuibuka kwa maadili mseto**

Ukoloni ulifanya juhudi za kutosha kudhoofisha na kudharau dini za jadi na falsafa ya jamii za Kitanzania. Pamoja na juhudi hizi za kikoloni, dini na falsafa hizo hazikupotea kabisa bali zilidhoofishwa tu. Jamii za Kitanzania ziliendelea kuzienzi, kuziishi na kuziendeleza mila na desturi na maadili yao. Lakini, Ukristo ulitaka waumini wayafuate mafundisho ya Kikristo na wajitahidi kuyaishi kulingana na matakwa ya Ukristo. Pamoja na hayo bado Watanzania Wakristo waliendelea kuzidumisha baadhi ya mila, desturi na maadili ya jamii. Wakristo kwa Waislamu waliendelea kuyadumisha na kuyaenzi maadili mema ya Kitanzania na wakiyakataa maadili ya kikoloni.

**Kazi za kufanya 8.4**

Chunguza jamii unayoishi, kisha bainisha mabadiliko ya kimaadili yanayotokana na athari zake.

**Kuibuka kwa maadili ya kitumwa na ubaguzi wa rangi**

Kuibuka kwa maadili ya kitumwa na ya ubaguzi wa rangi katika Tanzania kunatokana hasa na kukua kwa usasa huko Ulaya. Usasa huko Ulaya ulijengeka kwenye nguzo kuu tatu: matumizi ya akili badala ya imani katika kutatua matatizo ya binadamu, sayansi na teknolojia na kukua kwa viwanda na miji.

Usasa ni kipindi ambacho wazungu wa Ulaya Magharibi waliacha kabisa kutumia imani ya dini katika kutatua matatizo yao ya maisha ya kila siku na kuanza kutumia zaidi akili. Matumizi ya akili ndiyo yalizaa sayansi na teknolojia, ambayo ndiyo msingi wa maendeleo ya kisasa. Matumizi ya sayansi na teknolojia ndiyo yaliwawezesha wazungu kutengeneza bunduki, meli za kuja Afrika, magari, ndege, radio, na vitu vyote tunavyoviona na kuvitumia leo. Wakiwa wanaamini kwamba matumizi ya akili ndiyo msingi wa maendeleo, wakoloni hawakusita kuanzisha mifumo ya elimu ambayo ilianzia chekechea, shule za msingi, shule za kati, vyuo vya ufundi, na vyuo vikuu. Katika shule na vyuo, wakoloni walifundisha namna ya kutumia akili kutatua matatizo ya maisha na si imani. Mfumo wao wa elimu ulikuwa hautaki kabisa matumizi ya imani kwa sababu huko kwao imani ilishaonekana kuwa chanzo cha vurugu na umaskini. Kwa kufanya hivyo, walisambaza elimu ya usasa ambayo ilidhoofisha elimu ya maadili ya jadi ambayo ilikuwa inatolewa mahali ambapo jando na unyago vilifanyika katika jamii nyingi za Kitanzania.

Uenezaji wa elimu ulienda sambamba na falsafa ya usasa na uenezaji wa sayansi na teknolojia, ambayo ndiyo ilikuwa chanzo

FOR ONLINE READING ONLY

cha uzalishaji katika viwanda. Utendaji kazi katika viwanda ulikuwa unafuata maadili ya kiwanda kilicho husika yalikuwa yamewekwa na wakoloni wenyewe. Kwa hiyo, Watanzania waliofanya kazi katika viwanda hivyo walilazimika kufuata kanuni na sheria za kiwanda kilicho husika, sheria ambazo zilizaa maadili ya utumwa. Mtumishi alikuwa anafuata sheria kama mtumwa, bila kubisha wala kulalamika. Kwa sababu wakoloni walikuwa wabaguzi wa rangi, ilibidi Watanzania katika viwanda na sekta nyingine na katika ofisi za serikali wayafuate maadili ya rangi, ambapo uzuri au ubaya ulitegemea rangi ya mtu aliyelitenda. Maadili yaliyoibuliwa na mfumo wa maisha ya usasa yalififisha mfumo wa maadili ya Kitanzania na wafanyakazi wakaanza kuwa na maadili ya woga, utumwa na ya ubaguzi wa rangi.

### Zoezi 8.3

1. Ni kwa nini wakoloni walitumia njia ya ubaguzi wa rangi kama mkakati wa kuzitawala jamii za Kitanzania?
2. Fafanua faida na hasara za utamaduni mseto.
3. Eleza ni kwa namna gani dhana ya ubinafsi iliyoletwa na wakoloni ilitofautiana na maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ujio wa ukoloni.
4. Pamoja na mbinu mbalimbali kutumiwa na wakoloni kudhoofisha utamaduni wa jamii za Kitanzania bado utamaduni huo unaishi hadi sasa. Jadili.

### Zoezi la marudio

1. Eleza matukio muhimu katika historia ya Tanzania yanayodhihirisha uzalendo wa watu wake dhidi ya ukoloni.
2. Fafanua jinsi maadili yalivyobadilika wakati wa ukoloni nchini Tanzania na kuathiri elimu ya jadi iliyokuwepo zamani.
3. Eleza jinsi ukoloni ulivyouathiri utamaduni wa jamii za Kitanzania.
4. Ni mabadiliko gani katika utawala wa kikoloni yaliyaathiri maadili ya Kitanzania?
5. Ni kwa namna gani elimu ya jadi imeendelea kutoa mchango katika kujenga upya, kuyadumisha na kuyaenzi maadili ya jamii kwa sasa?
6. Eleza changamoto za kimaadili katika ngazi ya familia za sasa za Kitanzania zinazotokana na ukoloni.
7. Kuna tofauti gani kubwa katika maadili ya jamii ya Kitanzania kati ya kipindi cha kabla ya ukolono na kipindi cha ukoloni?
8. Eleza jitihada mbalimbali za kuyajenga maadili ya Kitanzania zinazochukuliwa na serikali baada ya uhuru.

### Kazimradi

Chagua jambo au changamoto yoyote inayohusu historia ya Tanzania na maadili, kisha fanya kazimradi.

FOR ONLINE READING ONLY

## Faharasa

**Amali** Shughuli anayoifanya mtu ya kumpatia riziki au kipato halali

**Enzi za mababu/mabibi** Kipindi kirefu (au enzi) huko nyuma ambacho wazazi wetu waliishi

**Falsafa** Stadi ya maarifa, imani, maisha na chanzo na sababu za kuwapo kwake

**Kufunda** Kufundisha, hasa mafundisho ya nyumbani au tia unyagoni

**Kungwi** Mtu mwenye ujuzi wa kumfunda mwari kunga za unyago au jando zinazohusu maisha na mienendo inayokubalika na jamii

**Mababu** Wahenga au wazee wa kiume wa zamani

**Mabibi** Wahenga au wazee wa kike wa zamani

**Makavazi** Mahali ambamo nyaraka na kumbukumbu za kihistoria, mathalani za mahali, taasisi au familia huhifadhiwa kwa lengo kuona na kujifunza

**Manamba** Mfanyakazi aliyetoka mbali kwa ajili ya kufanyakazi katika mashamba makubwa yaliyomilikiwa na watu wengine, hasa walowezi, kama kibarua

**Mtwana** Mtu, aghalabu mwanaume, anayemilikiwa na mtu mwingine na kufanyishwa kazi bila malipo ya fedha

**Mzimu** Roho au kivuli cha mtu aliyekufa au maskani ya watu waliokufa ambapo watu huamini kwamba wanaweza kwenda kufanya mawasiliano na mababu wao wa zamani kwa haja mbalimbali kama kuomba mvua au kitu kingine

**Ramli** Namna ya kubashiri mambo kwa kutumia elimu ya nyota ili kujua tatizo la mtu

**Tambiko** Ibada inayofanywa na mtu, ukoo au jamii kwa mizimu yao ili kuomba neema, baraka au kutoa shukrani, kuondoa mikosi na balaa katika maisha yake au jamii nzima

**Tovuti** Mahali katika mtandao penye ukurasa mmoja au zaidi zinazoweza kutoa taarifa kuuhusu jambo maalum kwenye mtandao

**Turadhi** Kitu cha kale cha makumbusho ya kihistoria

**Waajemi** Jamii ya watu au jamii kutoka ghuba ya Uajemi

**Wavuti** Mtandao wa kompyuta wa mawasiliano yenye taarifa mbalimbali za kimataifa

FOR ONLINE READING ONLY

## Bibliografia


Benki ya Dunia. (2023). *Ripoti ya matumizi mabaya ya rasilimali na maendeleo Endelevu*. Benki ya Dunia.

Biginagwa, T. J. (2020). Development of Cultural heritage registration in post-colonial Tanzania. *Tanzania Zamani, 12*(1).

Bushozi, P. (2014). Towards sustainable cultural heritage management in Tanzania: A case study of Kalenga and Mlambalasi sites in Iringa, Southern Tanzania. *The South African Archaeological Bulletin*, 69 (200), 136–141.

Bigambo, R. (2020). Safeguarding practices for intangible cultural heritage in Tanzania: national vs local perspectives. bham.ac.uk

Bentley, J. H. (1996). Cross-cultural interaction and periodization in world history. *The American Historical Review, 101*(3), 749-770.

Bowser, B. P. (2017). Racism: Origin and theory. Journal of black studies, 48(6), 572-590.

Burton, E. (2013). "What tribe should we call him?" The Indian Diaspora, the State and the Nation in Tanzania since ca. 1850. Stichproben: Wiener Zeitschrift für kri tische Afrikastudien, 13, 1-28.

Chami, M. F. & Kajiru, E. J. (2023). Assessment of 12 years (2011–2023) implementation of the 2003 UNESCO convention on safeguarding Intangible Cultural Heritage (ICH) in Tanzania. *Cogent Arts & Humanities*, 10:1, DOI: 10.1080/23311983.2023.2254044

Chinweizu. (1993). "Africa and the Capitalist Countries" in Mazrui, Ali and Wondi C. Africa since 1935, General History of Africa, VIII, 769-797.

Colonial Education and the State of Contemporary Socio-Cultural Relations in Africa (2021) Tanzania, *International Journal of Education and Research* IX (9)

Conn, H. M. (1978). Islam in East Africa: *an overview. Islamic Studies*, 17(2), 75-91.

Davidson B., Mhina F., Ogot A. (1967). *The growth of African civilization east and central Africa to the late nineteenth century*. Longman.

Disko, S. & Tugendhat, H. (Wah.). (2013). *World Heritage Sites and indigenous peoples' rights* (189–220). IWGIA.

Flores de León, R. M., Babere, N. J., & Swai, O. (2020). Implications of cultural heritage in urban regeneration: The CBD of Dar es Salaam. Revue Interventions économiques. Papers in Political Economy, (63).openedition.org

Haynes, B. (2009). Introduction to Special Issue: Patriotism and and citizenship education. Educational Philosophy and Theory, 41(4), 365-377. doi:10.1111/j.1469-5812.2009.00527.x

Historical Association of Tanzania. (1980). Tanzania Under Colonial Rule. (M. Kaniki, Ed.) Longman Group Limited.

Hobson, J. A. (2011). *Imperialism*. Cambridge University Press.

Igboin, B. O. (2011). Colonialism and African cultural values. *African Journal of*


FOR ONLINE READING ONLY

*History and Culture, 3*(6).

Iliffe, J. (1979). *A modern History of Tanganyika.* Cambridge University Press.

Institute of Curriculum Development. (1981). *The development of African Societies up to the 19th century: Secondary History book one*. Dar es Salaam University Press.

Itandala, A.B. (1992). "The Anglo- German Partition of East Africa, 1885-1895", *in Tanzania zamani*. pp. 1, *Africa*. VII,.152-153.

International Labour Organization. (2023). *Haki za wazawa na maendeleo ya uchumi*. ILO Publications.

Israel K. Katoke. (1984). Christianity and Culture: *An African Experience, Transformation*. 1(4) (1984), 7-10. Sage Publications, Ltd.

Jekshus, H. (2022). *Ecology control and economic development in East African history: the case of Tanganyika 1850–1950.* University of California Press.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2023). *Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Nne. 2023-2030*

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (1977). *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.*

Kjekshus, H. (2022). *Ecology control and economic development in East African history: the case of Tanganyika 1850–1950.* University of California Press.

Kieran, J. A. (1971). Christian villages in north-eastern Tanzania: *Trans African Journal of History*, 1 (1) (January 1971), 24-38. Gideon Were Publications

Kimambo, I. N., & Maddox, G. H. (2019). *A new history of Tanzania*. Mkuki na Nyota Publishers.

Kimambo. I.N. & A.J. Temu. (wah.). (1969). *A History of Tanzania.* Tanzania Publishing House

Langer. W.L. (1935). *The Diplomacy of Imperialism.*

Larsen, P., Oviedo, G., & Badman, T. (2014). World Heritage, indigenous peoples, communities and rights: *An IUCN perspective.* Katika *S. Disko, & H. Tugendhat (Wah.), World Heritage Sites and indigenous peoples' rights* (kur. 65–82). Copenhagen: IWGIA

Lenin, V.I. (1917). *Imperialism the Highest Stage of Capitalism.*

Lwoga, N. B. (2017). Cultural heritage tourism and the community in Tanzania. *African Heritage and Pillars of Sustainability Conference*.

Magesa L. (1997). "*African Religion, the Moral Traditions of Abundant Life*" Orbis Books,.35-161

Masamba, D. P.B. (2017). *Historia ya Kiswahili; Mtazamo Mpya 100kk hadi 2000k.*, Kiswahili Development Limited 12-20

Mapunda, H. (1976). *Historia ya Mapambano ya Mwafrika.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

FOR ONLINE READING ONLY

Mansour, J., & Mwambwiga, A. (2021). Marketing heritage assets in the National Museums of Tanzania: a case of National Natural History Museum in Arusha. *Journal of Tourism Quarterly, 3*(1), 21-39.

Masele, F. (2012). Private Business Investments in Heritage Sites in Tanzania: Recent Developments and Challenges for Heritage Management. *African Archaeological Review* 29:51–65.

Masebo, O. (2016). "Tanzania-Oman Historic Ties, the Past and Present" *A Journal of African*

Miller, R. (2005). Moral courage: Definition and development. *Ethics Resource Centre. Politics, Development and International Affairs*, 43(1),27-50.

Mbogoni, L. (2015). *Ukoloni na Harakati za Ukombozi wa Tanzania*. East African Education Publishers.

Melubo, K. (2020). *Is there room for domestic tourism in Africa?* The case of Tanzania. *Journal of Ecotourism*.academia.edu

Mwanzi, H. A. (1985). "African Initiatives and Resistance in East Africa 1880- 1914", *General History of Africa* 7,149-168.

MNRT. (2018). Hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Dkt Hamisi A. Kigwangalla (Mb) wakati akiwasilisha Bungeni makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Dodoma.

Nabudere, D.W. (2017). *The Political Economy of Imperialism*. Mkuki na Nyota Publishers

Nimtz Jr, A. H. (1980). *Islam and politics in East Africa: The Sufi order in Tanzania*. University of Minnesota Press.

Odhiambo. A.E.S, Ouso, T. I. & Williams, J.F.M. (1977). *A History of East Africa*. Longman Group UK Limited.

Olenasha, W. (2014). *A World Heritage Site in the Ngorongoro Conservation Area*: Whose world?

Pouwels, R. L., & Pouwels, R. L. (2002). Horn and crescent: *cultural change and traditional Islam on the East African coast, 800-1900* (Vol. 53). Cambridge University Press.

Rumishael P. N. & Losaru, J. (2017). Assessing the contribution of cultural heritage sites to tourism development: A case study of Oldupai and Alaitole footprint area, Tanzania. *African Journal of Hospitality, Tourism and Leisure, 6* (1), 1-24.

Ranger, T.O. (1985). "African Initiatives and Resistances in the Face of Partition and Conquest" in H. A, VII,45-62.

Schmidt, P. R., & Ichumbaki, E. B. (2020). Is there hope for heritage in former British colonies in eastern Africa? A view from Tanzania. *Journal of African Cultural Heritage Studies, 2*(1), 26-51.researchgate.net

Smith, T. W., & Jarkko, L. (1998). *National pride: A cross-national analysis*. Chicago, IL:

National Opinion Research Center, University of Chicago.


FOR ONLINE READING ONLY

Poole, R. (2008). Memory, history and the claims of the past. *Memory studies, 1*(2), 149-166.

Shija, M. (2008). *Historia ya Tanzania: Kutoka kabla ya ukoloni hadi uhuru.*Mkuki na Nyota Publishers.

Su, M. M., & Wall, G. (2014). *Community participation in tourism at a World Heritage Site*: Mutianyu

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. (2012). *Tenzi Tatu za Kale,* TUKI

Taasisi ya Elimu. (1987). *Historia Shule za Msingi. Jamii za Watanzania tangu mwaka 1880.* Dar es Salaam: Tanzan International Marketing (T) Ltd.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2021). *Historia ya Tanzania. Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano.* Dar es Salaam.

United Republic of Tanzania. (2022). *prevention and combating of corruption act, cap 329.*

United Nations Environment Programme. (2022). *Ripoti ya mazingira na biashara.* UNEP Publications.

Uslaner E.M & Hottug. N.L. (2021). "Natonal Identity and Social Cohesion"ECPR press,London, 1-298

Uzoigwe, G.N. (1985). "European Partition and Conquest of Africa: An Overview" in *General history of Africa*, 7,19-44.

Winant, H. (2000). Race and race theory. *Annual review of sociology, 26*(1), 169-185.

World Economic Forum. (2024). Ripoti ya uwekezaji wa sekta binafsi na maendeleo. WEF Publications.

FOR ONLINE READING ONLY